NAKALA YA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

# BUNGE LA TANZANIA

---

# MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

## Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 19 Mei, 2017

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Tukae, Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

## HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:**

Houtuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. MATTAR ALI SALUM (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIFUGO, KILIMO NA MAJI):**

Taarifa ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO (K.n.y. MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI):**

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani juu ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE–KATIBU MEZANI:**

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 234

### Posho ya Madaraka kwa Viongozi

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Serikali ilitoa Waraka Na.3 wa mwaka 2014 kuhusu Posho ya Madaraka kwa viongozi wa elimu wakiwemo Walimu Wakuu wa Shule za Msingi, Sekondari, Vyuo na Waratibu Elimu Kata lakini tangu waraka huo utolewe yapata karibu miaka miwili sasa posho hiyo haijaanza kulipwa.

Je, ni lini Serikali itaanza kulipa posho hiyo ya viongozi wa elimu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianza kutekeleza Waraka Na. 3 wa mwaka 2014 kuhusu Posho ya Madaraka kwa Viongozi kuanzia Julai, 2016. Walimu Wakuu wanalipwa kiwango cha shilingi 200,000 kila mwezi na Wakuu wa Shule na Waratibu wa Elimu Kata wanalipwa Posho ya Madaraka kwa kiwango cha shilingi 250,000 kwa mwezi. Kuanzia Julai, 2016 hadi Aprili, 2017, Serikali imelipa posho hiyo jumla ya shilingi bilioni 1.87. Posho hiyo inalipwa kwa viongozi hao kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa elimu katika ngazi ya shule nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cosato Chumi, swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza napenda kuipongeza Serikali kwa kuanza kutekeleza Waraka huo wa kuwalipa Posho ya Madaraka Walimu Wakuu wa Shule pamoja na Waratibu. Hata hivyo nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kuwa posho hii kama ilivyoelezwa katika Waraka ni Posho ya Madaraka. Je, Serikali sasa haioni ni wakati muafaka kuanza kulipa posho hii kwa ajili ya viongozi wengine kama vile Afisa Elimu, Afisa Elimu Taaluma pamoja na Afisa Elimu Takwimu na Vifaa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa kazi ya ualimu ni zaidi ya kufundisha, kuna kufanya maandalio, kufundisha, kusahihisha, kupanga matokeo na mengine mengi tu. Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kurejesha ile tulikuwa tunaita *Teaching Allowance* kwa ajili ya kuwalipa walimu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mbunge kwa sababu swali hili ni *concern* ya

walimu wote na hii kwanza mwanzo ilikuwa inajitokeza na Serikali tuliamua kuitekeleza kama tulivyosema hapo awali. Suala la jinsi gani tuangalie Maafisa Elimu Taaluma, Maasifa Elimu Takwimu watapata posho hii, nadhani vyeo hivi ni vya kimuundo ambavyo viko katika Halmashauri zetu maana yake kuna hao vilevile kuna Maafisa Kilimo na Maafisa mbalimbali. Kwa sasa kwanza tuendelee na utaratibu wa sasa na pale itakapoonekana kuna haja ya kuweza kufanya mabadiliko tutafanya hivyo. Lengo letu kubwa ni kupandisha *motivation* ya wafanyakazi hasa watendaji wetu katika ngazi mbalimbali waweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jambo lingine la *Teaching Allowance,* hata Mheshimiwa Masoud alisimama hapa hoja yake ilikuwa ni hiyo hiyo, jambo hili tumelichukua. Bahati nzuri Waziri wetu hapa wa Utumishi kutoka Ofisi ya Rais nakumbuka mwezi Mei, 2017 alifanya mkutano rasmi wa uzinduzi wa Bodi hii. Sasa tunakwenda kuangalia suala zima la wafanyakazi katika mazingira mbalimbali maana hatuzungumzii walimu peke yake, tuna Mabwana Shamba, tuna watu wa kada mbalimbali ambao na wenyewe wako katika mazingira hayo magumu. Ndiyo maana Serikali kupitia Ofisi ya Rais, Utumishi inashughulikia jambo hili kwa upana wake lengo kubwa ni kuja na ajenda pana ya Kitaifa ni nini tufanye kutatua matatizo ya wafanyakazi walio katika mazingira mbalimbali ya utendaji wa kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bilago.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Suala la *Teaching Allowance* huwa halieleweki vizuri ndiyo maana linachanganywa na kada zingine. *Teaching Allowance* lengo lake ni ku-*offset* zile saa nyingi ambazo mwalimu anatumia kusahihisha madaftari au kazi za wanafunzi mpaka nyumbani kazi ambayo haifanywi na sekta zingine. Hakuna Bwana Kilimo anakwenda kusimamia...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bilago uliza swali.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Najenga hoja.

**NAIBU SPIKA:** Usijenge hoja swali lako ni la nyongeza, kwa hiyo, utakuwa umeshalipanga tayari. Uliza swali lako ili tu-*save* muda.

**MHE. KASUKU S. BILAGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali lazima iangalie *Teaching Allowance* kwa walimu kama kitu pekee kabisa. Je, ni lini sasa Serikali itakuja na mkakati rasmi wa kuwasaidia walimu hawa kupata hiyo *Teaching Allowance? (Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Utumishi na Utawala Bora majibu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wazir wa Nchi, Ofisi ya Rais - TAMISEMI naomba kujibu swali la Mheshimiwa Bilago, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimueleze tu Mheshimiwa Bilago kwamba kama Serikali tunatambua umuhimu na thamani ya mwalimu na uzito na ugumu wa kazi wanayofanya na ndiyo maana ukiangalia katika kada za utumishi wa umma walimu wamepewa kipaumbele cha hali ya juu na bado hatutasita kufanya hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika,nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge, tumeanza zoezi la tathmini ya kazi, tunaangalia uzito, majukumu na aina za kazi kwa ujumla wake katika Utumishi wa Umma na posho zipi zitatakiwa kuwepo katika kada gani.

Nimuombe Mheshimiwa Mbunge aendelee kuvuta subira, zoezi hilo la tathmini ya kazi litakamilika katika mwaka huu wa fedha na baada ya hapo tutaweza kuainisha na kupitia na kuhuisha miundo mbalimbali ya kiutumishi vilevile kuangalia ni posho zipi ambazo zinahitajika kuwepo ikiwemo na hiyo ya *Teaching Allowance* kwa mapana yake. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daimu Mpakate, swali la nyongeza.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Makaimu Watendaji wa Vijiji karibu maeneo mengi ya Tanzania hawapewi posho. Je, Serikali haioni haja ya kuwapa posho Makaimu Watendaji wa Vijiji ili waweze kufanya kazi zao vizuri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, anachosema Mheshimiwa Mpakate ni kwamba katika maeneo mbalimbali ya vijiji vyetu watu wengi wanakaimu na kuna maeneo mengine walimu ndiyo walikuwa wanakaimu kama Watendaji wa Vijiji na tumetoa maelekezo katika Kurugenzi zetu kuacha kukaimisha Watendaji wa Vijiji hasa wale walimu kwa sababu wanaondoa nguvu kubwa sana ya ufundishaji. Katika jambo hili, kila Halmashauri tumeipa maelekezo na kila Mkurugenzi anajua ana watu wangapi wanakaimu sasa kupitia *own source* zao wataangalia utaratibu gani wa kufanya lakini lengo kubwa tunataka katika kila kijiji kazi ziweze kufanyika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea. Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 235

**Kupandisha Madaraja Walimu Wanaojiendeleza**

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA** aliuliza:-

Je, nini mkakati na sera ya Serikali kwa wafanyakazi hususani walimu wanaojiendeleza katika kuwapandisha madaraja na kuwaongezea mishahara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za 2009, watumishi wa umma hupandishwa vyeo kwa kuzingatia sifa na ufanisi na utendaji kazi. Mwalimu anapohitimu mafunzo yake anastahili kubadilishiwa muundo wake wa utumishi mfano, Mwalimu Daraja la III - Stashahada kwenda Daraja la II ngazi ya Shahada. Kupanda daraja kwa mtumishi kunategemea utendaji kazi utakaothibitishwa na matokeo katika Mfumo wa Wazi wa Upimaji Utendaji Kazi wa mtumishi husika yaani *OPRAS system.* Watumishi wote wanatakiwa kujaza fomu hizo na kupimwa utendaji wao wa kazi kama wanastahili kupandishwa daraja.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kama ilivyoelezwa na Ofisi ya Rais, Menejiment ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, walimu wakiwemo watumishi wengine wenye sifa watapandishwa madaraja katika mwaka wa fedha 2017/2018 baada ya kukamilika kwa zoezi la uhakiki wa watumishi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. MARY M. MWANJELWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu ya Naibu Waziri kwanza naishukuru sana Serikali yangu kwa maana ya kwamba iliweza kutatua tatizo la walimu waliokuwa wanapandishwa madaraja lakini hawapati mshahara. Nina maswali mawili madogo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, kwa kuwa taarifa ya uhakiki wa vyeti imeshatolewa na katika Jiji la Mbeya kuna walimu zaidi ya 200 waliobaki. Je, ni lini sasa

Serikali itaruhusu marekebisho ya mishahara kwa walimu hao waliokwishapandishwa vyeo vyao kufanyika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, kumekuwa na tatizo la watumishi kukaa katika kituo kimoja kwa muda mrefu sana na hivyo kushindwa kuleta changamoto mpya katika kipindi hiki cha Hapa Kazi Tu na kufanya kazi zao kwa mazoea. Nilitaka kujua nini mkakati wa Serikali katika hilo? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli alichosema Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, alitaka *time frame* ni kwamba katika mwaka ujao wa fedha zoezi hili litaanza. Mheshimiwa Mwanjelwa asihofu watumishi wake watapata hiyo stahiki yao inayotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini suala la watumishi wengi kukaa kituo kimoja muda mrefu, ni kweli tunafahamu kwamba mtumishi anapokaa miaka 15, 20 hana changamoto mpya ambayo anaweza akaileta katika eneo hilo. Ndiyo maana Ofisi yetu kila mwaka tumekuwa tukifanya utaratibu huo katika maeneo mbalimbali, lengo kubwa ikiwa ni kuleta hii changamoto mpya na tunaendelea kufanya zoezi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tuko makini sana katika kuhamisha watumishi. Kwa mfano, tumetoa maelekezo kwa Wakurugenzi wetu kwamba waangalie jambo hilo, lakini wasihamishe watumishi hivi hivi bila kuwa na pesa yao kuweza kuwalipa. Jambo hili tumelielekeza na bahati nzuri Mheshimiwa Rais siku ya Mei Mosi alilitolea maelekezo maalum kwamba sasa hakuna utaratibu wa kumhamisha mtu kabla ya pesa yake kuwa tayari.

Naomba nimhakikishie kwamba Ofisi ya Rais, TAMISEMI tutahakikisha tunakuza utendaji wa kazi na kuangalia mtu

kama ame-*over stay* kwa muda mrefu tutaona namna ya kumhamishia sehemu nyingine ili kuleta changamoto mpya.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan Lyimo.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipatia nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo ambalo linatusikitisha ni kwamba pamoja na kupandishwa madaraja walimu hawa hawalipwi pesa zao suala ambalo linapelekea kila mwaka walimu hao kudai takribani shilingi bilioni 21. Je, Serikali haioni kutokuwapandisha madaraja na kutokuwalipa kunasababisha kulimbikiza madeni yao na ndiyo sababu inafanya walimu kutokuwa na motisha wa kazi? Ni lini sasa Serikali itawalipa fedha zao wanapopandishwa madaraja? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, tafadhali jibu swali moja kati ya hayo mawili. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, unafahamu tumekuwa tukitoa taarifa mbalimbali ya madeni ya walimu ambayo tumekuwa tukiyalipa na tulisimama kwa ajili ya zoezi la uhakiki. Kwa hili naomba niwaambie, tumezungumza na hapa nilisema katika eneo langu la kwanza kwamba suala la malipo haya yote mwaka huu wa fedha unapokuja kila mtu atapata stahiki yake.

Serikali hii ya Awamu ya Tano lengo lake kubwa ni kuondoa hizi changamoto ndogo ndogo tulizokuwa nazo kwani tunataka tupate wafanyakazi wenye ari ya kutosha. Sisi ambao ni *beneficiaries* wa utekelezaji wa Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi lazima tuitekeleze, naomba nimhakikishie jambo hilo halina mashaka tutalitekeleza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hasunga, swali la nyongeza.

**MHE. JAPHET N. HASUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya walimu wamekuwa wakijiendeleza wao wenyewe katika vyuo mbalimbali na kupata vyeti lakini kwa muda mrefu Serikali imekuwa ikivikataa vyeti hivyo, imekuwa haivitambui. Je, Serikali ina mkakati gani wa kuvitambua hivyo vyeti ili waweze kupandishwa madaraja zaidi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kujiendeleza ni kujiendeleza tu aidha Serikali imekusomesha ama umejiendeleza mwenyewe kinachotakiwa ni kujiendeleza. Ndiyo maana katika jibu la msingi mwanzo nimesema mtu akijiendeleza maana yake ana-*submit* cheti chake, kinapitiwa na kuhakikiwa na Afisa Utumishi mtu huyo anastahili kupanda daraja na kuwekwa katika nafasi yake anayostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama kuna kesi kama hiyo, maana wakati mwingine hatuwezi tukajibu kesi hapa zote kwa ujumla, inawezekana kuna *case by case,* kama likiwa hilo basi tunaomba tujulishane hiyo kesi imejitokeza wapi tuweze kuifanyia kazi. Mtu yeyote aliyesoma *provided* kwamba amesoma na ana cheti halali jambo hilo halina mashaka la kuwekwa katika muundo anaostahili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mbarouk Salim Ali, Mbunge wa Wete sasa aulize swali lake.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuuliza swali kwa niaba ya Mhesbimiwa Mbarouk Salim Ali, naomba unipe dakika moja niwapongeze vijana wetu wa *Serengeti Boys* kwa ushindi wa mabao mawili dhidi ya Angola. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 236

**Mashamba ya Mpira-Tanga na Morogoro**

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS (K.n.y MHE. MBAROUK SALIM ALI)** aliuliza:-

Moja ya jitihada za Serikali za kufufua Kiwanda cha *General Tyre* kilichopo Arusha ni pamoja na kuendeleza kilimo cha mpira katika mashamba yaliyoko Tanga na Morogoro ili kupata malighafi.

Je, mashamba hayo yana ukubwa gani na umri gani?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbarouk Salim, Mbunge wa Wete, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Matairi Arusha *(General Tyre)* bado hakijaweza kuanza kufanya kazi kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo uchakavu wa mitambo na teknolojia inayotumika kupitwa na wakati. Serikali imelenga kukifufua kiwanda hicho ambapo imefanya utafiti ili kubaini namna bora ya kukifufua. Taarifa ya awali imeeleza kuwa, mitambo iliyopo ibadilishwe na kuweka mipya inayotumia teknolojia ya kisasa. Vilevile kiwanda kipanuliwe ili kiweze kuzalisha matairi ya aina mbalimbali kwa wingi ili kuzalisha kwa faida na uendeshaji wake uwe chini ya sekta binafsi na Serikali iwe mbia kwa kwa hisa zinazolingana na rasilimali za kiwanda zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kiwanda hicho na mashamba ya mpira hayana uhusiano wa karibu kwani hakitumii mpira unaozalishwa kwenye mashamba yetu. Hii

ni kwa kuwa kinatumia malighafi iliyo katika mfumo wa majora wakati teknolojia ya kugema mpira inayotumika kwenye mashamba yetu inatoa malighafi iliyo katika mfumo wa vipande. Mpira unaozalishwa nchini unatumika katika viwanda vingine kama vile *Ok Plastic, Bora Shoes* na viwanda vingine vidogo vidogo lakini vilevile unauzwa nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la mpira ni moja kati ya mazao ya biashara ambayo yamekuwa yakizalishwa nchini kwa muda mrefu katika mashamba yaliyopo Kalunga - Mang'ula katika Wilaya ya Kilombero Mkoa wa Morogoro na shamba la Kihuhwi lililopo Wilaya ya Muheza Mkoa wa Tanga ambayo yalianzishwa mwaka 1978. Shamba la Kihuhwi lina ukubwa wa hekta 790 na shamba la Kilunga Mang'ula lina ukubwa wa hekta 750. Mashamba ya mpira kwa upande wa Zanzibar yapo Machai na Mselem Unguja yenye hekta 637 na mashamba madogo saba yaliyopo Unguja na Pemba yenye ukubwa wa hekta 633.

Mheshimiwa Naibu Spika, mashamba haya, yaani ya Kilunga na Mang'ula yanazalisha utomvu kati ya tani 0.6 hadi 1.0 kwa hekta kwa mwaka kutokana na miti yake kuwa na umri mkubwa. Kitaalamu uzalishaji wa utomvu huwa kati ya tani 0.8 hadi 1.3 za utomvu kwa hekta kwa mwaka na kupungua kadri ya miti ya mipira inavyozidi miaka 35 tangu kupandwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mashamba ya Tanzania Bara uzalishaji umepungua kutoka kilo 183,420 mwaka 2009 hadi kilo 165,335 mwaka 2014. Kwa upande wa Zanzibar uzalishaji umeshuka kutoka kilo 4,229,226 mwaka 2008 hadi 2,249,021 mwaka 2011.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuwa mashamba haya yamezeeka na hayapati matunzo ya kutosha ndiyo maana uzalishaji umeendelea kushuka. Serikali kupitia Shirika la Maendeleo ya Taifa yaani *NDC* imeanza kuendeleza shamba la Mang'ula ambapo kiasi cha miche 212,500 imepandikizwa ili kuongeza uzalishaji wa utomvu. Aidha,

Serikali inahamasisha wakulima na wawekezaji kuzalisha zao hili kwa kuwa soko lipo kwa viwanda vingine vya ndani na nje ya nchi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf, swali la nyongeza.

**MHE. YUSSUF HAJI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu marefu ya Mheshimiwa Waziri, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshiwa Naibu Spika, katika majibu yake Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba mashamba haya yamekuwa ya muda mrefu na uzalishaji wake umekuwa mdogo sana. Pia mashamba haya yanatumia hekari nyingi sana, kwa hiyo, yamechukua sehemu kubwa ya ardhi ya Tanzania. Pamoja na kukiri kwamba hakuna uhusiano baina ya Kiwanda ya *General Tyre* na mashamba haya. Namuuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, je, Serikali iko tayari kuleta matumizi mbadala ya mashamba haya kwa sababu hayalisaidii Taifa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Kiwanda cha *General Tyre* si kiwanda kipya ni kiwanda cha zamani sana na kilikuwa kinazalisha. Hata hivyo, marekebisho yake naambiwa yafanyiwa utafiti, ukiuliza utafiti, ukiuliza utafiti, hakimaliziki kiwanda kufanyiwa utafiti ili kuzalisha. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri haoni kwamba hatujawa tayari kuingia katika Tanzania ya viwanda kwa mwendo huu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu mipira au zao la mpira kuchukua ardhi kubwa na hiyo ardhi kutoweza kutumika kwa tija zaidi, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa mashamba ya mpira tuliyonayo hayajachukua ardhi kubwa sana. Tunachofikiria sasa kama Wizara na Serikali ni kujaribu kutafuta ardhi nyingine ili

tuongeze uzalishaji wa mpira. Kwa sasa tunafikiri mpira soko lake limeimarika tena hata jirani nchini Kenya kuna soko, lakini vilevile China kuna soko kubwa. Kwa hiyo, sasa tunajaribu kuangalia namna ya kuwekeza tena kwenye mpira ili liwe tena ni zao ambao wakulima wetu wanaweza kunufaika nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwa sasa hatufikirii ile ardhi iende kwenye matumizi mengine lakini tunachofanya ni kuendelea kuimarisha mashamba yaliyopo lakini vilevile kujaribu kuongeza ardhi nyingine ili kilimo cha mpira kiweze kupanuka. Vilevile kujaribu kuimarisha teknolojia ambayo tunatumia kwa sasa ili iweze kuendana na mahitaji ya sasa ya soko la mpira duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kuhusiana na *General Tyre.* Kama nilivyosema kwenye jibu la msingi, Serikali inaendelea kufanya tathmini kuhusu namna bora ya kurejesha tena Kiwanda cha *General Tyre* kiingie katika uzalishaji. Kimsingi tulichosema ni kwamba taarifa ya awali inaonyesha kwamba tunahitaji kuboresha teknolojia iliyopo, lakini vilevile mfumo wa uendeshaji uwe ni kwa utaratibu wa kushirikiana na sekta binafsi kwa maana ya *PPP* ili Serikali iweze kubakia na hisa chache tu na hasa zile zinazolingana na mali au uwekezaji ambao Serikali tayari umeshaufanya, lakini huku Serikali ikijaribu kuvutia wawekezaji ili iendeshwe kwa ubia na sekta binafsi. Kwa hiyo, siyo kwamba Kiwanda cha *General Tyre* kimetupwa lakini ni kwamba sasa jitihada zinaendelea ili kukifufua ili kiweze kufanya kazi tena.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selasini, swali fupi tafadhali.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Katika nchi yetu ajali za barabarani zimekuwa nyingi sana na moja kati ya sababu za ajili hizi ni matairi ya mitumba yanayoagizwa kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, labda niseme Tanzania ni nchi pekee ambayo inaagiza matairi ya mitumba ikijua kabisa kwamba matairi haya yanakuwa yamemaliza muda

wake na inaweza ikawa kisababishi kikubwa cha ajali. Sasa wakati tukisubiri kiwanda hiki kufufuliwa, hadithi ambayo imekuwa ni ya miaka mingi, je, Serikali ina mpango gani wa kupiga marufuku uingizaji wa matairi yaliyotumika katika nchi ambayo yanasababisha ajali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba ajali za barabarani zimeendelea kuongezeka nchini na inawezekana kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba matairi yasiyo na ubora ni moja kati ya visababishi. Kimsingi suala la ajali za barabarani ni suala ambalo Serikali linalichukulia kwa uzito sana, ni kero kubwa inaondoa maisha ya wananchi wetu. Kwa hiyo, Serikali inaangalia ni namna gani ya kudhibiti ajali hizo ikiwa ni kuangalia visababishi kama hilo la matairi, kwa sababu kuna visababishi vingine mfano uendeshaji usiozingatia utaratibu, uendeshaji kupita *speed* inayotakiwa, lakini vilevile madereva kulewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kimsingi Serikali inaangalia suala la ajali katika ujumla wake na visababishi vile itahakikisha inavifanyia kazi ili tuendelee kupunguza ajali barabarani. Kwa hiyo, kama hilo la matairi ni moja ya visababishi kwa vyovyote vile Serikali inalifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, swali fupi.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, shamba la Kihuhwi ambalo lipo Wilayani Muheza ni kweli lilikuwa linalima mpira na linaendelea kulima mpira na lilikuwa lina- *supply* kwenye kiwanda cha *General Tyre* - Arusha. Sasa hivi shamba hilo ni moja ya mashamba ambalo limeshafutiwa hati na

Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Naibu Waziri, haoni sasa kutokana na matatizo ya Kiwanda cha *General Tyre* - Arusha, mikakati ifanyike kiwanda hicho kiwe na mashine za kisasa na kihamishiwe Wilayani Muheza ambapo nafasi tunaweza kutoa na kiwe karibu na malighafi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, nadhani hilo linahitaji majibu mafupi tu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anapendekeza kwamba tuhamishe Kiwanda cha *General Tyre* tupeleke Muheza. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kuna timu inafanya kazi ya kuangalia namna bora ya kufufua Kiwanda cha *General Tyre*.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimhakikishie tu kwamba nitawapelekea pendekezo la kuangalia kama inawezekana kupeleka Muheza, lakini zaidi zaidi ni vizuri vilevile kuangalia uwezekano wa kuanzisha kiwanda kipya Muheza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Shally Joseph Raymond, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na 237

**Kusuasua kwa Ushirika Nchini**

**MHE. SHALLY J. RAYMOND** aliuliza:-

Ushirika hususani wa mazao hauna maendeleo mazuri na umekuwa ukisuasua kwa sababu mbalimbali.

(a) Je, ni vigezo gani vinatumika kupima na kutathmini maendeleo ya ushirika?

(b) Je, ni hatua zipi zinachukuliwa na Serikali kuboresha mazingira ya ushirika kukua?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi naomba kujibu swali la Mheshimiwa Shally Josepha Raymond, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ili kupima na kutathmini maendeleo ya ushirika nchini, Serikali inatumia vigezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na ongezeko la idadi ya Vyama vya Ushirika vinavyoandikishwa na idadi ya wanachama kwenye vyama hivyo; idadi ya wananchi wanaopata huduma za kijamii na kiuchumi kupitia Vyama vya Ushirika nchini; uzalishaji na mauzo kupitia Vyama vya Ushirika; mitaji ya Vyama vya Ushirika na Vyama vya Ushirika vinavyouza mazao yaliyoongezwa thamani.

Pia uwekezaji wa Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii mfano, huduma za kifedha, shule na majengo ya vitega uchumi; ajira kupitia Vyama vya Ushirika pamoja na thamani na idadi ya mikopo inayotolewa kwa wananchama wake katika kutatua matatizo ya kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, vigezo vingine ni pamoja na kupima ufanisi wa uendeshaji wa shughuli za Vyama vya Ushirika kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Vyama vya Ushirika ikiwemo kupitia Ukaguzi wa mara kwa mara wa nje *(external audit)* kila mwaka.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali zenye lengo la kuboresha mazingira ya ukuaji wa sekta ya ushirika nchini. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini kwa lengo la kuijengea uwezo wa kiutendaji ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya Maafisa Ushirika katika ngazi ya Taifa, Mkoa na Wilaya na kuendeleza kuwachukulia hatua za

kisheria na kinidhamu watendaji wa Serikali, Wajumbe wa Bodi na Watendaji wa Vyama vya Ushirika kwa kushindwa kusimamia sheria katika kutekelza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua nyingine zinazochukuliwa ni pamoja na kutoa elimu na kuendelea kuboresha mifumo ya masoko hususan wa Stakabadhi Ghalani; kuendelea kuviwezesha Vyama vya Ushirika kuzitambua kwa kuzihakiki mali zao na kuweka mikakati ya kuziendeleza mali hizo kwa manufaa ya wanachama; kuimarisha usimamizi na ukaguzi katika Vyama vya Ushirika kuzitambua kwa kuzihakiki mali zao na kuweka miakkati ya kuziendeleza mali hizo kwa manufaa ya wanachama; kuimarisha usimamizi na ukaguzi katika Vyama vya Ushirika.

Pia kuwajengea uwezo wanachama; kusimamia upatikanaji wa viongozi waadilifu na wawajibikaji wanaozingatia madili na misingi ya ushirika na pia kushirikisha Wizara za Kisekta na wadau mbalimbali katika kuhamasisha na kuendele za ushirika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shally Raymond, swali la nyongeza.

**MHE. SHALLY J. RAYMOND:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ili wananchi waupende ushirika ni pamoja na kuona kuwa mali zao ziko salama na wananufaika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza Serikali, kwa Vyama vya Ushirika ambavyo mali zake zimetapanywa yakiwemo mashamba, viwanja, nyumba, hususani *KNCU,* Serikali inasaidiaje ili kurejesha mali hizo ili wananchi wanufaike? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Serikali inasaidiaje mikataba mibovu iliyoingiwa na Vyama vya Ushirika na wale ambao wamechukua mali za vyama hivyo iletwe ili irekebishwe wananchi hao waweze kuona sasa ushirika wao unaendelea vizuri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba baadhi ya mali za Vyama vya Ushirika zimetapanywa na hazitumiki kwa utaratibu unaotakiwa na ndiyo maana Wizara yangu kwa kushirikiana na Maafisa Ushirika nchini kote kwa sasa wanafanya tathmini kuhusiana na mali zote za Vyama vya Ushirika ili kujua ni zipi ambazo hazitumiki, zipi ambazo zimeingia mikononi mwa watu binafsi kinyume na taratibu, kwa lengo la kuhakikisha kwamba zile ambazo zimechukuliwa kinyemela ziweze kurudi, lakini vilevile ili mali hizo za ushirika ikiwa pamoja na ardhi ziweze kutumika katika mazingira ambayo yanaleta tija zaidi na kwa manufaa ya ushirika na wana ushirika wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile Mheshimiwa Mbunge ameuliza swali la pili kwamba tunafanyaje kurejesha mali ambazo zilichukuliwa kinyume na taratibu. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kwa sasa tokeo Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani, tumechukua hatua kadhaa za kuhakikisha kwamba uovu uliokuwa ukifanyika katika Vyama vya Ushirika hautokei tena. Kwa hiyo, wale wote ambao wamehusika katika kufanya ubadhirifu na upotevu wa mali za ushirika wanachukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile hata viongozi wa Vyama vya Ushirika ambao nao wanakuwa ni sehemu ya ubadhirifu huo tumeendelea kuwachukulia hatua. Ni hivi karibuni tu tumevunja Bodi za Vyama vya Ushirika zaidi ya 200 Mtwara na Lindi. Vilevile mmesikia yaliyotokea Nyanza, jitihada zinaendelea kurudisha mali za Ushirika wa Nyanza. Pia tunajitahidi kuendelea kusaidia vyama vingine ambavyo siku za nyuma kimsingi taratibu zilikiukwa na mali zao kwenda nje kwa watu binafsi bila kufuata utaratibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na maswali haya na jitihada za Serikali, naomba niendelee kuwaomba

Waheshimiwa Wabunge wahamasishe wanaushirika wawaeleze kwamba ushirika ni wa kwao, Serikali yenyewe inasaidia. Kwa hiyo, inatakiwa wenyewe wawajibike kuhakikisha kwamba mali za ushirika zinalindwa na pale kasoro zinavyotokea basi watoe taarifa kwa Serikali ili tuweze kuchukua hatua.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kiteto Koshuma.

**MHE. KITETO Z. KOSHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Naomba nianzie pale ambapo Naibu Waziri wa Kilimo ameishia, kwamba Bodi ya Nyanza *(Nyanza Cooperative Union)* na yenyewe pia imekuwa ikilegalega. Je, ni kwa namna gani Serikali inaweka mikakati ya kuhakikisha wakulima wa pamba Mkoani Mwanza wanafaidika na *Nyanza Cooperative Union* na kushirikishwa katika vikao vinavyoendelea katika Bodi hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, jitihada zinazoendelea kushughulikia changamoto ambazo zimekikumba Chama cha Ushirika wa Nyanza ni kwa ajili ya kuwanufaisha wakulima wa pamba ambapo kimsingi chama kile kilianzishwa kwa ajili ya kuwasaidia. Kwa hiyo, tunavyojaribu kurudisha mali zile ambazo zilichukuliwa kinyume na taratibu, tunaamini baadaye zitaendelea kuwaongezea wakulima wa pamba wanachama wa Nyanza katika kuendeleza zao la pamba. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba maboresho ambayo tunayafanya na ufuatiliaji ambao tunaufanya yote lengo lake kubwa ni kuwasaidia wakulima wa pamba.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mary Muro.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona. Kwa kuwa matatizo yaliyoko sehemu nyingine ya Vyama vya Ushirika ni sawa na tatizo lililoko

kwenye Mkoa wa Pwani kwa *Coastal Region Cooperative Union - CORECU,* majengo yake kutaka kuuzwa na kununuliwa na wajanja wachache. Je, Serikali ina kauli gani juu ya ku-*rescue* hali hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba Chama Kikuu cha Ushirika cha Pwani - *CORECU* kimekuwa kikipita katika wakati mgumu pamoja na mambo mengine kwa sababu ya madeni makubwa ambayo yameendelea kutishia uhai wa chama hicho. Hivi tunapozungumza *CRDB* ambao wamekuwa wakikidai chama hicho fedha nyingi, tayari walishaenda mahakamani na taratibu zilianza za kutaka kuuza mali za *CORECU*. Ni suala ambalo limetokana na mchakato wa kimahakama lakini pamoja na hayo, Serikali na Wizara inaendelea kufanya majadiliano kuangalia namna gani ya kunusuru mali zile zisiuzwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kurejea kusema kwamba naomba Waheshimiwa Wabunge tutoe elimu kwa wanaushirika kwamba wao ndiyo hasa inatakiwa wawe watu wa kwanza kulinda mali za ushirika. Kwa sasabu wanapoingia kwenye mikataba ambayo inahatarisha mali zile, baadaye ni vigumu sana Serikali kusaidia kwa sababu inakuwa ni suala la kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali ilisaidia sana kujaribu kuondoa changamoto ya *CORECU* kwa sababu hata kwenye mkopo ambao wanadaiwa Serikali ilishasaidia kulipa baadhi ya fedha, nafikiri imelipwa zaidi ya shilingi bilioni moja. Hata hivyo, nimueleze Mheshimiwa Mbunge kwamba jitihada zinaendelea kuangalia ni namna gani ya kunusuru mali za *CORECU* zisiuzwe.

**NAIBU SPIKA:** Swali la mwisho Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Zaidi ya nusu ya Vyama vya Ushirika nchini havijafanyiwa ukaguzi kazi ambayo ilipaswa kufanywa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Kutokana na uwezo mdogo wa Tume yetu wa kifedha na watendaji tumeshindwa kufanya hivyo. Serikali ina mkakati gani wa kuiwezesha Tume ya Ushirika iweze kufanya kazi yake kikamilfu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba kumekuwepo na changamoto ya kufanya ukaguzi kwenye Vyama vyote vya Ushirika. Kwa sasa Wizara na Tume ya Ushirika imejipanga kuhakikisha kwamba katika mwaka unaokuja wa fedha Vyama vyote vya Ushirika vinakaguliwa, lakini zaidi kuweka mfumo ambapo utaratibu wa ukaguzi utakuwa unafanyika mara kwa mara bila kukosa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, swali litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

Na. 238

**Kujenga Daraja katika Mto Momba**

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA (K.n.y. MHE. DAVID E. SILINDE)** aliuliza:-

Ili kurahisisha mfumo wa kimaendeleo na kukuza uchumi katika Bonde la Ziwa Rukwa, Serikali iliahidi kujenga daraja linalopita katika Mto Momba kati ya Kata ya Kamsamba (Jimbo la Momba) na Kata ya Kipeta (Jimbo la Kwela) mwaka 2009.

Je, ni lini ahadi hiyo ya Serikali itakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa David Ernest Silinde, Mbunge wa Momba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, daraja la Momba ni kiungo muhimu katika barabara ya Kibaoni - Kasansa - Muze - Ilemba - Kilyamatundu - Kamsamba hadi Mlowo ambayo inaunganisha mikoa mitatu ya Katavi, Rukwa na Songwe. Barabara hii ni kiungo muhimu sana kati ya mikoa hii mitatu ya Katavi, Rukwa na Songwe kwani inapita katika Bonde la Ziwa Rukwa ambalo ni maarufu sana kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo na mifugo. Hali ya barabara ni nzuri kwa wastani ila inapitika kwa shida wakati wa masika katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kufahamu umuhimu huo itaanza ujenzi wa daraja la Momba ambalo ni kiungo muhimu katika barabara hiyo katika mwaka wa fedha 2016/2017. Serikali imetenga shilingi milioni 2,935 kwenye bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 na kwa sasa Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* upo katika hatua za mwisho za kumpata mkandarasi kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika mwaka wa fedha 2017/2018 zimetengwa shilingi milioni 3,000 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa daraja hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Frank Mwakajoka, swali la nyongeza.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini zipo taarifa ambazo si rasmi sana kwamba zabuni ile ya kumpata mkandarasi wa kujenga daraja la Mto Momba zilisitishwa hivi karibuni na kuleta wasiwasi mkubwa sana kwa wananchi wa mikoa ya Songwe, Katavi na Rukwa kwamba daraja lao inawezekana lisijengwe. Leo Waziri anawathibitishia nini wananchi wa mikoa hiyo kwamba daraja hilo litaanza kujengwa lini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Wilaya ya Momba ina kanda mbili, kuna ukanda wa juu na kuna ukanda wa chini na katika Ukanda wa Chini kuna Kata za Msangano, Chitete, Chilulumo, Mkulwe, Kamsamba pamoja na Ivuna. Ukanda wa Juu kuna Kata za Kapele, Miunga Nzoka, Ikana pamoja na Ndalambo na Halmashauri ya Mji wa Tunduma. Barabara za kuingia katika Makao Makuu ya Wilaya mpya hazipitiki kabisa. Ni lini Serikali itahakikisha kwamba inatenga fedha za kujenga barabara ya kutoka Ikana mpaka Chitete na Tunduma kuelekea Chitete?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba katika mwaka huu wa fedha wa 2016/2017 tumetenga shilingi milioni 2,935 na taratibu za kumpata mkandarasi zinazofanywa na *TANROADS* ziko katika hatua za mwisho. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba taratibu hizo mara zitakapokamilika, mkandarasi akipatikana atalipwa fedha hizo kama *advance payment.* Mwaka unaofuata ambao ujenzi utaendelea zimetengwa tena shilingi bilioni tatu kwa ajili ya kuendeleza ujenzi huo, naomba nimhakikishie hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maeneo ya barabara aliyoyataja, hayo majina kwangu ni mageni kidogo lakini kama ana maana ya ile barabara inayounganisha hii mikoa mitatu ambapo sehemu kubwa inapita eneo la Mkoa

wako wa Songwe, nadhani anafahamu na mara nyingi tumekuwa tukijibu hapa kwamba mara tutakapomaliza kujenga hili daraja la Momba tutaingia sasa kwenye suala la ujenzi wa barabara. Kama ana maana ya barabara nyingine, naomba nimkaribishe ofisini tukutane na wataalam tupate ratiba ya nini hasa kitafanyika katika mwaka huu wa fedha na mwaka ujao wa fedha na hatimaye tupate majibu ya suala lake na tuweze kuwaridhisha wananchi anaowawakilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maftaha, swali la nyongeza.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba niulize swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo hili la kutokuwa na mawasiliano katika jimbo hilo la Momba linafanana kabisa na barabara ya ulinzi ambayo inaanzia Mtwara Mjini na kuzunguka Mikoa yote ya Kusini kwamba mvua zilizonyeesha hivi sasa barabara hii haipitiki na hasa katika maeneo ya kijiji cha Kivava na Mahurunga mvua imeweza kukata madaraja na barabara hii hivi sasa haipitiki. Je, Serikali hivi sasa ipo tayari kuharakisha ujenzi wa barabara hii ya ulinzi? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge anafahamu kwamba sasa hivi mkandarasi yuko *site* kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha kutoka Mtwara hadi Mnivata na baada ya hapo tunaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kuendelea kujenga barabara hiyo mpaka Newala na baadaye tunaendelea na ile barabara inayoambaa kwenye Mto Ruvuma ambayo tunasema ni barabara ya ulinzi, nadhani hilo analifahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madaraja yaliyobomoko, bahati nzuri Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa

Mtwara ni kati ya Mamaneja ambao ni wepesi sana na alishatujulisha hayo na tumempa maelekezo ya kufanya huku akiwasiliana na *Road Board* kwa ajili ya kutumia fedha za *emergency* kurekebisha zile barabara zilizokatika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ignas Malocha, swali la nyongeza.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ameeleza katika swali la msingi umuhimu wa ujenzi wa daraja la Mto Momba kwamba ni kiungo muhimu katika kuunganisha mikoa mitatu. Kwa kuwa Sera ya Serikali katika ujenzi wa barabara za lami inazingatia barabara zinazounganisha mikoa. Je, ni lini Serikali itajenga barabara hii muhimu kwa kiwango cha lami inayounganisha mikoa mitatu ya Katavi, Rukwa na Songwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Ignas Malocha kwa kazi kubwa anayoifanya ya kufuatilia ujenzi wa barabara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Malocha amekuja ofisini kwetu mara nyingi na tumeongea sana kuhusu barabara hii na tumemwambia mara tutakapokamilisha ujenzi wa daraja la Momba hatua itakayofuata ni kuhakikisha tunaanza na kazi ya *feasibility study and detail design* kwa ajili ya kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami. Tumeongea hayo ofisini na mimi nimwombe yale ambayo tulikubaliana ofisi tutayatekeleza kwa manufaa ya wananchi wa mikoa hii mitatu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 239

**Kuboresha Huduma katika Stesheni za Treni**

**MHE. HALIMA A. BULEMBO** aliuliza:-

Stesheni nyingi za reli hazina huduma nzuri kama maji, vyoo na sehemu za kukaa wakati wa mvua na hivyo abiria wengi hasa akina mama na watoto kupata shida.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuboresha huduma hizo ili kuwaondolea adha hiyo kubwa akina mama na watoto?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Reli Tanzania *(TRL)* ina jumla ya stesheni 124 katika mtandao wake wa reli. Aidha, kampuni ilishaanza ukarabati wa stesheni za treni ambao pamoja na mambo mengine umezingatia uboreshaji wa mifumo ya maji, vyoo na sehemu za kukaa abiria wakati wa mvua kwa kutumia vyanzo vya ndani ya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, stesheni zilizokwisha kukarabatiwa ni Kigoma, Kaliua, Pugu, Malindi na Mwanza ambapo ukarabati kwa Mwanza bado unaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kampuni inatambua changamoto ya ukosefu wa baadhi ya huduma katika stesheni chache za reli kutokana na kuwa na miundombinu chakavu na hivyo kuweka mpango mkakati wa kukarabati

na kuboresha stesheni hizo kukidhi mahitaji ya sasa hatua kwa hatua kadiri hali ya kifedha itakavyokuwa inaruhusu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima Bulembo, swali la nyongeza.

**MHE. HALIMA A. BULEMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nchi nyingi duniani stesheni za reli ni vituo vya biashara tofauti kabisa na nchini kwetu Tanzania. Serikali inaweza kueleza ni kwa nini stesheni kubwa kama Morogoro, Dodoma, Tabora na Mwanza huduma huwa zimedumaa na hakuna huduma za biashara? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, *TRL* ipo tayali kushirikiana na sekta binafsi kuendesha stesheni za reli kwa kuziboresha ikiwemo kuweka hoteli, huduma za maduka na kadhalika? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Halima Abdallah Bulembo kuuliza kitu ambacho Serikali nayo imekuwa ikijiuliza ni kwa nini wafanyabiashara hawachangamkii fursa za kufanya biashara katika maeneo ya stesheni za reli. Kwa sababu ametupa nguvu zaidi leo, suala hili tutaendelea kulisukuma, *TRL* waangalie uwezekano wa kuwahamasisha wafanyabiashara washirikiane nao kama wataona hili linafaa katika mazingira ambayo wanafanyia biashara hiyo ya reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa reli ya *standard gauge,* hayo yote anayoyaongelea yatakuwemo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Munde Tambwe Abdallah.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa na mimi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sisi wadau wa reli tuna imani kubwa na Wizara lakini tuna imani kubwa na Mkurugunzi wa *TRL,* Bwana Masanja lakini tumekuwa na kero kubwa ya kutokukata tiketi bila kuwa na kitambulisho huku tukijua mazingira ya stesheni za vijiji zilivyo, tukijua watu wetu wanaoishi vijijini walivyo. Mtu akiwa mgonjwa mahuhuti hana kitambulisho anataka kwenda stesheni yenye zahanati anakataliwa kupewa tiketi. Je, Wizara pamoja na Shirika inakubaliana na mimi kufuta hilo sharti la vitambulisho ili mtu aweze kupata tiketi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimia Naibu Spika, ni kweli kuna adha katika suala la uhitaji wa tiketi na tumeliona hilo, lakini kuna ukweli vilevile wapo watu wengi wamekuwa wakitumia fursa hiyo ya kutotumia kitambulisho kurusha tiketi, wanakusanya tiketi nyingi wanakuja kuwauzia watu wengine. Kwa upande wa pili vilevile suala la kiusalama, watu wengi sana ambao siyo Watanzania wamekuwa wakitumia safari zetu za reli na hivyo kuonekana kwamba *TRL* inashiriki katika kusafirisha wasafiri haramu. Kwa hiyo, tutaangalia katika hasara na faida ya suala hilo, kwa sasa naomba atuvumilie tutaendelea kufuata huo utaratibu hadi hapo tutakapoona kwamba changamoto hizi mbili kubwa zitafutiwe namna nyingine ya kuzishughulikia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kitwana Dau.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa fursa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya vituo vya reli yanafanana sana na matatizo ya vituo vya boti vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari - *TPA.* Kituo cha boti cha Nyamisati hakina vyoo, maji na migahawa. Je, ni lini Naibu Waziri ataielekeza Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari - *TPA* wakajenge vyoo, maji, umeme

pamoja na masuala mengine ya kijamii? Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, mlikumbushwa jana kuhusu masharti ya maswali ya nyongeza lakini naona Mheshimiwa Naibu Waziri amesimama hapa wacha alijibu. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nachukulia aliyoyasema ni mapendekezo, tumepokea mapendekezo yake na kwa sababu anajua kile kituo cha Nyamisati hivi sasa ndiyo kinaanza kufanyiwa kazi ya kujengwa basi watakapokuja katika hatua za ujenzi watu wa *TPA* wafikirie vilevile mapendekezo ambayo Mheshimiwa Dau ameyatoa ili yaweze kushughulikiwa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Joseph Kizito Mhagama.

Na. 240

**Kuikarabati Barabara ya Makambako**

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA (K.n.y. MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI)** aliuliza:-

Barabara ya Makambako - Songea yenye urefu wa kilometa 295 imeharibika sana na inahitaji kufanyiwa matengenezo.

Je, ni lini Serikali itakarabati barabara hiyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Jacqueline Ngonyani Msongozi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo la Serikali ni kuifanyia ukarabati kwa kiwango cha lami barabara ya Makambako hadi Songea yenye urefu wa kilometa 295 ili kupunguza gharama na muda wa kusafiri kwa watumiaji wa barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania –*TANROADS,* tayari imekamilisha kazi ya upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni. Lengo la kazi hiyo ni kuikarabati barabara hiyo kwa kiwango cha lami na kazi hii imefanyika kwa kutumia fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya ukarabati kwa kiwango cha lami barabara ya Makambako hadi Songea. Aidha, Wizara kupitia Wakala wa Barabara Tanzania inaendelea kuifanyia matengenezo barabara hii kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara ili iendelee kupitika wakati Serikali inatafuta fedha za kuifanyia ukarabati kamili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mhagama, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MHAGAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa vile barabara hii ya Makambako - Songea uharibifu wake umechangiwa kwa kiwango kikubwa na usafirishaji wa

magari na mizigo mizito kutoka na kuelekea Songea. Ni lini sasa Serikali itajenga reli kutoka Makambako kuelekea Songea kupitia Madaba? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile mizigo mingi pia inatoka Mbeya kuelekea Songea mpaka Mbinga, ni lini sasa Serikali itakamilisha meli ya kutoka Kyela kwenda Mbamba Bay ili mizigo mingi inayopita barabara ya Mbeya kuelekea Songea ipite kwa kutumia meli na kuokoa barabara zetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa Serikali haijafikiria kujenga reli kutoka Makambako kwenda Songea, badala yake inafikiria na kwa sasa inatekeleza upembezi yakinifu na usanifu wa kina wa reli kutoka Mtwara - Songea hadi Mbamba Bay. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu meli, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mhagama, hivi karibuni tu *TPA* wamekamilisha ujenzi wa meli mbili aina ya tishali zinazojiendesha ambazo zitafanya safari za kubeba mizigo kati ya Itungi pamoja na Mbinga. Kwa hiyo, meli hizo zitasaidia sana kupunguza mizigo inayopita katika barabara ya Makambako hadi Songea. Meli hizo zitazinduliwa hivi karibuni zinaitwa *Self Propelled Barges,* ni meli aina ya tishali.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Barabara ya Makambako - Songea imefanana sana na barabara ya Manyovu - Kasulu - Kibondo hadi Kabingo na bahati nzuri barabara hiyo Naibu Waziri ameitembelea. Ni kwa nini sasa barabara hiyo wasiingie kwenye ule mtindo wa kusanifu na kujenga *(design and build)* wakati usanifu unachukua muda mrefu kufika mpaka Kabingo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara anayoongelea ni karibu unakamilika, kwa hiyo, nadhani kubadilisha mfumo kwa sasa haina sababu sana. Mfumo wa jenga sanifu tunapenda kuutumia lakini tunajua gharama yake ni kubwa kidogo ukilinganisha na tukifanya usanifu wenyewe na baadaye tunatoa *tender.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nimuombe tu, tuhakikishe tunakamilisha kazi hii inayokamilika sasa hivi na baada ya hapo tuanze kutenga fedha za kujenga barabara hiyo. Kwa sababu lengo lako ni kuhakikisha barabara hii inajengwa kwa kiwango cha lami na inajengwa haraka iwezekanavyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suzana Mgonokulima, swali la nyongeza.

**MHE. SUZANA C. MGONOKULIMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la barabara la Makambako - Songea yanafanana na matatizo ya barabara inayotoka Mwatasi - Kimara – Idete - Idegenda ambako uzalishaji wa mbao pamoja na matunda aina ya *pears* ni wa kiwango kikubwa sana lakini hali ya barabara hii siyo nzuri. Ni lini Serikali sasa itafanya mpango mkakati kuhakikisha hizi barabara zinatengenezwa kwa kiwango cha lami ili kupelekea usafirishaji wa mbao uwe salama na safi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Songea - Makambako ni *trunk road* wakati barabara anayoongelea ni ya *district.* Ni kweli zinafanana kwa sababu

zote ni barabara lakini zina hadhi mbili tofauti na *district road* zinashughulikiwa na Halmashauri chini ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na hoja yake lakini naomba Watanzania wote tuungane kama watu wamoja, tuweke vipaumbele vya hizi barabara na vile ambavyo tunakubaliana tuanze navyo, tuanze navyo, kwa sababu hatimaye fedha zinahitajika na hatuwezi kujenga barabara zote kwa wakati mmoja, ni lazima tuanze hizi, baadaye tunafuata hizi, hatua kwa hatua. Kwa hiyo, nimuombe avute subira itafika wakati baada ya kukamilisha zile ambazo tumekubaliana ni vipaumbele chini ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2015 - 2020 tutakuja huku ambako Mheshimiwa Mgonokulima anakuongelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zaynabu Vulu, swali la nyongeza.

**MHE. ZAYNABU M. VULU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo la Makambako - Songea halina tofauti na tatizo la barabara ya Kimanzichana – Mkamba, Mkamba – Mkuruwili, Mkuruwili – Msanga hiyo ni kwa Wilaya ya Mkuranga na tatizo la Mpuyani - Mwanarumango, Mwanarumango – Msanga - Vikumbulu na hiyo inatokana na tatizo kubwa la mvua iliyonyesha na kupelekea barabara kukatika hadi kufanya wafanyabiashara ya kusafirisha abiria na magari ya mizigo yanayobeba malighafi kupeleka viwandani kushindwa kufanya safari zake.

Je, Serikali kwa kuwa haina pesa na lengo lake ni kuweka lami kwa barabara hizo, ni lini Serikali itakuwa tayari kuweka changarawe na kukarabati yale maeneo korofi ili kuweza kusaidia jamii ya maeneo hayo waweze kupita kwa usalama? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli lazima nitambue juhudi za Mheshimiwa Zaynabu Vulu katika kufuatilia barabara hizi na hasa hiyo barabara aliyoitaja ambayo inaharibiwa na magari makubwa yanayobeba malighafi zinazokwenda viwandani. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Vulu, kama ambavyo tumekuwa tukimhakikishia mimi na Waziri wangu wakati anafuatilia masuala hayo Ofisini kwetu mbele ya wataalam vilevile, aendelee kufanya kwa namna anavyofanya ili hatimaye yeye na sisi tufike hapo tunapotaka kufika. Tunajua katika barabara hii moja aliyoitaja ni ile barabara niliyosema ni kipaumbele namba mbili cha kuhamasisha viwanda au cha kuwezesha viwanda. Nikumhakikishie tuna nia thabiti na wakati wowote tutakapopata fedha tutahakikisha barabara hizi zinajengwa kwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama alivyosema kwa sasa tumeshatoa maelekezo kwa Mameneja wote wa Mikoa wa *TANROADS*, barabara zote zilizokatika zirudishiwe kwa kutumia fedha za *emergence.* Washirikiane *TANROADS* pamoja na Mfuko wa Barabara kuhakikisha wanarudisha mawasiliono katika maeneo yote ambayo mawasiliano yamekatika. Maelezo hayo tumeyatoa na nina hakika Meneja wetu wa Mkoa wa Pwani atahakikisha maeneo hayo anayoyataja Mheshimiwa Mbunge ambayo barabara zimekatika mawasiliano yanarudi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rashid Shangazi, swali fupi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kuniona.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tatizo lililopo kwenye barabara ya Makambako – Songea linafanana kabisa na tatizo lililopo Mombo – Soni - Lushoto kilometa 36 na juzi baada ya zile mvua kubwa imesababisha uharibifu mkubwa wa barabara ile. Je, ni lini sasa Serikali itaifanyia ukarabati mkubwa barabara hii ya Mombo – Soni - Lushoto kilometa 36?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu kwa kifupi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rashid Shangazi kwa sababu yeye alikuwa wa kwanza kunijulisha matatizo yaliyotokea katika barabara hii anayoongelea kabla hata ya wataalam wangu hawajaniambia. Nadhani sasa anafahamu kwamba barabara hiyo imeanza kupitika kwa sababu kazi imefanyika ya kurudisha mawasiliano na kutengeneza pale ambapo mawe yaliteremka na kuziba barabara. Tunashukuru barabara hiyo sasa inaanza kupitika baada ya matengenezo kukamilika na tutaendelea kuifanyia marekebisho pale ambapo tutaona panahitajika. Nakushukuru sana Mheshimiwa Shangazi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, Mbunge wa Ngara, sasa aulize swali lake.

Na. 241

**Maporomoko ya Maji ya Rusumo**

**MHE. ALEX R. GASHAZA** aliuliza:-

Maporomoko ya maji ya Rusumo yanapatikana katika Jimbo la Ngara nchini Tanzania na Wilaya ya Kirehe nchini Rwanda kwenye mpaka wa Tanzania na Rwanda na maporomoko haya yanaweza kuwa kivutio kizuri cha kitalii.

Je, Serikali iko tayari kufanya utafiti katika eneo hili ili liweze kurasimishwa kwa ajili ya shughuli za kitalii ili kuongeza pato la Wilaya na Taifa kupitia sekta hiyo ya utalii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Alex Raphael Gashaza, Mbunge wa Ngara, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa maporomoko ya maji ya Rusumo yaliyopo Wilayani Ngara, Mkoa wa Kagera, yana uwezo wa kuwa kivutio kizuri cha utalii katika Kanda ya Ziwa Victoria. Wizara iliwahi kutembelea eneo hilo na kushauri kuwa linaweza kutembelewa kama kivutio. Maeneo mengine yanayoweza kujumuishwa katika maporomoko hayo kama kivutio ni maeneo ya hifadhi za Burigi na Kimisi, Bioanuwai ya pekee katika katika misitu ya asili ya Minziro, mapango ya watumwa katika Kata ya Kenza na maporomoko ya maji katika Msitu wa Rubare pamoja na maji ya moto katika Msitu wa Mutagata.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iko tayari kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Ngara kufanya utafiti unaoweza kuendeleza na kurasimisha maporomoko hayo na mandhari yake kuwa kivutio cha utalii kitakachoongeza pato la Wilaya na Taifa kwa ujumla.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Alex Gashaza, swali la nyongeza.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na ambayo yanatia matumaini. Naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, kwa kutambua kwamba kuna vivutio hivyo katika Jimbo la Ngara, kama maporomoko hayo, lakini bado hifadhi hizo za Burigi na Kimisi na bado kuna vivutio vingine kama pango lililokuwa linasafirisha watumwa kutoka Burundi kupitia Tanzania, pango la Kenza Kazingati, kuna mlima mrefu kuliko milima yote Mkoa wa Kagera, kuna mito miwili ambayo unaweza ukafanya *boat riding* na ili vivutio hivi kufanya kazi

na kupata watalii ni lazima kuboresha miundombinu ya barabara na viwanja vya ndege, sasa tuna uwanja wa ndege wa Luganzo. Je, Wizara iko tayari kuboresha uwanja huu wa ndege wa Luganzo ambao unaweza ukasaidia kuleta watalii na wakafanya utalii katika eneo hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Ngara ilitegemea kupata gawio la asilimia 25 kutokana na utalii wa uwindaji katika Hifadhi za Burigi na Kimisi. Hata hivyo, takribani miaka 30 iliyopita tangu Hifadhi ya Burigi imeanzishwa na miaka takribani 12 tangu Hifadhi ya Kimisi imeanzishwa ni mwaka jana tu ambapo tumeweza kupata gawio la shilingi milioni 7, gawio ambalo ni dogo. Sasa nahitaji nipate ufafanuzi kwamba shilingi milioni 7 hizi zilitokana na mapato ya kiasi gani na ni wanyama kiasi gani waliowindwa katika hifadhi hizi mbili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, swali la mwisho linataka takwimu, nadhani kwa mujibu wa Kanuni zetu unaweza kuliacha, unaweza ukampa hizo takwimu hapo baadaye, kwa hiyo, jibu hayo maswali mengine.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Gashaza kwa ufuatiliaji wake wa karibu na mawazo mazuri katika kuendeleza na kuboresha maeneo haya kama maeneo yanayovutia watalii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuna uwanja wa ndege ambao umekuwa unatumiwa na wawindaji katika eneo lile ambao urefu wake ni mita 1,700. Tutatuma wataalam wetu wanaoshughulika na masuala ya uwindaji ili washirikiane na *TAA* katika kuboresha uwanja huu ili kuhakikisha kwamba vivutio hivi vinaweza kufikiwa kwa urahisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la uwindaji, Wizara yangu itafuatilia zaidi malipo ambayo yamefanywa ili kuona ni namna gani tunaweza kuboresha ushirikiano kati

ya wawindaji, Wizara na wananchi wa Ngara, ili kuboresha hali ya uwindaji katika eneo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Devota Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 242

**Mfuko wa Kutambua Kazi za Tasnia ya Habari**

**MHE. DEVOTHA M. MINJA** aliuliza:-

Waandishi wa Habari wanafanya kazi nzuri katika kuelimisha jamii.

Je, ni lini Serikali itaanzisha mfumo utakaotambua kazi zinazofanywa na tasnia ya habari?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kujibu swali hili, naomba uniruhusu nianze kwa kuipongeza timu yetu ya vijana ya Serengeti kwa ushindi wa mabao mbili kwa moja dhidi ya Angola jana nchini Gabon. *(Makofi)*

Vilevile nichukue nafasi hii kuwapongeza Watanzania wote kwa kushikamana na kushirikiana pamoja kuichangia na kuishangilia pamoja na kuitakia kheri timu yetu hii ya vijana ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huu mfupi, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Minja, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua na kuthamini kazi zinazofanywa na vyombo vya habari nchini. Mchango wa tasnia ya habari ni mkubwa katika kuhabarisha, kuelimisha na kuburudisha jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua mchango huo, Serikali imeruhusu uwepo wa vyombo vya habari vya umma na sekta binafsi, yakiwemo makampuni binafsi, mashirika ya kidini na kijamii. Aidha, mchango wa vyombo vya habari unatokana na sera, sheria, mipango na taratibu zilizowekwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo unaotambua kazi za tasnia ya habari nchini upo tayari. Katika kudhihirisha hilo, Serikali ilitunga Sera ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003, Sheria ya Magazeti ya mwaka 1976 na sasa ina Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 na Kanuni zake za mwaka 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ya kuwezesha wanahabari kufanya kazi zao kwa weledi na kwa kuzingatia kanuni, sheria na taratibu ili kulinda amani na utulivu katika nchi yetu. Wizara yangu kwa sasa inaainisha mahitaji ya wataalamu katika tasnia ya habari ili kushirikiana na wadau wa ndani na nje tuweze kuwapatia mafunzo kwa lengo la kuboresha kazi zao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Devotha Minja, swali la nyongeza.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa kuwa Sheria ya Huduma za Habari ya mwaka 2016 inaitaja kazi ya uandishi wa habari kuwa ni jukumu la kisheria. Serikali inawachukulia hatua gani watu wanaowazuia waandishi wa habari kutekeleza majukumu yao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa hivi karibuni kumekuwa na matukio kadhaa ya waandishi wa habari kuzuiwa kufanya kazi zao kama vile *RC* kuvamia kituo

cha *Clouds*, baadhi ya waandishi kuvamiwa wakiwa kwenye mkutano wa CUF, baadhi ya Wakuu wa Wilaya kuwakamata waandishi wa habari na kuwaweka ndani na hata jana kule Arusha katika Shule ya Msingi ya Lucky Vincent waandishi wa habari kumi walikamatwa wakiwa wanatimiza majukumu yao. Ni lini Serikali itaacha tabia hii mbaya ya kuwakamata kamata waandishi wa habari wakiwa kwenye majukumu yao? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, WASANII NA MICHEZO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana kwa maswali yake na kwa kutambua kwamba Sheria ya Vyombo vya Habari ya mwaka 2016 inahimiza kwamba kazi ya waandishi wa habari ni jukumu la kisheria, nadhani sote tunakubaliana na hilo. Hata hivyo, anaposema kwamba kuna watu wanaozuiwa kufanya kazi zao, mimi naamini kwamba kama kweli waandishi wa habari wanafuata maadili na wanatafuta habari kwa ajili ya kujenga na siyo kuvuruga nchi, siamini kabisa kwamba kuna watu wanaoweza kuwazuia.

Sera yetu ya Habari na Utangazaji ya mwaka 2003 inahimiza kwamba taasisi zote za Serikali na wadau wote wa habari kutoa taarifa kwa wanahabari na inahimiza kabisa kwamba wale Maafisa Habari katika Mikoa na Halmashauri wawe tayari kutoa ushirikiano kwa wanahabari ili kusudi wanahabari waweze kutekeleza majukumu yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama kuna hili la watu wanaozuia, mimi naomba baadaye tuonane na Mheshimiwa Devotha Minja aweze kuniambia ni wapi kwa sababu ndiyo kwanza nasikia hilo. Sera yetu inahimiza kwamba ni wajibu kwa Maafisa wa Habari kuwapa ushirikiano wanahabari kwa sababu jukumu lao linatambulika kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swali la pili Mheshimiwa Waziri alilitolea ufafanuzi vizuri sana wakati

anahitimisha hotuba yake hapa Bungeni. Kwa hiyo, naomba nisirudie tena maneno ambayo aliyasema Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutamalizia swali letu la mwisho la Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimwa Ussi Salum Pondeza, Mbunge wa Chumbuni, sasa aulize swali lake.

Na. 243

**Tatizo la chakula kwa Mahabusu Zanzibar**

**MHE. USSI SALUM PONDEZA** aliuliza:-

Askari Polisi Zanzibar kwa muda mrefu wamekuwa wakilazimika kutumia fedha zao za mfukoni kuwahudumia chakula mahabusu wanoshikiliwa katika Vituo vya Polisi Unguja wakati jukumu hilo ni la Serikali.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani za kuondoa tatizo hilo tangu kulalamikiwa na Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora baada ya kufanya ziara ya ukaguzi na kugundua tatizo hilo?

(b) Je, ni sababu gani zimepelekea chakula kutopelekwa katika Vituo vya Polisi wakati Bunge limekuwa likiridhia matumizi ya Wizara kila mwaka zikiwemo gharama za chakula kwa mahabusu?

(c) Je, haki za binadamu zinazingatiwa vipi inapotokea askari hawana fedha za kununua chakula cha mahabusu na kulazimika kulala na njaa wakati Serikali ndiyo yenye jukumu la kuwapatia huduma ya chakula?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ussi Pondeza, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, mahabusu wanaoshikiliwa katika Vituo ya Polisi huhudumiwa na Jeshi la Polisi kwa kuwapatia mahitaji muhimu kama chakula na malazi. Serikali kupitia Jeshi la Polisi imekuwa ikitenga bajeti kwa ajili ya chakula cha mahabusu kwa kila mwaka.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, si kweli kwamba chakula huwa hakipelekwi katika mahabusu za polisi. Chakula hupelekwa kulingana na idadi ya mahabusu kama ambavyo taratibu za utoaji wa chakula zinavyoelekeza katika *PGO* 356.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, kulisha mahabusu walioko katika Vituo ya Polisi ni jukumu la Serikali na si askari mmoja mmoja kutumia fedha zake za mfukoni kwa kufanya jukumu hilo. Serikali itaendelea kutimiza wajibu huo na hakuna uvunjaji wa haki za binadamu katika kuwapatia huduma za chakula mahabusu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimwa Ussi Pondeza, swali la nyongeza.

**MHE. USSI SALUM PONDEZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri japo hayakidhi ukweli halisi wa mahabusu.

Je, Waziri yuko tayari apewe ushahidi wa raia ambao wanawapelekea chakula raia ambao wanakuwa mahabusu Zanzibar? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusu haki za binadamu, kila mara kumekuwa na taarifa ya Tume ya Haki za Binadamu juu ya ukosefu wa hali ya amani katika vyuo vya mafunzo Zanzibar. Je, Serikali imeshatolea ufafanuzi kuhusu chombo hicho? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa ufuatiliaji wake lakini niseme tu kitu kimoja amekichanganya kwamba, sijakataa watu kupeleka chakula kwa mahabusu na hiyo ni *hospitality* ya Kitanzania. Mtu kama ana mtu wake yuko mahabusu akaamua kumpelekea chakula, Magereza ama Polisi hawazuii ndugu kuwapelekea ndugu zao chakula wanapokuwa wako mahabusu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, ndugu zao kuwapelekea chakula mahabusu haimaanishi kwamba Serikali haikupeleka chakula. Wakati mwingine hata mahabusu wenyewe wanakuwa na chaguo lao la chakula anachokula, wengine wana *diet* zao wanazotaka kula, kwa maana hiyo haingekuwa vyema sana kwa Serikali kusema lazima mtu akiwa mahabusu ale chakula cha Serikali na nadhani hata ninyi msingekubaliana na utaratibu wa aina hiyo. Sisi tunachosisitiza ni kwamba Serikali inaweka bajeti na huo ndiyo umekuwa utaratibu lakini haizuii watu kupelekewa chakula kufuatana na mahitaji yao ama ndugu wanapokuwa wamepeleka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu lile la pili la uvunjifu wa amani, tumelisisitiza na tumeendelea kulisisitiza kwamba vyombo vya dola vinafanya kazi kwa mujibu wa sheria na inapotokea kesi moja moja tunazishughulikia kama kesi moja moja na hatua huchukuliwa inapotokea makosa yamejitokeza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimwa Wabunge, muda wetu umekwisha sana hata ule wa kwangu mwenyewe pia umekwisha.

Waheshimwa Wabunge, nitaleta matangazo yaliyotufikia mezani leo, tunao wageni mbalimbali. Kundi la kwanza la wageni ni wageni wa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba kutoka Wizara ya

Kilimo, Mifugo na Uvuvi, wakiongozwa na Dkt. Yohana Budeba ambaye ni Katibu Mkuu (Sekta ya Uvuvi); yupo pia Dkt. Maria Mashingo ambaye ni Katibu Mkuu (Sekta ya Mifugo); yupo pia Mhandisi Mathew Mtigumwe ambaye ni Katibu Mkuu (Sekta ya Kilimo); tunaye pia Balozi Fred Kafeero ambaye ni Mwakilishi Mkaazi *FAO*; tunaye pia Ndugu Mathayo Mathew ambaye ni Afisa Mipango kutoka Umoja wa Ulaya *(EU)* na yupo pia Ndugu Mohamed Muya ambaye ni Katibu Mkuu Mstaafu. *(Makofi)*

Waheshimwa Wabunge, pia wapo Wenyeviti watatu wa Bodi na Taasisi na Mashirika yaliyo chini ya Wizara hiyo na wageni wengine mbalimbali ambao ni Wakurugenzi, Wakuu wa Idara, Taasisi, Vitengo na Maafisa mbalimbali waliopo chini ya Wizara hiyo. Karibuni sana wageni wetu. *(Makofi)*

Waheshimwa Wabunge, tunao pia wageni wa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa William Tate Olenasha ambao ni wapiga kura wake kutoka Jimboni kwake Ngorongoro, Mkoa wa Arusha wakiongozwa na Mheshimiwa Yanick Ndoinyo ambaye ni Diwani Kata ya Ololosokwan, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimwa Wabunge, tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge ambao wapo Bungeni pamoja na sisi. Pia tunao wanafunzi ambao wamekuja kwa ajili ya mafunzo. Karibuni sana wageni wetu, tunaamini kwamba waliokuja kujifunza wataweza kujifunza namna yetu ya ufanyaji kazi.

Waheshimwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club,* Mheshimiwa William Mganga Ngeleja, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kuwa kesho Jumamosi tarehe 20 Mei, 2017 kwenye Uwanja wa Jamhuri kutakuwa na michezo ya kirafiki ya mpira wa miguu yaani *football* na mpira wa pete yaani *netball* kati ya *Bunge Sports Club* na *NSSF,* saa kumi jioni. Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote wa Dodoma mnakaribishwa. *(Makofi)*

Waheshimwa Wabunge, tangazo lingine linatoka kwa Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Rais, Mheshimiwa Januari Makamba anawatangazia kuwa leo tarehe 19/5/2017, Mheshimiwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama Samia Suluhu Hassan atapokea taarifa kutoka timu aliyoiunda kufuatilia uchafuzi wa mazingira katika Mto Ruaha. Hivyo, Mheshimiwa Waziri anawaomba Wabunge wote marafiki wa mazingira kuhudhuria hafla hii itakayoanza saa 8.00 kamili mchana eneo la *Treasury Square.* Kwa hiyo, Mheshimiwa Makamu wa Rais atakuwepo hapo kupokea taarifa hii, Waheshimiwa wabunge mnakaribishwa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, hii asubuhi Wabunge wachache wametoa pongezi kwa timu yetu ya *Serengeti Boys,* lakini kwa sababu jana pengine wakati tukitoa hizo pongezi wengine hawakuwepo, Kanuni yetu ya 154 pongezi ziliishatolewa jana na Kiti kwa hivyo niwakumbushe tu maana leo michango itaendelea na tunaweza kujikuta kila mmojawetu anataka kutoa pongezi. Sasa Kanuni ya 154, pole ama pongezi zikishatolewa na Kiti zinakuwa zimetolewa kwa niaba yetu sote.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tutaendelea na ratiba iliyopo mbele yetu.

**MWONGOZO WA SPIKA**

**WABUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimwa Wabunge, kuna Waheshimiwa Wabunge wamesimama hapa kuhusu miongozo na mimi kama nilivyoahidi sitachoka kuwakumbusha tuzingatie masharti ya Kanuni ya 68(7), uwe unauliza swali kama jambo lililofanyika hapa linaruhusiwa ama haliruhusiwi na liwe limefanyika leo. Mheshimiwa Devotha Minja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasimama kwa Kanuni ya 68(7) na Kanuni ya 46 na kwa ajili ya muda sitazisoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nikiuliza swali langu la msingi leo kwenye swali la nyongeza, swali la pili ambapo nilitaka kupata ufafanuzi juu ya waandishi wa habari kumi ambao jana wamekamatwa na Jeshi la Polisi kule Mkoani Arusha katika shule ya Lucky Vincent ambao waliambatana na Meya wa Jiji la Arusha wakitoa misaada katika shule ile. Nilitaka kujua kauli ya Serikali ni nini juu ya kamatakamata hizi za waandishi wa habari wakiwa katika majukumu yao ya msingi lakini swali langu hili halikujibiwa, sikujua Naibu Waziri kwamba amelipotezea au hana majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nimesimama kwa Kanuni ya 68(7) na jambo ambalo limetokea mapema hapa Bungeni ni hili lifuatalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na tabia ya kukaribisha wageni mbalimbali hapa Bungeni na wachache huwa wanatajwa kwamba huyu ni mgeni wa fulani fulani fulani lakini kuna kitu mimi kinanipa taabu kidogo, wanapokuja wanafunzi hata jina la shule au chuo wanachotoka halitajwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba mwongozo wako kwa sababu wakati mwingine naona kwa maoni yangu kama hatuwatendei haki kwa sababu tunaona tu *uniform* na nini lakini hatujui wanatokea wapi. Kwa hiyo, ingekuwa ni bora watajwe na sehemu wanazotoka.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa mwongozo na Mheshimiwa Devotha Minja lakini pia Mheshimiwa Mussa Mbarouk. Mheshimiwa Devotha Minja ameomba mwongozo kuhusu majibu yaliyotolewa hapa Bungeni na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,

Sanaa na Michezo kuhusu swali lake la nyongeza ambalo kwa maelezo aliyoyatoa swali la nyongeza lilikuwa linahusu kamatakamata ya waandishi wa habari.

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 68(7) aliyosema anasimama kwa kutumia Kanuni hiyo Mheshimiwa Devotha Minja pia ameitaja Kanuni ya 46 inayotaka maswali yajibiwe kikamilifu. Kwa kuwa swali la nyongeza alilokuwa ameliuliza Mheshimiwa Devotha Minja na majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Waziri ni lazima niyapitie kwenye Taarifa za Bunge, nitaangalia swali lake la msingi, swali lake la nyongeza na majibu yaliyotolewa na nitatoa mwongozo huo baadaye kama Kanuni yetu inavyosema. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kuhusu mwongozo ulioombwa na Mheshimiwa Mussa Mbarouk kuhusu wageni Bungeni na kwamba wengine wanatambulishwa wengine hawatambulishwi na wakati mwingine wageni wanaokuja hapa kujifunza kama wanafunzi hawapati fursa hata ya kujulikana shule wanayotoka. Kanuni zetu kuanzia ya 139-142, Kanuni ya 142 inahusu utambulisho wa wageni na kwa sababu pengine tumesahau kidogo lakini wakati wa kikao cha Wabunge wote kabla ya Bunge kuanza katika Maelezo ya Spika alitoa maelekezo namna ambavyo utambulisho wa wageni utakuwa ndani ya Bunge hili. Sasa kwa sababu wakati mwingine si wote tunakuwepo kwenye kikao hicho niwakumbushe tu Kanuni ya 142 inatutajia pale utambulisho wa wageni, inasema:-

*"(1) Spika anaweza kuwatambulisha wageni wote wa kitaifa na kimataifa waliomo katika ukumbi wa Bunge.*

*(2) Spika vilevile anaweza kuwatambulisha wageni wengine waliomo katika Ukumbi wa Bunge ambao:-*
*(a) wanahusika moja kwa moja na shughuli za Majimbo;*
*(b) wanatembelea Bunge kwa ajili ya ziara za mafunzo; na*
*(c) wametoa mchango wa kitaifa unaohitaji kuenziwa."*

Waheshimiwa Wabunge, Kanuni ya 142 inasema, 'Spika anaweza.'

Kwa hiyo, matangazo yanapokuja hapa wageni wanaosomwa ni wale ambao yeye Spika kwa hekima yake ameona hao ndiyo wasomwe. Kwa hiyo, wale ambao ameona wasomwe kwa ujumla watasomwa kwa ujumla kwa sababu Kanuni yetu ya 142 inampa mamlaka hayo na alitoa maelekezo siku ya kikao cha Wabunge wote. Kwa hiyo, wageni wanaokuja hata wasipotajwa wasijisikie vibaya wao ni wageni wa Bunge ni sehemu ya nchi hii, wanaweza kuja muda wowote kufuatilia Bunge linaendaje lakini si lazima kila mmoja wao atangazwe kwa mujibu wa Kanuni yetu ya 142.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, tunaendelea, Katibu.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Kiti cha Spika.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Kiti cha Spika, tafadhali.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa miongozo sasa umeshapita, kwa hiyo tunaendelea.

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nilisimama.

**NAIBU SPIKA:** Jirani yako hapo aliposimama nilimtaja akakaa sikuona mtu mwingine amesimama mpaka nikapepesa nikamwangalia hata yule aliyekuwa amesimama mwanzo hakusimama tena. Waheshimiwa Wabunge, tuzielewe vizuri hizi Kanuni, ukitaka Kiti kikuone, aidha, usimame ama uandike. Kama Mbunge mwingine hakuna anayesema na wewe hukusimama, siwezi tena kutoa hiyo nafasi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, tunaendelea, Katibu.

**NDG. THEONEST RUHILABAKE - KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

## Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**WAZIRI WA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, inayohusu Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, sasa lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo tukiwa wa afya njema ili tuweze kujadili Bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania. Napenda pia kumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Kilimo Mifugo na Uvuvi. Napenda kutumia fursa hii kumuahidi Mheshimiwa Rais, viongozi wangu wengine, Waheshimiwa Wabunge, wakulima, wafugaji, wavuvi na Watanzania kwa ujumla kwamba nitatumia uwezo wangu wote kwa uaminifu na uadilifu kuhakikisha kuwa sekta za kilimo, mifugo na uvuvi zinachangia kikamilifu katika kuinua pato la mkulima, mfugaji na mvuvi na kuipeleka Tanzania kwenye uchumi wa kipato cha kati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuhimiza utunzaji wa mazingira ambayo ni muhimu katika maendeleo ya Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Waheshimiwa Wabunge na leo mmekaribishwa kwenda kushuhudia kupokea ripoti ya

namna gani mazingira yetu katika Mto Ruaha Mkuu yanaweza kutunzwa. Na mimi na wenzangu katika Wizara tunaomba kumuahidi kuwa katika shughuli zetu za kilimo, mifugo na uvuvi tutahakikisha utunzaji wa mazingira unakuwa ndiyo kipaumbele ili kuwa na kilimo endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia kutumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Majaliwa Kassim Majaliwa, Mbunge wa Ruangwa kwa kuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha viongozi kuwajibika katika kuwatumikia wananchi kwa kuhakikisha wanatatua migogoro ya ardhi kati ya Wakulima na Wafugaji. Aidha, Mheshimiwa Waziri Mkuu amekuwa mstari wa mbele kutembelea Bodi za Mazao, kampuni ya ranchi za Taifa na kutoa maelekezo kwa ajili ya kuleta ufanisi wa kuimarisha utendaji katika Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze pia Mheshimiwa Spika na wewe binafsi Mheshimiwa Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge na Kamati nzima ya Uongozi ya Bunge kwa kuliongoza vizuri Bunge letu Tukufu la Kumi na Moja. Ni imani yangu kuwa mtaendelea kuliongoza Bunge kwa hekima, weledi mkubwa na kwa kuzingatia sheria, kanuni, na taratibu ili Bunge letu liweze kuisimamia na kuishauri Serikali ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji chini ya Uenyekiti wa Mheshimiwa Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang, kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina Taarifa ya Utekelezaji ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ya Mwaka 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2017/2018 katika Kikao kilichofanyika Dodoma tarehe 29 na 30 mwezi Machi mwaka huu. Bajeti hii imezingatia maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo. Napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wa kuchaguliwa na kuteuliwa wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naahidi kushirikiana nanyi katika kuiletea nchi yetu maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza na kuwashukuru wananchi wa Jimbo langu la Buchosa kwa kunichagua na kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha na kuwahakikishiwa maendeleo yao. Aidha, nawapongeza kwa juhudi wanazofanya katika kujiletea maendeleo. Napenda pia kutumia nafasi hii kuishukuru familia yangu hasa mke wangu mpenzi Furaha Tizeba kwa msaada wake, uvumilivu na kunitia nguvu, mambo ambayo yananiwezesha kutekeleza majukumu yangu bila kutetereka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine nitumie fursa hii kumpongeza Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, kwa hotuba yake ambayo imeelezea kwa muhtasari hali ya kilimo, mifugo na uvuvi ilivyo hivi sasa na mwelekeo kwa mwaka ujao. Aidha, nampongeza pia Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa Mheshimiwa George Boniface Simbachawene na Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Isdory Mpango kwa hotuba zao zilizofafanua hali ya uchumi kwa mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako naomba nitumie fursa hii pia kuwapa pole wananchi wote na wana-CCM wa wilaya yetu ya Serengeti kwa kumpoteza Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake Tanzania (UWT) wa Wilaya yetu ya Sengerema ambaye pia ni Mama Mkubwa wa Mheshimiwa Mbunge mwenzetu Dada yangu Rosalia Kemirembe. Nimpe pole, Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi mama yetu huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba hotuba yote ichukuliwe kuwa kumbukumbu sahihi za Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya kilimo; Tanzania imeendelea kutegemea sekta ya kilimo katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi wake kwa kuwa sekta hii inatoa ajira kwa asilimia 65.5 ya Watanzania na inachangia zaidi ya asilimia 100 ya chakula kinachopatikana nchini

kwenye miaka yenye mvua za kutosha. Katika mwaka 2016 Sekta ya Kilimo ilichangia asilimia 29.1 ya pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 29.0 mwaka uliotangulia. Mchango mkubwa katika pato la Taifa ulitokana na sekta ya kilimo, ikifuatiwa na Sekta nyingine za kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kasi ya ukuaji wa sekta ya kilimo kwa mwaka 2016 imepungua ukilinganisha na mwaka 2015. Ukuaji kwa shughuli za kiuchumi za kilimo zinazojumuisha mazao, ufugaji, misitu na uvuvi ni asilimia 2.1 ukilinganisha na asilimia 2.3 ya mwaka 2015. Katika mwaka 2016 mchango wa mazao ni asilimia 1.4, mifugo asilimia 2.6, misitu asilimia 3.4 na uvuvi asilimia 4.2, ikilinganishwa na mazao asilimia 2.2, mifugo asilimia 2.4, mifugo 2.6 na uvuvi asilimia 2.5 vya mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa mazao ya chakula katika mwaka 2016 ulikuwa tani 16000.2 ikiwa ni ongezeko la tani milioni 0.7 yaani tani laki saba wastani wa asilimia 4.5 ikilinganishwa na tani milioni 15.5 za mwaka 2015. Uzalishaji wa mazao ya nafaka umeongezeka kutoka tani milioni 8.9 mwaka 2015 hadi tani milioni 9.5 mwaka 2016 ikiwa ni ongezeko asilimia 6.7. Aidha, uzalishaji wa mahindi umeongezeka kutoka tani milioni 5.9 mwaka 2015 hadi tani milioni 6.1 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 3.4. Uzalishaji wa mchele uliongezeka kutoka tani milioni 1.9 mwaka 2015 hadi tani milioni 2.2 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 15.8. Vilevile uzalishaji wa mazao ya chakula yasiyo nafaka umeongezeka kufikia tani milioni 6.7 ikilinganishwa na tani milioni 6.6 kwa mwaka 2015 ikiwa ni ongezeko la asilimia 1.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa mazao ya biashara. Katika msimu wa mwaka 2016/2017 uzalishaji wa mazao makuu ya asili ya biashara uliongezeka kufikia tani 881,583 ikilinganishwa na tani 796,502 mwaka uliotangulia.

Aidha, uzalishaji wa mazao ya bustani umeongezeka kutoka tani milioni 5.9 mwaka 2015/2016 hadi tani milioni 6.2 mwaka 2016/2017. Uzalishaji wa mbegu za mafuta

uliongezeka kutoka tani milioni 6.3 mwaka 2015/2016 hadi tani milioni 6.6 mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa mazao ya chakula 2015/2016 na upatikanaji wa chakula katika mwaka 2016/2017; tathmini ya awali ya hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa 2015/2016 na upatikanaji wa chakula 2016/2017 iliyofanyika mwezi Julai mwaka jana ilibainisha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula ungefikia tani milioni 16.1 za chakula na mahitaji ya chakula kwa mwaka 2016/2017 ingekuwa tani milioni 13.1 na hivyo nchi kuwa na ziada ya tani milioni 3. Aidha, tathmini ya kina ya hali ya chakula na lishe iliyofanyika mwezi Februari, 2017 ilibainisha pia kuwa hali ya upatikanaji wa chakula bado ilikuwa ni ya kuridhisha pamoja na kuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula hapa nchini uliochangiwa na kuchelewa kunyesha kwa mvua za vuli na msimu pamoja na ukame uliojitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kukabiliana na hali ya ukame uliojitokeza katika baadhi ya maeneo yakiwamo ya Halmashauri zilizobainishwa kuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula, jumla ya tani 1,969 za mbegu bora za mahindi na mtama zinazokomaa kwa muda mfupi na kustahimili ukame zilihitajika. Hadi mwezi Machi, 2017 Wizara kupitia Wakala wa Mbegu za Kilimo, makampuni binafsi na Mawakala wa Pembejeo walisambaza tani 377.4 za mbegu za mahindi, tani 100 za mtama na tani 20 za mpunga katika maeneo hayo. Vilevile Wizara kupitia Vituo vya Utafiti vya Kanda ilisambaza jumla ya vipando 14,252,000 zikiwemo pingili 12,772,000 za muhogo na 1,480,000 za viazi vitamu.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ulipanga kununua jumla ya tani 100,000 za chakula. Hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2017 Wakala ulinunua jumla ya tani 62,099 za mahindi sawa na asilimia 62 ya lengo ililojiwekea. Aidha, akiba ya chakula hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2017 ni tani 86,443.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya mifugo; katika

mwaka 2016/2017, idadi ya mifugo nchini inafikia ng'ombe milioni 28.44, mbuzi milioni 16.67 na kondoo milioni 5.01 (Kiambatisho Na. 1 kwenye kitabu chetu). Pia wapo kuku wa asili milioni 37.43, kuku wa kisasa takriban milioni 34, nguruwe milioni 1.8 na punda wapatao 572,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwango vya ulaji wa mazao ya mifugo nchini bado viko chini. Kwa mfano, ulaji wa nyama ni wastani wa kilo 15 kwa Mtanzania kwa mwaka, lita 47 za maziwa na mayai 106 kwa mtu kwa mwaka ukilinganisha na viwango vilivyowekwa na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa *(FAO)* mwaka 2011 ambavyo ni kilo 50 za nyama, lita 200 za maziwa na mayai 300 kwa mtu kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017, uzalishaji wa maziwa umepungua kwa asilimia 2.3 kutoka lita bilioni 2.14 mwaka 2015/2016 hadi bilioni 2.09. Kupungua kwa kiwango cha uzalishaji kumetokana na upungufu wa malisho katika maeneo mengi ya nchi kulikosababishwa na ukame wa muda mrefu. Hali hii imeendelea kuathiri viwanda vya kusindika maziwa hivyo kushusha uzalishaji wake. Sambamba na hali hiyo, kiwango cha usindikaji kimepungua kutoka lita milioni 61.1 kwenye viwanda 75 vilivyopomwaka 2015/2016 kufikia lita milioni 40.13 kwenye viwanda 65 vinavyofanya kazi katika kipindi cha mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017, uzalishaji wa nyama pia umepungua kutoka tani 648,810 mwaka 2015/2016 hadi tani 558,164. Aidha, mfumo wa unenepeshaji mifugo umeendelea kuhamasishwa ambapo ng'ombe walionenepeshwa kwenye mashamba na wafugaji waliosajiliwa wameongezeka kwa asilimia 12.9 kutoka ng'ombe 221,390 mwaka 2015/2016 hadi ng'ombe 250,000 mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, idadi ya mifugo iliyouzwa minadani imeongezeka kutoka ng'ombe milioni 1.4 mbuzi milioni 1.1 na kondoo 253,243 wenye thamani ya shilingi bilioni 976 mwaka 2015/2016 hadi kufikia ng'ombe milioni 1.618

wenye thamani ya shilingi trilioni 1.34, mbuzi 1,278,182 na kondoo 278,595 wenye jumla ya thamani ya shilingi trilioni 1.02 mwaka 2016/2017. Aidha, hadi kufikia Machi, 2017 jumla ya tani 3,162 za nyama ziliuzwa nje ya nchi katika nchi za Dubai, Iraq na Vietnam ikiwa tani 711.82 nyama ya mbuzi, tani 439 nyama ya ng'ombe, tani 222 za nyama ya kondoo na tani 1,789 za nyama ya punda. Aidha, Serikali inapanga kusitisha uchinjaji wa punda ambao wanakadiriwa kuwa 538,000 kuanzia tarehe 1 Julai, 2017 ili kukabiliana na changamoto ya upungufu au kumalizika kwa wanyama hawa kutokana na kasi ya uchinjaji inayoendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wale wanaochinja punda kwa sasa wanashauriwa kuanza kujiandaa kuchinja wanyama wengine pindi tunaposimamisha uchinjani wa punda hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2016/2017 vipande vya ngozi zilizosindikwa vimepungua kutoka vipande vya ngozi za ng'ombe 1,575,000 vyenye thamani ya shilingi bilioni 45 mwaka 2015/2016, hadi vipande 1,215,000 vyenye thamani ya shilingi bilioni 34.7. Pia mwaka 2016/2017 vipande vya ngozi za mbuzi/kondoo 928,000 vyenye thamani ya shilingi bilioni 6.2 vilivyosindikwa vimepungua ikilinganishwa na vipande 1,124,000 vyenye thamani ya shilingi bilioni 7.5 mwaka 2015/2016. Aidha, ngozi ghafi za ng'ombe vipande 241,773 vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.8 viliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na vipande 187,000 vya ngozi za ng'ombe vyenye thamani ya shilingi bilioni 2.4 mwaka 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba niongelee kidogo migogoro ya wakulima na wafugaji. Kama utakumbuka Serikali iliunda Tume kupitia taarifa na maandiko yote yaliyowahi kuwepo juu ya migogoro kati ya wakulima na wafugaji. Timu hiyo ya watendaji ilizunguka nchi nzima na kupitia ripoti 19 na tayari imewasilisha taarifa yake ya awali Serikalini. Taarifa yenyewe ni hiki kitabu kikubwa hiki nilichokishikilia. Baada ya taarifa hiyo kupokelewa imeanza kufanyiwa kazi na tayari timu ya Makatibu Wakuu imeipitia na kutoa mapendekezo yao. Baada ya kupitiwa na Makatibu

Wakuu, ripoti na mapendekezo yao imekabidhiwa kwa Mawaziri watano ambao nao wamefanya kikao chao cha kwanza kuijadili pamoja na mapendekezo yaliyowasilishwa na Makatibu Wakuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii ni nyeti na inayo mapendekezo yanayohitaji umakini mkubwa kuyatafakari ili pindi itakapokubalika kwamba yatekelezwe basi utekelezaji wake usiwe na athari hasi zinazoweza kuligawa Taifa. Kikao cha pili cha Mawaziri hawa kitakaa tarehe 10 Juni, 2017 na mapendekezo yao yatawasilishwa kwa Waziri Mkuu na baadae kwenye Baraza la Mawaziri kwa uamuzi wa mwisho. Jambo la msingi ni ardhi kupimwa na kupangiwa matumizi na hili halina budi kufanyika mara moja, Mamlaka ya Serikali za Mitaa zimeagizwa na ninasisitiza kila mmoja kuweka mpango kazi na madhubuti wa kupanga matumizi ya ardhi na kuipima, usimamizi wa sheria za ardhi pia, ni muhimu ili matumizi ya ardhi yatakayokubalika yaweze kufuatwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu imekamilisha uchambuzi wa vitalu vya mifugo katika Ranchi za Taifa na kuwa uchambuzi huo ni sehemu ya ripoti ya timu hiyo ya kitaifa yaani uchambuzi huo umo ndani ya hiki kitabu, mgao mpya utafanyika baada ya maamuzi ya ripoti nzima kufikiwa, Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara inaendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vya kuchakata nyama jambo ambalo litasaidia sana kuongeza kasi ya uvunaji wa mifugo nchini na pia kusaidia kupunguza msongamano wa malisho hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya uvuvi; katika mwaka 2016/2017 jumla ya wavuvi wadogo 203,000 wanaotumia vyombo vya uvuvi 59 kadhaa walijihusisha moja kwa moja shughuli za uvuvi na kuwezesha kuvunwa kwa tani 362, 000 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.4 za samaki, kiambatisho Na. 2 (a) na (b) katika kitabu chetu cha hotuba. Vilevile zaidi ya watu milioni nne wameendelea kunufaika na sekta ya uvuvi zikiwemo uchakataji wa samaki, utengenezaji wa zana na vyombo vya uvuvi biashara ndogo ndogo na mama lishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kusimamia sheria kutoa mafunzo na kuthibiti uvuvi haramu kwa ajili ya uvuvi endelevu, kuhamasisha ukuzaji viumbe kwenye maji na kuwezesha na kuratibu upatikanaji wa vifaranga bora vya samaki, kuimarisha vituo vitano na kuanzisha kituo cha ugani cha ufugaji samaki Mkoani Simiyu, aidha, sekta binafsi imeanzisha vituo vitano vya ukuzaji viumbe kwenye maji na kufikia vituo 13. Vilevile mabwawa ya samaki yameongezeka na kufikia 22,702 mwaka 2016/2017 ukilinganisha na 22,545 yaliyokuwepo mwaka 2015/2016 ambayo imewezesha kuongezeka kwa uzalishaji wa samaki kwenye mabwawa kutoka wastani wa tani milioni 3,613 mwaka 2015/2016 hadi tani 11,000 mwaka 2016/2017 bila ongezeko la asilimia 350.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017, leseni 96 za uvuvi zenye thamani ya shilingi milioni 968.59 zilitolewa kwa meli 27 kutoka nchi za China, Hispania, Taiwan, Ufaransa, Seychelles na Mauritania zinazovua katika Bahari Kuu. Aidha, tani 39, 691 za samaki na mazao ya uvuvi zenye thamani ya shilingi bilioni 526 yaliuzwa nje ya nchi na kuliingizia taifa shilingi bilioni 14.3 kiambatanisho Na. 3(a) na (b) katika kitabu chetu. Pia tani 12,743 za samaki kutoka nje ya nchi zilihakikiwa na kuruhusiwa na kuingizwa nchini kwa ajili ya soko la ndani na kuliingizia Taifa shilingi bilioni 10.1.

Kuhusu hali ya ushiriki; Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeendelea kufanya uhakiki ili kubaini uhai wa Vyama vya Ushirika na kuhamasisha wananchi kuanzisha na kujiunga na Vyama vya Ushirika ambapo hadi kufikia Machi, 2017 Idadi ya Vyama imefikia 10,566 na wanachama wameongeza kutoka milioni 1.4 hadi milioni 2.2 sawa na ongezeko la asilimia 55.9 kiambatanisho Na. 4. Aidha, jumla ya vyama vipya vya Ushirika 101 vimeanzishwa, Ushirika la Akiba na Mikopo umeendelea kutoa huduma za kifedha ambapo thamani ya hisa ya akiba na amana zimeongezeka kutoka shilingi bilioni 378 mwaka 2015 hadi shilingi bilioni 378.3 mwaka 2016. Vilevile thamani ya mikopo iliyotolewa kwa wanachama iliongezeka kufikia shilingi bilioni 855.3 mwaka 2016 kutoka shilingi bilioni 854.4 mwaka 2015.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeendelea kuhimiza matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Mfumo huu umesaidia kupanda kwa bei ya korosho na mapato kwa wakulima kupitia vyama vikuu vya ushirika vya *TANECU, MAMCU, RUNALI,* Lindi Mwambao, *TAMCU* na *CORECU.* Katika msimu wa 2016/2017 vyama hivyo viliuza korosho na kuwalipa wakulima jumla ya shilingi bilioni 809.1 ukilinganishwa na malipo ya shilingi bilioni 293 msimu wa 2015/2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, wanachama wa vyama vya ushirika wamehamasishwa kujiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii ukiwemo *NSSF* ambapo kupitia *Wakulima Scheme* idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika waliojiunga na mfuko imeongezeka kutoka 78,747 mwaka 2015 hadi 90,047 mwaka 2016.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni kuhusu Mapato na Matumizi ya Fedha katika kipindi cha mwaka 2016/2017, Fungu 43 - Kilimo; Makusanyo ya Maduhuli:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2016/2017 ilikadiria kukusanya mapato ya shilingi bilioni 4.02 kupitia Fungu 43 kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2017 Wizara ilikusanya jumla ya shilingi bilioni 3.30 sawa na asilimia 82.15 ya makadirio na Wizara inaendelea kukusanya maduhuli hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi kupitia Fungu 43 ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 210.3. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 109.8 ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 100.5 ni fedha za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Matumizi ya Bajeti ya Kawaida; katika mwaka 2016/2017 Fungu 43 lilitengewa jumla ya shilingi bilioni 109 na Wizara ilipokea kiasi cha shilingi bilioni 3.3 kwa ajili ya kulipia madeni ya watumishi, wazabuni na wakandarasi na maghala na skimu za umwagiliaji na kufanya fedha zilizoidhinishwa kuongezeka hadi kufikia shilingi

bilioni 113.1. Hivyo, kati ya fedha hizo shilingi bilioni 43.4 ni kwa ajili ya mishahara ya watumishi wa Wizara na Bodi/Taasisi na shilingi bilioni 69.7 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia tarehe 4 Mei 2017 jumla ya shilingi bilioni 61.7 za matumizi ya kawaida zimetolewa sawa na asilimia 54.5 ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha, fedha zilizotumika ni shilingi bilioni 59 sawa na asilimia 95.09 ya fedha zilizotolewa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 32 ni mishahara ya Fungu 43 na Bodi/Taasisi na shilingi bilioni 26.7 ilikuwa ni matumizi mengineyo. Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha unaoendelea, Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi ilitengewa shilingi bilioni 100.5 kupitia Fungu 43 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia tarehe 4 Mei 2017 shilingi bilioni 3.7 zimetolewa sawa na asilimia 3.3 ya fedha zilizoidhinishwa. Matumizi ni shilingi bilioni 2.88 sawa na asilimia 85.3 ya fedha zilizotolewa. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 1.8 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 1.07 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 99 - Mifugo; Makusanyo ya Maduhuli. Katika mwaka 2016/2017, Wizara kwa upande wa Idara Kuu za Mifugo na Uvuvi ilitarajia kukusanya shilingi bilioni 35.19. Hadi kufikia mwezi Aprili 2017, kiasi cha shilingi bilioni 26.9 kimekusanywa na Wizara ikiwa ni sawa na asilimia 77 ya lengo. Katika mwaka 2016/2017 Wizara kupitia Idara Kuu za Mifugo imetengewa kutumia jumla ya shilingi bilioni 60.01, kati ya kiasi hiki, shilingi bilioni 44.1 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi bilioni 15.8 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017 Wizara kupitia Fungu 99: Mifugo na Uvuvi ilitengewa shilingi bilioni 44.1 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, 22.2 ni za mishahara na shilingi bilioni 21.8 ni za matumizi mengineyo. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2017 jumla ya shilingi bilioni 29.8 zimetolewa, sawa na asilimia 68 kwa ajili ya

Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 21.9 ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara na Shilingi bilioni 7.9 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti ya Bajeti ya Maendeleo. Katika mwaka wa 2016/2017, Wizara kupitia Fungu 99: Mifugo na Uvuvi ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 15.8 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, shilingi bilioni 8 ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 7.8 ni fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2017 kiasi cha shilingi bilioni 1.25 kilikuwa kimetolewa na kutumika. Kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi milioni 280 na fedha za nje ni shilingi milioni 972.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 24 - Ushirika; katika mwaka wa fedha wa 2016/2017 Wizara kupitia Fungu 24 ilitengewa shilingi bilioni 4.89 na ukomo wa Bajeti ya Fungu 24 umeongezeka kwa kiasi cha shilingi milioni 175 zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya malipo ya madeni ya watumishi wa Tume ya Ushirika na hivyo kufikia ukomo wa shilingi bilioni 5.07. Katika fedha hizo, shilingi bilioni 1.62 ni fedha za matumizi mengineyo na shilingi milioni 644.51 ni za Tume ya Maendeleo ya Ushirika na shilingi milioni 971 ruzuku ya ndani kwa *COASCO*. Jumla ya shilingi bilioni 3.28 zilitengwa kwa ajili ya mishahara ambapo shilingi bilioni 1.83 ni mishahara ya watumishi wa Tume na shilingi bilioni 1.45 ni kwa ajili ya *COASCO*. Aidha, katika mwaka 2016/2017, Tume ya Maendeleo ya Ushirika haikutengewa fedha za bajeti ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika Matumizi ya Bajeti ya Kawaida; hadi tarehe 30 Aprili, 2017 fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa kutoka Hazina ni shilingi bilioni 3.43 sawa na asilimia 67ya kiasi kilichoidhinishwa. Matumizi yaliyofanyika ni shilingi bilioni 3.42 sawa na asilimia 99.9 ya kiasi cha fedha kilichotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa maeneo ya vipaumbele kwa mwaka 2016/2017 na mpango wa mwaka 2017/2018 Fungu 43 - Kilimo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2016/2017 umezingatia malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021); Malengo Endelevu ya Maendeleo; *Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan (TAFSIP)* na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020. Malengo hayo yalitekelezwa kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo, na Mpango wa Kukuza Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania *(SAGCOT).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wadau imetekeleza majukumu yake kulingana Maeneo ya vipaumbele vya kuboresha mfumo wa utafiti na utoaji wa matokeo ya utafiti kwa wadau; kuimarisha usimamizi kabla na baada ya mavuno na kuongeza upatikanaji wa masoko; kuimarisha mafunzo ya kilimo na huduma za ugani; kuongeza ushiriki wa vijana katika kilimo; kuratibu na kuboresha matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo kwa kutenga, kupima na kumilikisha maeneo hayo kwa wakulima; kuunda na kupitia sera, mikakati na mifumo ya kisheria katika sekta ndogo ya mazao; kuimarisha uratibu, ufuatiliaji na tathmini katika sekta ya kilimo; kuimarisha upatikanaji na utumiaji wa pembejeo, zana za kilimo na huduma za udhibiti na kuwezesha uwekezaji wa sekta binafsi katika kilimo ambapo tozo zilizokuwa kero katika sekta ndogo ya mazao zimefutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tozo ambazo zimefutwa tayari na Serikali ni pamoja na ada ya leseni ya kusindika Kahawa ya Dola za Kimarekani 250; mchango wa Mwenge kwa kila kiwanda cha kuchambua pamba wa shilingi 450,000; na kodi ya moto na uokoaji katika zao la chai. Aidha, kwa zao la korosho, ushuru ufuatao umefutwa; Chama Kikuu cha Ushirika wa shilingi 20 kwa kilo; kusafirisha korosho shilingi 50 kwa kilo; gharama za mtunza ghala shilingi 10 kwa kilo; kikosi kazi kwa ajili ya ufuatiliaji shilingi 10 kwa kilo na makato ya unyaufu. Vilevile Serikali imeondoa ushuru wa forodha wakati wa kuagiza soya inayotumika katika utengenezaji wa vyakula vya mifugo na unga wa lishe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018 kuanzia Julai Mosi, 2017, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kodi, tozo na ada ambazo ni kero kwa wakulima, wafugaji na wavuvi wa nchi hii zinafutwa na kubaki na zile zenye mahusiano ya moja kwa moja na uendelezaji wa tasnia husika. Kwenye sekta ndogo ya mazao, katika mwaka 2017/2018 Serikali itafuta jumla ya tozo 80 kati ya tozo 139 ambazo zimeonekana kuwa kero kwa wakulima na pia itapunguza viwango vya tozo nne zilizopo. Katika maamuzi hayo, kwenye tasnia ya tumbaku, jumla ya tozo kumi zifuatazo zimefutwa:-

(i) Mchango wa Ushirika wa Mkoa wa USD 0.072 kwa kilo moja

(ii) Mchango kwa chama cha msingi cha ushirika kwa kiwango cha USD 0.03 kwa kilo,

(iii) Mchango wa gharama za masoko ya ushirika kiwango cha USD 0.07 kwa kilo,

(iv) Dhamana ya Benki Kuu ya Tanzania kwa mikopo kwa kiwango cha asilimia moja *(1% Loan Guarantee);*

(v) Fomu ya maombi ya leseni za Tumbaku *(Licence Application Form)* - kwa kiwango cha USD 100;

(vi) Kodi ya leseni kununua tumbaku kavu kwa kiwango USD 4,000;

(vii) Leseni ya kununua Tumbaku mbichi kiwandani kwa kiwango USD 4,000;

(viii) Leseni ya kununua Tumbaku mbichi kwa kila Wilaya kiwango cha USD 3,500;

(ix) Leseni ya kuuza Tumbaku nje ya nchi USD 4,000; na

(x) Tozo ya Baraza Tumbaku USD 0.01 kwa kila kilo *(Tobacco Council fee of USD 0.01 per kg)* na tozo mbili yaani

moja ni kodi ya leseni kununua tumbaku kavu ya USD 4,000 imepunguzwa kwa asilimia 50 na kuwa USD 2,000 na ya pili Leseni ya kusindika tumbaku USD 10,000 imepunguzwa kwa asilimia 50 na kuwa USD 5,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Katika tasnia ya kahawa, jumla ya tozo 17 zimefutwa na, kodi hizo ni:-

(i) Ada ya leseni ya kuuza nje ya nchi kahawa ya kijani kwa makampuni na vyama vya ushirika kiwango cha USD 1,000 sasa leseni hii itapatikana bure;

(ii) Ada ya leseni ya ghala la kahawa kwa kampuni na vyama vya ushirika - USD 500;

(iii) Ada ya leseni ya *Premium Coffee* kwa kampuni kiwango cha USD 1,000;

(iv) Ada ya leseni ya kukoboa kahawa kwa kampuni na vyama vya ushirika - USD 1,000;

(v) Ada ya leseni ya *Premium Coffee* kwa vyama vya ushirika kiwango cha USD 500;

(vi) Ada ya leseni ya kuuza nje ya nchi kahawa iliyosindikwa kwa kampuni na vyama vya ushirika kiwango cha USD 500;

(vii) Ada ya leseni ya kununua kahawa kwa Kampuni kiwango cha USD 1,000 *(Patchment Dry Cherry Coffee Buying Licence);*

(viii) Tozo ya fomu ya kuomba leseni ya kuuza nje kahawa ya kijani kwa kampuni na vyama vya ushirika kiwango cha USD 20;

(ix) Tozo na fomu ya kuomba leseni ya ghala la kahawa kwa kampuni na vyama vya ushirika kiwango cha USD 20;

(x) Tozo na fomu ya leseni ya kukoboa kahawa kwa kampuni na vyama vya ushirika kiwango cha USD 20;

(xi) Tozo ya fomu ya kuomba leseni ya kuuza nje *premium coffee* kwa kwa kampuni kwa kiwango cha USD 20;

(xii) Tozo ya fomu ya kuomba leseni ya kuuza nje *premium coffee* Vyama vya ushirika kwa kiwango cha USD 20;

(xiii) Tozo ya fomu ya kuomba leseni ya kuuza nje kahawa iliyosindikwa kwa kampuni na vyama vya ushirika kiwango cha USD 20;

(xiv) Tozo ya fomu ya kuomba leseni ya usindikaji wa ndani kampuni na vyama vya ushirika kwa kiwango cha USD 20;

(xv) Tozo ya fomu ya kuomba leseni ya usindikaji wa kahawa kwa kiwango cha USD 20;

(xvi) Tozo ya fomu ya kuomba leseni ya kununua kahawa kwa kampuni kwa kiwango cha USD 20; na

(xvii) Ada ya uendeshaji wa minada ya Bodi ya kahawa kiwango cha 0.2 ya mauzo ya kahawa inayonunuliwa mnadani na kuchangiwa na wanunuzi wa kahawa, zimefutwa na tozo ya makato ya bei ya kahawa mnadani kwa ajili ya kugharamia shughuli za utafiti wa kahawa imepunguzwa kiwango kwa asilimia 50 kutoka asilimia 0.75 ya bei ya kahawa mnadani kuwa asilimia 0.375.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tasnia ya sukari, tozo 16 zimefutwa kama ifuatavyo:-

Ada ya leseni uingizaji wa sukari ya viwandani kwa viwango vya shilingi 200,000; ada ya leseni uingizaji wa sukari ya kuziba pengo *(gap sugar)* shilingi 200,000; ada ya leseni kamili ya uzalishaji sukari uwekezaji mkubwa mpya *licencing sugar millers for new establishment full licence* kiwango cha

dola 30,000; ada ya leseni ya muda wa uzalishaji sukari uwekezaji mkubwa mpya *(provisional licence)* kiwango cha dola 20,000; ada ya leseni kamili ya uzalishaji sukari uwekezaji mdogo mpya kiwango cha dola 5,000; ada ya leseni ya muda uzalishaji sukari uwekezaji mdogo mpya dola 2500 na leseni ya marudio kila baada ya miaka mitatu uwekezaji mkubwa shilingi 20,000,000.

Pia leseni kamili ya marudio kila baada ya miaka mitatu uwekezaji mdogo shilingi 5,000,000; leseni ya muda ya marudio kila baada ya miaka mitatu uwekezaji mdogo kiwango cha shilingi 2,000,000; ada ya leseni ya kuchakata miwa kwa kiwango cha shilingi 250,000; ada ya kusajili waagizaji wakubwa wa sukari ya viwandani *above 5000MT* kiwango cha shilingi 5,000,000; ada ya kusajili waagizaji wa kati wa sukari ya viwandani shilingi 2,000,000; ada ya kusajili waagizaji wadogo wa sukari ya viwandani shilingi 500,000; ada ya kusajili wafanyabiashara wa sukari ya matumizi ya kawaida shilingi 2,000,000; ada ya kupata kibali cha kuingiza sukari ya viwandani kila mwaka shilingi 200,000 na ada ya kupata kibali cha kuingiza sukari ya kuziba pengo shilingi 1,000,000. Hizi tozo zote na kodi kwenye tasnia ya sukari nazo zimefutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha maendeleo ya Ushirika nchini, Serikali imefuta tozo 20 zilizokuwepo katika ushirika katika ngazi mbalimbali kama ifuatavyo:-

(i) Ada ya usajili wa marekebisho ya masharti ya Chama cha Ushirika cha Msingi kiwango cha shilingi 20,000;

(ii) Ada ya usajili wa marekebisho ya masharti ya Chama cha Ushirika cha Upili kiwango cha shilingi 40,000;

(iii) Ada ya usajili wa marekebisho ya masharti ya Chama cha Ushirika cha Kati kiwango cha shilingi 80,000;

(iv) Ada ya usajili wa marekebisho ya masharti ya Chama cha Ushirika Shirikisho kiwango cha shilingi 200,000;

(v) Ada ya usajili wa marekebisho ya masharti ya Chama cha Ushirika katika uwekezaji wa pamoja kiwango cha shilingi 80,000;

(vi) Ada ya uchunguzi kwenye Rejista ya Chama cha Ushirika cha Msingi kiwango cha shilingi 5,000;

(vii) Ada ya uchunguzi kwenye rejista ya Chama cha Ushirika cha Upili kwa kiwango cha shilingi 10,000;

(viii) Ada ya uchunguzi kwenye rejista ya Chama cha Ushirika cha Kati kiwango cha shilingi 20,000;

(ix) Ada ya uchunguzi kwenye rejista ya Shirikisho la Vyama vya Ushirika kwa kiwango cha shilingi 20,000;

(x) Ada ya uchunguzi kwenye Rejista ya Chama cha Ushirika kwa ajili ya uwekezaji wa pamoja kiwango cha shilingi 15,000;

(xi) Ada ya ukaguzi wa kumbukumbu au taarifa za Chama cha Ushirika cha Msingi kiwango cha shilingi 5,000;

(xii) Ada ya ukaguzi wa kumbukumbu au taarifa za Chama cha Ushirika cha Upili kiwango cha shilingi 10,000;

(xiii) Ada ya ukaguzi wa kumbukumbu au taarifa za Chama cha Ushirika cha Kati kiwango cha shilingi 15,000;

(xiv) Ada ya ukaguzi na nyingine nyingi sana katika eneo la ushirika kama nilivyosema jumla tozo 20 zimefutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jitihada za Serikali kuongeza upatikanaji wa pembejeo, Serikali itafuta tozo tatu kwenye mbolea na Moja itapunguzwa kiwango. Aidha, tozo Saba zilizokuwa kwenye mbegu zitafutwa. Vilevile tozo pekee iliyokuwepo katika mfuko wa pembejeo ya ada ya nyaraka nayo itaondolewa. Orodha kamili ya tozo zilizofutwa katika eneo hili ni kama ilivyo katika kiambatisho namba 7 (a), 7(b) na 7(c).

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilihakikishie Bunge lako Tukufu, kuwa Serikali itaendelea kuchambua kwa kina tozo, ushuru na ada mbalimbali zilizobaki zinazotozwa katika kilimo, mifugo na uvuvi kwa lengo la kuangalia uhalali wa kuwepo kwake na viwango vya tozo, ushuru na ada hizo kwa lengo la kuziondoa au kuzipunguza ili kuwapunguzia wakulima, wafugaji na wavuvi mzigo wa tozo, ushuru na ada zisizokuwa na tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuimarisha upatikanaji na utumiaji wa pembejeo, Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Mbolea *(TFRA)* imeandaa Kanuni ya Manunuzi ya Mbolea kwa Pamoja za mwaka 2017 *(Fertilizer Bulk Procurement Regulations, 2017)* na mwongozo wa utekelezaji kwa madhumuni ya kuongeza upatikanaji na kupunguza bei za mbolea kwa wakulima. Katika mwaka 2017/2018 mfumo wa uagizaji wa mbolea kwa pamoja utaanza kwa kuagiza aina mbili tu za mbolea ambazo ni; mbolea ya kupandia *(DAP)* na mbolea ya kukuzia *(UREA)* kwa kuwa zinatumika kwa wingi. Mbolea zingine hususan *NPK, CAN, SA, MOP, TSP, blends* mbalimbali, *Biofertilizers* na zile za maji *(foliar)* zitaendelea kuletwa kwa utaratibu unaotumika sasa. Utekelezaji wa kina wa vipaumbele kwa mwaka 2016/2017 na mpango wa mwaka 2017/2018 umeainishwa katika ukurasa wa 30 hadi 101 wa kitabu cha hotuba ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna matumaini makubwa sana kwamba baada ya kuanzisha mfumo huu wa uingizaji wa mbolea aina hizi mbili kwa pamoja bei ya mbolea huenda ikashuka sana viwango vya kutufanya Serikali iangalie upya jambo ambalo imekuwa ikilifanya kwa takribani miaka 11 sasa la kuweka ruzuku kwenye pembejeo hasa mbolea kwa baadhi ya wakulima nchini. Kwa sababu mbolea itakuwa ya bei nafuu ambayo kila mkulima nchini atamudu na kununua na kwa hiyo, upatikanaji wake utakuwa rahisi na kutakuwa na ongezeko la matumizi ya mbolea kwa wakulima wetu. Leo tunapozungumza hapa malengo ya nchi za Ukanda wa Kusini mwa Afrika *(SADC)* ni kutumia angalau virutubisho kilo 50 kwa heka moja ya

mbolea ya shamba. Leo sisi bado tuko katika kilo 19 za virutubisho kwa kila hekta moja, bado tuna safari ndefu na kwa hivyo jitihada hizi ni za kuhakikisha kwamba tunafikia haya malengo ambayo tumejiwekea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 99 - Mifugo; katika mwaka 2016/2017 Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta ilitekeleza maeneo ya kipaumbele yaliyohusu sera, mikakati, sheria na kanuni, programu za maendeleo; uzalishaji wa mifugo na usindikaji wa mazao yake; udhibiti wa magonjwa mbalimbali ya mifugo, utafiti na mafunzo. Maeneo ya kipaumbele yaliyotekelezwa ni pamoja na kuongeza upatikanaji na matumizi ya pembejeo na zana za mifugo, kuboresha huduma za ugani, utafiti na mafunzo, kuendeleza na kuboresha miundombinu ya mifugo; malisho na nyanda za malisho, kuboresha upatikanaji wa masoko na kuongeza thamani ya mazao ya mifugo, kuimarisha na kujenga ushirika na hasa ule wa vyama vya wafugaji. Kuwezesha uwezo wa taasisi na mifumo ya taarifa kwa ajili ya maendeleo na usimamizi wa sekta za mifugo na kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya kukuza uwekezaji wa sekta binafsi katika sekta ya mifugo ikiwa ni pamoja na kufuta kodi, tozo na ada mbalimbali.

Katika mwaka 2017/2018 Serikali pia itafuta kodi, tozo na ada saba ambazo zimekuwa kero kwa wafugaji, wafanyabiashara na wawekezaji na kubakiza zile tu zenye uhusiano wa moja kwa moja na maendeleo ya sekta yenyewe. Hivyo, kodi zifuatazo pia zinafutwa kuanzia Julai Mosi mwaka huu katika sekta ya mifugo. Katika tasnia ya maziwa Serikali itafuta kodi zifuatazo:-

(i) Ada ya usajili wa wadau wazalishaji wakubwa zaidi ya lita 500 kwa siku shilingi 100,000, wazalishaji wa kati lita 101 hadi 5000 kwa siku shilingi 50,000 na shilingi 5000 kwa wazalishaji wadogo.

(ii) Wakusanyaji wa maziwa shilingi 250,000 wazalishaji wa maziwa wakubwa, wazalishaji wa kati shilingi 5,000 na wazalishaji wadogo shilingi 50,000 na zenyewe zitafutwa.

(iii) Wasambazaji wa kiwango cha shilingi 500,000, ada ya maombi ya uuzaji maziwa kwenda nje ya nchi *(export permit)* shilingi 30,000 kwa shehena zitafutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika tasnia ya nyama Serikali itafuta kodi nne ambazo ni ada ya usajili wa wafugaji, wafugaji wakubwa ni shilingi 75,000 imefutwa, wafugaji wa kati ni shilingi 50,000 imefutwa na wafugaji wadogo shilingi 15,000 imefutwa. Ada ya usajili wa minada yaani minada ya awali shilingi 30,000 yenyewe imefutwa, minada ya upili shilingi 50,000 imefutwa na ada ya usajili wa wafanyabiashara wa mifugo na nyama shilingi 52,000 pia imefutwa. Ushuru wa kuuza mifugo hai nje ya nchi *(export clearance certificate)* ng'ombe shilingi 50,000 imefutwa, mbuzi na kondoo shilingi 10,000, imefutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, katika eneo la huduma za Afya ya Mifugo Serikali itafuta tozo za vibali vya usafirishaji wanyama na mazao yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tozo ya kibali cha kuingiza ngozi za ng'ombe kwa kipande shilingi 5,000 na kutoa ngozi za ng'ombe kwa kipande shilingi 10,000 zote zimefutwa. Tozo ya kibali cha kuingiza ngozi za mbuzi na kondoo kwa kipande shilingi 200 na kutoa nje ya nchi shilingi 500 pia zimefutwa; tozo ya kibali cha afya cha kusafirisha ng'ombe ndani ya wilaya shilingi 1,000 imefutwa; tozo ya kibali cha afya cha kusafirisha kondoo na mbuzi ndani ya Wilaya shilingi 500 imefutwa. Niseme kwamba kodi nyingi katika eneo hili la mifugo pia zimefutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi hizi kama zilivyo ziko katika kiambatanisho namba 9 ndani ya kitabu chetu. Utekelezaji wa kina wa vipaumbele kwa 2016/2017 na mpango wa mwaka 2017/2018 umeainishwa katika ukurasa wa 102 hadi 156 wa kitabu chetu cha hotuba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 64 - Uvuvi; katika mwaka 2016/2017, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta ilitekeleza maeneo ya kipaumbele yaliyohusu sera,

mikakati na programu; sheria na kanuni za sekta ya uvuvi; uzalishaji na biashara ya mazao ya uvuvi; ukuzaji wa viumbe kwenye maji; uwezeshaji wa wavuvi wadogo na wakuzaji viumbe kwenye maji; usimamizi wa rasilimali za uvuvi, usimamizi wa uvuvi katika bahari kuu, hifadhi za bahari na maeneo tengefu; kuimarisha ulinzi wa rasilimali za uvuvi, kusimamia ubora na usalama wa mazao ya uvuvi, utafiti, mafunzo na ugani wa uvuvi, uwekezaji kwenye Sekta ya Uvuvi na Tozo na leseni katika Sekta Kuu ya Uvuvi ambapo katika mwaka 2017/2018 Serikali itafuta kodi, tozo na ada tano ambazo ni kero kwa wavuvi, wafugaji viumbe kwenye maji na wawekezaji na kubakiza zile tu zenye uhusiano wa uendelezaji wa sekta ya uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la ukuzaji wa viumbe kwenye maji, tozo moja imefutwa ambayo ni ushuru wa kuuza kaa hai nje ya nchi waliozalishwa *(Export royalty),* sasa watatozwa kwa kilo moja na daraja *USD* 0.60 kwa kilo. Eneo la maendeleo ya uvuvi tozo nne zimefutwa ambazo ni tozo ya kusafirisha mazao ya uvuvi *(Movement Permit)* zote zimefutwa. Ada ya ukaguzi wa kina wa kiwanda/ghala kila robo mwaka *(Auditing fees)* shilingi 100,000 na yenyewe imefutwa; tozo ya Cheti cha Afya *(Sanitary Certificate)* kukagua mazao ya uvuvi, shilingi 30,000 na yenyewe imefutwa; ada ya usajili wa chombo cha uvuvi chini ya mita 11 kwa wavuvi wadogo cha shilingi 20,000 imefutwa. Hili jambo naomba lisikike na lieleweke vizuri *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia ada ya usajili wa chombo cha uvuvi chini ya mita 11 kwa wavuvi wadogo cha shilingi 20,000 imefutwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na kufuta kodi katika sekta ya uvuvi, Serikali imepitia na kufanyia marekebisho makubwa kwenye kanuni zetu za uvuvi wa Bahari Kuu yaani *The Deep Sea Fishing Authority Regulations of 2017* ili uvuvi katika Bahari Kuu uweze kuwa wa manufaa kwa nchi yetu. Katika mabadiliko hayo mambo yafuatayo yameingizwa na kufanyiwa marekebisho:-

(i) Usafirishaji samaki nje ya nchi sasa utalipiwa mrabaha wa Dola za Kimarekani 0.4 kwa kilo;

(ii) *Performance Bond* ya Benki kwa uhakika *(assurance)* wa kuvua samaki itatakiwa;

(iii) Samaki ambao hawakulengwa kuvuliwa *(bycatch)* watashushwa kwenye Bandari ya Dar es Salaam na Zanzibar Gati Na. 3 na Gati Na. 6 kama hatua ya awali wakati tukijiandaa kujenga bandari ya uvuvi;

(iv) Kila meli inayopewa leseni ya kuvua samaki ni lazima ichukue mabaharia wa Kitanzania; na

(v) Kwenye kila meli iliyopewa leseni ya kuvua samaki lazima kuwe na waangalizi *(observers)* kwa lengo la kuhakikisha masharti ya leseni yanazingatiwa na pia kuimarisha ulinzi wa rasilimali zetu.

Mheshimmiwa Naibu Spika, ingawa pia jambo hili limepata upinzani, Serikali kwa kushauriana na nchi jirani zenye maeneo maalumu ya uvuvi kama sisi, imeendelea na msimamo wake na sasa wavuvi kutoka nje ya nchi wameanza kukata leseni kwa masharti mapya yaliyowekwa. Ni matarajio yetu kuwa sasa Tanzania nayo itakuwa nchi yenye kunufaika na uchumi wa bahari yaani "*Green Economy. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Maendeleo ya Ushirika; katika mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na wadau wa sekta inaimarisha ushirika na asasi za wananchi kama ilivyo kwenye kitabu chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani, naomba nitumie fursa hii kuzishukuru nchi na mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia sana Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo; kwanza napenda kuzishukuru nchi za Japan, Marekani, Uingereza, Ireland, Malaysia, China, Indonesia, Korea ya Kusini, India, Misri, Israel, Ubelgiji, Ujerumani, Finland,

Norway, Brazil, Uholanzi, Vietnam na Poland. Nayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa ambayo ni Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, *AU, IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, UNICEF, WFP, CIMMYT, ICRISAT, ASARECA, USAID, KOICA, ICRAF, IITA, IRRI, ILRI, CABI, CFC* na mashirika mengine, shirika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani, Shirika la Kudhibiti Nzige Wekundu, *Bill and Melinda Gates Foundation, Gatsby Trust*, *Rockfeller Foundation, Agha Khan Foundation* na *Unilever* kwa ushirikiano na misaada ya nchi na mashirika hayo bado tunauhitaji ili tuweze kuendeleza kilimo nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima wa nchi hii wafugaji na wavuvi kwa kazi kubwa wanayofanya katika uzalishaji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Napenda kumshukuru kwa namna ya pekee sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo Mifugo na Uvuvi Wiliam Tate Ole Nasha, Mbunge wa Ngorongoro; Makatibu Wakuu wangu, *Engineer* Mathew John Mtigumwe, Dkt. Yohana Budeba, na Dkt. Mary Mashingo; Wakurugenzi wa Idara, Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara, watumishi wote wa Wizara; Wenyeviti na Wakurugenzi wa Bodi mbalimbali za taasisi za Wizara hii na wadau mbalimbali wa Sekta ya Kilimo kwa juhudi, ushirikiano na ushauri uliowezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2016/2017. Ni matarajio yangu kwamba Wizara itaendelea kupata ushirikiano wao katika mwaka 2017/2018. Mwisho natoa shukrani kwa Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha kitabu cha hotuba ya bajeti ya mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya fedha. Katika mwaka 2017/2018, Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi kupitia Fungu 43, Fungu 99, Fungu 64 na Fungu 24 inaomba jumla ya shilingi 267,865,782,829 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 43 – Kilimo jumla ya shilingi 214,815,759,000 zinaombwa; kati ya fedha hizo shilingi 64,562,759,000 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 150,253,000,000 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 99 - Mifugo, jumla ya Shilingi 29,963,524,000 zinaombwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 25,963,524,000 ni fedha za Matumizi ya Kawaida na Shilingi 4,000,000,000 ni fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 64 - Uvuvi, jumla ya shilingi 16,792,705,829 zinaombwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 14,792,645,829 ni fedha za Matumizi ya Kawaida na shilingi 2,000,000,000 ni fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 24 - Tume ya Ushirika, kiasi cha shilingi 6,293,854,000 kinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika Tume ya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tena nitoe shukurani zangu za dhati kwako na kwa Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara kwa anuani zilizoko katika kitabu chetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono.

**HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO MIFUGO NA UVUVI MHESHIMIWA, ENG. DKT. CHARLES JOHN TIZEBA (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA 2017/2018 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

**1.** ***Mheshimiwa Spika***, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilishwa hapa Bungeni leo na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya

Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji inayohusu Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi, sasa lijadili na kukubali kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kawaida na ya Maendeleo ya Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2017/2018.

**2.** ***Mheshimiwa Spika,*** namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha siku ya leo tukiwa na afya njema ili tuweze kujadili bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya Watanzania. Napenda pia, kumshukuru Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuniamini na kuniteua kuwa Waziri wa Kilimo Mifugo na Uvuvi. Napenda kutumia fursa hii kumuahidi Mhe. Rais, Viongozi wangu wengine, Waheshimiwa Wabunge, Wakulima, Wafugaji, Wavuvi na Watanzania kwa ujumla kwamba nitatumia uwezo wangu wote kwa uaminifu na uadilifu kuhakikisha kuwa Sekta ya Kilimo inachangia kikamilifu katika kuinua pato la Mkulima, Mfugaji na Mvuvi na kuipeleka Tanzania kwenye uchumi wa kipato cha kati.

**3.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kumpongeza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuhimiza utunzaji wa mazingira ambayo ni muhimu katika maendeleo ya Sekta ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Nasi tunamuahidi kuwa katika shughuli zetu za kilimo, mifugo na uvuvi tutahakikisha utunzaji wa mazingira unakuwa ndio kipaumbele ili kuwa na kilimo endelevu.

**4.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kutumia fursa hii kumpongeza Mhe. Kassim Majaliwa, Majaliwa Mbunge wa Ruangwa kwa kuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha viongozi kuwajibika katika kuwatumikia wananchi kwa kuhakikisha wanatatua migogoro ya ardhi kati ya Wakulima na Wafugaji. Aidha, Mhe. Waziri Mkuu amekuwa mstari wa mbele kutembelea Bodi za Mazao, Kampuni ya Ranchi za Taifa na kutoa maelekezo kwa ajili ya kuleta ufanisi na kuimarisha utendaji katika Sekta za kilimo, mifugo na uvuvi.

**5.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa

kuliongoza vizuri Bunge letu Tukufu la 11. Ni imani yangu kuwa, mtaendelea kuliongoza Bunge kwa hekima, weledi mkubwa na kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo stahiki ili Bunge letu liweze kuisimamia na kuishauri Serikali.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** napenda pia kuwashukuru Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo Mifugo na Maji chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mbunge wa Hanang, kwa kuipokea na kuifanyia uchambuzi wa kina taarifa ya utekelezaji ya Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi ya mwaka 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mwaka 2017/2018 katika Kikao chake kilichofanyika mjini Dodoma tarehe 29 na 30 mwezi Machi 2017. Bajeti hii imezingatia maoni, ushauri na mapendekezo yaliyotolewa na Kamati hiyo. Aidha, napenda kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote wa kuchaguliwa na kuteuliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naahidi kushirikiana nao katika kuiletea nchi yetu maendeleo.

7. ***Mheshimiwa Spika,*** nawapongeza na kuwashukuru Wananchi wa Jimbo langu la Buchosa kwa kunichagua na kwa ushirikiano wanaoendelea kunipa katika kuwawakilisha hapa Bungeni. Aidha, nawapongeza kwa juhudi wanazofanya katika kujiletea maendeleo yao.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kwa mara nyingine tena kumpongeza Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), kwa hotuba yake ambayo imeelezea kwa muhtasari hali ya kilimo, mifugo na uvuvi ilivyo hivi sasa na mwelekeo kwa mwaka ujao. Aidha, nampongeza Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mhe. George Boniface Simbachawene na Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Dkt. Philip Isdory Mpango kwa hotuba zao zilizofafanua hali ya uchumi kwa mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2017/2018.

### *1.1 Hali ya Kilimo*

9. ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania imeendelea

kutegemea Sekta ya Kilimo katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi wake kwa kuwa inatoa ajira kwa asilimia 65.5 ya Watanzania na inachangia zaidi ya asilimia 100 ya chakula kinachopatikana nchini kwenye miaka yenye mvua za kutosha. Katika mwaka 2016 Sekta ya Kilimo ilichangia asilimia 29.1 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 29.0 mwaka 2015. Mchango mkubwa katika Pato la Taifa ulitokana na Sekta ya Kilimo, ikifuatiwa na Sekta nyingine za kiuchumi. Kwa kuwa asilimia kubwa ya Watanzania wanashiriki katika shughuli za kilimo, hivyo kilimo kinachangia kwa kiasi kikubwa kuongeza kipato na kupunguza umaskini.

**10.** ***Mheshimiwa Spika,*** ukuaji wa Sekta ya Kilimo kwa mwaka 2016 umepungua ukilinganishwa na mwaka 2015. Ukuaji kwa shughuli za kiuchumi za kilimo zinazojumuisha mazao, ufugaji, misitu na uvuvi ni asilimia 2.1 ukilinganisha na asilimia 2.3 ya mwaka 2015. Katika mwaka 2016, mchango wa mazao ni asilimia 1.4, mifugo asilimia 2.6, misitu asilimia 3.4 na uvuvi asilimia 4.2 ikilinganishwa na mazao asilimia 2.2, mifugo asilimia 2.4, misitu asilimia 2.6 na uvuvi asilimia 2.5 ya mwaka 2015.

**11.** ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya chakula katika mwaka 2016 ni tani milioni 16.2 ikiwa ni ongezeko la tani milioni 0.7(4.5%) ikilinganishwa na tani milioni 15.5 mwaka 2015. Uzalishaji wa mazao ya nafaka umeongezeka kutoka tani milioni 8.9 mwaka 2015 hadi tani milioni 9.5 mwaka 2016 ikiwa ni ongezeko la tani milioni 0.6 (6.7%). Aidha, uzalishaji wa mahindi umeongezeka kutoka tani milioni 5.9 mwaka 2015 hadi tani milioni 6.1 mwaka 2016 sawa na ongezeko la tani milioni 0.2 (3.4%). Uzalishaji wa mchele uliongezeka kutoka tani milioni 1.9 mwaka 2015 hadi tani milioni 2.2 mwaka 2016 sawa na ongezeko la tani milioni 0.3 (15.8%). Vilevile, uzalishaji wa mazao ya chakula yasiyo nafaka umeongezeka kufikia tani milioni 6.7 ikilinganishwa na tani milioni 6.6 kwa mwaka 2015 ikiwa ni sawa na ongezeko la tani milioni 0.1 (1.5%). Kwa ujumla uzalishaji wa mazao ya chakula ukilinganishwa na mahitaji ya tani milioni 13.2 ya chakula na matumizi mengineyo katika mwaka 2016/2017 unaonesha kuwepo kwa ziada ya tani milioni 3.0 za chakula.

Kutokana na hali hiyo Taifa limejitosheleza kwa chakula kwa asilimia 123 ambayo ni ongezeko la asilimia 3 ikilinganishwa na asilimia 120 mwaka 2015.

#### *1.1.1 Uzalishaji wa Mazao ya Biashara*

**12.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika msimu wa mwaka 2016/ 2017 uzalishaji wa mazao makuu ya asili ya biashara ambayo ni Korosho, Miwa ya Sukari, Pamba, Mkonge, Kahawa, Chai, Tumbaku na Pareto umepungua na kuongezeka kwa viwango tofauti ingawa uzalishaji wa jumla kwa mazao hayo umeongezeka kufikia tani 881,583 ikilinganishwa na tani 796,502 mwaka 2015/2016. Uzalishaji unaoendelea kwa mwaka 2016/2017 na matarajio kwa mwaka 2017/2018 ni kuzalisha jumla ya tani 953,825 ya mazao hayo kama ilivyooneshwa katika Jedwali Na. 3.

**13.** ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya bustani ambayo ni matunda, mboga, maua na viungo umeongezeka kutoka tani 5,931,906 mwaka 2015/2016 hadi tani 6,216,145 mwaka 2016/2017. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa matunda na mboga yakiwemo parachichi, Nyanya na matikiti. Wizara imeendelea kushirikiana na Taasisi ya mbalimbali kuhamasisha uzalishaji wa Matunda, Mboga, Maua na Viungo pamoja na ulaji wake.

**14.** ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mbegu za mafuta za Alizeti, Karanga, Ufuta, Mawese na Soya umeongezeka kutoka tani 6,301,147 za mwaka 2015/2016 hadi tani 6,667,893 mwaka 2016/2017. Kuongezeka kwa uzalishaji kumechangiwa na kuongezeka kwa hamasa kwa wakulima kutokana na uwepo wa soko la uhakika, ongezeko la matumzi ya mafuta hayi hapa nchini, ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi pamoja na uwekezaji katika viwanda vidogo na vya kati katika mikoa ya Manyara, Singida, Dodoma, Mbeya, Katavi, Lindi, Mtwara, Iringa, Njombe, Rukwa na Kigoma.

### *1.1.2 Uzalishaji wa Mazao ya Chakula 2015/2016 na Upatikanaji wa Chakula 2016/2017*

**15.** ***Mheshimiwa Spika,*** tathmini ya awali ya hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula nchini kwa msimu wa 2015/ 2016 na upatikanaji wa chakula 2016/2017 iliyofanyika mwezi Julai 2016 ilibainisha kuwa uzalishaji wa mazao ya chakula utafikia **tani 16,172,841** za chakula na mahitaji ya chakula kwa mwaka 2016/17 ni **tani 13,159,326,** na hivyo nchi kuwa na ziada ya chakula **tani 3,013,515.** Kati ya ziada hiyo, **tani 1,101,341** ni za mazao ya nafaka na **tani 1,912,174** ni za mazao yasiyo nafaka. Nchi ilikuwa na kiwango cha utoshelevu wa kiwango cha **asilimia 123** ikilinganishwa na kiwango cha utoshelevu cha **asilimia 120** kwa mwaka 2015/2016. Aidha**,** tathmini ya kina ya hali ya chakula na lishe iliyofanyika mwezi Februari 2017 ilibainisha pia kuwa hali ya upatikanaji wa chakula bado ilikuwa ni ya kuridhisha pamoja na kuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula hapa nchini uliochangiwa na kuchelewa kunyesha kwa mvua za vuli na msimu pamoja na ukame uliojitokeza. Wizara kwa kushirikiana na Mikoa imehamasisha Wafanyabiashara kusambaza chakula katika Halmashauri zilizobainishwa kuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula ili kuwezesha upatikanaji wa chakula katika maeneo hayo.

**16.** ***Mheshimiwa Spika,*** aidha**,** tathmini ya kina ya hali ya chakula na lishe iliyofanyika mwezi Februari 2017 ilibainisha pia kuwa hali ya upatikanaji wa chakula bado ilikuwa ni ya kuridhisha pamoja na kuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula hapa nchini. Tathmini ilibainisha kuwa jumla ya **tani 35,491** za chakula zilihitajika ili kukabiliana na hali ya upungufu wa chakula na lishe kati ya mwezi Februari hadi Aprili 2017 kwa **watu 1,186,028** walioainishwa kuwa wana upungufu wa chakula katika Halmashauri 55 uliochangiwa na kuchelewa kunyesha kwa mvua za vuli na ukame uliojitokeza. Wizara kwa kushirikiana na Mikoa imehamasisha Wafanyabiashara kusambaza chakula katika Halmashauri zilizobainishwa kuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula ili kuwezesha upatikanaji wa chakula katika maeneo hayoawali.

**17.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na hali ya ukame uliojitokeza katika baadhi ya maeneo yakiwamo ya Halmashauri zilizobainishwa kuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula, jumla ya tani 1,969 za mbegu bora za Mahindi na Mtama zinazokomaa kwa muda mfupi na kustahimili ukame zilihitajika. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 Wizara kupitia Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA), Makampuni Binafsi na Mawakala wa Pembejeo walisambaza tani 377.4 za mbegu za Mahindi, tani 100 za Mtama na tani 20 za Mpunga katika maeneo hayo. Vilevile, Wizara kupitia Vituo vya Utafiti vya Kanda imesambaza jumla ya vipando 14,252,000 zikiwemo pingili 12,772,000 za Muhogo na 1,480,000 za Viazi vitamu.

**18.** ***Mheshimiwa Spika,*** taarifa ya Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA), ilionyesha kuwa katika kipindi cha mwezi Machi hadi Mei, 2017 mvua zilitarajiwa kuwa za wastani katika maeneo mengi ya nchi. Kutokana na mwelekeo huu wa mvua, mazao yaliyoko mashambani katika mikoa inayopata mvua za msimu yanatarajiwa kutoa mavuno ya kuridhisha. Aidha, kwa upande wa mikoa iliyokosa mvua za vuli wakulima walipanda mazao na yako katika hatua mbali mbali za ukuaji. Kwa ujumla mwenendo wa unyeshaji wa mvua katika maeneo mengi ya nchi ni wa kuridhisha na inatarajiwa kuwa na mavuno mazuri. Wizara kwa kushirikiana na Mikoa inaendelea na juhudi za kuhamasisha wananchi kupanda mazao yanayokomaa mapema na kustahimili ukame na kutumia vizuri mvua zinazoendelea kunyesha.

**19.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kwa mwaka wa fedha 2016/2017 umepanga kununua jumla ya tani 100,000 za chakula. Hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2017, Wakala umenunua jumla ya tani 62,099.319 za mahindi sawa na asilimia 62 ya lengo ililojiwekea. Aidha, akiba ya chakula hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2017 ni tani 86,443.773.

**20.** ***Mheshimiwa Spika,*** usalama wa chakula nchini,unahusisha kuiwezesha nchi kuwa na utoshelevu wa chakula kupitia uzalishaji wa mazao ya chakula. Aidha,

kutokana na hali ya mwenendo wa mvua kwa msimu wa kilimo 2016/2017 na upatikanaji wa chakula nchini iliyojitokeza ikiwa ni pamoja na upandaji wa bei ya mazao hususan mahindi na kupelekea baadhi ya vyombo vya habari pamoja na viongozi wa kisiasa kutoa taarifa za uwepo wa njaa na kuishinikiza Serikali kutangaza baa la njaa.

**21.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na hali hiyo Serikali imeona ni vyema kutoa ufafanuzi wa hatua za kupitia ili nchi iweze kutangaza baa la njaa. Kabla ya kutangaza baa la njaa tathmini ya kina ya hali ya chakula na lishe hufanyika ili kubaini hali ya usalama wa chakula. Katika kufanya tathmini hii hatua tano (5) zinapaswa kuzingatiwa ili kuweza kutangaza baa la njaa. Hatua hizi ni pamoja na; (i) Hali ya kujitosheleza kwa chakula (*Minimal-generally food secure*) ambapo nchi ina uhakika wa upatikanaji wa chakula cha kutosha, (ii) Upungufu wa chakula wa wastani (*Stress-moderately food insecure*) ambapo upatikanaji wa chakula upo katika kiwango cha wastani, (iii) Upungufu mkubwa wa chakula (*Crisis*) unaosababisha kiwango cha juu cha utapiamlo, (iv) dharura za kibinadamu (*Humanitarian emergency*) hatua inayohusisha upungufu mkubwa wa chakula na kiwango cha juu cha utapiamlo na vifo kutoka na njaa, (v) Baa la Njaa (*Famine/ Humanitarian Catastrophe*) unaotokana na ukosefu kabisa wa chakula na mahitaji mengine na watu wengi kukabiliwa na njaa, vifo na watu wengine kuhamia maeneo mengine.

**22.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na ufafanuzi huu, na kwa kuzingatia tathmini ya hali ya chakula na lishe iliyofanyika mwezi Februari, 2017 ilibainisha kuwa hali ya chakula na lishe katika maeneo yaliyokuwa na upungufu wa chakula yalikuwa katika hatua ya pili yaani Upungufu wa chakula wa wastani (*Stress*) ambapo upatikanaji wa chakula upo katika kiwango cha wastani. Hivyo serikali haikuona umuhimu wa kutangaza baa la njaa nchini. Lakini ikumbukwe kwamba kutokana na Ibara ya 32 (2) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania 1977, inampa mamlaka Mheshimiwa Rais ya kutangaza hali ya hatari kutokana na baa la njaa na kutambua kwamba ili kukabiliana na baa la

njaa Taifa litachukua hatua za dharura ikiwa ni pamoja na kuelekeza rasilimali fedha kukabiliana na baa hilo.

### *1.2 Hali ya Mifugo*

**23.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2016/2017, idadi ya mifugo nchini inafikia ng'ombe milioni 28.44, mbuzi milioni 16.67 na kondoo milioni 5.01 (**Kiambatisho Na. 1**). Pia, wapo kuku wa asili milioni 37.43, kuku wa kisasa milioni 34.5, nguruwe milioni 1.85 na punda wapatao 572,357 (*Tanzania Livestock Master Plan 2016 – TLMP*).

**24.** ***Mheshimiwa Spika*,** viwango vya ulaji wa mazao ya mifugo nchini bado viko chini. Kwa mfano, ulaji wa nyama ni wastani wa kilo 15, lita 47 za maziwa na mayai 106 kwa mtu kwa mwaka ukilinganisha na viwango vya Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO, 2011) ambavyo ni kilo 50 za nyama, lita 200 za maziwa na mayai 300 kwa mtu kwa mwaka.

**25.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2016/2017, uzalishaji wa maziwa umepungua kwa asilimia 2.3 kutoka lita bilioni 2.14 mwaka 2015/2016 hadi bilioni 2.09. Kupungua kwa kiwango cha uzalishaji kumetokana na upungufu wa malisho katika maeneo mengi ya nchi kulikosababishwa na ukame wa muda mrefu. Hali hii imeendelea kuathiri viwanda vya kusindika maziwa hivyo kuendelea kuzalisha chini ya uwezo wake. Sambamba na hali hiyo, kiwango cha usindikaji kimepungua kutoka lita milioni 61.18 kwenye viwanda 75 mwaka 2015/2016 kufikia lita milioni 40.13 kwenye viwanda 65 vinavyofanya kazi kwa mwaka 2016/2017.

**26.** ***Mheshimiwa Spika*,** jumla ya mitamba 634 ilizalishwa kutoka mashamba ya Serikali na Kampuni ya Ranchi za Taifa - NARCO ikilinganishwa na mitamba 646 iliyozalishwa mwaka 2015/2016. Aidha, jumla ya mitamba 10,820 ilizalishwa na Sekta binafsi na kusambazwa kwa wafugaji wadogo nchini ikilinganishwa na mitamba 10,803 iliyozalishwa mwaka 2015/2016. Vituo vya Kanda vimeendelea kuimarishwa kwa kupatiwa vitendeakazi na ukarabati wa

miundombinu na mitambo ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya uhimilishaji wakati wote. Jumla ya dozi 100,000 za mbegu bora za mifugo zilizalishwa ikilinganishwa na dozi 80,000 mwaka 2015/2016. Pia, ng'ombe waliohimilishwa wameongezeka kutoka 221,390 mwaka 2015/2016 hadi ng'ombe 457,557 mwaka 2016/2017.

**27.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/2017, uzalishaji wa nyama umepungua kutoka tani 648,810 (ng'ombe 323,775; mbuzi na kondoo tani 129,292; nguruwe tani 91,451; na kuku tani 104,292) mwaka 2015/2016 hadi tani 558,164 (ng'ombe tani 394,604; mbuzi tani 61,109, kondoo tani 19,955, nguruwe tani 18,899 na kuku tani 63,597). Aidha, mfumo wa unenepeshaji mifugo umeendelea kuhamasishwa ambapo ng'ombe walionenepeshwa kwenye mashamba na Wafugaji waliosajiliwa wameongezeka kwa asilimia 12.9 kutoka ng'ombe 221,390 mwaka 2015/2016 hadi ng'ombe 250,000 mwaka 2016/2017.

**28.** ***Mheshimiwa Spika,*** idadi ya mifugo iliyouzwa minadani imeongezeka kutoka ng'ombe 1,470,805 mbuzi 1,161,840 na kondoo 253,243 wenye thamani ya shilingi bilioni 976.474 mwaka 2015/2016 hadi kufikia ng'ombe 1,618,047 wenye thamani ya shilingi trilioni 1.34, mbuzi 1,278,182 na kondoo 278,595 wenye jumla ya thamani ya shilingi trilioni 1.02 mwaka 2016/2017. Aidha, hadi kufikia Machi 2017 jumla ya tani 3,162.65 za nyama ziliuzwa nje ya nchi katika nchi za Dubai, Iraq na Vietnam ikijumuisha tani 711.82 za nyama ya mbuzi, tani 439.03 za nyama ya ng'ombe, tani 222.74 za nyama ya kondoo na tani 1,789.06 za nyama ya punda.

**29.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2016/2017 vipande vya ngozi zilizosindikwa vimepungua kutoka vipande vya ngozi za ng'ombe 1,575,139 vyenye thamani ya shilingi bilioni 45.0 mwaka 2015/2016 hadi vipande 1,215,030 vyenye thamani ya shilingi bilioni 34.7. Pia, katika mwaka 2016/2017 vipande vya ngozi za mbuzi/kondoo 928,115 vyenye thamani ya shilingi bilioni 6.2 vilivyosindikwa vimepungua ikilinganishwa na vipande 1,124,000 vyenye thamani ya shilingi bilioni 7.5. Aidha, ngozi ghafi za ng'ombe vipande 241,773 vyenye

thamani ya shilingi bilioni 1.89 viliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na vipande 187,000 vya ngozi za ng'ombe vyenye thamani ya shilingi bilioni 2.4 mwaka 2015/2016.

**30.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, jumla ya marobota ya hei 456,016 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.14 yamezalishwa kutoka mashamba ya Serikali ya kuzalisha malisho na marobota 684,230 yamezalishwa kutoka mashamba ya sekta binafsi yenye thamani ya shilingi bilioni 2.05 na kuuzwa kwa wadau. Aidha, mbegu za malisho bora za nyasi kilo 3,717.1 zenye thamani ya shilingi milioni 55.8 na jamii ya mikunde kilo 731.5 zenye thamani ya shilingi milioni 11.0 zimezalishwa kutoka mashamba ya Serikali na kuuzwa kwa wadau mbalimbali ikilinganishwa na tani 49.96 za mbegu bora za malisho zenye thamani ya shilingi milioni 749.4 na marobota ya hei 544,650 yenye thamani ya shilingi bilioni 1.36 yaliyozalishwa kutoka mashamba ya Serikali mwaka 2015/2016.

### *1.3 Hali ya Uvuvi*

**31.** ***Mheshimiwa Spika,*** nchi yetu imejaliwa kuwa na maeneo mengi ya maji ambayo ni muhimu katika shughuli za uvuvi ambazo huwapatia wananchi lishe, kipato na ajira. Maeneo hayo hujumuisha eneo la maji baridi na maji bahari. Eneo la maji baridi hujumuisha maziwa makuu matatu ambayo ni Ziwa Victoria (35,088 km2), Ziwa Tanganyika (13,489 km2) na Ziwa Nyasa (5,700 km2), maziwa ya kati na madogo 45, mito 29, mabwawa ya asili na ya kuchimbwa pamoja na maeneo oevu. Aidha, kwa upande wa maji bahari, nchi yetu ina Ukanda wa Pwani wa Bahari ya Hindi wenye urefu wa kilometa 1,424 ambao umegawanyika katika eneo la Maji ya Kitaifa (*Territorial Sea*) lenye ukubwa wa kilometa za mraba 64,000 na eneo la Ukanda wa Uchumi wa Bahari (*Exclusive Economic Zone-EEZ*) lenye ukubwa wa kilometa za mraba 223,000. Katika maeneo haya kuna rasilimali nyingi za uvuvi ambamo shughuli za uvuvi hufanyika. Aidha, maji hayo yanaweza kutumika katika ufugaji wa samaki na viumbe wengine. Pia, taarifa za utafiti zilizofanyika kwa vipindi tofauti zinaonesha kwamba, kiasi cha samaki kilichopo katika

maziwa makubwa ni takriban tani 2,914,296 (Ziwa Victoria tani 2,451,296, Ziwa Tanganyika tani 295,000 na Ziwa Nyasa tani 168,000).

**32.** ***Mheshimiwa Spika,*** shughuli za uvuvi hufanywa na wavuvi wadogo kwenye maji baridi na ya Kitaifa katika Ukanda wa Bahari ya Hindi na huchangia takriban asilimia 95 ya samaki wote wanaozalishwa nchini. Uvuvi wa kibiashara katika Bahari Kuu hufanywa na meli kubwa kutoka nchi za kigeni. Katika mwaka 2016/2017, jumla ya wavuvi wadogo 203,529 wanaotumia vyombo vya uvuvi 59,338 walijihusisha moja kwa moja na shughuli za uvuvi na kuwezesha kuvunwa kwa tani 362,595 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.49 za samaki **(Kiambatisho Na.2a na 2b).** Vilevile, zaidi ya watu milioni nne wameendelea kunufaika na Sekta ya uvuvi zikiwemo uchakataji wa samaki, utengenezaji wa zana na vyombo vya uvuvi, biashara ndogondogo na mama lishe. Aidha, idadi ya wavuvi imeendelea kuongezeka wakati kiasi cha samaki kinachovunwa kimeendelea kushuka mwaka hadi mwaka kutokana na uvuvi haramu, matumizi ya zana duni na matumizi kidogo ya teknolojia zenye tija. Hali hiyo imejidhihirisha kuanzia mwaka 2013 ambapo kumekuwa na ongezeko la asilimia 10.96 ikilinganishwa na idadi ya wavuvi mwaka 2016, wakati uvunaji wa samaki umeonekana kupungua kwa asilimia 3.35 katika kipindi husika.

**33.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kusimamia sheria, kutoa mafunzo na kudhibiti uvuvi haramu kwa ajili ya uvuvi endelevu; kuhamasisha ukuzaji viumbe kwenye maji na kuwezesha na kuratibu upatikanaji wa vifaranga bora vya samaki, kuimarisha vituo vitano (5) na kuanzisha kituo cha ugani cha ufugaji samaki mkoani Simiyu. Aidha, sekta binafsi imeanzisha vituo vitano (5) vya ukuzaji viumbe kwenye maji na kufikia vituo 13. Vilevile, mabwawa ya samaki yameongezeka na kufikia 22,702 mwaka 2016/2017 ikilinganishwa na mabwawa 22,545 mwaka 2015/2016 ambayo imewezesha kuongezeka kwa uzalishaji wa samaki kwenye mabwawa kutoka wastani wa tani 3,613.55 mwaka 2015/2016 hadi tani 11,000 mwaka 2016/2017. Vilevile, Wizara

imeendelea kusimamia uvuvi katika Bahari Kuu na ukuzaji viumbe kwenye maji ikiwa ni mkakati wa kuongeza uzalishaji wa samaki. Katika Mwaka 2016/2017, jumla ya leseni 96 za uvuvi zilitolewa kwa meli 27 za kigeni kutoka mataifa ya China, Hispania, Taiwan, Ufaransa, Shelisheli na Mauritania zinazovua katika Bahari Kuu zikiwa na thamani ya shilingi 968,591,643. Katika mwaka 2016/2017, jumla ya tani 39,691.5 za samaki na mazao ya uvuvi yenye thamani ya shilingi bilioni 526.99 yaliuzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa jumla ya shilingi bilioni 14.30 ikiwa ni ushuru (**Kiambatisho Na. 3a na 3b**). Pia, tani 12,743.96 za samaki kutoka nje ya nchi zilihakikiwa na kuruhusiwa kuingizwa nchini kwa ajili ya soko la ndani na kuliingizia Taifa jumla ya shilingi bilioni 10.1 ikiwa ni ushuru.

### *1.4 Hali ya Ushirika*

**34.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuimarisha Ushirika katika sekta mbalimbali zikiwemo kilimo, ufugaji, uvuvi, madini, viwanda, nyumba na fedha (SACCOS na Benki). Maeneo yaliyofanyiwa kazi ni pamoja Kuijengea uwezo Tume ya Maendeleo ya Ushirika kutekeleza majukumu yake; Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa Vyama vya Ushirika; Kusimamia misingi ya utawala bora na uwajibikaji katika Vyama vya Ushirika; Kuhamasisha maendeleo ya ushirika katika Sekta mbalimbali; Kuvijengea uwezo wa kiushindani Vyama vya Ushirika katika utafutaji wa masoko ya mazao yao; Kuimarisha teknolojia ya habari na mawasiliano; Kufanya tafiti, mafunzo na kuboresha mifumo ya upatikanaji na utoaji wa taarifa.

**35.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika imeendelea kufanya uhakiki ili kubaini uhai wa Vyama vya Ushirika na kuhamasisha wananchi kuanzisha na kujiunga na Vyama vya Ushirika ambapo hadi kufikia Machi, 2017 idadi ya vyama imefikia 10,596 na wanachama wameongezeka kutoka 1,432,978 hadi kufikia 2,234,016 sawa na ongezeko la asilimia 55.91**(Kiambatisho Na. 4)** Aidha, jumla ya Vyama vipya vya Ushirika 101 vimeanzishwa vikiwemo vya ushirika wa akiba na mikopo (SACCOS) 51, kilimo na Masoko (AMCOS) 21, madini 13,

viwanda 1, huduma mbalimbali 8, umwagiliaji 1 na ufugaji 6. Ushirika wa Akiba na Mikopo umeendelea kutoa huduma za kifedha ambapo thamani ya hisa, akiba na amana zimeongezeka kutoka Sh. bilioni 378 mwaka 2015 na kufikia Sh. Bilioni 378.34 mwaka 2016 sawa na ongezeko la asilimia 0.1. Aidha, thamani ya mikopo iliyotolewa kwa wanachama iliongezeka kufikia Shilingi bilioni 855.29 mwaka 2016 kutoka Shilingi bilioni 854.34 mwaka 2015.

**36.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhimiza matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Mfumo huu umesaidia kupanda kwa bei ya korosho na mapato kwa wakulima kupitia vyama vikuu vya ushirika vya TANECU, MAMCU, RUNALI, Lindi Mwambao, TAMCU na CORECU. Katika msimu wa 2016/17 vyama hivyo viliuza korosho na kuwalipa wakulima jumla ya Shilingi bilioni 809.18 ikilinganishwa na malipo ya Shilingi bilioni 293.09 msimu wa 2015/16. Aidha, kwa zao la kahawa vyama vimekusanya na kuuza kahawa yenye thamani ya shilingi bilioni 296.47 sawa na asilimia 27 ya mauzo yote ya kahawa.

**37.** ***Mheshimiwa Spika,*** wanachama wa vyama vya ushirika wameendelea kuhamasishwa kujiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii ukiwemo NSSF ambapo kupitia "Wakulima Scheme" idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika waliojiunga na mfuko imeongezeka kutoka 78,747 mwaka 2015 hadi 90,047 mwaka 2016.

## 2.0 MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA KIPINDI CHA MWAKA 2016/2017

### FUNGU 43: KILIMO

### *Makusanyo ya Maduhuli*

**38.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi kwa mwaka 2016/2017 ilikadiria kukusanya mapato ya Shilingi **4,017,010,000** kupitia Fungu 43, kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2017 Wizara ilikusanya jumla ya Shilingi **3,299,773,587.22** sawa na asilimia

**82.15** ya makadirio na Wizara inaendelea kukusanya maduhuli hayo.

***Fedha Zilizoidhinishwa***

**39.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi kupitia Fungu 43 ilitengewa jumla ya Shilingi **210,359,133,000**. Kati ya Fedha hizo, Shilingi **109,831,636,000** ni Fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi **100,527,497,000** ni Fedha za maendeleo.

***Matumizi ya Bajeti ya Kawaida***

**40.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Fungu 43 lilitengewa jumla ya Shilingi **109,831,636,000**. Aidha, Wizara ilipokea kiasi cha Shilingi **3,337,655,152.20** kwa ajili ya kulipia madeni ya watumishi, wazabuni na wakandarasi wa maghala na skimu za umwagiliaji na kufanya fedha zilizoidhinishwa kuongezeka hadi kufikia Shilingi **113,169,291,152.** Hivyo, kati ya fedha hizo Shilingi **43,417,238,000** ni kwa ajili ya mishahara ya Watumishi wa Wizara na Bodi/ Taasisi, na Shilingi **69,752,053,153** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Kati ya fedha za matumizi mengineyo, Jumla ya Shilingi **15,000,000,000** ni kwa ajili ya ununuzi wa nafaka, Shilingi **20,000,000,000** kwa ajili ya ruzuku ya mbolea, Shilingi **15,220,520,000** Ruzuku kwa Mashirika ya Ndani, Shilingi **3,500,000,000** kwa ajili ya Chakula cha Wanafunzi, Shilingi **5,000,000,000** ruzuku ya Madawa ya Viuatilifu na Shilingi **11,031,533,153** ni kwa ajili ya matumizi ya Idara, Vitengo na Vituo vya Wizara.

**41.** ***Mheshimiwa Spika,*** hadi kufikia tarehe 04, Mei 2017 jumla ya Shilingi **61,702,709,784** za matumizi ya kawaida zimetolewa sawa na asilimia **54.52** ya fedha zilizoidhinishwa. Aidha, fedha zilizotumika ni Shilingi **59,056,706,476** sawa na asilimia **95.09** ya fedha zilizotolewa. Kati ya fedha hizo Shilingi **32,339,782,582** ni mishahara ya Fungu 43 na Bodi /Taasisi na Shilingi **26,716,923,894** ni matumizi mengineyo.

***Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo***

**42.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa 2016/2017, Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi ilitengewa jumla ya Shilingi **100,527,497,000** kupitia Fungu 43 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Aidha, Wizara ilipokea fedha kwa ajili ya kulipia madeni ya wakandarasi wa skimu za umwagiliaji na kufanya fedha zilizoidhinishwa kuongezeka hadi kufikia Shilingi **101,527,497,000**. Hivyo, kati ya fedha hizo, Shilingi **23,000,000,000** ni Fedha za ndani na Shilingi **78,527,497,000** ni Fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 04, Mei 2017 Shilingi **3,369,416,666** zimetolewa sawa na asilimia **3.31** ya Fedha zilizoidhinishwa. Matumizi ni Shilingi **2,877,137,820** sawa na asilimia **85.39** ya Fedha zilizotolewa. Kati ya Fedha hizo Shilingi **1,806,022,404** ni Fedha za ndani na Shilingi **1,071,115,416** ni Fedha za nje.

**FUNGU 99: MIFUGO**

***Makusanyo ya Maduhuli***

**43.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara kwa upande wa Idara Kuu za Mifugo na Uvuvi ilitarajia kukusanya kiasi cha shilingi **35,191,332,382.00.** Hadi kufikia mwezi Aprili 2017, kiasi cha shilingi **26,972,495,687** kimekusanywa na Wizara ikiwa ni sawa na asilimia **77** ya lengo la makusanyo. Kati ya hizo Shilingi 10,952,827,500 ni za Sekta ya Mifugo na Shilingi 16,019,668,687 za Sekta ya Uvuvi.

***Fedha Zilizoidhinishwa***

**44.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017 Wizara kupitia Idara Kuu za Mifugo na Uvuvi imetengewa kutumia jumla ya shilingi **60,013,252,440.56**. Kati ya kiasi hiki, shilingi **44,140,037,440.56** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi **15,873,215,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

***Matumizi ya Bajeti ya Kawaida***

**45.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017 Wizara kupitia Fungu 99: Mifugo na Uvuvi ilitengewa kiasi cha shilingi

**44,140,037,440.56** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya hizo, shilingi **22,260,324,000** ni za mishahara na shilingi **21,879,713,440.36** ni za Matumizi Mengineyo. Hadi kufikia mwezi Aprili 2017, jumla ya shilingi **29,845,921,489.56** zimetolewa, sawa na asilimia **68** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kati ya shilingi **44,140,037,440.36** zilizotengwa. Kati ya hizo, shilingi **21,915,681,063** ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi wa Wizara (PE) na shilingi **7,930,240,426.56** ni kwa ajili ya Matumizi Mengine (OC).

***Matumizi ya Bajeti ya Maendeleo***

**46.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka wa 2016/2017, Wizara kupitia Fungu 99: Mifugo na Uvuvi ilitengewa kiasi cha shilingi **15,873,215,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kati ya hizo, shilingi **8,000,000,000 (50.4%)** ni fedha za ndani na shilingi **7,873,215,000 (49.60%)** ni fedha za nje. Programu zilizotekelezwa ni Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II); na Mradi wa South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth – SWIOFish. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017, kiasi cha shilingi **1,252,230,662.49** (**12.3%**) ya bajeti iliyoidhinshwa ya shilingi **15,873,215,000** kimetolewa. Kati ya hizo, fedha za ndani ni shilingi **280,000,000** (**4**%) na fedha za nje ni shilingi **972,230,662.49** (**12.3%**).

**FUNGU 24: USHIRIKA**

***Fedha Zilizoidhinishwa***

**47.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha wa 2016/2017, Wizara kupitia Fungu 24 ilitengewa jumla ya Shilingi **4,894,921,000**. Ukomo wa Bajeti ya Fungu 24 umeongezeka kwa kiasi cha Shilingi **175,387,754.68** zilizotolewa na Hazina kwa ajili ya malipo ya madeni ya watumishi wa Tume na hivyo kufikia Ukomo wa Shilingi **5,070,308,754.68**.

**48.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika fedha hizo, Shilingi **1,616,345,000** ni fedha za matumizi mengineyo ambapo Shilingi **644,507,000** ni za Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Shilingi **971,838,000** ruzuku ya ndani kwa COASCO. Jumla ya

Shilingi **3,278,576,000** zilitengwa kwa ajili ya mishahara ambapo Shilingi **1,833,182,000** ni mishahara ya watumishi wa Tume na Shilingi **1,445,394,000** ni kwa ajili ya COASCO. Aidha, katika mwaka 2016/2017, Tume ya Maendeleo ya Ushirika haikutengewa fedha za bajeti ya matumizi ya maendeleo.

***Matumizi ya Bajeti ya Kawaida***

***Mheshimiwa Spika,*** hadi tarehe 30 Aprili, 2017 fedha za matumizi ya kawaida zilizopokelewa kutoka Hazina ni Shilingi **3,425,573,146.45** sawa na asilimia **67.6** ya kiasi kilichoidhinishwa. Matumizi yaliyofanyika ni Shilingi **3,423,928,837.53** sawa na asilimia **99.9** ya kiasi cha fedha kilichotolewa.

## 3.0 UTEKELEZAJI WA MAENEO YA VIPAUMBELE KWA MWAKA 2016/2017 NA MPANGO WA MWAKA 2017/2018

### FUNGU 43

**49.** ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2016/2017, umezingatia malengo ya Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/2017 – 2020/2021); Malengo Endelevu ya Maendeleo (*Sustainable Development Goals - SDGs*); *Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan (TAFSIP)*; na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 - 2020. Malengo hayo yalitekelezwa kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Development Program – ASDP* ), na Mpango wa Kukuza Kilimo katika Ukanda wa Kusini mwa Tanzania *(Southern Agricultural Growth Corridor of Tanzania – SAGCOT)*. Maeneo mengine yaliyozingatiwa ni pamoja na masuala mtambuka yakiwemo Jinsia, Mazingira, Mabadiliko ya Tabianchi, UKIMWI na Ajira ya Watoto katika Sekta ya Kilimo.

**50.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kufanikisha majukumu yake, Wizara imetekeleza Maeneo ya Kipaumbele tisa (9) kupitia Fungu 43 katika Idara, Vitengo, Asasi na Taasisi za Wizara. Maeneo ya kipaumbele yaliyotekelezwa ni kama ifuatavyo:

(i) Kuboresha Mfumo wa Utafiti na Utoaji wa Matokeo ya Utafiti kwa Wadau;

(ii) Kuimarisha usimamizi kabla na baada ya mavuno na kuongeza upatikanaji wa masoko;

(iii) Kuimarisha upatikanaji na utumiaji wa pembejeo, zana za kilimo na huduma za udhibiti;

(iv) Kuimarisha mafunzo ya kilimo na huduma za ugani;

(v) Kuongeza ushiriki wa Vijana katika Kilimo;

(vi) Kuratibu na kuboresha matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo kwa kutenga, kupima na kumilikisha maeneo hayo kwa wakulima;

(vii) Kuunda na kupitia Sera, Mikakati na Mifumo ya kisheria katika Sekta ndogo ya mazao;

(viii) Kuwezesha uwekezaji wa Sekta binafsi katika kilimo;

(ix) Kuimarisha uratibu, ufuatiliaji na tathmini katika Sekta ya kilimo;

### *3.1 Kuboresha Mfumo wa Utafiti na Utoaji wa Matokeo ya Utafiti kwa Wadau*

**51.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Vituo vya Utafiti na kwa kushirikiana na Taasisi Binafsi za kilimo imegundua na kuidhinisha mbegu bora mpya 35 (21 Wizara na 14 Taasisi Binafsi) za mazao ya Maharage, Viazi vitamu, Mahindi, Korosho na Viazi mviringo (**Kiambatisho Na. 5)**. Aidha, Wizara imezalisha Mbegu mama na za awali (*Breeder and Pre-basic seeds*) za mazao mbalimbali za msimu 2015/2016. Mbegu mama zilizozalishwa ni: Pamba kilo 2,600 na Viazi mviringo miche 60,000. Mbegu za awali zilizozalishwa ni: Pamba kilo 21,600; Muhogo pingili 2,008,000; Viazi vitamu vipando 3,476,750; Viazi mviringo kilo 5,150; Mpunga kilo 2,940; Mahindi kilo 11,300; Ngano kilo 1,560; Soya kilo1,900; Maharage kilo 43,900; Migomba miche 1,830 na Parachichi miche 3,390.

Pia vizazi (*germplasm*) 1,228 vya mbegu za Mpunga na 172 vya Ulezi vilikusanywa na kutunzwa Vituoni. Ororodha ya aina ya mbegu na za awali zilizozalishwa ni kama zinavyoonekana kwenye (**Kiambatisho Na.6).**

**52.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri imeendelea kutoa elimu kwa wakulima wa Kanda ya Kaskazini kuhusu ugonjwa mpya wa Mahindi (*Maize Necrosis Lethal Disease-MNLD*) na dalili zake. Takribani wakulima 3,000 wa Kanda ya Kaskazini wana ufahamu kuhusu ugonjwa wa MNLD na dalili zake kupitia semina zilizofanyika kila wilaya na matangazo ya redio na runinga. Pia, Wizara imeendelea kushirikiana na Tume ya Sayansi na Teknolojia na CIMMYT kufanya utafiti na wanatarajia kutoa aina 10 za mbegu zinazoonyesha kustahimili ugonjwa huo, zikishapitishwa zitapelekwa kwa wadau wa kilimo.

**53.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na utafiti wa zao la mpunga, ambapo matokeo yameonesha kuwa, mkulima akitumia mbegu bora za mpunga kwenye kilimo shadidi huongeza mavuno mara tatu zaidi ya mkulima aliyetumia mbegu za asili. Pia, utafiti umethibitisha kuwa mkulima aliyetumia mbegu bora za Mpunga katika kilimo shadidi alipata faida ya Shilingi 1,126,500 kwa hekta ambayo ni mara saba zaidi ya mkulima aliyetumia mbegu za asili. Hata hivyo, uzoefu wa utekelezaji wa Kilimo Shadidi katika maeneo mbalimbali ya nchi yameonesha kuwa, kilimo hicho kimeongeza mavuno mara mbili kutoka magunia kati ya 15-20 kwa ekari hadi 30-40 kwa ekari.

**54.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, Wizara imeendelea na utafiti wa kuboresha Rutuba ya Udongo kwa kutumia Udhibiti Husishi (*Intergrated Soil Fertility Management – ISFM*). Utafiti huo umethibitisha kuongezeka kwa mavuno ya Pamba kutoka wastani wa kilo 728 hadi kilo 985 kwa misimu 3 kwa hekta katika maeneo ya Ukiriguru, Mkanza, Ipililo-Maswa na Mwamishali-Meatu. Wastani wa nyongeza kwa mashamba ya majaribio kituoni ilikuwa asilimia 18 na kwa mashamba ya wakulima ni asilimia 12.

**55.** ***Mheshimiwa Spika,*** Muswada wa kuunda Sheria ya kuanzishwa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo (TARI) uliwasilishwa na kupitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Muswada huo ulisainiwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Septemba 23, 2016. Vilevile, Waziri mwenye dhamana alisaini *notice* ya kuridhia kuanzishwa kwa TARI Januari 20, 2017.

**56.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itakamilisha Muundo wa Taasisi na wa Utumishi pamoja na kanuni zitakazofafanua utekelezaji wa sheria iliyoanzisha Taasisi ya Utafiti (TARI). Pia kupitia Programu ya ASDP II Wizara itakarabati na kuvipatia vifaa muhimu vya kufanyia utafiti vituo 7 vya Utafiti nchini ili viweze kuendesha utafiti kwa mazao ya kipaumbele katika mnyororo wa thamani (CVCs) na kukarabati Kituo cha Taifa cha Utunzaji Nasaba za mimea (*National Plant Genetic Resource Centre*) ili kiweze kutoa huduma bora. Wizara pia kupitia Mradi wa ERPP itazalisha tani 10 za mbegu mama za mpunga na kusafisha aina 11 za mbegu ya mpunga kwa lengo la kutumiwa na wakulima. Vilevile, Wizara itaendelea kuzalisha mbegu mama za mazao ya kilimo; kufanya utafiti wa mazao yenye thamani kubwa; yanayostahimili magonjwa na wadudu na kukarabati miundo mbinu ya vituo vya utafiti wa kilimo.

### *3.2 KUIMARISHA USIMAMIZI KABLA NA BAADA YA MAVUNO NA KUONGEZA UPATIKANAJI WA MASOKO*

**57.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kuongeza upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo ili kuwanufaisha wakulima wadogo. Wizara kupitia Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko imenunua tani 3,300.04 za Mahindi kutoka kwa wakulima wa Mikoa ya Iringa, Njombe na Ruvuma na kuongeza thamani ya zao kwa kusagisha tani 1,047.8 za Mahindi ambapo tani 896.8 ni za unga na tani 145.2 ni za pumba zilipatikana.

**58.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mradi wa ERPP inakamilisha utaratibu wa kujenga maghala matano (5)

katika skimu za umwagiliaji za Njage, Mbogo Komtonga, Msolwa Ujamaa, Mvumi na Kigugu katika mkoa wa Morogoro kwa lengo la kuhifadhi mazao, kuimarisha usalama wa chakula na kuongeza kipato cha mkulima. Vilevile, Wizara kupitia Programu ya ASDP imeweka vifaa vya kutunza ubora wa nafaka katika maghala 79 yanayohifadhi Mahindi katika Mikoa ya Rukwa – Halmashauri ya Kalambo (9), Ruvuma – Songea Vijijini (20), Songwe – Mbozi Vijijini (20), Mbeya – Mbeya Vijijini (13), Iringa – Mufindi (10), Njombe - Njombe Vijijini (7).

**59.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza thamani ya mazao Wizara kupitia Mradi wa Sera na Maendeleo ya Rasilimali Watu (*Policy and Human Resource Development - PHRD*) imenunua mashine 14 za kusindika mpunga katika skimu za Mombo (Korogwe), Kivulini (Mwanga), Mawemairo (Babati), Ipatagwa, Ituro na Mbuyuni (Mbarali), Lekitatu (Meru), Mkula (Kilombero), Musa Mwinjanga (Hai), Nakahuga (Songea), Magozi (Iringa Vijijini), Kilangali (Kilosa), Mkindo (Mvomero) na BIDP (Bagamoyo). Mashine hizo zina uwezo wa kusindika kati ya tani 10 hadi 30 kwa siku. Mzabuni kwa kushirikiana na Wizara anaendelea kutoa mafunzo ya uendeshaji na utunzaji kwa waendesha mitambo 28 (*Plant Operators*) na Maafisa Zana 12 kutoka kwenye skimu na Halmashauri husika.

**60.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya tathmini katika Halmashauri za Mikoa 12 ya Mwanza (Sengerema, Buchosa, Kwimba na Misungwi), Simiyu (Meatu, Maswa na Itilima), Geita (Geita Vijijini, Bukombe na Masumbwe), Tabora (Igunga, Kaliua na Nzega), Kigoma (Kakonko, Kasulu na Uvinza), Shinyanga (Msalala, Shinyanga Vijijini, Kishapu na Kahama Mjini), Dodoma (Bahi, Chemba na Mpwapwa), Singida (Iramba, Ikungi na Mkalama), Tanga (Lushoto, Handeni na Kilindi), Morogoro (Kilombero, Kilosa na Mvomero), Arusha (Karatu, Meru, Arusha Manispaa na Longido) na Manyara (Mbulu, Kiteto na Babati) kwa lengo la kufahamu mahitaji ya ukarabati; ujenzi wa maghala mapya kwa ajili ya hifadhi ya mazao ya Mpunga au Mahindi; na kubaini matumizi ya maghala yaliyojengwa na Wizara kupitia Miradi mbalimbali. Tathmini imebaini mahitaji ya maghala

mpya 130 na ukarabati wa maghala 276 ambayo hayatumiki ipasavyo.

**61.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika tathmini zilizofanyika (tathmini ya awali na ya kina) zilibaini uwepo wa upugufu wa chakula uliosababishwa na changamoto mbalimbali ikiwemo na ukame. Wizara katika kukabiliana na changamoto hizo katika baadhi ya maeneo yakiwamo ya Halmashauri zilizobainishwa kuwa na maeneo yenye upungufu wa chakula, jumla ya tani 1,969 za mbegu bora za Mahindi na Mtama zinazokomaa kwa muda mfupi na kustahimili ukame zilihitajika. Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 Wizara kupitia Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA), Makampuni Binafsi na Mawakala wa Pembejeo walisambaza tani 377.4 za mbegu za Mahindi, tani 100 za Mtama na tani 20 za Mpunga katika maeneo hayo. Vilevile, Wizara kupitia Vituo vya Utafiti vya Kanda imesambaza jumla ya vipando 14,252,000 zikiwemo pingili 12,772,000 za Muhogo na 1,480,000 za Viazi vitamu. Aidha, Serikali na wadau mbali mbali ilifanya juhudi mahsusi kwa ajili ya kukabiliana na athari za tetemeko na ukame uliojitokeza katika mkoa wa Kagera. Juhudi hizo ni pamoja na kutoa chakula, madawa na mahitaji mengine. Wizara kwa kushirikiana na FAO imeanza kutekeleza mradi wa kurejesha hali ya utengemano wa jamii (*Restorations of livelihood of community affected by earthquake and prolonged drought*) katika Halmashauri za mkoa wa Kagera. Mradi huu utagharimu kiasi cha **dola za kimarekani 299,000** sawa na **shilingi 668,265,000** na utanufaisha watu 5,000 na utatekelezwa kwa kipindi cha miaka miwili.

**62.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pamoja na kutumia mfumo uliopo wa ukusanyaji wa takwimu za uzalishaji wa mazao ya chakula hapa nchini, bado inakumbana na changamoto ya usahihi wa takwimu na upatikanaji kwa wakati. Katika kukabiliana na changamoto hizo, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO) na Ofisi ya Taifa ya Takwimu iliandaa na inatekeleza mradi wa majaribio wa mfumo ulioboreshwa wa ukusanyaji wa takwimu za utabiri na makadirio ya hali ya

chakula nchini (*Support for improving the reliability of food crop production forecast data in Tanzania*) kwa kutumia teknolojia ya *GIS and Remote Sensing.* Majaribio ya mradi huu yameanza kutekelezwa katika Halmashauri za mkoa wa Morogoro. Aidha, mradi huu utapanuliwa na kuzishirikisha Halmashauri za mikoa ya Ruvuma, Singida na Kagera na baadaye nchi nzima.

**63.** ***Mheshimiwa Spika,*** taarifa ya Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), ilionyesha kuwa katika kipindi cha mwezi Machi hadi Mei, 2017 mvua zilitarajiwa kuwa za wastani katika maeneo mengi ya nchi. Kutokana na mwelekeo huu wa mvua, mazao yaliyoko mashambani katika mikoa inayopata mvua za msimu yanatarajiwa kutoa mavuno ya kuridhisha. Aidha, kwa upande wa mikoa iliyokosa mvua za vuli wakulima walipanda mazao na yako katika hatua mbali mbali za ukuaji. Kwa ujumla mwenendo wa unyeshaji wa mvua katika maeneo mengi ya nchi ni wa kuridhisha na inatarajiwa kuwa na mavuno mazuri. Wizara kwa kushirikiana na Mikoa inaendelea na juhudi za kuhamasisha wananchi kupanda mazao yanayokomaa mapema na kustahimili ukame na kutumia vizuri mvua zinazoendelea kunyesha.

**64.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ulipanga kununua jumla ya tani 100,000 za chakula. Hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2017, Wakala umenunua jumla ya tani 62,099.319 za mahindi sawa na asilimia 62 ya lengo ililojiwekea. Aidha, akiba ya chakula hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2017 ni tani 86,443.773.

**65.** ***Mheshimiwa Spika,*** usalama wa chakula hapa nchini unakabiliwa na changamoto nyingi zikiwamo za upotevu wa mazao kabla na baada ya mavuno na sumu kuvu (*Afflatoxin*). Ili kukabiliana na changamoto hizo, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekamilisha kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Hifadhi ya Mazao (*National Post harvest Management Strategy*) kwa lengo la kuwa na dira ya kupunguza upotevu unaojitokeza katika mazao ya

chakula na upo katika hatua ya kujadiliwa na wadau mbalimbali katika ngazi ya kanda.

**66.** ***Mheshimiwa Spika,*** itakumbukwa kuwa mwaka 2016, wilaya za Chemba na Kondoa mkoani Dodoma na Kiteto mkoani Manyara zilikabiliwa na tatizo kubwa la sumu kuvu na kupelekea vifo vya watu 9. Kufuatia tatizo hili, Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kukabiliana na tatizo hilo. Mojawapo ya hatua zilizochukuliwa na Wizara ni kuandaa Andiko lililowasilishwa FAO na kupata ufadhili wa kudhibiti sumukuvu katika mikoa hiyo. Jumla ya **dola za kimarekani 151,000 sawa na shilingi milioni 300** zimetolewa na utekelezaji umeanza. Aidha, Wizara iliandaa Andiko Shindani la mradi (*Call for Proposal*) lililotangazwa na Umoja wa Afrika (AU) kupitia *Global Agriculture and Food Security Programme* – GASFP. Mradi huu *(Tanzania Initiative for Preventing Aflatoxin Contamination –TANIPAC)* utahusisha Udhibiti wa Sumukuvu kwa mazao ya mahindi na karanga***.*** Ninapenda kulifahamisha Bunge lako tukufu kwamba Wizara imepata tuzo ya ushindi (*award*) kwa Andiko ililoliwasilisha na imepata fedha za msaada (*Grant*) wa kiasi cha **dola za kimarekani milioni 20 ambazo ni sawa na shilingi bilioni 44.** Wizara imeanza kuandaa Andiko la kina *(Detailed Proposal)* na mradi huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano.

**67.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO) na Ofisi ya Taifa ya Takwimu itaendelea kutekeleza mradi wa majaribio wa mfumo ulioboreshwa wa ukusanyaji wa takwimu za utabiri na makadirio ya hali ya chakula nchini (Support for improving the reliability of food crop production forecast data in Tanzania). Majaribio ya mradi huu yameanza kutekelezwa katika Halmashauri za mkoa wa Morogoro. Aidha, mradi huu utapanuliwa na kuzishirikisha Halmashauri za mikoa ya Ruvuma, Singida na Kagera na baadaye nchi nzima. Vilevile Wizara kupitia Programu ya ASDP II itaboresha mfumo wa kielektroniki wa kukusanya taarifa za mvua katika vituo 600 vya mvua katika mikoa ya Tanzania Bara kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa takwimu za mvua ili kutoa ushauri

sahihi kwa wakulima na kuboresha uchambuzi wa takwimu za hali ya uzalishaji wa mazao ya chakula nchini. Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na wadau wengine itaendelea kutoa elimu na ushauri kwa wakulima juu ya matumizi sahihi ya taarifa zinazotolewa kuhusu hali ya hewa nchini.

**68.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha ubora na usalama wa mazao ya chakula nchini Wizara kupitia Programu ya ASDP II itajenga makaushio (*drying platforms*) ya kisasa 30 na kusambaza vifaa vya kukaushia *(drying sheets)* 30 kwa wakulima wa nafaka, katika Halmashauri za Sikonge, Chemba, Kondoa, Chamwino, Kiteto na Manispaa ya Dodoma kwa lengo la kudhibiti sumukuvu na madhara yake. Sambamba na hilo Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine itaainisha maeneo muhimu katika mnyororo wa thamani ambapo athari ya sumukuvu ni kubwa na kuweka mikakati ya udhibiti ikiwemo kuandaa miongozo ya kufundishia wakulima kuhusu madhara na udhibiti wa sumukuvu katika mazao ya chakula. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kutekeleza miradi wa kuthibiti Sumukuvu (Tanzania Initiative for Preventing Aflatoxin Contamination –TANIPAC) katika Wilaya 18 za Tanzania Bara na Wilaya 2 za Tanzania Zanzibar katika mikoa ya Dodoma, Manyara, Tabora, Kigoma, Morogoro, Ruvuma na Mtwara kwa Tanzania Bara na Wilaya 2 kutoka Tanzania Zanzibar.

**69.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha mazao ya wakulima yanaongezewa thamani na kuwa na soko zuri, Wizara kupitia Programu ya ASDP II itajenga maghala manne yenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 katika Mikoa ya Singida (Mahindi), Mwanza (Mpunga), Kigoma (Mahindi) and Manyara (Mahindi). Vilevile, Wizara itakamilisha ujenzi wa masoko na maghala ya kimkakati katika mipaka ya Mulongo, Sirari, Kabanga, Kahama na Kyerwa-Nkwenda ili kuleta ufanisi katika biashara za mipakani na kudhibiti wafanyabiashara kutoka nje ya nchi kuingia moja kwa moja mashambani na kununua mazao ya wakulima kwa bei ndogo.

**70.** ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Mradi wa ERPP, Wizara itajenga maghala matano (5) yenye uwezo wa kuhifadhi tani 8,400 katika skimu za umwagiliaji za Njage (1,700), Msolwa Ujamaa (3,400), Mvumi (1,300), Kigugu (1,000) na Mbogo Komtonga (1,000). Vilevile, Wizara kupitia Programu ya ASDP II itakamilisha ujenzi/ukarabati wa maghala 33 katika Wilaya za Iringa, Njombe, Nsimbo, Mlele na Songea kwa ajili ya hifadhi ya Mahindi. Kupitia maghala haya wakulima watahifadhi na kuuza mazao yao kwa pamoja, watajengewa uwezo kuhusu umuhimu na uendeshaji wa ushirika, masoko na ujasiriamali wa kilimo, matumizi ya teknolojia bora za hifadhi ya nafaka ili kupunguza upotevu, kulinda ubora na usalama wa mazao na kupanga madaraja ya mazao yao ili kupata soko zuri. Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Hifadhi ya Mazao (*National Post harvest Management Strategy*) kwa lengo la kupunguza upotevu wa mazao ya chakula nchini.

**71.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo, Wizara kupitia Bodi za Mazao itaendelea kuimarisha soko la mazao ya asili ya biashara ili kuwanufaisha wakulima wadogo. Kwa upande wa mazao ya jamii ya Mikunde na zao la Muhogo, Wizara itahamasisha wakulima kuzalisha Muhogo kibiashara ili kukidhi soko la China na mazao ya jamii ya Mikunde kwa soko la India.

**72.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Programu ya ASDP II itashirikiana na Sekta Binafsi kuanzisha viwanda vidogo vya usindikaji mazao vijijini ili kuongeza thamani ya mazao. Wizara itasimamia na kufanya tathmini ya ufanisi wa mashine za kuvuna, kupura, kukata na kukoboa mpunga kwa matumizi endelevu katika skimu 14 za umwagiliaji. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itatoa mafunzo kwa wakulima na vikundi juu ya matumizi bora ya utumiaji mashine ili kupunguza hasara itokanayo na upotevu wa mazao shambani *(reduce post-harvest losses)*.

### *3.3 Kuimarisha Upatikanaji na Utumiaji wa Pembejeo, Zana za Kilimo na Huduma za Udhibiti*

#### *Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo*

**73.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania ni nchi mojawapo Barani Afrika kusini mwa jangwa la Sahara yenye matumizi ya chini sana ya mbolea katika ngazi ya wakulima wadogo *(smallholder farmers).* Azimio la Maputo *(The Maputo Declaration, 2003)* liliazimia masuala mbalimbali katika kilimo, pamoja na mambo mengine; kuongeza matumizi ya mbolea katika eneo la ukanda wa SADC kufikia angalau kilo 50 za virutubisho kwa hekta. Kwa sasa Tanzania imefikia kiwango cha kilo 19 za virutubisho kwa hekta ambayo ni sawa na asilimia 38 ya lengo. Aidha matumizi haya yamekuwa changamoto kubwa kwa serikali. Kwa miaka hamsini iliyopita Wizara ya Kilimo imekuwa ikiweka mikakati na mifumo mbalimbali yenye lengo la kuongeza matumizi na upatikanaji wa mbolea kwa wakulima wadogo ili kuongeza uzalishaji wenye tija. Katika mwaka 2016/2017, upatikanaji wa mbolea umefikia tani 277,935 sawa na asilimia 57 ya mahitaji ya tani 485,000 ya mbolea.

**74.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali iliwezesha utoaji wa ruzuku ya mbolea kwa wakulima wa Mazao ya Mahindi na Mpunga katika mikoa 25 ya Tanzania Bara kwa kaya 378,900 kupitia Kampuni ya Mbolea Tanzania - TFC. Hadi mwezi Machi 2017, jumla ya tani 30,823 kati ya tani 32,394 za mbolea sawa na asilimia 95 ya lengo zilipatikana. Kati ya hizo, tani 12,850 ni za mbolea ya kupandia sawa na asilimia 89 ya lengo la tani 14,421 na tani 17,973 ni za mbolea ya kukuzia sawa na asilimia 100 ya lengo. Tani 26,999 sawa na asilimia 83 zimesambazwa katika vituo vya mauzo vya Kampuni ya TFC katika mikoa 25 ya Tanzania Bara na jumla ya tani 23,515 sawa na asilimia 73 ya lengo zimeshawafikia wakulima na kazi ya usambazaji inaendelea ambapo Kanda ya Mashariki na Kanda ya Kaskazini zoezi la usambazaji limeanza mwezi Machi, 2017. Katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea kutoa ruzuku ya mbolea kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya Mahindi na Mpunga.

**75.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilifanya uhakiki wa awali wa madai ya mawakala na makampuni waliosambaza pembejeo za ruzuku msimu wa 2015/2016. Uhakiki huo ulifanyika katika mikoa minane (8) ya Morogoro, Iringa, Njombe, Ruvuma, Songwe, Rukwa, Arusha na Kilimanjaro ambapo makampuni na mawakala 187 kati ya 280 waliofanya kazi ya kusambaza pembejeo za ruzuku wamehakikiwa na mawakala 93 hawakuhakikiwa kwa sababu mbalimbali. Aidha, Mhe. Waziri Mkuu ameiagiza Wizara ya Fedha na Mipango kufanya uhakiki wa kina kwa mikoa yote 26 ya Tanzania Bara isipokuwa Dar es Salaam katika kipindi cha mwezi mmoja (1) ili madai halali ya mawakala waliosambaza pembejeo kwa wakulima katika msimu wa 2015/2016 yaweze kulipwa.

**76.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Udhibiti wa Ubora wa Mbolea Tanzania (TFRA) imesajili mawakala wa mbolea 311 na imetoa vibali 172 vya kuingiza mbolea nchini. Aidha, tani 297,000 za mbolea ziliingizwa nchini na tani 140,000 zilitolewa nje ya nchi hadi Machi, 2017. Kati ya kiasi kilichotolewa nje ya nchi, tani 74,000 ni za mbolea ya Minjingu iliyopelekwa katika nchi za Kenya, Uganda na Afrika Kusini.

**77.** ***Mheshimiwa Spika,*** TFRA imefanya ukaguzi wa maghala na maduka na kutoa elimu kwa wafanyabiashara wa mbolea katika mikoa ya Mbeya, Njombe, Ruvuma, Morogoro, Iringa, Arusha na Dar es Salaam. Pia ukaguzi maalum wa mbolea za kilimo cha Tumbaku zinazosimamiwa na Vyama vya Ushirika wa Tumbaku umefanyika katika mikoa ya Iringa, Mbeya, Katavi, Kigoma, Tabora, Shinyanga na Singida. Vilevile, Mamlaka ilifanya mapitio ya Kanuni za Mbolea za mwaka 2011 ili kuondoa changamoto zilizojitokeza katka utekelezaji wake ili kuboresha mazingira ya biashara ya mbolea. Wizara kupitia TFRA imeandaa Kanuni ya Manunuzi ya Mbolea kwa Pamoja za mwaka 2017 (*Fertilizer Bulk Procurement Regulations, 2017*) na mwongozo wa utekelezaji kwa madhumuni ya kuongeza upatikanaji na kupunguza bei za mbolea kwa Mkulima.

**78.** ***Mheshimiwa Spika,*** msimu 2017/2018 mfumo wa uagizaji wa mbolea kwa pamoja utaanza kwa kuagiza aina mbili tu za mbolea ambazo ni; mbolea ya kupandia *(DAP)* na mbolea ya kukuzia *(UREA)* kwa kuwa zinatumika kwa wingi. Mbolea zingine hususan NPK, CAN, SA, MOP, TSP, blends mbalimbali, Biofertilizers na zile za maji "foliar" zitaendelea kuletwa kwa utaratibu unaotumika sasa.

**79.** ***Mheshimiwa Spika,*** mfumo unaopendekezwa utakuwa na faida kuu moja ambayo ni ongezeko la matumizi ya mbolea nchini kutokana na sababu zifuatazo:-
-Mfumo huu utasaidia kuimarisha utaratibu wa usambazaji wa mbolea ambapo wadau wote watapata uhakika wa upatikanaji wa mbolea kwa bei ya ushindani.

-Kuwezesha wafanyabaishara wadogo kukua *(locals)* na kushiriki katika biashara ya mbolea hata wenye mitaji midogo watapata fursa ya kuagiza na hivyo kuimarisha mtandao wa usambazaji hadi ngazi ya mkulima.

-Utaratibu huu, utawezesha waagizaji kununua mbolea wakati bei ni ndogo na TFRA kufuatilia bei hiyo na kuioanisha na mazingira ya nchi ili kuepuka mwanya kwa waagizaji kuongeza bei zaidi ya ile iliyonunuliwa kwa bei ndogo. Suala hili litatekelezwa kwa kushirikiana na mashirika ya kimataifa yanayofuatilia mwenendo wa bei za mbolea katika soko la dunia ili mbolea inunuliwe kutoka kwenye viwanda vinavyouza kwa bei ya chini bila kuathiri ubora wake.

**80.** ***Mheshimiwa Spika,*** makadirio ya mahitaji ya mbegu bora zikiwemo mbegu za nafaka, mikunde na mbegu za mafuta ni tani 60,000 kwa mwaka. Katika mwaka 2016/2017 upatikanaji wa mbegu bora umefikia tani 28,278.2 sawa na asilimia 47.13 ya mahitaji ya mwaka. Kati ya kiasi cha mbegu bora kilichopatikana tani 11,802.44 zimezalishwa hapa nchini na tani 16,475.76 zimeingizwa kutoka nje ya nchi.

**81.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) imeongeza uzalishaji wa mbegu bora za nafaka na mikunde kutoka tani 2,804 msimu wa 2015/

2016 hadi tani 2,884 msimu 2016/2017 zikiwemo tani 661 za mikunde na tani 2,223 za nafaka ambayo ni sawa na asilimia 92.4 ya lengo la kuzalisha tani 3,120. Vilevile, ASA imezalisha miche bora ya matunda 20,435 sawa na asilimia 68.11 ya lengo na vipando bora vya Muhogo pingili 12,772,210 kwa kushirikiana na Jeshi la Magereza pamoja na Taasisi zisizo za Kiserikali. Uzalishaji huo ni sawa na asilimia 106.43 ya lengo la kuzalisha vipando vya Muhogo pingili 12,000,000. ASA pia kwa kushirikiana na Sekta Binafsi imezalisha tani 1,141 za mbegu ya Mahindi katika shamba la Mbozi.

**82.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, ASA imeratibu jumla ya mashamba darasa 120 katika Wilaya za Malinyi, Ulanga, Mvomero, Morogoro vijijini, Kilombero, Gairo na Kilosa yanayolenga kusaidia wakulima kuchagua mbegu bora za mpunga tano (5) aina za Nerica 1, Nerica 2, Nerica 4, WABU-450 na Nerica 7 zinazolimwa kwenye maeneo yenye mwinuko (*Upland rice*) na aina saba (7) za TXD 88, MWANGAZA, KALALU, TAI, TXD 306, KOMBOA na SUPA zinazolimwa kwenye mabonde ya umwagiliaji na mabonde yanayotegemea mvua.

**83.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Serikali iliwezesha utoaji wa ruzuku ya mbegu kwa wakulima wa Mazao ya Mahindi na Mpunga kwa kaya 378,900 kwa utaratibu wa Wizara kuingia makubaliano na Makampuni yanayozalisha na kuagiza mbegu bora kusambaza na kuuza tani 3,731.5 za mbegu bora zenye ruzuku. Mbegu hizo ni tani 3,407 za Mahindi na tani 333.5 za Mpunga ambazo zilisambazwa katika mikoa 25 ya Tanzania Bara isipokuwa mkoa wa Dar es Salaam.

**84.** ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha katika mwaka 2016/2017 Serikali imetoa ruzuku ambapo jumla ya miche bora ya Kahawa 2,412,805 imezalishwa katika vituo mbalimbali ikiwemo Lyamungo (Miche 535,207), Mbimba (373,267), Ugano (889,580), Mwayaya (67,250), Maruku (467,245) na Sirari (50,256). Miche hiyo iliyozalishwa imesambazwa katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Tanga, Manyara na Morogoro; Mbeya, Katavi; Ruvuma, Njombe, Iringa; Kigoma; Kagera na Mara. Aidha, miche bora ya chai 7,100,000 imezalishwa na Wizara

kupitia Wakala wa Kuendeleza Wakulima Wadogo wa Chai (TSHTDA) kwa kushirikiana na *Njombe Outgrowers Services Company* (NOSC) katika eneo la Igominyi Mkoa wa Njombe. Aidha, Serikali imetoa ruzuku kwa ajili viuatilifu vya zao la korosho na ekapaki 1,803,586 za viuatilifu vya zao la pamba.

**85.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Taasisi ya Udhibiti wa Ubora Mbegu (TOSCI) imehakiki aina mpya 20 za mbegu ili kulinganisha na aina zingine zilizo kwenye soko (*DUS test*) ambapo aina 15 zimekidhi viwango. Aidha, aina mpya 37 za mbegu zinaendelea kuhakikiwa kubaini ubora na sifa zake ikiwemo kutoa mavuno mengi, uvumilivu wa magonjwa na ukame katika Kanda za Nyanda za Juu Kusini, Mashariki, Kusini, Kaskazini na Kanda ya Ziwa. Vilevile, Taasisi ya Kuthibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI) wamekagua jumla ya hekta 4,178 za mashamba ya mbegu ambapo hekta 4,165.5 (99.7%) zilikidhi viwango vya ubora wa mbegu na hekta 12.5 (0.3%) hazikuweza kukidhi viwango.

**86.** ***Mheshimiwa Spika,*** Aidha sampuli 2,239 za mbegu za mazao mbalimbali zimefanyiwa vipimo vya maabara kwa ajili ya kuangalia usafi na uotaji. Asilimia 98 ya sampuli zote zilikidhi viwango na asilimia 2 ya sampuili zote hazikukidhi viwango, hivyo wazalishaji husika walizuiliwa kuuza mbegu hizo. Vilevile, maduka 296 ya mbegu za kilimo yalikaguliwa ili kuhakiki ubora wa mbegu ambapo asilimia 95 ya sampuli zilikidhi viwango vya uotaji na asilimia 5 ya mbegu hazikukidhi viwango na kuzuiwa kuuzwa.

**87.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza biashara ya mbegu kimataifa, Wizara imekamilisha taratibu za kujiunga na mashirika ya kimataifa yanayosimamia ubora wa mbegu na biashara ya kimataifa. Mashirika ambayo tayari tumejiunga nayo ni pamoja **na OECD na UPOV.** Aidha, Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za kupata ithibati ya ISTA kwa ajili ya maabara ya mbegu ya Morogoro.

**88.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea kutoa ruzuku ya mbegu ya Mahindi na Mpunga kwa kuingia mkataba na makampuni ya mbegu.

Aidha, Serikali itatoa ruzuku kwa aili yakuzalisha miche bora ya Chai milioni 10 na miche bora ya Kahawa milioni 12 na; usambazaji wa viatilifu tani 8,600 na lita 980,000 kwa wakulima wa zao la Korosho na ekapaki 1,537,500 za viuatilifu vya zao la Pamba. Aidha, Wizara itafuatilia na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu pembejeo za kilimo ikiwemo ruzuku ya pembejeo za kilimo katika mikoa na Halmashauri nchini ifikapo Juni 2018.

**89.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) imepanga kuzalisha mbegu bora za nafaka na mikunde tani 2,500. Pia kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itazalisha tani 1,500 katika shamba la Mbozi. Aidha, itazalisha vipando bora vya Muhogo pingili 24,000,000 na miche bora ya matunda 50,000. Aidha, Wizara kupitia Mradi wa ERPP itaendelea kujenga na kuboresha miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la Kilangali, kufanya tathimini ya aina ya mbegu 13 za mpunga kupitia mashamba darasa 120.

**90.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TOSCI itahakiki upya, uhalisia na sifa kwa aina 70 za mbegu mpya na kukagua hekta 10,000 za wakulima wa mbegu. Tangu Desemba, 2016 Tanzania ni mwanachama halali wa *Organization for Economic Cooperation and Development* (OECD). Aidha, kupitia Programu ya ASDP II, TOSCI itaboresha vitendea kazi na kuimarisha ukaguzi wa mbegu bora za mpunga kabla na baada ya mavuno kupitia Mradi wa ERPP.

***Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea na Mazao***

**91.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kudhibiti visumbufu vya milipuko katika maeneo yaliyovamiwa na Nzige, Panya, Kweleakwelea na visumbufu vipya ili kupunguza upotevu wa mimea na mazao. Jumla ya ndege aina ya Kweleakwelea milioni 71.58 ambao wangekula tani 715.8 za mazao wamedhibitiwa nchini katika wilaya za Same katika mashamba ya Skimu ya Umwagiliaji ya Ndungu kwenye kata za Kalemawe, Maore, Ndungu na Kihurio. Katika wilaya ya Moshi Vijijini ndege hao walidhibitiwa katika

mashamba ya "Lower Moshi" na Kahe. Milipuko zaidi ya kweleakwelea iliendelea kutokea na kudhibitiwa katika maeneo mbalimbali nchini. Milipuko hiyo ilidhibitiwa katika mkoa ya Dodoma wilaya za Bahi na Chamwino na maandalizi ya udhibiti yanaendelea katika mikoa ya Shinyanga, Mbeya (Mbarali) na Morogoro. Wilaya zingine walipothibitiwa ni Singida vijijini, Ikungi, Iramba, Shinyanga vijijini, Sengerema, Kishapu na Hanang. Aidha, kulitokea milipuko ya viwavijeshi aina ya "*African armyworms*" katika mikoa ya Lindi, Pwani na Morogoro. Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi iligawa viuatilifu na kuratibu udhibiti wa Janga hilo ambao ulifanikiwa vizuri. Aidha, inaendelea kukagua mazao yanayoingia nchini na yanayotoka nje ya nchi, kuboresha vituo vya mipakani, kusajili viuatilifu na kukagua wafanyabiashara wa viuatilifu na kutoa Elimu kwa Wakaguzi.

**92.** ***Mheshimiwa*** Wizara imefanikiwa pia kudhibiti milipuko ya panya katika eneo la ekari 229.5 katika wilaya ya Shinyanga katika kata za Salawe, Mwenge, Solwa, Mwakitolyo, Lyabusalu na Pandikichiza kwa kutumia kilo 90 za sumu aina ya *Bromodialone*; kilo 4.8 za Zinki; na kilo 288 za chambo. Wizara imeendelea kufuatilia hali ya Nzige wekundu katika mikoa ya Rukwa, Katavi, Kigoma na Tabora ili kuchukua za kudhibiti visumbufu hivyo.

**93.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilitathmini na kuruhusu uingizwaji wa aina 10 za viumbe marafiki kwa ajili ya udhibiti wa visumbufu kibiolojia kwenye mazao ya Mahindi, Karanga, Mboga, Matunda na Maua. Vilevile, uzalishaji na utunzaji kizazi cha wadudu marafiki mbawakavu na manyigu umeendelea kwenye maabara zilizopo kwenye kituo cha udhibiti wa Visumbufu Kibiolojia kilichopo Kibaha, Pwani.

**94.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Shirika la Kilimo na Chakula la Umoja wa Mataifa (FAO) na Halmashauri za Wilaya imetoa mafunzo kwa Maafisa Ugani 180 katika Wilaya za Kondoa, Chemba, Mufindi, Kilolo, Kilombero, Mbalizi na Mpwapwa kuhusu athari na mbinu za kudhibiti sumu kuvu. Wizara pia imetoa elimu kwa wadau 837 kuhusu mbinu za udhibiti wa

sumu kuvu kupitia maonesho ya Wakulima (NaneNane). Wadau hao ni Wakulima, Maafisa Ugani, Watafiti, Wakufunzi, Wanafunzi na Wafanyabiashara wa mikoa 14 ya Dodoma, Singida, Simiyu, Manyara, Kilimanjaro, Arusha, Kagera, Mbeya, Iringa, Dar Es Salaam, Shinyanga, Morogoro, Lindi na Mtwara. Aidha, Wizara imeendelea kufanya majaribio kwenye mashamba 100 ya Wakulima kwenye Halmashauri nane za Masasi, Nanyumbu, Babati, Kilosa, Kilombero, Mpwapwa, Kongwa na Chamwino kwa ajili ya kutathmini viwango vya *Aflasafe* kwenye udhibiti wa sumu kuvu.

**95.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), Shirika la Kilimo na Chakula Duniani (FAO) na Halmashauri za Mwanza, Misungwi, Singida, Mufindi, Kilolo, na Kilosa imeendelea kutoa mafunzo rejea kwa Wawezeshaji (ToT) na Wakulima juu ya Udhibiti Husishi wa Visumbufu vya mimea na mazao. Kwa mwaka 2016/ 2017, Jumla ya Wataalam 29 wa zao la pamba, Vikundi 24 vya shamba darasa kutoka Kanda ya Ziwa, Wakulima 650 wa Kanda ya Ziwa na Wataalam 30 wa Bonde la Mto Kihansi walipatiwa mafunzo rejea ya udhibiti Husishi wa Visumbufu vya Mazao.

**96.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kudhibiti nzi waharibifu wa matunda kwa kutoa mafunzo na usambazaji wa kivutia wadudu aina ya *Methyl eugenol* (ME). Kiasi cha lita 105 ziligawiwa katika Mikoa ya Arusha, Dar es Salaam, Mtwara, Pwani, Morogoro, kwenye Vituo vya Utafiti vya Kilimo vya Naliendele, Kibaha na Mikocheni na kwa Umoja wa Wakulima wa Maembe (*Association of Mango Growers* - AMAGRO). Vilevile, Wizara imethibitisha uwepo wa aina mpya ya viwavijeshi nchini wajulikanao kwa jina la "*Fall armyworm*" (*Spodoptera frugiperda*) wanaosababisha uharibifu wa mazao mbalimbali mashambani.

**97.** ***Mheshimiwa Spika,*** mlipuko wa aina hiyo ya viwavijeshi umetokea kwa mara ya kwanza katika mkoa wa Rukwa wakiaminika kutokea nchini Zambia. Kwa kuwa mashambulizi ya viwavijeshi hawa yalikuwa makubwa Wizara iliagiza ndege toka DLCO-EA na kuua wadudu hao

kwenye mashamba makubwa mkoani Rukwa ya Msipazi, Empien, Abasia na mashamba ya wakulima wadogo ambapo jumla ya ekari 2,640 ziliokolewa kwa asilimia zaidi ya 85. Kwa kuwa wadudu hawa wanaweza kujitokeza tena msimu ujao, maandalizi yameanza mapema ili wadudu wadhibitiwe mapema na madhara ya mashambulizi yasiwe makubwa.

**98.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na ukaguzi wa usafi wa mimea na mazao katika vituo vya ukaguzi vya Sehemu ya Afya ya Mimea vilivyoko katika viwanja vya ndege, bandari na mipakani. Hadi mwezi Machi 2017, tani 776,379.16 za mimea na mazao zilikaguliwa na kusafirishwa nje ya nchi. Jumla ya tani 597,837.33 za mimea/mazao zilikaguliwa na kuingizwa nchini, vyeti 8,736 vya usafi wa mimea "*Phytosanitary Certificate*" kwa ajili ya kusafirisha mazao nje ya nchi na vibali 1,232 vya kuingiza mazao na mimea nchini (*plant import permits*) vilitolewa. Jukumu hili limewezesha biashara ya mazao yetu ya Kilimo kukidhi masharti ya Soko la Kikanda na Kimataifa.

**99.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira) na Shirika la Kilimo Chakula Duniani (FAO) imetoa mafunzo kuhusu matumizi sahihi na salama ya viuatilifu kwa Maafisa Ugani na wakulima katika Halmashauri za Kilombero, Kilolo na Mufindi. Aidha, mafunzo juu ya matumizi sahihi ya viuatilifu yalitolewa kwa wadau 30 wa Bonde la Mto Kihansi katika Halmashauri za Mufindi, Kilolo na Kilombero. Ufuatiliaji, ukusanyaji na uratibu wa takwimu/ taarifa za athari za viuatilifu vyenye sumu kali kwa afya ya binadamu na mazingira ulifanyika kwa wakulima 100 wa Wilaya ya Kilolo - Iringa. Pia zoezi la ukaguzi wa maduka ya pembejeo za Kilimo ulifanyika, ambapo lita 14,671 za viuatilifu visivyo na ubora vilikamatwa na kuhifadhiwa ili kusubiri taratibu za uteketezaji. Aidha, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kufunga baadhi ya maduka ya wafanyabiashara waliohusika na kuuza viuatilifu vilivyo chini ya ubora na ambavyo havijasajiliwa.

**100.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018,

Wizara itaendelea kudhibiti visumbufu vya mazao na mimea kwa kufanya tathmini ili kudhibiti milipuko ya nzige, kweleakwelea, panya, viwavijeshi na magonjwa ya mimea. Aidha, Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wakulima ili kubaini milipuko na jinsi ya kudhibiti na itaendelea kuimarisha vituo vya ukaguzi vya mipakani ili kudhibiti mazao yanayosafirishwa na yanayoingia nchini. Vilevile, kituo cha kudhibiti milipuko cha KILIMO ANGA kitaendelea kuimarishwa ili kutoa huduma bora ya udhibiti wa milipuko ya visumbufu vya magonjwa ya mazao na mimea. Wizara itaendelea kutoa elimu kwa wakulima ili kubaini milipuko na jinsi ya kudhibiti na itaendelea kuimarisha vituo 36 vya ukaguzi vya mipakani ili kudhibiti mazao yanayosafirishwa na yanayoingia nchini.

***Kusimamia Bodi za Mazao na Asasi nyingine za kilimo***

**101.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuboresha utendaji wa bodi za mazao zinazoratibu na kusimamia uendelezaji wa mazao makuu ya biashara, Wizara imeanza kuchukua hatua kwa kuboresha miundo ya bodi hizo. Aidha, katika lengo la kuboresha uendeshaji na usimamizi wa Tasnia za Mazao, Wizara imefanya maboresho ya Bodi ya Wakurungezi ya Korosho kwa lengo la kuleta ufanisi. Vilevile, Wizara imesimamisha baadhi ya majukumu ya Mfuko wa Maendeleo ya Zao la Korosho na hivyo majukumu hayo yamehamishiwa kwenye Bodi ya Korosho Tanzania. Pia Wizara imevunja Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Tumbaku na pia ipo katika maandalizi ya mwisho ya kuunda Bodi mpya ya Tumbaku ili kuboresha utendaji.

**102.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya maendeleo ya mazao nchini ikiwemo kuwawezesha wajasiriamali wadogo na wa kati (SMEs); kuweka mazingira mazuri ya wawekezaji wakubwa kuwekeza na kufuatilia utekelezaji wa Mkakati wa Mazao ya Bustani katika kanda 5 (*Agroecological Zones*); kuhamasisha uzalishaji wa kibiashara wa zao la Muhogo katika Kanda za Ziwa, Mashariki na Kusini na kutekeleza programu ya

*Supporting Indian Trade Investment in Africa - SITA* kwa kuzalisha kibiashara kwa mfumo wa kilimo cha mkataba mazao ya mikunde na mafuta kwa kushirikiana na Halmashauri za Wilaya.

***Uzalishaji wa Mazao Makuu ya Asili ya Biashara***

**103.** ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao makuu ya asili ya biashara ambayo ni Korosho, Miwa ya Sukari, Pamba, Mkonge, Chai, Kahawa, Pareto na Tumbaku katika msimu wa mwaka 2016/2017, umeongezeka kwa viwango tofauti. Uzalishaji wa jumla kwa mazao makuu ya biashara umeongezeka kufikia tani 881,583 ikilinganishwa na tani 796,562 mwaka 2015/2016. Aidha, uzalishaji wa mazao unaendelea kwa mwaka 2016/2017 na matarajio ya uzalishaji kwa mwaka 2017/2018 yameoneshwa katika **Jedwali Na.1**. Uzalishaji wa mazao ya Korosho, Sukari na Pareto umeongezeka kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo bei nzuri katika zao la Korosho kutokana na Mfumo wa Stakabadhi Ghalani na bei nzuri ya Pareto kwa wakulima wadogo iliyochangiwa na ongezeko la bei ya Pareto katika soko la Dunia. Uzalishaji wa sukari umeongezeka kutokana na uzingatiaji wa kanuni za kilimo bora cha miwa na matumizi ya teknolojia na zana za kisasa katika kilimo cha miwa.

**104.** ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa Pamba, Chai, Mkonge na Kahawa umeshuka kwa viwango tofauti ikilinganishwa na mwaka 2015/2016. Kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya Pamba, Chai, Mkonge na Kahawa kumesababishwa na sababu mbalimbali zikiwemo uhaba wa mvua katika maeneo ya uzalishaji na matumizi hafifu ya pembejeo hususan mbegu bora na mbolea; mgogoro kati ya wakulima wadogo wa chai na mwekezaji katika kiwanda cha chai Mponde na kusababisha wakulima wengi kutelekeza mashamba yao; na uharibifu wa miundombinu ya barabara za mashambani kwenda viwandani hususan kwa viwanda vya chai. Aidha, uzalishaji wa Tumbaku umelingana na msimu uliopita kwa kuwa huzaliswa kwa mkataba kati ya wakulima na wanunuzi. Katika msimu wa 2017/2018 matarajio ni

kuzalisha jumla ya tani 953,825 za mazao hayo kama ilivyochanganuliwa katika **Jedwali Na.1.**

**Jedwali Na. 1 Uzalishaji wa Mazao ya Asili ya Biashara (Tani) kati ya 2015/2016 na 2017/2017 na matarajio kwa mwaka 2017/2018**

| Zao | 2015/2016 | 2016/2017* | 2017/2018** |
|---|---|---|---|
| Pamba | 149,445 | 122,000 | 150,000 |
| Chai | 32,629 | 31,000 | 35,000 |
| Pareto | 2,011 | 2,500 | 2,600 |
| Korosho | 155,416 | 260,000 | 300,000 |
| Mkonge | 42,314 | 42,000 | 43,000 |
| Sukari | 293,075 | 329,840 | 324,325 |
| Kahawa | 60,921 | 47,999 | 43,000 |
| Tumbaku | 60,691 | 60,691 | 55,900 |
| **Jumla** | **796,502** | **881,583** | **953,825** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi*

**Msimu wa uzalishaji bado unaendelea* ********Makadirio kwa msimu ujao*

***Uzalishaji wa Mazao ya Bustani***

**105.** ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya bustani ambayo ni matunda, mboga, maua na viungo umeongezeka kutoka tani 5,931,906 mwaka 2015/2016 hadi tani 6,216,145 mwaka 2016/2017. Hii inatokana na kuongezeka uzalishaji wa zao la Parachichi katika mikoa ya nyanda za juu kusini ambako wakulima wamehamasika baada ya kuwa na soko la uhakika, pia uzalishaji wa zao la nyanya na matikiti umeongezeka katika sehemu nyingi nchini. Wizara imeendelea kushirikiana na Taasisi mbalimbali ili kuhamasisha kilimo cha Matunda, Mboga, Maua na Viungo pamoja na ulaji wake. Matarajio ya uzalishaji mazao hayo msimu 2017/2018 na mchanganuo wa uzalishaji wa kila zao ni kama ilivyokatika **Jedwali Na. 2.**

**Jedwali Na. 2: Uzalishaji wa Mazao ya Bustani (Tani)**

| Na. | Zao | 2015/2016 | 2016/2017* | Matarajio 017/2018 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Matunda | 4,711,000 | 4,946,550 | 5,243,343 |
| 2 | Mboga | 1,189,000 | 1,236,560 | 1,298,388 |
| 3 | Maua | 11,500 | 11,615 | 11,847 |
| 4 | Viungo | 20,400 | 21,420 | 22,062 |
| **Jumla** | | **5,931,906** | **6,216,145** | **6,575,640** |

**Chanzo:** *Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi;*
** Uzalishaji unaendelea*

***Uzalishaji wa Mazao ya Mbegu za Mafuta***

**106.** ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mbegu za mafuta za Alizeti, Karanga, Ufuta, Mawese na Soya umeongezeka kutoka tani 6,301,147 za mwaka 2015/2016 hadi tani 6,667,893 mwaka 2016/2017. Kuongezeka kwa uzalishaji kumechangiwa na kuongezeka kwa hamasa kwa wakulima kutokana na uwepo wa soko la uhakika, ushirikiano kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi pamoja na uwekezaji katika viwanda vidogo na vya kati katika mikoa ya Manyara, Singida, Dodoma, Mbeya, Katavi, Lindi, Mtwara, Iringa, Njombe, Rukwa na Kigoma. Katika msimu wa 2017/2018 matarajio ni kuzalisha tani 6,903,820 kama ilivyochanganuliwa katika **Jedwali Na. 3.**

**Jedwali Na. 3: Uzalishaji wa Mbegu za Mafuta (Tani)**

| Na. | Zao | 2015/2016 | 2016/2017 | Matarajio 2017/2018 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Alizeti | 2,995,500 | 3,112,500 | 3,229,220 |
| 2 | Karanga | 2,025,595 | 2,215,257 | 2,281,710 |
| 3 | Ufuta | 1,232,092 | 1,291,724 | 1,343,390 |
| 4 | Mawese | 41,925 | 42,277 | 43,120 |
| 5 | Soya | 6,035 | 6,135 | 6,380 |
| | **Jumla** | **6,301,147** | **6,667,893** | **6,903,820** |

**Chanzo:** *Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi*

***Zana za Kilimo***

**107.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhamasisha Sekta Binafsi kuingiza nchini zana bora za kilimo kwa lengo la kuongeza upatikanaji wake kwa wakulima. Kwa kipindi cha Mwezi Januari, 2016 hadi Machi, 2017 jumla ya Matrekta makubwa 1,459 na Matrekta ya mkono 312 yaliingizwa nchini.

**108.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza matumizi ya zana bora za kilimo na kusogeza karibu huduma kwa wakulima, Serikali kupitia Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) imekamilisha zoezi la kubainisha maeneo katika kanda nane (8) yatakayotumika kuanzisha vituo nane (8) vitakavyotumika kutoa huduma za matrekta kama vile uuzaji wa matrekta mapya, uuzaji wa vipuri, utoaji wa mafunzo na huduma za kiufundi kwa wakulima. Vituo hivyo vitaanzishwa katika Mikoa ya Morogoro, Dodoma, Manyara, Katavi, Geita, Simiyu, Njombe na Lindi.

**109.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mradi wa Sera na Maendeleo ya Rasilimali Watu (*Policy and Human Resource Development – PHRD*) imenunua na kusambaza mashine 14 za kusindika mpunga katika skimu za Mombo (Korogwe), Kivulini (Mwanga), Mawemairo (Babati), Ipatagwa, Uturo na Mbuyuni (Mbarali), Lekitatu (Meru), Mkula (Kilombero), Musa Mwinjanga (Hai), Nakahuga (Songea), Magozi (Iringa vijijini), Kilangali (Kilosa), Mkindo (Mvomero) na BIDP (Bagamoyo). Mashine hizi zina uwezo wa kusindika kati ya tani 10 hadi 30 kwa siku. Mzabuni kwa kushiriakana na Wizara anaendelea kutoa mafunzo ya uendeshaji na utunzaji kwa maopereta 28 na Maafisa zana 12 kutoka kwenye skimu na Halmashauri husika.

**110** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kushirikiana na Taasisi nyingine na Sekta Binafsi kuhakikisha matumizi bora na upatikanaji wa zana za kilimo unaongezeka. Serikali kupitia NDC imeanza ujenzi wa kiwanda cha kuunganisha matrekta Kibaha Mkoani Pwani ambacho kitatumika kuunganisha matrekta 2,400 aina

ya URSUS kutoka nchini Poland katika kipindi cha miaka mitatu. NDC itashirikiana na Wizara, Halmashauri za Wilaya, Taasisi na Sekta Binafsi katika kuunganisha, kuuza na kutoa huduma za kiufundi, mafunzo na matengenezo ya matrekta hayo. Wizara kupitia Programu ya ASDP II itafanya upembuzi wa mahitaji ya mashine na zana za kilimo katika Kanda saba za Kilimo kwa ajili ya kuanzisha au kukarabati vituo vya zana za kilimo nchini, ambapo Wizara itatoa mafunzo kwa Sekta Binafsi kuhusu ujasiriamali na uwekezaji wa zana za kilimo katika usimamizi, matengenezo na utoaji wa huduma.

***Mikopo ya pembejeo kutoka Mfuko wa Taifa wa Pembejeo***

**111.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) ilipanga kutumia Shilingi 6,320,500,000 ili kutoa mikopo ya matrekta mapya 79, matrekta madogo ya mikono 10, mikopo 40 kwa ajili ya pembejeo za kilimo, mifugo na vifungashio, mikopo 8 kwa ajili ya zana za umwagiliaji, mikopo 4 kwa ajili ya mashine za usindikaji, mikopo 2 kwa ajili ya mashine za kuvuna na mikopo 5 kwa ajili ya ukarabati wa zana za kilimo. Hadi mwezi Februari, 2017 AGITF imepata na kutumia Shilingi 4,103,884,804 na kutoa mikopo kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 4**.

**Jedwali Na. 4: Mikopo Iliyotolewa katika Kipindi cha Julai 2016 hadi Februari, 2017**

| Na | Aina ya Mkopo | Utekelezaji | | Thamani ya Mikopo (Shilingi) |
|---|---|---|---|---|
| | | Lengo | Halisia | |
| 1 | Matrekta mapya makubwa | 79 | 43 | 2,232,846,804 |
| 2 | Matrekta ya mkono (*Power Tillers*) | 10 | 0 | 0 |
| 3 | Pembejeo za Kilimo na Mifugo | 40 | 23 | 1,183,158,000 |
| 4 | Zana za Umwagiliaji maji | 08 | 11 | 628,208,000 |
| 5 | Mashine za uvunaji (*Combine harvester*) | 02 | 0 | 0 |
| 6 | Mashine za usindikaji | 04 | 01 | 29,972,000 |
| 7 | Ukarabati wa zana za kilimo | 05 | 02 | 29,700,000 |
| | **JUMLA** | | | **4,103,884,804** |

***Chanzo***: *Mfuko wa Taifa wa Pembejeo*

**112.** ***Mheshimiwa Spika,*** AGITF imeendelea kufuatilia marejesho ya mikopo kwa mafanikio kama ifuatavyo; mwaka 2014/2015 lengo lilikuwa kurejesha Shilingi 5,101,693,624 na iliyorejeshwa ilikuwa ni Shilingi 5,111,112,041 sawa na asilimia 100; mwaka 2015/2016 lengo lilikuwa kurejesha Shilingi 5,764,141,824 na iliyorejeshwa ilikuwa ni Shilingi 5,009,547,428 sawa na asilimia 87; mwaka 2016/2017 lengo lilikuwa kurejesha Shilingi 6,749,151,392 na iliyorejeshwa ilikuwa ni Shilingi 3,244,119,751 sawa na asilimia 48.1. Katika mwaka 2016/2017 marejesho ya mikopo yameathiriwa sana na hali ya hewa.

**113.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Mfuko wa Taifa wa Pembejeo za Kilimo (AGITF) imepanga kutumia Shilingi 7,781,000,000 ili kutoa mikopo ya matrekta mapya 71, mikopo 80 kwa ajili ya pembejeo za kilimo na mifugo, mikopo minne (4) kwa ajili ya ukarabati wa zana za kilimo, mikopo sita (6) kwa ajili ya miundombinu ya kilimo, mifugo na uvuvi, mikopo mitatu (3) kwa ajili ya fedha za kuendeshea shughuli za shamba, mikopo mitatu (3) kwa ajili ya kununua ardhi kwa ajili ya kilimo, mifugo na ufugaji samaki, mikopo mitatu (3) kwa ajili ya zana unganishi na mikopo mitato (5) kwa ajili ya zana za kusindika na vifungashio vya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi Mpango huo ni kama inavyooneshwa katika **Jedwali Na. 5.**

**Jedwali Na. 5: Mikopo Iliyopangwa kutolewa katika Kipindi cha Julai 2017 hadi Juni, 2018**

| Na | Aina ya Mkopo | Malengo | Thamani ya Mikopo (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | Matrekta mapya makubwa | 71 | 3,950,000,000 |
| 2 | Pembejeo za Kilimo na Mifugo | 80 | 2,596,000,000 |
| 3 | Matrekta ya mkono (*Power Tillers*) | 0 | 0 |
| 4 | Ukarabati wa zana za kilimo | 4 | 60,000,000 |
| 5 | Miundombinu ya kilimo, mifugo na uvuvi | 6 | 600,000,000 |
| 6 | Fedha za kuendeshea shughuli za shamba | 3 | 90,000,000 |
| 7 | Kununua ardhi kwa ajili ya kilimo, mifugo na ufugaji wa samaki | 3 | 120,000,000 |
| 8 | Zana unganishi | 3 | 165,000,000 |
| 9 | Zana za kusindika na vifungashio vya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi | 5 | 200,000,000 |
| | **JUMLA** | | **7,781,000,000** |

***Chanzo:*** *Mfuko wa Taifa wa Pembejeo.*

**114.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefadhili na kufundisha wanafunzi 2,000 kwenye mafunzo ya kilimo ngazi ya Astashahada na Stashahada katika Vyuo vya Ilonga, Mlingano, Mtwara, Tumbi, Ukiriguru, Uyole, HORTI Tengeru, Mubondo, Maruku, KATC Moshi, Igurusi, KATRIN, Chuo cha Sukari Kidatu na Inyala. Vilevile, Wizara imedahili wanafunzi 456 wanaojilipia wenyewe ngazi ya Astashahada na Stashahada. Wanafunzi wa mwaka wa pili ngazi ya Stashahada ni 275 na ngazi ya Astashahada ni 904 ambao wanategemea kuhitimu masomo yao mwezi Juni 2017. Kozi wanazosomea ni Astashahada na Stashahada ya Kilimo, Stashahada ya Umwagiliaji, Matumizi Bora ya Ardhi, Uzalishaji Chakula na Lishe, Matumizi ya Zana za Kilimo, Uzalishaji wa Mazao, Mboga, Maua na Matunda. Pia Wizara kupitia Mradi wa PHRD imejenga miundombinu kwa ajili ya kuandaa shamba la mfano kwa mafunzo ya teknolojia mbalimbali za umwagiliaji (*Irrigation Demonstration Pilot*) pamoja na ujenzi wa mfumo wa kusambaza maji kwenye chuo cha Kilimo Igurusi.

**115.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia mradi wa kuongeza uzalishaji na tija katika zao la mpunga (ERPP) imefanya uhamasishaji wa upatikanaji wa pembejeo kwa viongozi wa Halmashuri pamoja na wakulima viongozi wa skimu za umwagiliaji za Njage, Msolwa Ujamaa, Mvumi, Kigugu na Mbogo-Komtonga katika halmashauri za Mvomero, Kilosa na Kilombero mkoani Morogoro ambapo wakulima watachangia asilimia 20 wakati wa kukabidhiwa pembejeo na wakala, na asilimia 30 watalipa baada ya mavuno ambapo asilimia 50 watalipiwa na Wizara. Aidha, Wizara imetoa mafunzo ya kilimo bora cha mpunga kupitia mfumo wa shadidi mkoani Morogoro kwa wataalam 70 kuanzai ngazi ya Mkoa na Hamashauri. Mafunzo yalihusisha Afisa Ushauri kilimo Mkoa, Mhandisi umwagiliaji Mkoa, Maafisa Kilmo Wilaya, Maafisa mazao Wilaya, Wahandisi umwagiliaji Wilaya. Vilevile mafunzo yalihusisha maafisa ugani pamoja na mafundi sanifu umwagiliaji kutoka skimu za umwagiliaji za Njage, Msolwa Ujamaa, Signali, na Mkula (Kilombero), Lupilo, Minepa, Euga (Ulanga); Tindiga, Mwasa, Mwega, Lumuma, Chanzuru, Ilonga, Madizini, Mvumi (Kilosa); Kiroka,

Mbarangwe (Morogoro) na Kigugu, Mbogo Komtonga Mkindo A, Mkindo B, Dihombo (Mvomero).

**116.** Aidha Wizara imetoa elimu ya kilimo bora cha mpunga kupitia mfumuo wa shadidi kwa wakulima wawezeshaji 100 kutoka skimu za Njage, Mbogo Komtonga, Mvumi, Kigugu na Msolwa Ujamaa. Wakulima hawa walikwenda kufundisha wakulima wenzao kupitia mashamba darasa na kufikia idadi ya wakulima 454. Wizara kwa kupitia mradi wa ERPP itatoa mafunzo kwa wakulima 4,800 kuhusu kilimo bora cha mpunga kupitia mfumo wa shadidi kutoka katika skimu 22 za umwagiliaji mkoani Morogoro na kuanzisha mashamba darasa (FFS) 80. Baada ya mafunzo wakulima watapatiwa pembejeo za kilimo kwa njia ya uchangiaji. Wizara itatoa mafunzo ya kilimo shadidi (SRI) kwa wataalam 50 pamoja na kuwezesha ziara ya mafunzo kwa wakulima viongozi 200 na wataalam 40 kutoka wizarani, mkoani na Halmashauri zinazotekeleza mradi.

**117.** ***Mheshimiwa Spika,*** Vilevile, Wizara imeratibu maonesho ya kilimo ya Nanenane Kitaifa Mkoani Lindi katika viwanja vya Ngongo, ambapo wakulima walifundishwa teknolojia mbalimbali za kilimo. Aidha maonesho hayo yalifanyika kikanda katika viwanja vya John Mwakangale - Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya, Nzuguni - Kanda ya Kati Dodoma, Mwalimu Julius Nyerere - Kanda ya Mashariki - Morogoro na Themi - Kanda ya Kaskazini Arusha.

**118.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itafadhili na kufundisha wanafunzi 2,200 kwenye mafunzo ya kilimo ngazi ya Astashahada na Stashahada katika vyuo vya Ilonga, Mlingano, Mtwara, Tumbi, Ukiriguru, Uyole, HORTI Tengeru, Mubondo, Maruku, KATC Moshi, Igurusi, KATRIN, Chuo cha Sukari Kidatu na Inyala. Pia Wizara itakarabati miundombinu ya vyuo vya Maruku na Mubondo ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.

**119.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itafuatilia utekelezaji wa mradi wa TANRICE - 2 *(Project for supporting Rice Industry)* unaofundisha wakulima kwenye skimu teule

za mpunga kupitia vyuo vya mafunzo ya kilimo vya KATC – Moshi, Ukiriguru – Mwanza, Tumbi – Tabora, Ilonga – Morogoro, Mtwara, Igurusi – Mbeya. Vilevile, Wizara itawezesha kufanyika kwa kikao cha kamati ya pamoja ya uratibu wa mradi (*Joint Coordinating Committee*) kati ya Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) na Wizara.

**120.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kusimamia huduma za ugani na kuboresha usambazaji wa teknolojia za kilimo bora kwa wakulima kwa kutumia njia mbalimbali hususan shamba darasa na utoaji wa ushauri wa kitaalam, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa kazi za Ugani katika Halmashauri 168. Pia Wizara itawezesha vituo vya Inyala (Mbeya), Ichenga (Njombe), Bihawana (Dodoma), Mkindo (Morogoro) na viwanja vya maonesho ya kilimo (Nanenane) ili kutoa mafunzo kwa wakulima wengi zaidi. Pia kwa kupitia Programu ya ASDP II itafanya tathmini ya mahitaji ya Vituo vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (WARCs) na kufundisha teknolojia ya kilimo cha Zabibu ili kuongeza uzalishaji na tija kwa wakulima viongozi 200 na Maafisa Ugani 20.

**121.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutoa ushauri wa kitaalam na kuandaa miongozo na mafunzo ya huduma za ugani na kuboresha usambazaji wa teknolojia za kilimo bora kwa wakulima kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo utoaji wa ushauri wa kitaalam, ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa kazi za Ugani katika Halmashauri 168. Kuwezesha vituo vya Inyala (Mbeya), Ichenga (Njombe), Bihawana (Dodoma), Mkindo (Morogoro) na viwanja vya maonesho ya kilimo (Nanenane) ili kutoa mafunzo kwa wakulima wengi zaidi.

***VVU na UKIMWI***

***122.*** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI mahali pa kazi, Wizara imeendelea kuwahamasisha watumishi kupima afya ili kutambua hali zao. Katika mwaka 2016/2017 watumishi 17 wanaoishi na VVU wameendelea kupata huduma za lishe

na dawa. Aidha, mwezi Januari, 2017 watumishi wawili (2) walistaafu na kuwa na idadi ya watumishi 15 ambao Wizara inaendelea kuwahudumia watumishi hao kulingana na miongozo ya Serikali.

**123.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018 Wizara itaendelea kuwahamasisha watumishi kupima afya zao na itaendelea kuwawezesha watumishi 15 waishio na virusi vya Ukimwi kupata huduma za afya na lishe bora.

***Jinsia***

**124.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo - SUA kupitia mradi wa "*Sweet potato Fast Truck*" ilitoa mafunzo kwa wadau wa kilimo 36 wa Kanda ya Ziwa na Mashariki ya uhusishi wa Jinsia katika miradi ya kilimo ikiwemo viazi vitamu ambapo Mwongozo wa Jinsia wa 2015 wa Wizara umetumika kufundishia. Lengo la mafunzo ni kuhakikisha mahitaji ya mkulima wa kike, kiume na vijana yanazingatiwa katika Sekta ya Kilimo.

***3.5 Kuongeza Ushiriki wa Vijana Katika Kilimo***

**125.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kuongeza Ushiriki wa Vijana Katika kilimo ili kutatua tatizo la ajira nchini. Wizara kupitia RUBADA kwa kushirikiana na *Sokoine University Graduate Entrepreneurs Cooperatives* (SUGECO), Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji imefundisha vijana wapatao 261 katika Kambi ya Vijana ya Mkongo elimu na stadi za kazi katika uzalishaji wa mazao ya bustani na ufugaji wa mbuzi, kuku wa kienyeji, nyuki na Sungura pamoja na kilimo cha bustani kwa kutumia nyumba ya kioo ya kuzalisha mimea (*Greenhouse farming*). Katika kuhakikisha eneo la Kambi linakuwa na miundombinu muhimu eneo hilo limewekwa miundombinu ya umwagiliaji wa matone, umeme wa nguvu za jua, kisima cha maji, jengo la jiko la shamba na bustani ya maonesho (*demonstration plot)* kwa ajili ya kilimo cha

zao la muhogo na uzalishaji wa mbegu za muhogo. Mbegu za muhogo zinazopatikana zinasambazwa kwa vikundi vya vijana katika vijiji vya jirani. Zaidi ya vijiji 20 vya vijana vimeanzishwa katika wilaya mbalimbali baada ya kupata mafunzo kwenye kambi hii, baadhi ya vikundi hivyo ni kama RUSUYA (Mkuranga), RUYOFO, Faraja Group, Kiemi Group na Amani Group (Rufiji), Maisha Youth Agriculture Group (Bagamoyo), Viwawaki (Kisarawe) na New Vision Group (Kibaha) ambapo vikundi vinne (4) vimeunganishwa na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi.

**126.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kuona umuhimu wa kutoa elimu ya kilimo kwa jamii kupitia kambi hii, Wizara kupitia RUBADA kwa kushirikiana na SUGECO imeanza ushirikiano na majirani wanaozunguka kambi ikiwemo shule ya sekondari Mkongo, Aidha, mpaka sasa imeshaanzishwa *club* ya Kilimo ya Wanafunzi 270 ambao kambi itashirikiana nao kwa kuwapa elimu ya kilimo na kuanzisha mashamba ya mfano pale shuleni. Mashamba hayo yatasaidia kubadili mitizamo na fikra za vijana juu ya kilimo na kujenga kizazi kinachothamini kilimo.

**127.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018 Wizara kwa kushirikiana na Wizara za kisekta pamoja na wadau wengine wakiwemo Wabia wa Maendeleo na Sekta Binafsi itaendelea kutekeleza Mkakati Kabambe wa miaka mitano wa Vijana kushiriki katika kilimo lengo kubwa likiwa ni kutatua tatizo la ajira. Aidha, Wizara itatekeleza maazimio yaliyofikiwa katika mkutano wa kilele cha kuhamasisha vijana kushiriki katika kuleta mapinduzi ya kilimo kilichoitwa "*Young Africa Summit*" uliofanyika mjini Kigali-Rwanda mwezi Oktoba, 2016. Maazimio hayo, yanayohusu kuhamasisha matumizi ya teknolojia katika kilimo, kuzingatia masuala ya jinsia pamoja na kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi (*Climate Smart Agriculture*). Mkutano huo uliandaliwa na Shirika Binafsi la Canada linalojulikana kama *"MasterCard Foundation*" ambapo Tanzania ilikuwa nchi pekee iliyotolewa mfano wa kuigwa katika Afrika Mashariki na Kusini mwa Jangwa la Sahara kubuni Mkakati wa aina hiyo.

### 3.6 Kuratibu na Kuboresha Matumizi Endelevu ya Ardhi ya Kilimo kwa Kutenga, Kupima na Kumilikisha Maeneo Hayo kwa Wakulima

**128.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mradi wa *Lake Victoria Environmental Management Project II* (LVEMP II) imetoa mafunzo yanayohusu teknolojia za hifadhi ya udongo na maji mashambani kwa vikundi 27 vyenye wakulima 969 katika Wilaya ya Meatu Mkoani Simiyu. Aidha kutokana na mafunzo hayo wakulima wameweza kuzuia mmomonyoko wa udongo mashambani kwa kutengeneza makinga maji.

**129.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi inaendelea kupima mashamba ya wakulima 850 wanaozunguka shamba la uwekezaji la Mkulazi lililopo Halmashauri ya Wilaya Morogoro ili kupata hati ya hakimiliki za kimila. Wizara pia imeshiriki katika timu ya kitaifa inayoshughulikia utatuzi wa migogoro ya ardhi ili kuandaa taarifa itakayotumika kupanga mikakati ya kudumu ya namna ya kumaliza tatizo la migogoro ya ardhi. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maji na Umwagiliaji katika kutekeleza mradi wa*"Securing Watershed Services Through Sustainable Land Management in the Ruvu and Zigi Catchments*" imeainisha matatizo ya ardhi ya kilimo yanayoathiri uzalishaji katika kijiji cha Kibangile (Morogoro) na Manza (Mvomero) ambavyo viko katika lindimaji la mto Ruvu Mkoani Morogoro na kuandaliwa mpango wa utatuzi. Mpango huo utatekelezwa na wanavijiji wenyewe baada ya kujengewa uwezo.

**130.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia mradi wa *Resilient Natural Resources Management for Growth* (REGROW) imeandaa mtaala wa kufundisha namna bora ya kuendesha mafunzo ya shamba darasa yenye lengo la kupunguza matumizi ya maji mashambani kwenye vijiji vinavyozunguka skimu za umwagiliaji katika uwanda wa Usangu ili kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabianchi.

**131.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeshiriki kuandaa Mpango Kazi wa Usimamizi na uratibu wa pamoja wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi nchini utakaotekelezwa na Sekta za Umma na Sekta Binafsi kuanzia mwaka wa fedha wa 2017/2018 chini ya uratibu wa Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi. Utekelezaji wa Mpango Kazi huo utaongeza ufanisi katika kupanga na kusimamia matumizi ya ardhi nchini, kuboresha taarifa za mipango na kanzidata ya mipango iliyopo na kuchangia katika juhudi za serikali za kupunguza migogoro ya ardhi kati ya makundi mbalimbali ya watumiaji wa ardhi nchini.

**132.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara iko katika hatua za mwisho za kuanza kazi za kuainisha shughuli mbalimbali zinazofanywa ili kutunza vyanzo vya maji na pia kuchagua njia au mbinu bora zaidi kwa ajili ya kuzisambaza maeneo mengine ya vyanzo vya maji Tanzania yakiwemo maeneo ya SAGCOT. Pia wizara imehamasisha Mfumo wa Hifadhi ya Mazingira na Jamii (*Environmental and Social Management Framework*); Mfumo wa Sera ya Makazi Mapya (*Resettlement Policy Framework*) pamoja na mpango shirikishi wa kudhibiti visumbufu vya mimea (*Integrated Pest Management Plan*) kwa watekelezaji wa Mradi wa ERPP walioko katika ngazi ya Taifa, Wilaya, Skimu pamoja na wakulima.

**133.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi Wizara imeandaa Mwongozo wa Kilimo kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi (*Climate Smart Agriculture Guideline*) ambao utaongoza utekelezaji wa Programu ya Taifa ya Kilimo kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi (2015 – 2025). Mwongozo huo upo kwa Mhariri ambao ukikamilika utasainiwa na hatimaye kuchapishwa na kusambazwa kwenye Halmashauri za Wilaya.

**134.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia kwa kushirikiana na *African Climate Smart Agriculture Alliance* (ACSAA) ilifanikiwa kuendesha Warsha ya wadau wa kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi na kusababisha kuanzishwa kwa chombo cha uratibu wa shughuli za ukabili na uhimili wa mabadiliko ya tabianchi nchini (*Tanzania Climate Smart*

*Agriculture Alliance - TCSAA*). Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na CIAT, DfID na Benki ya Dunia wamekamilisha rasimu ya kwanza ya *Climate Smart Agriculture Profile* ya Tanzania ambayo itatumika kuvutia uwekezaji katika kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi.

**135.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018**,** Wizara ina jukumu la kupanga na kusimamia matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo kwa lengo la kuongeza tija ya ardhi na uzalishaji wa mazao. Ili kuendeleza jukumu hilo, Wizara itaendelea kuandaa mipango ya kina ya matumizi bora ya ardhi ya kilimo kwa kupima mashamba na ubora wa udongo, kuzuia mmomonyoko wa udongo na kutoa elimu kwa wataalamu wa Halmashauri zenye vijiji vinavyozunguka mashamba makubwa ya kibiashara ya Pangani (Pangani), Bagamoyo (Bagamoyo), Mkulazi (Morogoro vijijini), Lukulilo (Rufiji) na Kitengule (Karagwe). Mafunzo yatakayotolewa yatahusu teknolojia mbalimbali za matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo na uanzishaji wa Kanzidata ya ardhi ya kilimo.

**136.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia itajenga uwezo wa wakulima kuhusu mbinu na teknolojia za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi katika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Tabora, Lindi, Mtwara, Iringa na Mbeya. Aidha, Wizara itasambaza Mwongozo wa Kilimo Kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi (*CSA guideline*) katika baadhi ya mikoa. Wizara kupitia Mradi wa ERPP itaandaa na kusambaza Mwongozo wa Hifadhi ya Mazingira na Mpango Shirikishi wa Kudhibiti Visumbufu vya Mimea na Matumizi sahihi ya Viuatilifu kwenye skimu tano (5) za umwagiliaji za Mbogo komtonga, Kigugu, Mvumi, Njage na Msola Ujamaa.

### *3.7 Kuunda na Kupitia Sera, Mikakati na Mifumo ya Kisheria Katika Sekta Ndogo ya Mazao*

**137.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017 Wizara imeendelea na hatua za kuboresha mazingira ya kisera, Sheria, kanuni na mikakati mbalimbali katika kilimo ili kuimarisha utendaji kazi na huduma inazozitoa kwa

wakulima, wasindikaji, wafanyabiashara wa mazao na jamii kwa ujumla. Katika jitihada za kuwezesha upatikanaji na matumizi ya mbolea na mbegu bora, Wizara kwa kushirikiana na Sekta Binafsi na Wadau wa Maendeleo ilipitisha Marebisho ya Kanuni za Mbolea (*The Fertilizers (Amendments)Regulations, 2017*) ili kupunguza muda na gharama za kusajili mbolea. Kufuatia marekebisho hayo, mbolea mpya kutoka nje ya nchi itafanyiwa majaribio kwa msimu mmoja tofauti na ilivyokuwa awali ambapo majaribio yalikuwa kwa misimu mitatu. Aidha, gharama za majaribio ya mbolea mpya zimepungua kutoka Dola za Kimarekani 30,000 mpaka Dola 10,000. Ili kuwezesha upatikanaji wa mbolea kwa bei nafuu na kwa wakati, Wizara kwa kushirikiana na wadau imepitisha Kanuni za Ununuzi wa Mbolea wa Pamoja (*The Fertilizers Bulk Procurements Regulations, 2017*).

**138.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara pia imefanya mapitio ya Kanuni za Mbegu, 2007 kwa marekebisho ya Kanuni za Mbegu (*Seed Amendments Regulations, 2016)*. Kanuni hizo zimerekebishwa ili kuipa Taasisi ya Udhibiti wa Mbegu (TOSCI) mamlaka zaidi ya udhibiti wa mbegu na kupunguza viwango vya gharama zinazohusu shughuli za udhibiti wa mbegu. Ili kuwezesha mbegu kupatikana kwa wingi kwa wakulima, Wizara imepitisha Waraka wa kuwezesha Sekta binafsi kutumia mbegu zenye Hakimiliki zinazozalishwa na vituo vya Utafiti vya Umma. Wizara imeendelea kutoa mafunzo kwa wataalamu wanaohusika na utekelezaji wa sheria mbalimbali za sekta ya kilimo ili kuwezesha sheria hizo kutekelezwa kikamilifu. Aidha, Wizara imefanya utafiti wa kina wa kisera na kisheria ili kubaini mapungufu yaliyopo katika mfumo wa utekelezaji wa Sera na Sheria zilizopo kwa lengo la kupendekeza marekebisho. Vilevile, Katika kuimarisha utafiti wa mazao ya kilimo, Serikali imepitisha Sheria ya Kuanzisha Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Kilimo Tanzania (TARI) yenye hadhi ya kujitegemea kiasi *(semi-autonomous).* Taasisi hii itawezesha kuboresha rasilimali watu, miundombinu na rasilimali fedha katika kutekeleza shughuli za utafiti kwa ufanisi zaidi na kwa wakati.

**139.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018 Wizara

itaendelea kuboresha mazingira ya kisera na Sheria katika sekta ya kilimo ili kuimarisha utendaji kazi na huduma inazozitoa kwa wakulima, wasindikaji, wafanyabiashara na jamii kwa ujumla. Katika mpango huo, Wizara itaandaa mapendekezo ya kufanya marekebisho ya Sheria ya Mbegu, 2003; Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Viutatilifu vya Kitropiki ya mwaka, 1979; Sheria ya Hifadhi ya Mimea ya mwaka 1997; Sheria ya Mfuko wa Pembejeo wa Taifa ya mwaka 1994; na Sheria ya Usalama wa Chakula ya mwaka 1991. Aidha, Wizara inatarajia pia kuwasilisha Bungeni miswada ya Sheria mpya za Kulinda na Kusimamia Nasaba za Mimea kwa ajili ya Kilimo na Chakula; Sheria Usimamizi wa Ardhi ya Kilimo; Sheria ya Usimamizi wa Kilimo cha Mkataba; Sheria ya Zana za Kilimo na Sheria ya Kusimamia Huduma za Ugani. Aidha, Serikali inakusudia pia kuweka mfumo wa kisheria wa kuratibu Maonesho ya Kilimo (NaneNane) ili kuyafanya Maonesho hayo yawe endelevu na yenye tija kwa wakulima na wadau kwa ujumla. Ili kuwajengea uwezo wasimamizi wa Sheria na kusaidia upatikanaji wa huduma bora zakilimo, Wizara itatoa mafunzo kwa wakaguzi wa mbolea, mbegu na viutilifu vya kilimo. Vilevile, katika jitihada za kuimarisha uwezo wa wataalam kuandaa mapendekezo mbalimbali yanayohitaji maamuzi ya Serikali na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika mwaka 2017/2018 Wizara itaandaa mafunzo maalum ya namna ya kuandaa mapendekezo yanayohitaji maamuzi ya ngazi hizo kulingana na miongozo iliyopo ili kuendelea kukabiliana na changamoto mbalimbali katika kilimo.

### *3.8 Kuwezesha Uwekezaji wa Sekta Binafsi Katika Kilimo*

**140.** ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali katika kuendeleza utekelezaji wa Sera ya mashirikiano kati ya Sekta ya Umma na Binafsi hasa kwenye Ukanda wa SAGCOT imeweza kuendeleza kongani sita (*Six Clusters*) zenye tija katika uzalishaji, uongezaji wa thamani wa Mazao, upatikanaji wa wasambazaji wa pembejeo, Masoko na watoa huduma mbalimbali (*Key Private Service Providers*). Kongani hizo ni Ihemi (Iringa), Ludewa (Njombe), Mbarali (Mbeya), Rufiji (Pwani), Kilombero (Morogoro) na Sumbawanga (Rukwa).

**141.** ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua umuhimu wa kongani hizo, Kituo cha SAGCOT kimeweza kuwaunganisha wakulima na wadau wa kilimo ili kuleta tija, kuongeza kipato kwa wakulima na kuongeza chakula na lishe kwenye kaya za wakulima wa Viazi vitamu, Soya, Nyanya, Chai na wafugaji wa ng'ombe wa maziwa (*High potential commodities in clusters).* Katika mwaka wa fedha 2016/17, Kituo cha SAGCOT kimefanikiwa kufanya yafuatayo:

(i) Hekta 38,477 za Mazao zimelimwa kwa kutumia Teknolojia Bora za Kilimo kama vile utumiaji wa mbegu bora na matumizi ya njia bora na za kisasa za Umwagiliaji.

(ii) Wakulima wadogo 16,384 wamefikiwa na Kampuni Binafsi zinazoshirikiana na SAGCOT na wameshirikishwa kwa kutumia njia mbalimbali za ushirikishwaji.

(iii) Jumla ya fursa mpya za ajira za kudumu 547 zimetolewa kupitia shughuli za uongezwaji thamani wa mazao kupitia Kampuni Binafsi 17 zinazoshirikiana na Kituo cha SAGCOT.

(iv) Mapato yatokanayo na mazao yamefikia takribani Shilingi Bilioni 880 sawa na Dola za Kimarekani Bilioni 0.4 kwa mwaka.

(v) Wakulima 752 wamepatiwa mafunzo juu ya Kilimo Bora, mfano Kikundi cha Mtanga Iringa Vijijini kinacholima Viazi Mviringo na Kikundi cha kina mama kinacholima Soya Ludewa Mkoani Njombe.

(vi) Hadi kufikia Desemba, 2016 mashirikiano mapya 14 yamesainiwa na kufikisha jumla ya washiriki (SAGCOT Partners) 104.

(vii) Mikataba yenye thamani ya Shilingi Bilioni 154 sawa na Dola za Kimarekani Milioni 70 imesainiwa kati ya Serikali na Benki ya Dunia.

***Tozo na Ada Katika Sekta Ndogo ya Mazao ya Kilimo***

**142.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017,

Serikali imefuta baadhi ya kodi na tozo ambazo zimekuwa ni kero katika sekta ndogo ya mazao ambazo ni pamoja na ada ya leseni ya kusindika Kahawa ya Dola za Kimarekani 250. Kwa upande wa zao la Pamba, mchango wa Mwenge kwa kila kiwanda cha kuchambua pamba wa Shilingi 450,000 umefutwa. Katika zao la Chai kodi ya moto na uokoaji imefutwa. Aidha, kwa zao la korosho, ushuru ufuatao umefutwa; Chama Kikuu cha Ushirika wa Shilingi 20 kwa Kilo; Kusafirisha korosho Shilingi 50 kwa kilo; Gharama za Mtunza Ghala Shilingi 10 kwa Kilo; Kikosi Kazi kwa ajili ya ufuatiliaji Shilingi 10 kwa Kilo na makato ya unyaufu. Aidha, Serikali imeondoa ushuru wa forodha wakati wa kuagiza soya inayotumika katika utengenezaji wa vyakula vya mifugo na unga wa lishe.

**143.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, mpango wa Serikali ni kuhakikisha kodi, tozo na ada ambazo ni kero kwa wakulima, wafugaji na wavuvi zinafutwa na kubaki na zile zenye mahusiano ya moja kwa moja na uendelezaji wa tasnia husika. Kwenye Sekta ndogo ya mazao, katika mwaka 2017/2018 Serikali itafuta jumla ya tozo 80 kati ya tozo 139 ambazo zimeonekana kuwa kero kwa wakulima na pia itapunguza viwango vya tozo nne (4) zilizopo. Katika maamuzi hayo, kwenye tasnia ya tumbaku, jumla ya tozo 10 zitafutwa na tozo mbili (2) zitapunguzwa viwango; katika tasnia ya kahawa, jumla ya tozo 17 zitafutwa na tozo moja (1) itapunguzwa kiwango; na katika tasnia ya sukari, jumla tozo 16 zitafutwa. Aidha, katika tasnia ya pamba tozo zitakazofutwa ni mbili (2) na katika tasnia ya korosho tozo zitakazofutwa ni mbili (2) na tozo moja (1) iliyokuwa kero itafutwa katika tasnia ya chai.

**144.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za Serikali kuongeza upatikanaji wa pembejeo, Serikali itafuta tozo tatu (3) kwenye mbolea na moja (1) itapunguzwa kiwango. Aidha, tozo saba (7) zilizokuwa kwenye mbegu zitafutwa. Vilevile, tozo pekee iliyokuwepo katika Mfuko wa Pembejeo ya Ada ya Nyaraka nayo itaondolewa. Katika kuimarisha maendeleo ya Ushirika nchini, Serikali itafuta tozo 20 zilizokuwepo katika Ushirika katika ngazi mbalimbali. Orodha kamili ya tozo

zilizofutwa katika kila eneo ni kama ilivyo katika **Kiambatisho Na: 7a, 7b na 7c.**

**145.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nilihakikishie Bunge lako tukufu, kuwa Serikali itaendelea kuchambua kwa kina tozo, ushuru na ada mbalimbali zilizobaki zinazotozwa katika kilimo, mifugo na uvuvi kwa lengo la kuangalia uhalali wa kuwepo kwake na viwango vya tozo, ushuru na ada hizo kwa lengo la kuziondoa au kuzipunguza ili kuwapunguzia wakulima, wafugaji na wavuvi mzigo wa tozo, ushuru na ada zisizokuwa na tija.

### *3.9 Kuimarisha Uratibu, Ufuatiliaji na Tathmini Katika Sekta ya Kilimo*

**146.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushiriana na AU – CAADP, SADC na EAC imeendelea kuratibu masuala mbalimbali ya kilimo kikanda na kimataifa ambapo mifumo ya Tathmini, Utekelezaji, Ushirikishwaji wa Sekta Binafsi na Wadau mbalimbali wa kilimo imeboreshwa. Aidha, Wizara imeendelea kuratibu utekelezaji wa mradi wa ERPP ambao hutekelezwa Tanzania Bara na Zanzibar.

### Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili

**147.** ***Mheshimiwa Spika,*** maandalizi ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) itakayotekelezwa katika kipindi cha miaka kumi yamekamilika mwezi Desemba, 2016. Programu hiyo inatarajiwa kuanza utekelezaji rasmi katika mwaka wa 2017/2018. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Benki ya Dunia imeanzisha Mradi wa *Catalyzing the Future Agri-Food Systems of Tanzania – CFAST* unaolenga kuendeleza skimu za umwagiliaji 20 katika Ukanda wa SAGCOT kwenye Mikoa ya Iringa, Mbeya, Rukwa na Katavi kuanzia mwaka 2017/2018. Mradi wa CFAST unalenga kuchangia lengo kuu la awamu ya pili ya programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (*ASDP II*) la kubadili Sekta ya Kilimo ili kuwa na tija zaidi, kukuza viwanda, kuongeza mapato ya wakulima wadogo na kuboresha hali ya maisha, kuwa na uhakika wa chakula na kuboresha lishe.

Aidha, CFAST italenga kuendeleza mnyororo wa thamani wa zao la mpunga pamoja na mseto (*diversification*) utakaofanyika katika skimu za umwagiliaji kama vile kilimo cha mboga, matunda, ufugaji wa samaki na uyoga ili kupanua wigo wa uzalishaji, kuongeza mapato na kuboresha lishe kwa Wananchi.

**148.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeanzisha mfumo wa ukusanyaji wa Takwimu za Kilimo, Mifugo na Uvuvi unaotumika kwenye Halmashauri za Wilaya 187 nchini (ARDS) na mafunzo yametolewa mwezi Februari, 2017 kwa Maafisa Takwimu, Ufuatiliaji na Tathmini wa Halmashauri zote pamoja na Maafisa Kilimo na Mifugo wa Mikoa yote ya Tanzania Bara. Mafunzo hayo yametolewa kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan (JICA) ambao ndio wafadhili wakuu wa mfumo huo. Wizara pia imekamilisha mfumo wa NAMIS utakaojumuisha takwimu na taarifa za uzalishaji wa mazao, masoko na matumizi bora ya Ardhi ya Kilimo kutoka kwenye mifumo mbalimbali ya TEHAMA ili kuongeza tija katika utendaji kazi. Aidha, Wizara inaendelea kuweka na kusimamia miundombinu ya TEHAMA katika Ofisi za Dodoma, kuratibu mfumo wa barua pepe kwa watumishi wa Wizara, Kanzidata ya ARDS na Tovuti ya Wizara.

**149.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Program ya ASDP II itaendelea kutekeleza Mpango wa Uwekekezaji katika Sekta ya Kilimo Nchini (*Tanzania Agriculture and Food Security Investment Plan - TAFSIP)* ambapo mpango huo ndio hutekeleza nguzo nne za CAADP na Azimio la Malabo zinazolenga kuendeleza Sekta ya Kilimo kwa bara la Afrika. Vilevile Wizara itaendelea kutekeleza maamuzi mbalimbali yatokanayo na wakuu wa nchi likiwemo Baraza la Mawaziri ili kuendelea kuboresha Sekta ya kilimo nchini. Aidha, Wizara itaendelea na uratibu wa mradi wa ERPP ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa mradi huo Bara na Visiwani.

**150.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia ASDP II itaendelea kuratibu utekelezaji wa miradi ya kilimo katika ngazi ya Taifa na Halmashauri kupitia Mipango ya Maendeleo

ya Kilimo ya Wilaya (DADPs). Sambamba na kazi hiyo, Wizara itaboresha taarifa ya viashiria vya matokeo (ASDP II *Results Framework*) kwa ajili ya kupima ufanisi wa utekelezaji wa Programu hiyo. Aidha, kwa kushirikiana na Wabia wa Maendeleo na Wadau wengine wa Sekta ya Kilimo, Wizara itaandaaa miradi katika maeneo 24 ya kipaumbele ya ASDP II. Vilevile, Wizara itaendelea kuratibu Mapitio ya Sekta ya Kilimo (*Agriculture Joint Sector Review – AJSR*) na (*Public Expenditure Review – PER*) na kufuatilia matumizi ya fedha katika miradi mbalimbali (*Expenditure Tracking*). Pia Wizara itafanya tathmini kubaini mafanikio na changamoto za utekelezaji wa Mfumo wa Pamoja wa Hifadhi na Uuzaji (COWABAMA); kutathmini matumizi ya Vituo vya Kata vya Rasilimali ya Kilimo (WARCs) katika kuimarisha utoaji wa huduma za ugani; na kufanya uchambuzi wa mazao katika mnyororo wa thamani (*Crop Value Chain Analysis*).

**151.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itatekeleza na kusimamia mfumo wa uendeshaji na uratibu wa ASDP II katika ngazi zote za utekelezaji (kuanzia kijijini hadi Taifa). Mfumo huu utawezesha kuwepo kwa uratibu wa shughuli zinazofanywa na Serikali kwa ushirikiano na wadau wengine kama vile; Wabia wa Maendeleo, Sekta Binafsi na Asasi zisizo za Kiserikali kwa kuoanisha mifumo ya Kikanda na Kimataifa. Aidha, mfumo huu unahusisha Kamati ya Uendeshaji wa Programu (*ASDP II Steering Committee*), Kamati ya Wataalam ya Wakurugenzi (*Technical Committee of Directors*), Vikosi Kazi (*Thematic Working Groups*), Timu ya Uratibu wa Programu (*Coordination and Management Team*) ambayo itahusika na kuratibu matukio na tathmini, mapitio ya pamoja ya Sekta ya Kilimo (*Joint sector Review*), mkutano wa mashauriano wa wadau wa Sekta ya Kilimo (*Agricultural Sector Consultative Group*), na hatimaye Mkutano wa Kitaifa wa Wadau wa Kilimo (*National Agricultural Sector Stakeholders Meeting*). Mfumo huu utawezesha Wizara kusimamia miradi mingi ndani ya Sekta ya Kilimo ambayo inatekelezwa na Serikali, mashirika ya umma, Sekta Binafsi na Taasisi zisizo za Kiserikali. Aidha, Kitengo cha Uratibu wa Wafadhili katika Sekta ya Kilimo (DAC) kwa kuhusisha maeneo mbalimbali ya ushirikiano wa

nchi na wafadhili wa maendeleo na Sehemu ya Ufuatiliaji, Tathmini na Takwimu (*Monitoring, Evaluation and Statistics – MES*) ya Wizara vitaimarishwa kwa kuongezewa rasilimali ili kufanikisha majukumu yake.

**152.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika kuhakikisha uzoefu na matokeo chanya yaliyojitokeza katika utekelezaji wa SAGCOT katika Ukanda wa Kusini itatumia uzoefu huo katika utekelezaji wa ASDP Awamu ya Pili kuandaa Ukanda katika maeneo mengine ya nchi.

**FUNGU 99**

**153.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa sekta ilitekeleza maeneo ya kipaumbele yaliyohusu sera; mikakati; sheria na kanuni zake; programu za maendeleo; uzalishaji wa mifugo na usindikaji wa mazao yake; udhibiti wa magonjwa mbalimbali ya mifugo, utafiti na mafunzo. Maeneo ya kipaumbele yaliyotekelezwa ni pamoja na:

(i) Kuongeza upatikanaji na matumizi ya pembejeo na zana za mifugo;

(ii) Kuboresha huduma za ugani, utafiti na mafunzo;

(iii) Kuendeleza na kuboresha miundombinu ya mifugo; malisho na nyanda za malisho;

(iv) Kuboresha upatikanaji wa masoko na kuongeza thamani ya mazao ya mifugo;

(v) Kuimarisha na kujenga ushirika na hasa ule wa vyama vya wafugaji;

(vi) Kuimarisha uwezo wa taasisi na mifumo ya taarifa kwa ajili ya maendeleo na usimamizi wa sekta za mifugo; na

(vii) Kujenga mazingira mazuri kwa ajili ya kukuza uwekezaji wa sekta binafsi katika sekta ya mifugo.

### *3.10 Sera, Mikakati na Programu*

**154.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu, kupitia na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria, mikakati na programu mbalimbali za kuendeleza sekta ya mifugo. Katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kutoa elimu kwa wadau 1,800 kuhusu Sera ya Taifa ya Mifugo ya mwaka 2006 na Mkakati wa Taifa wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo wa mwaka 2011. Aidha, imesambaza kwa wadau nakala 200 za Sera ya Taifa ya Mifugo, nakala 100 za Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Mifugo na nakala 150 za Fursa za Uwekezaji katika sekta ya mifugo. Pia, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imekamilisha kuandaa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo nchini Awamu ya Pili (ASDP II) mwezi Desemba, 2016 ya miaka kumi na itatekelezwa kwa awamu mbili ya miaka mitano kila moja. Programu hii itatekelezwa na Serikali pamoja na wadau wengine, wakiwemo washirika wa maendeleo, sekta binafsi na Taasisi zisizo za Serikali (NGOs) na inatarajiwa kuanza kutumika rasmi mwezi Julai, 2017.

**155.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara kwa kushirikiana na wadau ilianza kutekeleza Mpango Bunifu wa Modenaizesheni ya Sekta ya Mifugo Tanzania (*Tanzania Livestock Modernisation Initiatives –TLMI*) wa mwaka 2015. Lengo kuu la mpango huu ni kuongeza usalama wa chakula na lishe, kuongeza ajira, kuchangia zaidi katika uchumi wa nchi, kuboresha maisha ya jamii na hifadhi ya mazingira. Aidha, Wizara imekamilisha kuandaa Mpango Kabambe wa Sekta ya Mifugo Tanzania (*Tanzania Livestock Master Plan - TLMP*) wa miaka 15 ukiwa na lengo la kuwaongoza wadau wa sekta ya mifugo kuhusu maeneo ya uwekezaji. Mpango huu utatekelezwa kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Nchini Awamu ya Pili (ASDP II) utakaoanza kutekelezwa mwaka 2017/2018.

### *3.11 Sheria na Kanuni za Sekta ya Mifugo*

**156.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau, imeendelea kupitia sheria za sekta ya mifugo ili

ziendane na Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D) na kuboresha mazingira ya kibiashara. Katika mwaka 2016/2017, Wizara imeandaa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Mbari Bora za Wanyama (*Tanzania Animal Breeding Act*). Aidha, Kanuni, Notisi na Amri zifuatazo zimeandaliwa na kupelekwa kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na kutangazwa katika Gazeti la Serikali:

(i) *Veterinary (Procedure for Registration Examination for Veterinarian and Veterinary Specialists (Amendment) Regulations, 2016.* Tangazo la Serikali Na. 322 la mwaka 2016;

(ii) *The Veterinary (Retained Registered Veterinarians Inspectors) Notice, 2016.* Tangazo la Serikali Na. 316 la mwaka 2016;

(iii) Notisi ya Wakaguzi chini ya Sheria ya Vetenari, 2016; Tangazo la Serikali Na. 310 la mwaka 2016; na

(iv) Amri chini ya Sheria ya Utambuzi na Usajili na Ufuatiliaji Mifugo (*Livestock identification and Registration Compusory Livestock Identification and Registration Areas Order, 2017).*

**157.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2017/2018, Wizara itakamilisha mapendekezo ya kutunga Sheria ya Mbari za Mifugo za Wanyama (*Animal Breeding Act*) na kupitia Sheria na Kanuni za Mifugo kwa lengo la kuboresha huduma na biashara za mifugo na mazao yake.

### *3.12 Uzalishaji na Biashara ya Mifugo na Mazao yake Zao la Maziwa*

**158.** ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji wa maziwa umepungua kwa asilimia 2.3 kutoka lita bilioni 2.14 mwaka 2015/2016 hadi bilioni 2.09 mwaka 2016/2017. Kupungua kwa uzalishaji maziwa kumetokana na upungufu wa malisho katika maeneo mengi ya nchi kulikosababishwa na ukame wa muda mrefu. Aidha, hali hii imeendelea kuathiri viwanda vya kusindika maziwa hivyo kuendelea kuzalisha chini ya uwezo wake. Kutokana na hali hiyo, kiwango cha usindikaji maziwa kimepungua kutoka lita milioni 61.18 kutokana na

viwanda 75 mwaka 2015/2016 kufikia lita milioni 40.13 kutoka katika viwanda 65 vinavyofanya kazi katika mwaka 2016/2017 (**Kiambatisho Na. 6**).

**159.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Bodi ya Maziwa Tanzania iliendelea kuratibu Mpango wa Unywaji Maziwa Shuleni katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Njombe, Tanga na Dar es Salaam. Aidha, kwa kushirikiana na Mradi wa Kuendeleza Tasnia ya Maziwa Afrika ya Mashariki (*East Africa Dairy Development - EADD*) ina mpango wa kuongeza mikoa ya Mbeya na Iringa.

**160.** ***Mheshimiwa Spika*,** Bodi ya Maziwa imeendelea kuhamasisha unywaji wa maziwa nchini kwa lengo la kuboresha afya na lishe ya jamii,hususan watoto na ili kukuza soko la maziwa nchini. Bodi ya maziwa imehamasisha wadau mbalimbali kugharamia Programu ya Unywaji wa Maziwa Shuleni ambapo jumla ya shule **23** zenye wanafunzi **20,019**walikunywa jumla ya lita za maziwa **385,860** katika mikoa ya Arusha (Arusha mjini) Shule **3** wanafuzi **3,047** walipatiwa kiasi cha lita **60,940** za maziwa, Kilimanjaro (Wilaya ya Hai) shule **10** wanafunzi **7,229** walipatiwa kiasi cha lita 144,580 za maziwa, Dar es Salaam (Manispaa ya Kinondoni) Shule **6** wanafunzi **6,137** walipatiwa kiasi cha lita **122,740** za maziwa na Tanga (Tanga Mjini) Shule **4** zenye wanafuzi **3,606** walipatiwa lita **57,600** za maziwa. Aidha, Bodi na wadau wa tasnia ya Maziwa wameandaa Wiki ya Uhamasishaji wa Unywaji wa Maziwa itakayofanyika Mkoani Kagera kuanzia tarehe 29 Mei hadi tarehe 1 Juni, 2017 ikiwa na Kaulimbiu ya *'Kunywa Maziwa Jenga Afya Furahia Maisha'.* Pia, Bodi ya Maziwa imeendelea kusimamia uingizaji wa Maziwa kutoka nje ya nchi kwa kutoa vibali **396**vyenye thamani ya shilingi **17,189,226,511**katika kipindi cha mwezi Julai 2016 hadi Machi 2017.

**161.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kuboresha mashamba ya uzalishaji mifugo ya Serikali kwa kuyapatia vitendea kazi kwa lengo la kuongeza uzalishaji. Katika mwaka 2016/2017, Wizara imetekeleza yafuatayo:-

(i) Kununua madume manne (4) ya Boran na mbuzi 22 wa kienyeji (SEAG) katika Shamba la Kuzalisha Mitamba Ngerengere;

(ii) Kuendeleza malisho ekari (40) na kilimo cha mahindi ya mifugo ekari 73 katika shamba la Sao Hill;

(iii) Kujenga na kukarabati mabanda (5) ya mifugo, maboma (5), uzio wa mazizi Kilomita (10), nyumba za watumishi (3) na maeneo ya kupumzikia mifugo (Hekta 4) katika mashamba ya Kuzalisha Mitamba ya Kitulo, Mabuki, Ngerengere na Sao Hill;

(iv) Kukarabati vibanio vinne (4), mashine ya maji moja (1), mfumo na usambazaji wa maji mita 750 na uimarishaji wa shughuli za uhimilishaji katika shamba la Kitulo na Ngerengere;

(v) Kutengeneza barabara za kuzuia moto km 25 na ujenzi wa kibanio kimoja (1) katika shamba la Nangaramo; na

(vi) Kukarabati mtambo wa kuzalisha Kimiminika cha Hewa Baridi ya Naitrojeni wa kituo cha Lindi na NAIC – Arusha.

**162.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuzalisha mitamba ya maziwa ili kuongeza uzalishaji wa maziwa nchini. Katika mwaka 2016/17, jumla ya mitamba **11,454** ilizalishwa na kusambazwa kwa wafugaji wadogo nchini ikilinganishwa na jumla ya mitamba **11,349** iliyozalishwa mwaka 2015/2016. Mashamba ya Serikali na NARCO yamezalisha mitamba **636** katika mwaka 2016/17 ikilinganishwa na mitamba **546** katika mwaka 2015/16 (**Jedwali Na. 6).** Kupugua kwa uzalishaji katika mashamba ya Serikali na NARCO kunatokana na ubinafsishaji wa ranchi za NARCO ambapo mitamba mingi ya maziwa hivi sasa inazalishwa na ranchi (vitalu) za NARCO zilizobinafsishwa na wafugaji wadodo wa ngombe wa maziwa.

**Jedwali Na.6: Uzalishaji na Usambazaji wa Mitamba kutoka Mashamba ya Serikali 2011/2012-2016/2017**

| Jina | Wilaya lilipo | 2011/12 | 2012/13 | 2013/14 | 2014/15 | 2015/16 | 2016/17 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Sao Hill | Mafinga | 198 | 198 | 194 | 187 | 144 | 158 |
| Mabuki | Misungwi | 299 | 215 | 113 | 223 | 200 | 153 |
| Kitulo | Makete | 72 | 104 | 61 | 66 | 62 | 72 |
| Ngerengere | Morogoro Vijijini | 122 | 96 | 90 | 98 | 80 | 93 |
| Nangaramo | Nanyumbu | 98 | 47 | 67 | 70 | 80 | 70 |
| **Jumla** | | **789** | **660** | **525** | **644** | **566** | **546** |
| NARCO | | 504 | 60 | 40 | 30 | 80 | 88 |
| **Jumla Kuu** | | **1,393** | **720** | **565** | **674** | **646** | **[illegible]** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi, 2017*

**163.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018 Wizara itaendelea kuimarisha mashamba ya kuzalisha mitamba kwa kununua ng'ombe wazazi 100 na kuboresha miundombinu ya maji na malisho. Kupitia Mradi wa SAGCOT Catalytic Trust Fund, jumla ya mitamba 70 itasambazwa kwa wafugaji katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Pia, sekta binafsi itahamasishwa kuongeza uzalishaji wa mitamba na kusambaza kwa wafugaji.

**164.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Kituo cha Taifa cha Uhimilishaji – NAIC Usa River (Arusha) kimeimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na Chiller kwa ajili ya mtambo wa kuzalisha kimiminika cha hewa baridi ya Naitrojeni. Aidha, vituo vya Kanda vimeendelea kuimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi na ukarabati wa miundombinu na mitambo ili kuhakikisha upatikanaji wa huduma ya uhimilishaji wakati wote. Jumla ya dozi 100,000 zilizalishwa ikilinganishwa na dozi 80,000 mwaka 2015/2016. Pia, ng'ombe waliohimilishwa wameongezeka kutoka 120,688 mwaka 2015/2016 hadi ng'ombe 457,557 mwaka 2016/2017 **(Jedwali Na.7)**

**Jedwali Na. 7: Huduma ya Uhimilishaji Nchini 2010/2011 – 2016/2017**

***Chanzo: Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi, 2017***

**165.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya *Bill & Melinda Gates Foundation* inaendelea kutekeleza kazi ya kuimarisha huduma ya uhimilishaji nchini kwa kupitia Taasisi ya *Land O' Lakes International Development* kwenye Mradi wa *Public Private Partnership for Artificial Insemination Delivery (PAID)*. Jumla ya wataalam wa uhimilishaji 230 kutoka mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Dar es salaam, Pwani, Tanga na Morogoro, mikoa yote ya Kanda za Nyanda za Juu Kusini na Ziwa walipata mafunzo.

**166.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Bill & Melinda Gates Foundation kupitia Mradi wa PAID, itaimarisha Kituo cha Taifa cha uhimilishaji cha NAIC Usa River kwa kuimarisha maabara ya kuzalisha mbegu kutokana na madume bora, kununua matenki ya kusafirishia na kuhifadhia kimiminika cha Naitrojeni, kununua madume bora ya ng'ombe manane (8), kutoa mafunzo kwa watumishi wa NAIC na kununua trekta na vifaa vyake. Pia, watatoa mafunzo kwa wahimilishaji 104 ili kufikia lengo la wahimilishaji 300. Vilevile, wataalam wawili wa Wizara watapatiwa mafunzo ya namna

ya kufanya matengenezo kwenye mitambo ya kuzalisha kimiminika baridi cha naitrojeni.

***Zao la Nyama***

**167.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/2017, kulingana na takwimu za mifugo zilizopo, uzalishaji wa nyama umepungua kutoka tani 648,810 (ng'ombe 323,775; mbuzi na kondoo tani 129,292; nguruwe tani 79,200; na kuku tani 104,292) mwaka 2015/2016 hadi tani 558,164 (ng'ombe tani 394,604; mbuzi tani 61,109, kondoo tani 19,955, nguruwe tani 18,899 na kuku tani 63,597) (**Kiambatisho Na. 8).** Kupungua kwa uzalishaji wa nyama kumetokana na upungufu wa malisho katika maeneo mengi ya nchi kulikosababishwa na ukame wa muda mrefu. Aidha, mfumo wa unenepeshaji mifugo umeendelea kuhamasishwa ambapo ng'ombe walionenepeshwa wameongezeka kwa asilimia 12.9 kutoka ng'ombe 221,390 mwaka 2015/2016 hadi ng'ombe 250,000 mwaka 2016/17. Katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa nyama itaendelea kuhamasisha wafugaji na wafanyabiashara ya mifugo kuwekeza kwenye ufugaji wa kisasa ukiwemo wa ranchi na unenepeshaji ili kuongeza idadi ya ng'ombe wanaonenepeshwa kufikia 350,000 kwa mwaka.

**168.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko imeendelea kuratibu biashara ya mifugo na mazao yake ndani na nje. idadi ya mifugo iliyouzwa minadani imeongezeka kutoka ng'ombe 1,470,805 mbuzi 1,161,840 na kondoo 253,243 wenye thamani ya shilingi bilioni 976.474 mwaka 2015/2016 hadi kufikia ng'ombe 1,618,047 wenye thamani ya shilingi trilioni 1.34, mbuzi 1,278,182 na kondoo 278,595 wenye jumla ya thamani ya shilingi trilioni 1.02 mwaka 2016/2017.

**169.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia Bodi ya nyama imeendelea kufuatilia biashara ya nyama ndani na nje ya nchi ambapo hadi kufikia Machi 2017 jumla ya tani 3,162.65 za nyama ziliuzwa nje ya nchi katika nchi za Dubai, Iraq na Vietnam ikiwa tani 711.82 nyama ya mbuzi, tani 439.03

nyama ya ng'ombe, tani 222.74 za nyama ya kondoo na tani 1,789.06 za nyama ya punda. Pia, jumla ya tani 890.66 za nyama na ziliingizwa nchini kutoka Kenya, Afrika Kusini, na Uingereza. Ikiwa tani 366.34 za nyama ya nguruwe, tani 512.06 za nyama ya ng'ombe na tani 12.27 za nyama ya kondoo. Pia, jumla ng'ombe 26,515 na mbuzi 11,553 wameuzwa nje ya nchi kati ya hao ng'ombe 23,594 na mbuzi 9,851 waliuzwa Kenya na ng'ombe 2,921 na mbuzi 1,702 waliuzwa Comoro. Vilevile, vifaranga 237,700 na mayai 250,960 viliuzwa katika nchi za Comoro, Kenya na Ethiopia.

**170.** ***Mheshimiwa Spika*,** Serikali itasitisha uchinjaji wa punda ambao wanakadiriwa kuwa 500,000 kuanzia tarehe 1 Julai, 2017 ili kukabiliana na changamoto ya upungufu au kumalizika kwa wanyama hawa kutokana na kasi ya uchinjaji inaoendelea. Lengo ni kuendelea kuhakikisha kuwa nguvu kazi itokanayo na punda inawanufaisha wananchi vijijini hususan akina mama.

**171.** ***Mheshimiwa Spika***, ili kuwezesha biashara yenye tija, katika mwaka 2016/2017, Wizara imeboresha baadhi ya miundombinu ya masoko ya mifugo kwa lengo la kukuza biashara ya mifugo katika minada ya upili na ya mipakani ikiwemo minada ya Pugu (Ilala), Mhunze (Kishapu), Kizota (Manispaa ya Dodoma) na Nyamatala (Mwanza). Aidha, ujenzi wa mazizi ya kuhifadhi mbuzi katika minada wa Nyamatala na kituo cha Polisi umefanyika. Pia, ukarabati wa mfumo wa maji na usimikaji wa matenki ya kuhifadhia maji katika mnada wa Pugu pamoja na mafunzo kuhusu matumizi ya mizani wakati wa kuuza mifugo yametolewa kwa wafanyabiashara 350. Vilevile, kazi ya kuwatoa wavamizi katika maeneo ya minada ya Kizota na Kasesya imeendelea kufanyika. Katika mwaka wa fedha 2017/2018, ili kuwawezesha wafanyabiashara kufanya biashara kwa ufanisi, usalama ikiwemo kuboresha ukusanyaji wa maduhuli ya Serikali Wizara itashirikiana na taasisi za kibenki nchini kusimika mifumo ya ki-eletroniki katika minada ya Upili ya Kizota(Manispaa ya Dodoma), Igunga, Nyamatala (Misungwi) Mhunze(Kishapu), Meserani (Monduli) na minada ya mipakani ya Kirumi (Butiama) na Kasesya (Kalambo).

**172.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itakarabati minada mitatu ya mpakani ya Longido, Kirumi na Kasesya na mnada wa upili wa Nyamatala. Aidha, itatoa elimu kwa wafugaji na wafanyabiashara ya mifugo kuwekeza katika ufugaji bora. Pia, Wizara itahamasisha wadau kuwekeza katika ujenzi wa viwanda na biashara ya mifugo na mazao yake ili kupanua soko la mazao ya mifugo ndani na nje ya nchi. Vilevile, Wizara itaanza kutekeleza Mpango Kabambe wa Sekta ya Mifugo Tanzania (*Tanzania Livestock Master Plan - TLMP*).

***Uzalishaji wa Nyama katika Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO)***

**173.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, NARCO imetekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kuchinja ng'ombe 2,134 wakiwa wamenenepeshwa wenye thamani ya shilingi bilioni 1.51. Aidha, NARCO imezalisha na kukuza ndama 3,753 kutokana na ng'ombe wazazi 5,294 sawa na asilimia 70.9 ya malengo ya uzalishaji. Kwa upande wa biashara, NARCO imeuza ng'ombe 3,892 wenye thamani ya shilingi bilioni 2.62. Pia, NARCO imenunua ng'ombe 1,864 kutokana na vyanzo vya ndani vya mapato ya Kampuni wenye thamani ya shilingi milioni 890 kutoka kwa wafugaji wa asili kwa ajili ya programu ya unenepeshaji. Vilevile, NARCO imesimamia na kutoa ushauri wa ufugaji bora katika ranchi ndogo zilizomilikishwa kwa wawekezaji wadogowadogo ambapo ranchi hizo zimewekeza ng'ombe 60,546, mbuzi 6,735 na kondoo 3,428.

**174.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, NARCO inatarajia kuzalisha jumla ya ndama 4,269 kutokana na ng'ombe wazazi 5,344. Aidha, NARCO inatarajia kununua ng'ombe 2,100 kutokana na vyanzo vya ndani vya mapato na itauza ng'ombe 3,898 walionenepeshwa wanaotarajiwa kufikia thamani ya takribani shilingi bilioni 2.7. Aidha, NARCO itawezeshwa kununua ng'ombe wazazi 100. Pia, Wizara kwa kushirikiana na NARCO itaendelea na ujenzi wa machinjio ya Ruvu, kuongeza idadi ya mifugo na kujenga viwanda kwenye eneo la ranchi ya Ruvu kwa kutengeneza bidhaa za

ngozi kwa ajili ya kuongeza ajira ya wanawake na vijana kutokana na mkopo wa riba nafuu wa Dola za Kimarekani milioni 50 kutoka Mfuko wa Maendeleo wa Ushirikiano wa Kiuchumi kwa Serikali ya Korea (EDCF).

### *Zao la Ngozi*

**175.** ***Mheshimiwa Spika,*** mwaka 2016/2017, vipande vya ngozi zilizosindikwa vimepungua kutoka vipande vya ngozi za ng'ombe 1,575,139 vyenye thamani ya shilingi bilioni 45.0 mwaka 2015/2016 hadi vipande 1,215,030 vyenye thamani ya shilingi bilioni 34.7. Pia, vipande vya ngozi za mbuzi/kondoo 928,115 vyenye thamani ya shilingi bilioni 6.2 vilivyosindikwa vimepungua ikilinganishwa na vipande 1,124,000 vyenye thamani ya shilingi bilioni 7.5. Aidha, ngozi ghafi za ng'ombe vipande 241,773 vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.89 viliuzwa nje ya nchi ikilinganishwa na vipande 187,000 vya ngozi za ng'ombe vyenye thamani ya shilingi bilioni 2.4 mwaka 2015/2016. Hii imetokana na kushuka kwa bei ya ngozi katika soko la dunia kwa mwaka 2016/2017 hadi sasa, hali ambayo imesababisha kuendelea kurundikana kwa ngozi zilizosindikwa kwenye viwanda pia ngozi ghafi katika machinjio na maghala ya waboreshaji wa ngozi.

**176.** ***Mheshimiwa Spika, ,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Ngozi (Leather Sector Development Strategy 2016-2020), ambao unalenga kuongeza thamani katika mnyororo wa zao la ngozi kwa lengo la kupata malighafi kwa ajili ya viwanda vya kusindika na vya kutengeneza bidhaa za ngozi. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Viwanda Biashara na Uwekezaji, na Elimu, Sayansi na Mafunzo ya Ufundi (DIT – Mwanza) itatekeleza majukumu yafuatayo:- kutoa mafunzo kwa wataalam wa mifugo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa75 kuhusu uendelezaji wa zao la ngozi, kuboresha upatikanaji wa ngozi viwandani kupitia matumizi ya Mfumo wa Ufuatiliaji wa Uzalishaji na Biashara ya ngozi kutoka machinjioni hadi viwandani (Hides and skins Tracking System) ili kuzuia utoroshwaji wa ngozi nje ya nchi. Aidha, Wizara itaendelea kutoa mafunzo katika

taaluma ya ngozi ili kuziba pengo lililopo la wataalam wa ngozi. Katika mwaka 2017/18 wizara itasomesha wataalam 4 katika ngazi ya stashahada na 2 katika ngazi ya shahada ya teknolojia ya ngozi ili kuwa na wataalam mahiri katika tasnia ya ngozi.

**177.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Ngozi (Leather Sector Development Strategy 2016-2020), ambao unalenga kuongeza thamani katika mnyororo wa zao la ngozi kwa lengo la kupata malighafi kwa ajili ya viwanda vya kusindika na vya kutengeneza bidhaa za ngozi. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Viwanda Biashara na Uwekezaji, na Elimu Sayansi na Mafunzo ya Ufundi (DIT – Mwanza) itatekeleza majukumu yafuatayo:- kutoa mafunzo kwa wataalam 15 wa mifugo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 15 kuhusu uendelezaji wa zao la ngozi, kuboresha upatikanaji wa ngozi viwandani kupitia matumizi ya Mfumo wa Ufuatiliaji wa Uzalishaji na Biashara ya ngozi kutoka machinjioni hadi viwandani (Hides and skins Tracking System) ili kuzuia utoroshwaji wa ngozi nje ya nchi.

### *Uzalishaji wa Kuku*

***178.*** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea kuhamasisha ufugaji wa kuku kibiashara. Uzalishaji wa vifaranga vya kuku wa nyama na mayai umepungua kutoka vifaranga milioni 68.28 mwaka 2015/2016 hadi vifaranga milioni 64.3 mwaka 2016/2017. Aidha, jumla ya mayai 2,825,480 ya kutotolesha vifaranga yaliingizwa nchini kutoka nchi za Zambia, Kenya, Uholanzi na Mauritius ikilinganishwa na mayai 1,290,000 yaliyoingizwa mwaka 2015/2016. Aidha, uzalishaji wa mayai katika mwaka 2016/2017 umepungua kutoka mayai bilioni 4.35 mwaka 2015/16 hadi mayai bilioni 2.76. Kupungua kwa uzalishaji wa mayai na vifaranga kumetokana na kupanda kwa gharama za vyakula vya kuku na kulazimisha baadhi ya wadau kusitisha uzalishaji ikiwa ni pamoja na kupunguza idadi ya kuku.

**179.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018 Wizara itahamasisha sekta binafsi kuongeza uzalishaji wa vifaranga ili kukidhi mahitaji na kuimarisha vyama vya wafugaji wa ndege hususan kuku. Aidha, mradi wa kusambaza vijijini vifaranga wa aina ya *Kuroiler* katika mikoa **25** nchini utaboreshwa. Pia, utekelezaji wa mradi wa miaka minne wenye lengo la kuongeza tija katika uzalishaji wa kuku wa asili (*African Chicken Genetic Gains - ACGG*) chini ya TALIRI kwa ufadhili wa *Bill and Melinda Gates Foundation* unaendelea.

***Uzalishaji wa Nguruwe***

**180.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa imeendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika ufugaji, usindikaji na biashara ya nguruwe hai. Uzalishaji na biashara ya nyama ya nguruwe umepungua kutoka tani 79,200 mwaka 2015/2016 hadi kufikia tani 18,899 mwaka 2016/2017. Hii imetokana na kuongezeka kwa bei ya vyakula na mlipuko wa ugonjwa wa Homa ya Nguruwe katika mikoa ya Rukwa, Morogoro, Mbeya, Songwe na Iringa. Aidha, Sekta binafsi imehamasishwa na kuanzisha chama cha wazalishaji nguruwe nchini kijulikanacho kama *Tanzania Association of Pig Farmers* (TAPIFA). Kupitia chama hiki, Sekta Binafsi imenunua na kuingiza nguruwe 40 kutoka Zambia aina ya *Cambarough*. Pia, nguruwe saba (7) aina ya *Duro*c kutoka Afrika ya Kusini na 15 (*Duroc* 5, *Landrace* 5 na *Large white* 5) kutoka Denmark wamenunuliwa kwa lengo la kuboresha kosaafu za nguruwe nchini.

**181.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kuhamasisha uzalishaji wa nguruwe na kudhibiti ugonjwa wa homa ya nguruwe katika maeneo yaliyoathiriwa na ugonjwa huu, kuendelea kuhimiza uingizaji wa nguruwe wazazi kutoka nje ya nchi kwa lengo la kupunguza tatizo la kuzaliana kiukoo kwa nguruwe waliopo hapa nchini na kuhimiza uzalishaji wa vyakula vya mifugo kwa kuweka mazingira wezeshi katika uzalishaji wa vyakula hivyo.

### 3.13 Tozo za leseni katika Sekta ya mifugo

**182.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara imefanya mapitio ya tozo/kodi na ada mbalimbali katika sekta ya mifugo zinazotozwa na Wizara na Taasisi chini ya Wizara na kubaini baadhi ya kodi, tozo na ada hizo ni kero kwa wafugaji na maendeleo ya sekta ya mifugo kwa ujumla. Hivyo, katika mwaka 2017/2018, Serikali itafuta kodi, tozo na ada saba (7) ambazo zimekuwa kero kwa wafugaji, wafanyabiashara na wawekezaji; na kubakiza zile tu zenye uhusiano wa moja kwa moja katika uendelezaji wa sekta ya mifugo kwa mchanganuo ufuatao; tasnia ya maziwa tozo mbili (2), tasnia ya nyama jumla ya tozo nne (4) na eneo la afya ya mifugo tozo moja (1) (**Kiambatisho Na. 9**).

**183.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nilihakikishie Bunge lako tukufu, kuwa Serikali itaendelea kuchambua kwa kina tozo, ushuru na ada mbalimbali zilizobaki zinazotozwa katika mifugo na mazao yake kwa lengo la kuangalia uhalali wa kuwepo kwake na viwango vya tozo, ushuru na ada hizo kwa lengo la kuziondoa au kuzipunguza ili kuwapunguzia wafugaji mzigo wa tozo, ushuru na ada zisizokuwa na tija.

### 3.14 Matumizi ya Rasilimali za Ardhi, Maji na Malisho kwa Mifugo

**184.** **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/2017, Wizara ilendelea kuhamasisha uzalishaji na uhifadhi wa malisho kwa njia za kitaalam ambapo jumla ya marobota ya hei 456,016 yenye thamani ya shilingi 1,140,040,000 yamezalishwa na kuuzwa kutoka mashamba ya kuzalisha mbegu bora za malisho ya Serikali na marobota 684,230 ya hei yalizalishwa na sekta binafsi yenye thamani ya shilingi 2,052,690,000. Aidha, mbegu za malisho bora za nyasi kilo 3,717.1 zenye thamani ya shilingi 55,756,500 na jamii ya mikunde kilo 731.5 zenye thamani ya shilingi 10,972,500 zimezalishwa na kuuzwa kwa wadau mbalimbali toka mashamba ya Serikali (**Kiambatisho Na. 10a na 10b).**

**185.** ***Mheshimiwa Spika,*** kutokana na kuendelea kuwepo kwa migogoro ya matumizi ya ardhi inayohusisha wafugaji, wakulima na watumiaji wengine wa ardhi, Serikali iliunda Timu ya wataalam kutoka sekta zote zinazohusika na ardhi. Timu ilipewa jukumu la kupitia taarifa za kamati Teule, Vikosi Kazi na Timu mbali mbali zilizowahi kuundwa kuhusu migogoro ya ardhi, kupitia Katiba, Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo kutoka katika sekta zote na kubaini vyanzo na sababu za migogoro na hatimaye kupendekeza kwa serikali kuhusu njia muafaka za kumaliza migogoro ya matumizi ya ardhi hapa nchini. Rasimu ta taarifa imeandaliwa kwa ajili ya kuwasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri.

**186.** ***Mheshimiwa Spika*** katika mwaka 2017/18, Wizara itawezesha uandaaji wa mipango ya matumizi ya ardhi katika wilaya za Kiteto, Kilindi, Muheza, Korogwe, Mvomero, Morogoro na Bagamoyo kupitia miradi wa *Sustainable Rangeland Management Project* na *Securing Watershed Services through Sustainable Land Management for Ruvu and Zigi Catchments*. Miradi hiyo inafadhiliwa na IFAD kupitia Asasi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo na Global Environmental Facility. Aidha, kupitia miradi hiyo wizara itaandaa mipango ya kina (management plans) katika maeneo ya malisho katika vijiji 50 ambayo yatatengwa kutokana na utekelezaji wa miradi hiyo. Mipango hiyo itaambatana na utoaji wa hati miliki za kimila kw wilaya za Kiteto, Kilindi, Mvomero, Morogoro na Bagamoyo a wafugaji katika maeneo hayo ili kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi.

**187.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/18 Wizara itawezesha ujenzi wa vyanzo vya maji kwa matumizi ya mifugo katika Halmashauri za Wilaya za Hanang, Kilosa, Ngorongoro, Same na Songwe kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa maji kwa mifugo katika maeneo ya ufugaji. Aidha wizara itajenga na kukarabati malambo na mabwawa kwa lengo la kusaidia juhudi zinazofanywa na Mamlaka za Serikali za Mitaa pale ambapo kuna mifugo mingi au katika maeneo ambayo mifugo huwa inahamia wakati wa kiangazi. Pia, wizara itaendelea kuwashirikisha wadau husussan wafugaji katika ujenzi na ukarabati wa

vyanzo vya maji kwa mifugo ili kupunguza tatizo la uhaba wa maji.

### *Athari za Ukame kwa Mifugo*

**188. Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/2017 ukame uliathiri hali ya mifugo hasa katika maeneo ya mikoa ya Pwani, Dodoma, Mororgoro, Singida, Manyara, Shinyanga, Mara, Kagera na Arusha ambayo haikupata mvua za vuli za kutosha na kusababisha ukame uliopelekea vifo vingi vya mifugo kutokana na upungufu mkubwa wa maji na malisho. Jumla ya mifugo **131,725** ilikufa kati ya hao, ng'ombe 102,987, punda 646, mbuzi 14,881 na kondoo 13,815. Aidha, kati ya mikoa iliotoa takwimu ya idadi ya vifo vya mifugo, mkoa wa Manyara ulionekana kuadhirika sana ambapo vifo vilikua ng'ombe 48,460, mbuzi 13,967, kondoo 12,773 na punda 646. **(Kiambatisho Na.11)**. Katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kushirikiana na Mamlaka ya Hali ya Hewa kutoa tahadhari ya mabadiliko ya hali ya hewa ambayo yanaweza kuwa na madhara kwa wafugaji. Aidha, Wizara itaendelea kushirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira na wadau wengine katika kutoa elimu kwa wafugaji kuhusu madhara yanayoletwa na mabadiliko ya tabianchi na tahadhari za kuchukua ili kuunguza madhara hayo.

### *3.15 Usindikaji wa Vyakula vya Mifugo*

**189.** ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa vyakula vya mifugo unaofanywa na sekta binafsi umepungua kutoka tani 1,500,000 mwaka 2015/2016 hadi tani 1,100,000 mwaka 2016/2017 kutokana na wafugaji wengi kujitoa katika uzalishaji kwa sababu ya kupanda kwa bei ya vyakula kulikosababishwa na kuanzishwa kwa tozo ya VAT kwenye vyakula vya mifugo, madawa na kushuka kwa bei ya kuku. Pia, usajili wa wazalishaji na wasambazaji wa vyakula vya mifugo umeendelea kufanyika ambapo jumla ya wazalishaji na wasambazaji wa vyakula vya mifugo **20** walisajiliwa na kufanya Idadi ya waliosajiliwa kufikia **35**.

**190.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imefanya ukaguzi wa ubora wa vyakula vya mifugo katika jumla ya viwanda 24 vinavyosindika vyakula vya mifugo ili kuona kama vinakidhi viwango. Kupitia kaguzi hizo wamiliki ambao hawakuwa wamekidhi masharti yanayosimamia uzalishaji wa vyakula vya mifugo walielekezwa kufanya marekebisho na kufanya usajili wa viwanda pamoja na maeneo ya kuhifadhi na kuzalisha rasilimali za vyakula vya mifugo. Kaguzi hizo zilifanyika katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Iringa, Ruvuma, Arusha na Dodoma. Vilevile, sampuli zilizochukuliwa katika viwanda vingi zilionyesha vyakula kuwepo kwa upungufu wa protini na wanga na ushauri umetolewa ili kuondoa kasoro hizo.

**191.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kuratibu uzalishaji wa vyakula vya mifugo na usajili wa wazalishaji na wasambazaji wa vyakula vya mifugo. Aidha, Wizara itaendelea kusimamia na kudhiti ubora katika uzalishaji na usindikaji wa vyakula vya mifugo nchini, ambapo itatoa mafunzo kwa wakaguzi wa vyakula vya mifugo 50 na watengenezaji wa vyakula vya mifugo 70 na kuendelea kukagua maeneo na viwanda vya kusindika vyakula vya mifugo.

### 3.16 *Udhibiti wa Magonjwa ya Mifugo Maeneo Huru ya Magonjwa ya Mifugo*

**192.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Biashara Duniani (*World Trade Organization – WTO*) imeendelea kufanya tathmini ya kuanzisha eneo huru na magonjwa ya mifugo (*Disease Free Zone*) katika wilaya za Nkasi na Kalambo mkoa wa Rukwa. Tathmini hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Juni 2017. Katika mwaka 2017/ 2018, Wizara itatumia matokeo ya tathmini hiyo katika utekelezaji wa uwekezaji katika eneo hilo na maeneo mengine yatakayoainishwa nchini.

#### *Magonjwa ya Mlipuko*

**193.** ***Mheshimiwa Spika,*** Magonjwa ya mlipuko

ambayo ni Homa ya Mapafu ya Ng'ombe (CBPP), Homa ya Mapafu ya Mbuzi (CCPP), Ugonjwa wa Miguu na Midomo (FMD), Mapele ya Ngozi (LSD), Homa ya Nguruwe (ASF), Mdondo (NCD) na Sotoka ya Mbuzi na Kondoo (PPR) ni tishio kwa mifugo na biashara hapa nchini. Katika mwaka 2016/ 2017, matukio ya Homa ya Mapafu ya Ng'ombe yalihusisha mikoa 20 na Halmashahuri 51; Homa ya Mapafu ya Mbuzi mikoa 16 na Halmashauri 32; Ugonjwa wa Miguu na Midomo mikoa 21 na Halmashauri 54; Mapele ya Ngozi mikoa 18 na Halmashauri 52; Homa ya Nguruwe mikoa mitano (5) na Halmashauri sita (6). Ili kupambana na milipuko hiyo ya magonjwa ya mifugo Wizara ilihamasisha na kuratibu wadau wa mifugo katika kununua chanjo mbalimbali za magonjwa ya mifugo, ambapo, chanjo zifuatazo zilinunuliwa na kutumika sehemu mbalimbali nchini, Mdondo 27,901,360; PPR 275,275; CBPP 409,286; CCPP 29,852 na Kichaa cha mbwa 574,259 kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa chanjo kwa wafugaji.

**194.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kudhibiti magonjwa haya kwa kushirikiana na Halmashauri na sekta binafsi katika kununua na kutoa chanjo kwa mifugo. Aidha, elimu itaendelea kutolewa kwa wadau kuhusu umuhimu wa magonjwa haya katika biashara ya mifugo na mazao yake kitaifa na kimataifa ili kuchukua hatua za tahadhari.

**195.** ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia kuzuka kwa ugonjwa wa Mafua Makali ya Ndege nchini Uganda yaliyojitokeza kwenye ndege wanaohama hama kutoka bara moja hadi jingine; mikoa inayozunguka ziwa Victoria na maeneo mengine wanapopita ndege hao; yalikuwa katika hatari ya kupata mlipuko wa ugonjwa huo. Hata hivyo, Wizara ilifuatilia kwa karibu kwa kutembelea maeneo yaliyopata maambukizi nchini Uganda ambapo tulikuta ugonjwa huo umedhibitiwa. Hata hivyo, Wizara pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa za mikoa yote ziliendelea kuchukua tahadhari ikiwa ni pamoja na kuchukua sampuli

ambazo matokeo yake pia yalionesha kuwa hakuna maambukizi. Halmashauri zilizokuwa katika hatari ya kuambukizwa ugonjwa huo zipo katika mikoa ya Kagera, Geita, Mwanza, Simiyu, Mara, Tabora, Kigoma na Rukwa. Aidha, katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto itaendelea kuratibu na kufuatilia mwenendo wa ugonjwa huo na kutoa elimu kwa wadau.

### *Magonjwa Yaenezwayo na Kupe na Mbung'o*

**196.** ***Mheshimiwa Spika****,* Kupe na magonjwa wayaenezayo, hususan ugonjwa wa Ndigana Kali (ECF) ambapo usipodhibitiwa husababisha asilimia zaidi ya 60 ya vifo vya ndama pamoja na kupunguza uzalishaji wa ng'ombe na mazao yake nchini. Jumla ya majosho yaliyopo nchini ni 2,428, kati ya hayo majosho 1,014 yanafanya kazi, majosho 507 ni mazima lakini hayafanyi kazi na majosho 907 ni mabovu. Katika mwaka 2016/2017, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi ilitoa mafunzo kwa Maafisa ugani 300 kuhusu namna ya kutoa chanjo dhidi ya Ndigana Kali. Aidha, makampuni yanayoagiza chanjo hiyo yameongezeka kutoka mawili (2) mwaka 2015/2016 na kufikia manne (4) mwaka 2016/2017. Jumla ya ng'ombe 70,260 wamechanjwa dhidi ya ugonjwa huo. Katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kuhimiza Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhakikisha kuwa majosho ambayo ni mazima na hayafanyi kazi yanatumika na kukarabati majosho mabovu. Aidha, kwa kushirikiana na Sekta Binafsi itahamasisha wafugaji kuchanja na kuogesha mifugo ili kuikinga Ndigana kali.

### *Magonjwa ya Wanyama yanayoambukiza Binadamu Kichaa cha Mbwa*

**197.** ***Mheshimiwa Spika,*** Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa uliendelea kudhibitiwa ambapo Wizara kwa kushirikiana na Wakfu wa Bill & Melinda Gates imetekeleza Mradi wa Majaribio wa Kutokomeza Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa (*Rabies Elimination Demonstration Project*) kwenye wilaya 24 za mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Morogoro, Dar es Salaam

na wilaya 4 za Pemba. Jumla ya mbwa 86,080 kati ya mbwa 106,974 sawa na asilimia 80.4 walichanjwa. Aidha, Mpango Mkakati wa Kutokomeza Kichaa cha Mbwa nchi nzima ifikapo mwaka 2030 umeandaliwa. Katika mwaka 2017/2018, Wizara itatekeleza Mpango Mkakati wa kutokomeza Ugonjwa wa Kichaa cha Mbwa chini ya uratibu wa Kitengo cha dhana ya Afya Moja chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine.

***Ugonjwa* wa Ebola**

**198.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017***,*** Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) kwa ufadhili wa Shirika la Misaada la Watu wa Marekani (USAID) imeendelea kufuatilia uwepo wa virusi vya Ebola kwenye wanyama. Jumla ya sampuli 796 zilichukuliwa kutoka kwenye mbuzi, mbwa, ng'ombe, kondoo na nguruwe katika Halmashauri za Kibondo na Uvinza na uchunguzi wa maabara katika sampuli zilizochukuliwa ulionesha kutokuwepo kwa ugonjwa huo. Katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea na uchunguzi wa virusi hivyo na kupitia upya mpango huo wa ufuatiliaji kwa kuingiza magonjwa mengine yanayoambukiza binadamu yakiwemo magonjwa ya Kichaa cha Mbwa (*Rabies*), Homa ya Bonde la Ufa (RVF) na Ugonjwa wa Kutupa Mimba (*Brucellosis*).

***Ugonjwa* wa Kimeta**

**199.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, ugonjwa wa Kimeta uliendelea kuwa tishio kwa mikoa ya Arusha na Kilimanjaro. Aidha, mlipuko mkubwa uliohusisha wanyama pori na wafugwao pamoja na binadamu katika maeneo ya Selela, Kata ya Mto Mbu wilayani Monduli. Wizara kwa kushirikiana na Wizara za Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto; Mali Asili na Utalii; Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serkali za mitaa na Taasisi za TANAPA na NCCA chini ya dhana ya Afya Moja chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu ugonjwa huu ulidhibitiwa. Aidha, elimu juu

ya madhara ya ugonjwa kwa maana ya kutokula mizoga na mifugo kuchanjwa iliendelea kutolewa. Pia, jumla ya ng'ombe 726,042 walichanjwa. Katika mwaka 2017/2018, Wizara inatarajia ng'ombe 2,947,581 watachanjwa, na itaendelea kushirikiana na Wizara zingine husika pamoja na wadau wengine katika kutoa elimu kuhusu ugonjwa huu ili kuudhibiti kila unapojitokeza.

### *3.17 Uchunguzi na Utambuzi wa magonjwa ya mifugo*

**200.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Wakala wa Maabara ya Veterinari Tanzania (Tanzania Veterinary Laboratory Agency -TVLA) imefanya uchunguzi na utambuzi wa magonjwa ya mifugo nchini katika sampuli 4,908 zilizopokelewa. Magonjwa yaliyotambuliwa ni pamoja na Ndigana Kali, Ndigana Baridi, Kimeta, Kichaa cha Mbwa, Mdondo, Gumboro, Sotoka ya Mbuzi, Homa ya Nguruwe, Minyoo, Ugonjwa wa Kutupa Mimba na *Blue Tongue*. Aidha, jumla ya sampuli 1,111 za vyakula vya mifugo zilifanyiwa uhakiki wa ubora na usalama wake ambapo asilimia 18 ya sampuli hizo zilibainika kuwa na upungufu wa protini na nishati.Kutokana na matokeo hayo, wafugaji walipewa elimu ya namna ya kudhibiti magonjwa na watengenezaji wa vyakula vya mifugo walipewa ushauri wa namna ya kuboresha vyakula vya mifugo.

**201.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika 2016/2017 TVLA kupitia Taasisi yake ya utafiti na uzalishaji wa chanjo iliyopo Kibaha imezalisha na kusambaza chanjo dozi 30,055,100 za ugonjwa wa mdondo, dozi 680,900 za ugonjwa wa Kimeta, dozi 121,550 za ugonjwa wa Chambavu na dozi 10,000 za chanjo ya ugonjwa wa Kutupa Mimba. Chanjo ya Kimeta iliweza kutumika kukinga mifugo kufuatia mlipuko wa ugonjwa katika Kanda ya Kaskazini na hivyo kudhibiti ugonjwa usisambae kwenye maeneo mengine. Uzalishaji wa Chanjo ya Ugonjwa wa Kutupa Mimba kwa Ng'ombe na chanjo inayokinga kwa pamoja magonjwa ya Kimeta na Chambavu unasubiri majibu kutoka Maabara Kuu ya chanjo Afrika ya PANVAC iliyoko nchini Ethiopia kulikopelekwa

sampuli za chanjo hizo kwa ajili ya kupima ubora wake. Aidha, TVLA ipo katika mpango wa kuzalisha chanjo za homa ya mapafu ya ng'ombe (CBPP) na chanjo ya sotoka ya mbuzi na kondoo (PPR) ili kutimiza lengo mafunzo yametolewa kwa mtalaam mmoja huko PANVAC nchini Ethiopia na pia imeshapokea mbegu (Master seeds) ya chanjo hizo kama mchakato wa awali wa uzalishaji wa chanjo hizo.

**202.** ***Mheshimiwa Spika,*** TVLA kupitia vituo vyake vya utafiti wa teknolojia za kuangamiza mbun'go waenezao ugonjwa wa Nagana na Malale vya Tanga na Kigoma imeendelea kufanya utafiti wa njia nzuri za kupunguza au kumaliza mbung'o katika maeneo mbalimbali nchini. Utafiti huo pia umejikita katika kuangalia mwenedo wa mbung'o na ndorobo kati ya wanyama pori na wafugwao na uwezo wao wa kuambukiza wanyama na binadamu. Hata hivyo ndorobo wote waliopatikana ni wale wasioambukiza binadamu. Ili kuendeleza tafiti za kudhibiti mbung'o, maabara imeendelea kuzalisha na kuhifadhi mbung'o wazima 506 na mabuu 556.

**203.** ***Mheshimiwa Spika,*** tafiti za kudhibiti magonjwa mengine ya mifugo na kujenga uwezo wa kuyatambua zimeendelea kufanyika ikiwa ni pamoja na kufuatilia mwenendo wa ugonjwa wa Sotoka ya Mbuzi katika wilaya za Handeni, Mbarali, Masasi, Ruangwa, Kiteto, Simanjiro na Ngorongoro ambapo uwepo wa ugonjwa wa *Blue Tongue* uligunduliwa. Aidha, Maabara Kuu ya Mifugo (CVL) imekuwa maabara ya kwanza Afrika kuwa na uwezo wa kutambua ugonjwa wa *Trichnella* kwa nguruwe.

**204.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, TVLA itaendelea kufanya uchunguzi na utambuzi wa magonjwa ya wanyama; kufanya uhakiki wa ubora wa vyakula vya mifugo vinavyozalishwa. Aidha, Wakala utazalisha na kusambaza chanjo dozi milioni 100 za Mdondo, 500,000 za Kimeta, 500,000 za Chambavu na 500,000 za ugonjwa wa Kutupa Mimba. Pia, inategemea kuanza uzalishaji wa chanjo inayokinga kwa pamoja magonjwa ya Kimeta na Chambavu na kuendeleza majaribio ya

kutengeneza chanjo dhidi ya magonjwa ya Homa ya Mapafu ya Ng'ombe na Sotoka ya Mbuzi na kondoo. Vile vile, TVLA itaendelea kufanya tafiti zinazolenga kuthibiti mbung'o wanaoeneza ugonjwa wa Nagana kwa mifugo na Homa ya Malale kwa binadamu na namna ya kudhibiti au kutokomeza magonjwa mengine ya mifugo.

### *3.18 Usalama wa Chakula Kitokanacho na Mifugo*

**205.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kufuatilia usafi na usalama wa vyakula vitokanavyo na mifugo na mazao yake. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa ilifanya ukaguzi wa mifugo na mazao yake katika machinjio mbalimbali kwa lengo la kulinda afya ya walaji. Katika mwaka 2016/2017, jumla ya ng'ombe 357,365, mbuzi 105,910, kondoo 62,559, kuku 1,991,694 na nguruwe 42,156 walikaguliwa na kuchinjwa kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi. Katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea na kazi za usimamizi na ukaguzi ili kudhibiti usalama wa vyakula vitokanavyo na mifugo ili kulinda afya ya mlaji.

**206.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea na ukaguzi na uandikishwaji wa vituo vya kutotolesha vifaranga na Mashamba ya Kuku wazazi kwa madhumuni ya kuboresha viwango vya mazao yanayozalishwa kwenye Tasnia ya kuku. Aidha, vituo vya kutotolesha vifaranga tisa (9) kati ya 22 na mashamba ya kuku wazazi saba (7) kati ya 12 ya kuku wazazi yamekidhi viwango na kuandikishwa kwa mujibu wa Sheria ya Magonjwa ya Mifugo. Katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itafuatilia viwango vya ubora wa mazao yanayozalishwa kwenye Tasnia ya kuku.

### *3.19 Utafiti, Mafunzo na Ugani wa Mifugo Utafiti*

**207.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/2017 Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Tanzania (TALIRI) iliendelea

kutekeleza miradi mbalimbali ya utafiti katika kanda za ki-ikolojia nchini kupitia vituo vyake saba vilivyopo Mpwapwa (Dodoma), Mabuki (Mwanza), Kongwa (Dodoma), Tanga, Naliendele (Mtwara), Uyole (Mbeya), na West Kilimanjaro. Aidha, TALIRI iliendeleza mahusiano na mashirikiano na Taasisi za Kimataifa, hususani Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI), Bill and Melinda Gates Foundation, Kituo cha Kuratibu Utafiti wa Kilimo Kusini mwa Afrika (CCARDESA), The African Union - Inter African Bureau for Animal Resources (AU-IBAR) na Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ili kutekeleza Miradi ya Kipaumbele inayohusu utafiti na maendeleo ya uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa, uboreshaji na uzalishaji wa malisho, mbuzi, kondoo na kuku.

***Tafiti za Uzalishaji wa Mbari za Mifugo na Uhifadhi wa Mifugo Bora***

**208.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, TALIRI iliibua na kuendelea na teknolojia sahihi za kuongeza tija katika uzalishaji wa ng'ombe wa maziwa na nyama, ambapo jumla ya ng'ombe 1,695 walifanyiwa tafiti katika taasisi sita kati ya saba zilizopo chini ya TALIRI. Aidha, jumla ya ng'ombe bora 46 wa maziwa walisambazwa kwa wafugaji katika wilaya za Morogoro (V) 3, Bagamoyo 2, Mufindi 6, Mbeya (V) 4, Misungwi 2, Dodoma (M) 9, Mpwapwa 12, Kongwa 1, Ilala 2, Kibaha 3 na Lushoto 2. Pia, taasisi ilisambaza ng'ombe 44 wa nyama kwa ajili ya ufugaji katika wilaya ya Mpwapwa. Ng'ombe aina ya Mpwapwa na uzao wake wameendelea kufanyiwa tathmini na kuhifadhiwa katika vituo vya Mpwapwa, Kongwa, Tanga na Uyole. Aidha, TALIRI imeendeleza kutekeleza Programu yake ya miaka 12 ya uzalishaji wa ng'ombe yenye lengo la kuongeza uzalishaji wa maziwa kutoka lita 2,500 hadi lita 2,800 katika siku 305. Taasisi imeendelea kutunza na kuhifadhi mbari za ng'ombe, mbuzi, kondoo na kuku kwa lengo la kutathmini uzalishaji na ukuaji.

**209.** ***Mheshimiwa Spika,*** TALIRI kwa kushirikiana na Taasisi ya Kimataifa ya Utafiti wa Mifugo (ILRI) na wadau wengine hususani wafugaji imeendelea kutekeleza mradi wa

miaka mitatu wa kuboresha uzalishaji wa mbari bora za maziwa (*African Dairy Genetic Gain-ADGG*) kwa wafugaji 8,292 katika Halmashauri 23 za Jiji la Arusha, Jiji la Mbeya, Manispaa ya Iringa, Halmashauri za Miji ya Njombe na Korogwe; na Halmashauri za Arusha, Meru, Tanga, Muheza, Korogwe, Lushoto, Bumbuli, Rombo, Moshi, Siha, Hai, Iringa, Mufindi, Mafinga, Makambako, Njombe, Rungwe na Mbozi. Chini ya ushirikiano huo, TALIRI imepokea pikipiki 30 ambazo zimesambazwa katika kanda zinazotekeleza mradi kwa ajili ya kuwawezesha waratibu kufanya ufuatiliaji, ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu kwenye vijiji vinavyoshiriki kwenye mradi huo. Pia, AU-IBAR inafadhili Mradi wa Kuelimisha na kushirikisha wafugaji jinsi ya kuboresha na kuhifadhi mbari za mbuzi aina ya *Pare White* katika wilaya za Same na Mwanga.

**210.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, TALIRI ilizalisha na kuhifadhi kosaafu za mbuzi 1,116 aina ya Malya, wa asili na chotara, katika vituo vya Mpwapwa, Tanga, Mabuki, West Kilimanjaro, Naliendele na Kongwa. Jumla ya mbuzi 47 jamii ya Malya na Gogo-White wamesambazwa katika Wilaya za Dodoma (M) 22, Chamwino 15, Misungwi 5, Morogoro (V) 2, Kibaha 2 na Ilala 1 kwa ajili ya kufanyiwa utafiti. Pia, jumla ya kondoo 302 aina ya *Red* Maasai na 58 aina ya *Black Head Persian* wametunzwa na kuhifadhiwa katika kituo cha TALIRI–West Kilimanjaro.

**211.** ***Mheshimiwa Spika****,* katika mwaka 201620/17, vituo vya TALIRI vya Mpwapwa, Naliendele na Uyole vilifanya tathmini ya ubora wa kuku 693 aina za Kuchi, Sasamala, Kawaida, Mtewa, Kishingo, Bukini, Kisunzu, Kuza, Sukuma, Msumbiji, Katewa, Njachama, Yangeyange na Mandendenga. Aidha, utekelezaji wa mradi wa miaka minne wenye lengo la kuongeza tija katika uzalishaji wa kuku wa asili (*African Chicken Genetic Gains - ACGG*) chini ya TALIRI na ufadhili wa Bill and Melinda Gates Foundation uliendelea na unahusisha nchi za Tanzania, Ethiopia na Nigeria. Jumla ya wafugaji 3,200 wanashiriki katika majaribio yanayohusisha aina tano za kuku kutoka nchini Uganda, Afrika ya Kusini, Ufaransa na Brazil. Jumla ya kuku 32,200 aina ya Kroiler na Sasso wamesambazwa kwa wafugaji. Pia, wafugaji 9,218

walipata mafunzo katika Kanda ya Kusini na Wilaya za Kilombero, Mvomero, Muheza na Korogwe. Taasisi kwa kushirikiana na wadau wa ACGG wamezindua mradi uitwao *The Agriculture to Nutrition Project* (ATONU) kwa lengo la kutathmini shughuli zinazotekelezwa na ACGG. Jumla ya kuku 8,578 walipatiwa chanjo ya kuwakinga na ugonjwa wa mdondo katika vijiji vinne (4) vya wilaya ya Nanyumbu, ambapo jumla ya sampuli za damu 320 zilikusanywa kwa lengo la kufanya ufuatiliaji na tathmini ya afya za kuku hao kabla na baada ya kupatiwa chanjo. Pia, utafiti wa nguruwe 103 unaendelea katika vituo vya Mpwapwa na Uyole, ambapo nguruwe 27 wanafanyiwa utafiti wa ukuaji na uhimili wa magonjwa kwa wafugaji katika Wilaya za Mpwapwa, Bahi na Chamwino.

**212.** ***Mheshimiwa Spika,*** TALIRI imeibua na kusambaza teknolojia za matumizi sahihi ya malisho ya mifugo (nyasi, mikunde na miti malisho) katika kanda zote za ki-ikolojia ikiwa ni pamoja na kuvuna na kuhifadhi chakula cha mifugo wakati wa kiangazi. Utafiti wa kuhifadhi malisho ukihusisha wafugaji katika nyanda kame umefanyika katika wilaya za Kilwa na Maswa ambapo kumekuwepo ongezeko la uzalishaji wa nyasi malisho kutoka tani 1.2 hadi 8.0 kwa hekta na tani 1.4 hadi 5.0 kwa hekta ya mchanganyiko wa malisho ya mikunde/nyasi (*grass/legume mixture*).

**213.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/2018, TALIRI itaendelea kuibua, kutathmini na kuendeleza kosaafu bora za mifugo ili kuongeza tija katika uzalishaji wa maziwa, nyama, mayai na wanyama hai pamoja na kuendeleza uzalishaji wa malisho na mbegu bora za malisho kwa ajili ya njanda za malisho. Aidha, Taasisi itafanya yafuatayo:-

(i) Kuzalisha mifugo bora kwa kutumia teknolojia ya uhimilishaji, uhawilishaji kiinitete (MOET) na matumizi ya madume bora yaliyochambuliwa kijenetiki;

(ii) Kufanya tafiti 40 zinazolenga kuibua, kutathmini, kuendeleza na kuhifadhi kosaafu na kuainisha sifa za kosaafu mbalimbali za mifugo na kuibua, kujaribu na

kusambaza teknolojia 20 za malisho ya mifugo katika kanda 7 za ikolojia;

(iii) Kutekeleza miradi ya kikanda (*Regional*) na ushirikiano wa taasisi za kimataifa ILRI, AU-IBAR, Bill and Melinda – miradi ya ACGG, ADGG na CARDESA na kuanza kwa mradi mpya wa EMRAPA Brazil/Tanzania wa kutumia teknolojia zenye kuhusisha kilimo-mifugo kuondoa umaskini;

(iv) Kufanya tafiti shirikishi kwa wafugaji zinazolenga kuwapatia teknolojia bora za mifugo na kuongeza wingi na ubora wa mazao yatokanayo na ng'ombe, mbuzi, kuku, nguruwe na malisho pamoja na usindikaji wa mazao ya mifugo; na

(v) Kusambaza teknolojia sahihi 10 zinazozalishwa vituoni kwa wafugaji ili kuwaongezea kipato na lishe, sanjari na kupata masoko ya uhakika ya mazao yao na kutoa elimu inayolenga kuongeza thamani ya mazao ya mifugo kupitia vipindi vya redio 52, luninga 12, vipeperushi na vijarida 1,500.

***Mafunzo***

**214.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo (*Livestock Training Agency – LITA*) imefanya udahili wa wanachuo 1,962, kati ya hao 726 ni wa Stashahada na 1,236 ni wa Astashahada. Wanachuo 1,324 (Stashahada 582 na 742 Astashahada) watahitimu mafunzo yao mwezi Juni, 2017. Vilevile, watumishi 22 wanaendelea na mafunzo, shahada ya Uzamivu wawili (2), shahada ya Kwanza 19 na Stashahada mmoja (1). Aidha, Wizara kupitia LITA imekarabati miundombinu ya vyuo vya mafunzo na kununua vitendea kazi, ambapo ukarabati wa maabara tatu (3) za Parasitolojia katika Kampasi za Mpwapwa, Morogoro na Madaba ulifanyika na kuziwekea vifaa vipya. Aidha, jengo lenye ofisi za wakufunzi lilikarabatiwa katika Kampasi ya Morogoro. Pia, kisima cha maji kwa ajili ya wanachuo kilikarabatiwa na kuwekewa pampu mpya katika Kampasi ya Tengeru. Vilevile, mabanda mawili kwa ajili ya ufugaji wa nguruwe yalikarabatiwa katika Kampasi za Buhuri na Tengeru.

**215.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia LITA itadahili wanachuo 2,600 wa Stashahada na Astashahada, na kutoa mafunzo kwa wafugaji 2,000 juu ya ufugaji bora wenye tija. Aidha, itajenga madarasa mawili (2) katika kampasi ya Madaba na Mpwapwa na kukarabati vitengo vya uzalishaji 20 katika Kampasi za Tengeru, Madaba, Mpwapwa, Mabuki, Buhuri, Kikulula na Morogoro. Vilevile, Wakala itawezesha wakufunzi wapya 16 kuhudhuria mafunzo ya mbinu bora za ufundishaji.

***Huduma za Ugani wa Mifugo***

**216.** ***Mheshimiwa Spika***, katika Mwaka 2016/2017, Wizara kwa kushirikiana na Halmashauri na sekta binafsi ilitoa elimu kwa wadau 5,430 kupitia mafunzo, mikutano ya uhamasishaji na semina zilizokuwa zikiendeshwa wakati wa maonyesho ya Nane nane. Aidha, Wizara imechapisha jumla ya nakala 9,800 ya vitabu vya ufugaji, vya kuku 5,000, ng'ombe 3,000, nguruwe 1,000 na mbuzi 800. Aidha, vipeperushi 18,000 na mabango 200 yamechapishwa na yanaendelea kusambazwa kwa wadau. Pia, Wizara ilirusha hewani vipindi 40 vya redio na sita (6) vya luninga kuhusu tekinolojia za hifadhi na uzalishaji wa malisho, uzalishaji wa nyama bora na udhibiti wa magonjwa ya mifugo. Vilevile, Wizara imekamilisha ukarabati wa kituo cha Maarifa ya Mifugo cha Lugoba (Bagamoyo) na inaendelea na ujenzi wa bweni utakaowezesha kituo kutoa elimu kwa wafugaji 11,600 kwa mwaka.

**217.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia utoaji wa huduma za ugani nchini kwa kuandaa na kurusha hewani vipindi 52 vya radio na 12 vya luninga juu ya ufugaji bora wa mifugo na kutoa teknolojia sahihi za uzalishaji wa mifugo. Aidha, Wizara itaendelea kuandaa maonyesho ya NaneNane na Siku ya Chakula Duniani. Pia, Wizara itaimarisha na kuboresha mashirikiano miongoni mwa watoa huduma za ugani kwa kuendesha mafunzo mrejesho kwa maafisa ugani wa mifugo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 50. Vilevile, Wizara itaandaa miongozo ya mafunzo kuhusu teknolojia zilizoboreshwa.

**218.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/2017, Wizara kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mradi wa Kuendeleza Mbari za Uzalishaji wa Maziwa katika Bara la Afrika, *(African Dairy Genetic Gain - ADGG)* na Mradi wa Ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kuboresha Uhimilishaji *(Public Private Partinership for Artifial Insermination Delivery - PAID)* imetoa mafunzo kwa wataalam 158 juu ya namna nzuri ya kutekeleza Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro, Tanga, Simiyu na Shinyanga. Pia, mafunzo ya utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo yametolewa kwa wataalam wa Mifugo wa Wilaya zote Tanzania Bara katika Mkutano wa Wadau wa Bodi ya Nyama uliofanyika Dodoma mwezi Januari 2017. Vilevile, vifaa vya utambuzi na regista vimesambazwa katika mikoa ya Kanda ya Kati, Magharibi, Kusini, Kaskazini na Nyanda za Juu Kusini. Aidha, uhamasishaji wa utekelezaji wa zoezi la utambuzi wa mifugo nchi nzima unaendelea ikiwa ni utekelezaji wa Agizo la Mhe. Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania la kuhakikisha Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo inatekelezwa na hadi sasa jumla ya mifugo 1,101,000 imetambuliwa.

**219.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kuratibu utekelezaji wa Mfumo wa Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Mifugo kwa njia ya kupiga chapa ya moto na kuvisha hereni ng'ombe katika Halmashauri zote**.** Aidha, Wizara itaandaa machapisho ya uhamasishaji na kuendesha kampeni za kuelimisha umma kuhusu mfumo wa utambuzi, usajili na ufuatiliaji wa mifugo (TANLITs) katika mikoa yote ya Tanzania Bara.

### *3.20 Usimamizi wa Ubora wa Mazao, Taaluma na Huduma za Veterinari*

#### *Tasnia ya Nyama*

**221.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kuimarisha uwezo wa kiutendaji wa Bodi ya Nyama Tanzania kwa kuweka mfumo wa fedha [EPICOR 10] na kutoa mafunzo ya uendeshaji wa mfumo huo kwa

watumishi nane (8) wa Bodi pamoja na kuipatia vitendea kazi muhimu. Vilevile, Bodi imetambua na kusajili wadau 276 na minada 9 katika mikoa ya Singida, Dar es Salaam, Dodoma na Arusha. Aidha, Bodi imeendelea kutoa mafunzo kuhusu Taratibu na Viwango vya Usafi na Uendeshaji wa Machinjio, Bucha na Viwanda vya kusindika nyama, Sheria ya Tasnia ya Nyama, usajili na ukaguzi wa wadau wa tasnia ya nyama kwa watumishi 152 katika Mamlaka za serikali za Mitaa 25 za mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma pamoja na mafunzo ya ufuatiliaji wa biashara ya mifugo na nyama kwa watumishi nane (8) katika mipaka ya Tunduma na Kasumulo iliyopo mikoa ya Songwe na Mbeya.

**222.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, wadau 638 wameelimishwa kuhusu Sheria ya Nyama na taratibu na viwango vya usafi na uendeshaji wa machinjio, bucha na viwanda vya kusindika nyama. Pia, jumla ya bucha 406, machinjio mbili (2) na mashamba manne (4) ya nguruwe na kuku (Brick Company, Boko, Misugusugu na Mitoboto) katika mikoa ya Pwani, Morogoro, Singida na Dar es Salaam yamekaguliwa, ambapo bucha 211, machinjio moja (1) na mashamba manne (4) yamekidhi matakwa ya Sheria ya Tasnia ya Nyama.

**223.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Bodi ya nyama imeendelea na kusimamia na kuhamasisha wadau ili kushiriki katika biashara ya nyama ndani na nje ya nchi ambapo hadi kufikia Machi 2017 jumla ya tani 3,162.65 za nyama ziliuzwa nje ya nchi katika nchi za Dubai, Iraq na Vietanam ikijumuisha tani 711.82 za nyama ya mbuzi, tani 439.03 za nyama ya ng'ombe, tani 222.74 za nyama ya kondoo na tani 1,789.06 za nyama ya punda. Pia, jumla ya tani 890.66 za nyama ziliingizwa nchini kutoka nchi za Kenya, Afrika Kusini na Uingereza zikijumuisha tani 366.34 za nyama ya nguruwe, tani 512.06 za nyama ya ng'ombe na tani 12.27 za nyama ya kondoo.

**224.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Bodi ya Nyama itaendelea kuhimiza ulaji wa nyama nchini kwa kutoa elimu kwa wananchi kuhusu

umuhimu wa kuzalisha nyama bora, safi na salama, kusindika na kutengeneza bidhaa mbalimbali za nyama zinazoweza kudumu kwa muda mrefu ili ziweze kuwafikia wananchi katika maeneo mengi zaidi zikiwa katika viwango stahiki ili kujenga afya na lishe na hivyo kuongeza ulaji wa nyama nchini.

**225.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kuijengea uwezo wa kiutendaji Bodi ya Nyama kwa kuajiri watumishi 14. Aidha, Bodi itasajili wadau 10,000 wa tasnia ya nyama na vyama vyao; kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Tasnia ya Nyama Sura 421; Kutoa mafunzo ya Taratibu na Viwango vya Usafi na Uendeshaji wa Machinjio, Bucha na Viwanda vya kusindika nyama kwa watumishi 144 kutoka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 48 za mikoa ya Kigoma, Kagera, Mara, Mwanza, Shinyanga, Iringa, Mbeya na Arusha. Pia, Bodi itaendelea kuhamasisha ulaji nyama bora na salama kwa kutumia vyombo vya habari na matamasha ya nyama; Kuhamasisha na kutoa mafunzo kwa wafugaji 2,500 kuhusu ufugaji wa kibiashara na kutambua wafugaji wakubwa na kuwaunganisha na wasindikaji ili kuboresha upatikanaji wa mifugo; Kusimamia biashara ya mifugo na nyama katika masoko ya ndani na kufuatilia uingizaji na uuzaji nje ya nchi mifugo, nyama na bidhaa zake na Kuendelea kuimarisha vyama sita (6) vya wadau kitaifa (TALIMETA, CCWT, TANZEBA, TAPIFA, PAT na TAMEPA) kwa kutoa ushauri na kuratibu maendeleo ya vyama hivyo.

***Tasnia ya Maziwa***

**225.** ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Maziwa imefanya ukaguzi wa viwanda vya maziwa (7) katika mikoa ya Dar es Salaam (3), Tanga (2) na Arusha (2). Ukaguzi huo pia ulifanyika kwa wafugaji 34 katika mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Pwani na vituo sita (6) vya kukusanyia maziwa mkoani Tanga. Aidha, Bodi imesajili wadau 172 ambao ni wazalishaji wa maziwa (139), wasambazaji wa maziwa (5), vituo vya kukusanyia maziwa (6), waingizaji wa maziwa kutoka nje (17), wauza pembejeo (5) na vyombo vya kusafirishia maziwa (58).

Pia, Bodi ya Maziwa imeendelea kusimamia uingizaji wa Maziwa kutoka nje ya nchi kwa kutoa vibali 396 vyenye thamani ya shilingi 17,189,226,511 katika kipindi cha mwezi Julai 2016 hadi Machi 2017.

**226.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018 itasimamia sheria ya maziwa na kanuni kwa kutoa elimu kupitia programu thelathini (30) za redio, program nne (4) za television na matangazo thelatini (30) ya redio na televisheni, itawezesha uanzishwaji wa vyama 10 vya wadau, majukwaa 16 (DDF) na kuimarisha vyama viwili (2) vya kitaifa (TAMPA na TAMPRODA), itatoa mafunzo na vifaa kwa wakaguzi wa maziwa 75 pamoja na kuanzisha mfumo wa ukaguzi katika kanda za Kaskazini, Mashariki na kanda ya Ziwa. Aidha, itatoa mafunzo ya teknolojia za usindikaji na udhibiti wa ubora kwa wasindikaji wadogo 45 kutoka Kanda za Kaskazini, Mashariki na Ziwa na itawezesha huduma za uendelezaji wa biashara kwa kuwaunganisha wadau 100 na huduma za kibenki.Pia, Bodi itafanya ukaguzi katika miji mitano (5), Arusha, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Mwanza na Zanzibar ili kubaini uingizwaji wa maziwa usiofuata utaratibu.

***Taaluma na Huduma za Veterinari***

**227.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania imesajili Madaktari wa Mifugo wapya 11 na kufikisha idadi ya Madaktari 761 walioko nchini. Aidha, imesajili vituo 97 vya kutolea huduma za mifugo na kuoodhesha au kuandikisha wataalam wasaidizi 189 na kufanya idadi yao kufikia 2,765. Vilevile, wakaguzi 103 wamepewa leseni za kuwawezesha kutoa huduma za mifugo. Aidha, Barara la Veterinari lilifanya ukaguzi wa mitaala katika vyuo saba (7) vya mafunzo ya mifugo vya Kaole (Bagamoyo), CANRE (Dar es Salaam), Visele (Mpwapwa), LITA Mpwapwa, Morogoro, Tengeru na Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine - SUA.

**228.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Baraza la Veterinari Tanzania itakagua na kutambua vituo vya mafunzo ya mifugo na mitaala

inayotumika kufundishia na itasajili Madaktari wa mifugo 60, kuandikisha na kuorodhesha wataalamu wasaidizi 1,000 na kutoa leseni 100 kwa wakaguzi wa nyama, 50 kwa wataalam wa maabara na 50 kwa wahimilishaji na kusajili vituo 400 vya kutolea huduma za mifugo. Aidha, itafanya ukaguzi katika vituo vya kutolea huduma za mifugo na uzingatiaji wa maadili ya taaluma husika katika Kanda zote nane (8) za ikolojia ya Kilimo (*Agro-ecological zones*).

**FUNGU 64 : UVUVI**

**3.21 Sera, Mikakati na Programu**

**229.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Uvuvi ya Mwaka 2015 kwa lengo la kuimarisha usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi. Pia, Wizara imesambaza kwa wadau nakala 1,000 za Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 2015, nakala 100 za Fursa za Uwekezaji katika sekta ya uvuvi na nakala 670 za Mpango wa Kusimamia samaki wanaopatikana katika Tabaka la Juu la Maji. Katika mwaka 2017/2018, Wizara itakamilisha mandalizi ya Mkakati wa kutekeleza Sera ya Uvuvi ya Mwaka 2015. Vilevile, Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi Bahari Kuu itakamilisha Sera ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu.

***3.22 Sheria na Kanuni za Sekta ya Uvuvi***

**230.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Muswada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania ulipitishwa na Bunge na kusainiwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania Na. 11 ya mwaka 2016. *Notisi ya tarehe ya kuanza kutumika Sheria ya TAFIRI Tanzania Fisheries Research Institute (Commencement Date) Notice 2017;* imetolewa kwenye Tangazo la Serikali Na. 128 la mwaka 2017. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wadau imefanya marekebisho ya Sheria za Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya mwaka 1994 na mapendekezo ya marekebisho yamewasilishwa Serikalini kwa hatua husika. Pia, Wizara

imeainisha maeneo yanayohitaji marekebisho katika Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu (*The Deep Sea Fishing Authority Act*) SURA 388 kwa ajili ya kujadiliwa na wadau. Vilevile, marekebisho ya Kanuni za Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu (*The Deep Sea Fishing Authority Regulations*), 2016, yamefanyika na kutangazwa katika Gazeti la Serikali Na.323 la mwaka 2016 na Pia, Wizara imeendelea kuhamasisha wadau wa Sekta ya Uvuvi kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za Uvuvi; athari za uvuvi haramu na faida za uvuvi endelevu kupitia mikutano, vikao na maonesho ya Nanenane na Siku ya Mvuvi Duniani ambapo jumla ya wadau 2,226 walipata elimu hiyo.

**231.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itakamilisha mapitio ya Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003; Sheria ya Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu Na. 29 ya mwaka 1994 na Sheria ya Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi katika Bahari Kuu Na. 1 ya mwaka 1998 na marekebisho yake ya mwaka 2007. Aidha, itaandaa kanuni mpya za kutekeleza Sheria ya Uvuvi Na 22 ya mwaka 2003. Pia, itaendeleza taratibu za kuanzisha Shirika la Uvuvi Tanzania kwa lengo la kuwa na meli za kitaifa (*National fleet*) zitakazokuwa zinavua Bahari Kuu kwa utaratibu wa ubia na sekta binafsi. Kuwepo kwa meli za kitaifa kutasaidia kuongeza upatikanaji wa samaki hususan kutoka Ukanda wa Uchumi wa Bahari na hivyo kuongeza ajira, malighafi kwa ajili ya viwanda, pato la Taifa na kuboresha lishe.

### *3.23 Uzalishaji na Biashara ya Mazao ya Uvuvi*

**232.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, jumla ya tani 362,595 za samaki wenye thamani ya shilingi trilioni 1.49 zilivunwa na wavuvi 203,529 ikilinganishwa na tani 362,645.3 za samaki wenye thamani ya shilingi trilioni 1.48 waliovunwa mwaka 2015/2016 **(Kiambatisho Na.2a na 2b)**. Pia, jumla ya tani 39,691.5 za samaki na mazao ya uvuvi yenye thamani ya shilingi bilioni 526.99 yaliuzwa nje ya nchi na kuliingizia Taifa jumla ya shilingi bilioni 14.30 ikiwa ni ushuru **(Kiambatisho Na.3a na 3b).** Aidha, kanzidata ya takwimu za uzalishaji na uuzaji wa mazao ya uvuvi imeendelea

kuboreshwa kwa lengo la kuimarisha uhifadhi na upatikanaji wa takwimu za uvuvi.

**233.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017 Wizara imeendelea kutoa elimu kwa wavuvi na wadau wengine wa uvuvi kuhusu njia endelevu za uvunaji kwa lengo la kuwezesha sekta hii kutoa mchango wake ipasavyo katika pato la Taifa, kuongeza ajira, kipato na uhakika wa chakula na lishe. Jumla ya wavuvi 249 walipatiwa mafunzo kuhusu usimamizi wa uvuvi unaozingatia ikolojia na mazingira (*Ecosystem Approach to Fisheries Management*) katika Halmashauri za Wilaya za Mkinga (32), Mtwara (47), Kilwa (49), Kinondoni (43), Kigambaoni (52) na Temeke (26).

**234.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017 Wizara imeendelea kutekeleza Mpango wa Kusimamia Uvuvi wa Samaki Wanaopatikana katika Tabaka la Juu la Maji (*Pelagic Fishery Management Plan*), Mpango wa Kusimamia Uvuvi wa Pweza (*Octopus Fishery Management Plan*), na Mpango wa Kusimamia Uvuvi wa Kambamiti (*Prawn Fishery Management Plan*) kwa lengo la kuhakikisha kuwa aina ya samaki walioainishwa kwenye mipango hiyo wanavuliwa kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu zinazoongoza uvuvi.

**235.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018 Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia uvunaji na matumizi endelevu ya raslimali za uvuvi nchini. Aidha, kwa kushirikiana na Mamlaka za Serikali za Mitaa itafanya sensa saba (7) za uvuvi na kufuatilia ukusanyaji na uchakataji wa takwimu za uvuvi katika maeneo ya maji makubwa na madogo.

### *3.24 Ukuzaji wa Viumbe kwenye Maji*

**236.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/2017, Wizara kwa kushirikiana na taasisi za serikali, vikundi mbalimbali pamoja na watu binafsi imeendelea kuhimiza na kusimamia shughuli za ukuzaji viumbe kwenye maji zikiwemo ufugaji samaki, kambamiti, kilimo cha mwani na ukuzaji wa chaza wa lulu kwa lengo la kuongeza upatikanaji wa samaki kwa ajili ya lishe, ajira, kipato kwa wananchi na kuchangia pato la Taifa.

**237.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuimarisha na kuongeza miundombinu ya uzalishaji wa vifaranga bora vya samaki kwa kujenga mabwawa na kuweka matenki katika vituo vya serikali vilivyopo Bagamoyo (Pwani), Kingolwira (Morogoro), Machui (Tanga), Mwamapuli (Tabora), Nyamirembe (Geita), Nyengedi (Lindi) na Ruhila (Ruvuma). Aidha, vitotoleshi (*incubators*) 15 vya samaki aina ya perege vyenye uwezo wa kuzalisha vifaranga **11,520,000** kwa mwaka katika kituo cha Kingolwira vimewekwa.

**238.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, jumla ya vifaranga vya samaki na Kambamiti 14,119,272 vimezalishwa na vituo vya Serikali (421,368) na sekta binafsi (13,697,904) ikilinganishwa na jumla ya vifaranga 18,000,000 vilivyozalishwa mwaka 2015/2016. Kushuka kwa uzalishaji wa vifaranga kilisababishwa na kufungwa kwa kituo cha Kingolwira-Morogoro ili kupisha maboresho ya miundombinu ya Maji na umeme, kutokupatikana kwa chakula cha samaki cha ruzuku kwa sekta binafsi na baadhi ya mabwawa kubomoka kutokana na mafuriko. Aidha, kati ya vifaranga 421,368 vilivyozalishwa na vituo vya Serikali, kituo cha Ruhila-Songea (153,000), Mwamapuli-Igunga (120,000), Machui - Tanga (10,000) na TAFIRI - Mwanza (138,368). Vifaranga hivi vilisambazwa kwa wafugaji wa samaki katika mikoa ya Mbeya, Iringa, Tanga, Tabora, Njombe, Singida, Ruvuma na Mwanza.

**239.** ***Mheshimiwa Spika,*** sekta binafsi vilevile, imezalisha vifaranga 13,697,904 kutoka makampuni ya Eden, Dar es Salaam (2,219,800), Roela – Mwanza (150,000), Sisso, Kigoma mjini (18,404), Kasulu (2,000) na Dola-Kigoma (11,000), Pwani-Kisarawe (5,300), SOFFA Ruvuma (2,000), Chifive & Consultant-Mara (2,000), Safina Big Fish-Dar-es-salaam (285,200), Kitungwa-Morogoro (600) na Lamadi-Simiyu (1,600). Aidha, Kampuni ya "Alphakrust Ltd" ilizalisha vifaranga ("Post larvae") vya Kambamiti 11,000,000 na kupandikizwa katika mabwawa ya kampuni na vingine kusambazwa kwa wafugaji binafsi waliopo mkoa wa Pwani.

**240.** ***Mheshimiwa Spika***, uzalishaji na usafirishaji wa

mazao ghafi ya mwani nje ya nchi umeongezeka kutoka tani 1,176.51 zenye thamani ya Shilingi milioni 350 mwaka 2015/2016 hadi tani 1,197.5 zenye thamani ya shilingi milioni 412 mwaka 2016/2017. Aidha, kiwango cha uzalishaji wa samaki kimefikia tani 11,000 zenye thamani ya shilingi bilioni 55 ukilinganisha na tani 3,613.55 zenye thamani ya shilingi bilioni 18.1 mwaka 2015/2016.

**241.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka wa fedha 2016/2017, jumla ya mabwawa ya samaki 159 yamechimbwa katika mikoa ya Geita (23), Ruvuma (51), Mara (14), Pwani (53), Tanga (2), Dodoma (3), Morogoro (3), Tabora (7), Dar es Salaam mabwawa (2) na Kigoma (1) na kufikisha jumla ya mabwawa 22,702 yakilinganishwa na mabwawa 22,545 ya mwaka 2015/2016 **(Kiambatisho Na. 10)**.

**242.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za Serikali za kupanua wigo wa ufugaji samaki hapa nchini, teknolojia ya ufugaji samaki kwenye vizimba (*Cage fish culture technology*) kwa ajili ya kufuga samaki aina ya sato imeanza kutekelezwa kwa kuhusisha sekta binafsi na SUMA JKT katika Ukanda wa Ziwa Victoria, Tanganyika na Nyasa. Teknolojia hii inawezesha uzalisha wa samaki wengi kwenye eneo dogo la maji (*Low Volume High Density*). Ili kuwa na ufanisi katika utekelezaji wa teknolojia hii, Wizara inashirikiana na sekta mtambuka ambazo ni Taasisi za Serikali kama Baraza la Mazingira la Taifa (NEMC), Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) na Wizara ya Maji. Hadi sasa, jumla ya Vizimba 109 vimewekwa katika maziwa ya Victoria (63), Tanganyika (4) na Nyasa (42).

**243.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Ziwa Victoria jumla ya makampuni binafsi sita (6) yameweka vizimba ya Mpanju Fish Farm (Ilemela), Kirio Makori Wambura – Sengerema, Aquasol Co. Ltd – Bunda, Vend Commodities Ltd-Katwe, Simon Mseti Wangwe – Ilemela, Rehema Kassimu – Sengerema na SUMA JKT – Bunda ambapo SUMA JKT inamiliki vizimba 50 na inasimamia vizimba 8 vinavyomilikiwa na Kijiji cha Karukekere Wilaya ya Bunda na vizimba 5 vinavyomilikiwa na Kikundi cha kijiji cha Kemondo (Bukoba vijijini). Katika ziwa

Nyasa, Kampuni ya ROFACOL TANZANIA CO. LTD imeweka vizimba 42 na katika ziwa Tanganyika, Kampuni ya QP Group Co. Ltd imeweka vizimba 4.

**244.** ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha na kudhibiti usalama wa soko la ndani na nje kwa mazao yatokanayo na ukuzaji viumbe kwenye maji, Wizara imefanya yafuatayo:-

(i) Kupitia Mpango wa Ufuatiliaji Ubora wa Mazao ya Kambamiti kutoka kwenye mabwawa ya kambamiti ya Kampuni ya "*Alphakrust*" yaliyopo katika Wilaya ya Mafia kwa kuchunguza mabaki ya madini tembo na kemikali ili kuhakikisha kuwepo kwa soko la Jumuiya ya Nchi za Ulaya na mazao yaliyokuwa salama kwa walaji;

(ii) Kutoa mafunzo ya kudhibiti magonjwa na usalama wa mazingira ya ufugaji samaki kwa mameneja 10 wa vituo vya kuzalisha vifaranga Jijini Dar es salaam;

(iii) Kupitia na kuboresha Kanuni za Ufugaji Samaki katika Vizimba vya Jumuia ya Afrika Mashariki (*Cage Fish Farming Guidelines for East African Community*);

(iv) Kupitia na kuboresha Mwongozo wa Ukuzaji Viumbe kwenye Maji bahari chini ya Mradi wa SWIOFish; na

(v) Wizara imeingia Makubaliano na Halmashauri ya Wilaya ya Chato ili kuendeleza Kituo cha Ufugaji Samaki cha Nyamirembe kwa lengo la Halmashauri kusimamia na kuendesha kituo hicho.

**245.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/2017, jumla ya wananchi 4,146 wamepata elimu ya ukuzaji viumbe kwenye maji kupitia mafunzo ya moja kwa moja vituo 15 vya serikali, makao makuu, maonesho ya Nane Nane na Siku ya Mvuvi Duniani. Aidha, katika kuendeleza ukuzaji viumbe kwenye maji Bahari, vikundi 10 vinavyozalisha zao la mwani vilipata mafunzo ya kuongeza thamani kwa kutengeneza sabuni na shampoo kutoka katika wilaya ya Kilwa-Lindi. Vilevile, jumla ya vikundi 55 vyenye wanachama 373

vimeundwa katika mikoa ya Ruvuma (4), Morogoro (9), Mbeya (3), Tanga (1), Dar es Salaam (1), Mara (9), Lindi (21), Njombe (5) na Geita (2) kwa ajili ya kuendeleza kuendeleza ufugaji wa samaki kwenye maji baridi.

**246.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/2018, Wizara itatekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuimarisha na kuendeleza vituo saba (7) vya ufugaji samaki vya Ruhila (Songea), Mwamapuli (Tabora), Kingolwira (Morogoro), Nyengedi (Lindi), Machui (Tanga), Mbegani (Bagamoyo),i na Nyamirembe - Chato kwa kuvipatia vitendea kazi na kuimarisha miundombinu ili viweze kuzalisha vifaranga milioni 13;

(ii) Kuanisha, kuyatambua kwa kufanya upembuzi yakinifu na tathmini ya mazingira, kuingiza kwenye ramani na kuyatangaza kwenye gazeti la Serikali maeneo yanayofaa kwa ufugaji samaki kwenye vizimba katika Ziwa Victoria;

(iii) Kuwezesha vituo vinne (4) vya ufugaji samaki wa maji baridi vya Bukoba, Kilimanjaro, Mwanza na Mara kwa kuwapatia usafiri na vitendea kazi;

(iv) Kutoa ruzuku ya tani 200 za chakula cha samaki kwa wafugaji;

(v) Kuzalisha na kupandikiza vifaranga vya samaki katika malambo na mabwawa ya asili kumi (10) katika mikoa ya Shinyanga, Tanga, Lindi, Mtwara, Songwe, Manyara, Arusha, Pwani, Simiyu na Mwanza na kwenye skimu tano (5) za umwagilianji miwa na mpunga (Namtumbo, Kilombero, Lower Moshi, Korogwe na Mvomero) ili kuongeza upatikanaji wa samaki; na

(vi) Kuhamasisha ufugaji mseto wa samaki na kilimo cha mpunga katika wilaya za Igunga na Mbarali.

### *3.25 Uwezeshaji wa Wavuvi wadogo na Wakuzaji Viumbe kwenye Maji*

**247.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kuhamasisha wavuvi kuwekeza katika ununuzi wa zana bora za uvuvi ili waweze kuvua kwenye maji ya kina kirefu katika Maziwa na Bahari ambapo idadi ya boti zenye injini imeongezeka kutoka 11,284 mwaka 2015/2016 hadi 14,136 mwaka 2016/2017 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 25.3. Pia, Wizara kupitia Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu, imeweka jumla ya vifaa 36 vya kuvutia samaki (*Fish Aggregating Devices – FADs*) ili kuvutia samaki wakusanyike mahali pamoja na hivyo kuwarahishia wavuvi kuwafikia kwa urahisi. Vifaa hivyo vimewekwa katika eneo la mfano la Bagamoyo na wavuvi wameendelea kuhamasishwa kuhusu matumizi ya teknolojia hiyo. Aidha, Wizara inaendelea na mpango wa kutoa ruzuku kwa vikundi vya wavuvi ambapo jumla ya injini 22 zimelipiwa na kuchukuliwa na vikundi kutoka Halmashauri za wilaya za Mafia (1), Nkasi (7), Muheza (6), Bagamoyo (4) na Manispaa za Dar es Salaam (4) kati ya injini 73 zilizonunuliwa na Serikali katika mwaka 2015/2016. Wizara inaendelea kuwasiliana na Halmashauri husika ili kukamilisha Mipango na vikundi vyao ili kulipia asilimia 60 na kuzichukua injini 51 zilizobaki.

**248.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeendelea kutoa ushauri wa kisera, sheria, kanuni na miongozo ya utunzaji na uhifadhi wa mazao ya uvuvi katika masoko ya Kimataifa ya Magogoni (Dar es Salaam) na Kirumba (Mwanza), masoko madogo ya mazao ya uvuvi na kwenye mialo 35 ya kupokelea samaki katika Ukanda wa Ziwa Victoria (28), Ukanda wa Pwani (3) na Ziwa Tanganyika (4). Aidha, Wizara imeanza ukarabati wa Soko la Samaki la Kasenda katika Wilaya ya Chato Mkoa wa Geita. Soko hili litakuwa na uwezo wa kupokea samaki kutoka mialo ya Kome Mchangani, Chakazimbwe, Zilagula, Kasarazi, Yozu na visiwa vingine katika Ziwa Victoria.

**249.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya wavuvi 273 wamepatiwa mafunzo kuhusu teknolojia sahihi ya ukaushaji

wa dagaa katika mikoa ya Mara (70), Mwanza (63) Kagera (69) na Kigoma (71). Aidha, vichanja 30 vimejengwa kwa ajili ya kukaushia dagaa katika wilaya za Musoma (10), Bukoba (10) na Mwanza (10). Kutokana na mafunzo hayo, tanuru moja la kukaushia dagaa limejengwa katika eneo la Kimoyomoyo Wilaya ya Muleba, banda la kuhifadhia dagaa limejengwa katika eneo la Kubumbilo Wilaya ya Muleba. Pia, wachakataji 218 kutoka mikoa ya Geita (76), Mwanza (51), Kagera (43) na Mara (48) wamepewa mafunzo kuhusu matumizi ya vifungashio ili kuongeza thamani na ubora wa mazao ya uvuvi.

**250.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kuhamasisha wavuvi na wadau wengine wa uvuvi kuwekeza katika sekta ya uvuvi. Aidha, Wizara itatoa mafunzo kuhusu upatikanaji na matumizi ya teknolojia na miundombinu inayofaa kwa ajili ya uandaaji, uchakataji, usambazaji na upatikanaji wa masoko ya samaki na mazao yake wa uvuvi. Vilevile, Wizara itatoa mafunzo kwa wadau 400 juu Usalama na Ubora wa mazao ya uvuvi. Pia, Wizara itaendelea kuwezesha wavuvi wadogo kupata zana za uvuvi kupitia Mpango wa ruzuku.

### *3.26 Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi*

**251.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, ili kuwa na uvuvi endelevu wa samaki aina ya kambamiti, Wizara ilikubaliana na wadau kufungua uvuvi wa kambamiti ambao ulifungwa mwaka 2008 kwa wavuvi wakubwa na kati kufuatia kupungua kwa rasilimali hiyo. Hatua hiyo ilifikiwa kufuatia taarifa ya utafiti kuonesha kuongezeka kwa rasilimali hiyo. Masharti yaliyowekwa ni (i) kuanza na meli 12 za wavuvi wa kati na wakubwa (ii) uvuvi huo kufanyika kwa kipindi cha miezi mitano (5) kuanzia Aprili hadi Agosti (iii) kufunga uvuvi huo kwa miezi saba kuanzia mwezi Septemba hadi Machi kila mwaka kwa wavuvi wote. Tangazo kwa umma kuhusu kufunguliwa kwa uvuvi huo lilitolewa mwezi Machi, 2017 ambapo Jumla ya maombi kumi (10) yalipokelewa na kufanyiwa uhakiki kabla ya kuruhusiwa kufanya uvuvi wa kambamiti.

**252.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Ufundishaji wa Masuala ya Usimamizi wa Uvuvi Unaozingatia Ikolojia na Mazingira kwa lengo la kuwezesha kutoa mafunzo sahihi kuhusu dhana ya usimamizi wa uvuvi unaozingatia ikolojia na mazingira kwa wadau wote nchini. Aidha, Wizara imetoa elimu kuhusu dhana ya usimamizi wa uvuvi unaozingatia ikolojia na mazingira kwa wavuvi 249 kutoka Halmashauri za Wilaya za Mkinga (32), Mtwara (47), Kilwa (49), Kinondoni (43), Kigamboni (52) na Temeke (26). Pia, uhamasishaji kuhusu dhana hiyo ulifanyika kwa Madiwani na Viongozi wa ngazi za juu 53 katika Halmashauri ya Mkinga.

**253.** ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Kitaifa wa Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi kwa lengo la kuimarisha usimamizi shirikishi wa rasilimali za uvuvi kupitia Vikundi Shirikishi vya Rasilimali za Uvuvi (Beach Management Units-BMUs). Wizara kupitia Mradi wa South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth (SWIOFish) ilifanya tathmini ya utendaji kazi wa Vikundi vya Usimamizi Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMUs) na kubainika kuwa uongozi uliokuwa madarakani kwa BMUs nyingi umemaliza muda wake. Kutokana na hali hiyo, BMUs 48 kutoka Halmashauri zinazotekeleza mradi wa SWIOFish za Mkinga (14), Tanga Jiji (5), Pangani (10), Bagamoyo (9) na Lindi Vijijini (10) ziliwezeshwa kufanya chaguzi za viongozi na hivyo kuzifanya kutekeleza majukumu ya kusimamia uvuvi endelevu kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Uvuvi.

**254.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika Mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia upatikanaji wa takwimu na taarifa sahihi za Sekta ya Uvuvi kwa kutoa mafunzo kwa wakusanyaji kutoka Halmashauri 16 za Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi. Aidha, Wizara kupitia Mradi wa Kuhifadhi Mazingira ya Ziwa Victoria (Lake Victoria Environmental Management Project) na SWIOFish imefanya sensa za uvuvi katika Ukanda wa Ziwa Victoria na Pwani ya Bahari ya Hindi. Matokeo ya sensa yameonesha kuongezeka kwa nguvu ya uvuvi (nyavu 14%, wavuvi 50.8% na vyombo

vya uvuvi 26%) katika Ukanda wa Bahari ya Hindi ukilinganisha na sensa ya uvuvi ya mwaka 2009. Katika Ukanda wa Ziwa Victoria kwa upande wa Tanzania matokeo yameonesha kuongezeka pia kwa nguvu ya uvuvi ikilinganishwa na sensa ya mwaka 2014. Ongezeko hili kwa upande wa pwani ya Bahari ya Hindi linaashiria kwamba watu wengi zaidi wanavutiwa kujihusisha na shughuli za uvuvi. Ongezeko hili kwa upande wa Ziwa Victoria linatishia uendelevu wa Raslimali za Uvuvi kwani kuna ongezeko kubwa la matumizi ya nyavu haramu zisizoruhusiwa kisheria kama vile makokoro, nyavu za timba, utali, nyavu zenye macho madogo pamoja na kuunganisha nyavu (vertical integration).

**255.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kuratibu na kusimamia uvunaji na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi ikiwemo uvuvi wa samaki aina ya kambamiti; kuendelea kuhamasisha jamii za wavuvi kusimamia, kuendeleza na kutunza rasilimali za uvuvi kwa kuzingatia mfumo wa ikolojia na mazingira nchini; kupitia upya mfumo wa ufanyaji kazi wa Vikundi vya Usimamizi wa Rasilimali za Uvuvi kulingana na Mwongozo mpya wa BMU; kufanya sensa za uvuvi na kufuatilia ukusanyaji na uchakataji wa takwimu za uvuvi katika maeneo ya maji makubwa na madogo na kuboresha mfumo wa Wizara wa ukusanyaji na uhifadhi wa takwimu za uvuvi.

### *3.27 Usimamizi wa Uvuvi katika Bahari Kuu*

**256.** ***Mheshimiwa Spika*****,** Mamlaka ya Usimamizi wa Uvuvi katika Bahari Kuu kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania (TAFIRI) inafanya tafiti za uwezekano wa kutambua maeneo mapya ya uvuvi na samaki wanaoweza kupatikana katika maeneo hayo. Tafiti hizo zinahusisha uwekaji wa vifaa vya kuvutia samaki na kutambua maeneo yenye kutembelewa na samaki, hasa aina ya jodari. Hatua hizi zinasaidia kuwarahisishia wavuvi kupunguza gharama na muda wa kutafuta samaki. Aidha, kupitia TAFIRI, FADs zipatazo 72 zimetengenezwa, kati ya hizo, FADs 36 zimewekwa maeneo ya Bagamoyo katika mkoa wa Pwani na 36 zitawekwa Nungwi Zanzibar.

**257.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka kwa kushirikiana na *WWF* imefanya tathimini ya mnyororo wa thamani ya samaki aina ya Jodari na jamii zake kwa kuwajengea uwezo watafiti na watalaam wa uvuvi kuhusu Utafiti na Uhifadhi wa Raslimali za Uvuvi kwenye Bahari Kuu; kutoa elimu ya biashara kwa wadau; kufanya bandari ya Dar es Salaam ivutie meli za uvuvi kutoka Bahari Kuu kwa kuweka miundombinu ya kupokea na kuhifadhi samaki na kuboresha uratibu, udhibiti na doria katika Bahari Kuu.

**258.** ***Mheshimiwa Spika,*** Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu imeimarisha ulinzi wa rasilimali za uvuvi wa Bahari Kuu kwa kufanya doria za angani na baharini. Katika kipindi cha mwaka 2016/2017, jumla ya masaa 100 ya doria za angani na baharini zilifanyika kwa kushirikiana na Kamisheni ya Bahari ya Hindi (Indian Ocean Commission (IOC). Nchi zilizoshiriki katika doria hizo ni Comoro, Madagaska, Ushelisheli, Kenya, Msumbiji na Tanzania. Kuimarika kwa doria kumepelekea kuongezeka kwa meli zinazokata leseni hivyo kuongeza mapato ya Serikali. Aidha, Mamlaka imo katika hatua za kufunga mtambo mkubwa na wa kisasa (Themi web centre) kwa ajili ya kuimarisha ulinzi katika Bahari Kuu utakaohusisha Wizara zetu mbili za uvuvi za Serikali ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), Marine Polisi, Jeshi la Wanamaji (Navy), MRCC (SUMATRA) na Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM), ili kufuatilia Zaidi mienendo ya meli za uvuvi na kudhibiti uvuvi haramu.

**259.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu imechukua hatua za kuzifanyia marekebisho baadhi ya kanuni za Mamlaka yanayolenga kuongeza mapato kwa nchi yetu na kutoa ajira kwa wananchi wetu. Miongoni mwa marekebisho hayo ni kuzitaka meli zinazokata leseni za uvuvi wa Bahari Kuu kushusha samaki wasiolengwa katika bandari za Tanzania, kutoza mrahaba kwa samaki watakaovuliwa katika Bahari Kuu, kuruhusu uvuvi wa kukokota kwa nyavu za juu (*Mid and Surface Trawling*) na kuajiri vijana wa Kitanzania ili kufanyakazi melini. Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi,

Mawasiliano na Uchukuzi wamekubaliana kuboresha gati Na. Sita (6) katika Bandari ya Dar es Salam na gati namba tatu (3) ya Zanzibar ili ziweze kuhudumia meli za uvuvi wa Bahari Kuu. Matumizi ya bandari zetu yatawezesha meli za uvuvi wa Bahari Kuu zinazokuja kushusha samaki wanaolengwa na wasiolengwa kununua mafuta, chakula na maji na hivyo kuongeza mapato kwa nchi yetu.

**260.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2017/2018, Mamlaka itashiriki katika kufanya mapitio ya Sheria na Kanuni za Uvuvi wa Bahari Kuu na kuboresha mfumo wa kufuatilia meli zinazovua katika Bahari Kuu (*Vessel Monitoring Sytem - VMS*). Vilevile, kwa kushirikiana na Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi Kampasi ya Mbegani itatoa mafunzo ya Uvuvi wa Bahari Kuu kwa wavuvi 50, kuendesha doria za anga na itahamasisha wadau kuwekeza kwenye Uvuvi wa Bahari Kuu. Aidha, Mamlaka itaendelea kushirikiana na nchi wanachama wa Kamisheni ya Usimamizi wa Uvuvi wa Samaki aina ya Jodari katika Bahari ya Hindi ya (*Indian Ocean Tuna Commission*), Mashirika ya Kikanda na Kimataifa katika usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za Uvuvi wa Bahari Kuu na usimamizi wa mazingira. Pia, itaboresha na kusimamia ukusanyaji takwimu na maduhuli katika Uvuvi wa Bahari Kuu.

### *3.28 Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu*

**261.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) iliendelea kusimamia rasilimali za bahari na mwambao zilizomo katika maeneo 18 yaliyohifadhiwa, ambayo ni Hifadhi za Bahari tatu (3) na Maeneo Tengefu 15 pamoja na maeneo yaliyoko jirani na mipaka ya maeneo hayo. Jumla ya doria 135 za baharini na nchi kavu zenye siku kazi 675 zilifanyika. Matokeo ya doria hizo ni pamoja na kukamatwa kwa watuhumiwa 29 waliokuwa wakijishughulisha na uvuvi haramu na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria. Vilevile, doria hizo zilihusisha ukamataji wa nyavu ndogo na makokoro 19, vyombo vya uvuvi 26, samaki waliovuliwa kwa vilipuzi kilo 265, samaki waliovuliwa

kwa juya kilo 20, *detonator* za kutengenezea vilipuzi vipande 26, fito za mikoko 282 na mbao 202 za mikoko.

**262.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara inaendelea na taratibu za kutangaza Maeneo Tengefu matatu (3) ya visiwa vya Nyuni, Ukuza na Simaya. Pia, Kitengo kiliendelea kutangaza vivutio na fursa za utalii zilizomo katika maeneo yaliyohifadhiwa na kuhamasisha wawekezaji kuwekeza katika ujenzi wa hoteli ndani ya hifadhi (*eco-lodge*) ili kuongeza kasi ya uendelezaji wa maeneo tengefu yenye vivutio. Katika kipindi hicho, eco-lodge yenye hadhi ya nyota tano ilifunguliwa katika Eneo Tengefu la Shungumbili lililoko Wilayani Mafia.

**263.** ***Mheshimiwa Spika*,** MPRU iliendelea kuwezesha jamii kwa njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na mgao wa mapato ya maduhuli kiasi cha shilingi 124,285,160.50 zilizotokana na shughuli za utalii. Aidha, utekelezaji wa miradi inayoibuliwa na vijiji vilivyopo ndani ya Hifadhi ya Bahari ya Kisiwa cha Mafia (HIBAMA) umeanza kufanyika kwa kukamilisha miradi ya ujenzi wa madarasa matatu (3) katika shule ya msingi Kibaoni na ghala la kutunzia mwani kwenye kijiji cha Jibondo.

**264.** ***Mheshimiwa Spika*,** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia MPRU itaendelea kusimamia, kulinda na kuhifadhi rasilimali zilizomo katika maeneo tengefu kwa kufanya doria zenye siku kazi 1,200; kutangaza vivutio vya utalii vilivyomo katika maeneo ya hifadhi; kushirikisha jamii na wadau katika usimamizi wa raslimali za bahari; kukamilisha taratibu za kutangaza maeneo ya visiwa vya Ukuza, Nyuni na Simaya kuwa Maeneo Tengefu; kuperemba na kufuatilia raslimali za bahari na kupanua shughuli za usimamizi wa rasilimali za uvuvi na uhifadhi hadi kwenye maeneo ya maji baridi kama maziwa, mito na maeneo oevu.

### *3.29 Kuimarisha Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi*

**265.** ***Mheshimiwa Spika,*** Katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kuimarisha vituo **25** vya Usimamizi wa

Railimali za Uvuvi kwa kuvipatia vitendea kazi na kufanya ukarabati wa miundombinu katika vituo vya Kasanga (Rukwa), Buhingu (Kigoma), Mbambabay (Ruvuma) Kipili (Rukwa) ili kuviwezesha kuendesha oparesheni za kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu na utoroshaji wa mazao ya uvuvi katika maeneo ya mipakani. Vilevile, Wizara imeanzisha vituo viwili vya Geita na Mbeya kwa kupeleka watumishi na kuvipatia vitendea kazi. Aidha, vituo hivyo kwa kushirikiana na wadau wengine wa Sekta ya Uvuvi wakiwemo Ofisi ya Rais TAMISEMI na Wizara ya Mambo ya Ndani, imeendesha doria za kawaida zenye siku kazi 6,118 katika maeneo ya maji makubwa ya Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Ziwa Nyasa na Ukanda wa Bahari ya Hindi. Operesheni hizo zimewezesha kukamatwa kwa zana haramu zikiwemo kokoro 695, kamba za kokoro mita 100,920, nyavu ndogo za makila 6,592, nyavu ndogo za dagaa chini ya mm 8, 5,145, nyavu za utali 3,865, vyandarua 10, mitungi ya gesi 74, baruti 59, *detonators* 105, *compressors* 3, kilo 41 za Urea, regulators 9, jozi 44 za viatu vya kuogelea, na boti 232. Pia, kilo 16,478 za sangara wachanga, kilo 16,557 za dagaa, kilo 140 za kaa, kilo 9 za majongoo bahari, na makombe 104. Kutokana na uhalifu huo jumla ya watuhumiwa 241 walikamatwa, kesi 21 zimefunguliwa mahakamani, nyavu haramu ziliteketezwa kwa moto kwa amri ya mahakama na samaki waligawiwa kwa wananchi na Taasisi za Serikali ikiwemo Magereza, Shule na Vituo vya Watoto Yatima.

**266.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika udhibiti wa uingizaji na matumizi ya nyavu haramu za uvuvi nchini, Wizara imeweka utaratibu kwa wafanyabishara wa nyavu kupata vibali vya kuagiza nyavu kabla ya kuagiza akieleza aina ya nyavu, ukubwa wa macho, na idadi. Aidha, mzigo husika hufanyiwa ukaguzi wa kuhakiki usahihi wa taarifa na uhalali wa zana hizo. Aidha, kaguzi za kuhakiki uingizaji wa vyavu za uvuvi hufanyika kwenye bandari, maghala, na maduka na viwanda vinavyotengeneza nyavu za uvuvi.

**267.** ***Mheshimiwa Spika*,** Wizara kupitia Mradi wa Udhibiti wa Uvuvi na Maendeleo Shirikishi Kusini Magharibi

mwa Bahari ya Hindi "South West Indian Ocean Fisheries Governance and Shared Growth – SWIOFish" iliwezesha Kikosi Kazi cha Kushughulikia Uhalifu wa Kimazingira ikiwemo uvuvi wa mabomu (Multi - Agency Task Team - MATT) kinachoundwa na wajumbe kutoka Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara za: Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Mambo ya Ndani; Ulinzi na Jeshi la Kujenda Taifa, Katiba na Sheria; Maliasili na Utalii; Nishati na Madini; pamoja na Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na Mwanasheria Mkuu wa Serikali kufanya doria katika mikoa ya Dar es Salaam na Mtwara iliyowezesha kukamatwa kwa vifaa vinavyotumika katika utengenezaji wa milipuko ya kienyeji ya *tambi (detonators)* 45, milipuko *V-6* 735 , mitungi ya gesi 21 , regulator 4 , *fuses* 55, kilo 273 za mbolea , *scoop nets* 14, injini 3, boti 10 na miwani ya kuzamia 10. Idadi ya watuhumiwa waliokamatwa ni 21 na kesi 2 zinaendelea mahakamani.

**268.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Kikosi Kazi cha Kushughulikia Uharibifu wa Mazingira (Multi Agency Task Team - MATT) iliendelea kutekeleza mkakati wa kutokomeza uvuvi wa baruti katika maeneo ya Ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi kwa kufuatilia vyanzo vya vilipuzi hususan katika maeneo ya machimbo na sehemu za Hifadhi za milipuko. Katika kutekeleza mkakati huo, wachimbaji wa madini na wahifadhi wa milipuko 110 katika machimbo ya Mererani, Arusha walihamasishwa namna ya kushughulikia na kuisimamia milipuko. Aidha, Wizara ilishiriki kikao cha Mawaziri kilichoandaliwa na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira kuhusu hatua za kupambana na Uvuvi haramu wa kutumia milipuko Bahari ya Hindi na kukubaliana kubuni mbinu na kuweka mikakati na mipango ya muda mfupi na muda mrefu ikiwemo kuliomba Jeshi la Wananchi wa Tanzania kufanya operesheni maalum ya kuwasaka na kuwakamata wavuvi haramu kwa lengo la kukabiliana na changamoto zinazosababishwa na uvuvi huo.

**269.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itaimarisha vituo vya Ulinzi wa Rasilimali za Uvuvi na kufanya doria zenye Siku kazi 6,000 ili kudhibiti uvuvi na biashara haramu katika maeneo ya maji baridi, Maji ya Kitaifa

na maeneo ya mipakani. Aidha, kuwezesha Kikundi Kazi cha kudhibiti Uvuvi haramu na uharibifu wa mazingira kutekeleza kazi zake kwa kufanya operesheni 12 kwa mwaka.

### *3.30 Kusimamia Ubora na Usalama wa Mazao ya Uvuvi*

**270.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia ubora, usalama na viwango vya samaki na mazao yake ili kulinda soko la ndani na nje ya nchi pamoja na afya ya mlaji kwa kufanya kaguzi. Aidha, kaguzi 3,930 za kuhakiki ubora, usalama na viwango vya samaki na mazao ya uvuvi katika viwanda (3,049) vya uchakataji, mialo (87) ya kupokelea samaki, maboti (43) na magari (129) ya kusafirisha samaki na mazao ya uvuvi, masoko (134) ya kuuzia samaki na maghala (491) ya kuhifadhi samaki. Ukaguzi huo umewezesha kutoa Hati ya Afya ya kusafirisha nje ya nchi tani 39,720.05 za samaki na mazao ya uvuvi. Pia, kaguzi za kina 129 zilifanyika kwenye viwanda na maghala ambapo jumla ya tani 63,122.37 za samaki zilihakikiwa na kuruhusiwa kuingizwa katika soko la ndani. Vilevile, Wizara ilifanya uchunguzi wa kimaabara kwa sampuli 1,713 za samaki, mazao ya uvuvi, udongo na maji ili kubaini uwepo wa mabaki ya viuatilifu, madini tembo na uwepo wa vimelea katika Maabara ya Uvuvi Nyegezi (Mwanza), Shirika la Viwango la Afrika Kusini na *Intertek (India*).

**271.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara imekarabati vituo vitatu (3) vya uthibiti wa ubora wa mazao ya uvuvi vya Kasanga na Kipili (Rukwa) na Geita. Vituo hivyo vimekarabatiwa ili kuwezesha kutoa huduma za ukaguzi wa ubora na usalama wa mazao ya uvuvi. Pia, Wizara imeendelea kuimarisha Maabara ya Uvuvi Nyegezi ambapo Sehemu ya uchunguzi wa Kemikali imekidhi vigezo na kukubaliwa kupata ithibati kupitia Bodi ya Taasisi ya Ithibati ya SADC ya *Southern Africa Development Community Accredation Services* (SADCAS). Aidha, Wizara imeendelea kujenga uwezo kwa watumishi ili kuboresha utendaji hususan katika kusimamia na kufanya chunguzi za kimaabara ambapo watumishi 13 wamenufaika na mafunzo hayo. Pia,

miundombinu ya Maabara ya Uvuvi Nyegezi na Maabara ya kutambua sumu kwenye mwani (*Harmful Algal Blooms* -HABs) ya Dar es Salaam zimeimarishwa kwa kufanyiwa matengenezo ya vifaa na kupatiwa vitendea kazi vipya.

**272.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itafanya yafuatayo:-

(i) Kuimarisha vituo vya Ubora na Uthibiti wa Mazao ya Uvuvi na kufanya kaguzi 7,200 za ubora wa samaki na mazao yake wakati wa kusafirisha nje ya nchi, na kaguzi 120 za kina kwenye viwanda vinavyochakata samaki na maghala ya kuhifadhi mazao ya uvuvi;

(ii) Kuimarisha Maabara za uvuvi – Nyegezi na HABs ya Dar es Salaam kwa kuzipatia vitendea kazi na mafunzo kwa watalaam ili kuwezesha kufanya chunguzi za kimaabara kwa sampuli 4,800 za minofu ya samaki, maji, udongo, masalia ya madawa ya mimea, asidi, alikali na madini tembo; na

(iii) Kufanya tathmini katika maeneo ya vijijini 10 vya Mahehe na Katembe (Kagera) Kibuyi, Busekela na Kisonya (Mara), Kayenze na Bukima (Mwanza), Chifunfu, Kijiweni na Nyamikoma (Sengerema) ili kutambua changamoto za masoko ya mazao ya uvuvi, usalama na miundombinu iliyopo.

### *3.31 Utafiti, Mafunzo na Ugani wa Uvuvi*

#### Utafiti wa Uvuvi

**273.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kuimarisha Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI) kwa lengo la kuendeleza sekta ya Uvuvi. Taasisi imeendelea kufanya utafiti na kuishauri Serikali na wadau wa uvuvi kuhusu hali ya rasilimali za uvuvi na jinsi ya kuzihifadhi na kuzivuna kwa uendelevu. Ushauri huo umetolewa kupitia tafiti mbalimbali, ikiwemo tathmini ya uwingi wa samaki (*Hydro-acoustic survey*) katika Ziwa Victoria ambapo

matokeo yanaonyesha samaki aina ya Sangara waliongezeka kutoka tani 471,634 mwaka 2011 hadi kufikia tani 651,353 mwaka 2014, na kupungua hadi tani 621,253 mwaka 2015. Tathmini nyingine ya uwingi wa samaki katika ziwa hili imefanyika mwishoni mwa mwaka 2016 kwa kushirikiana na nchi za Uganda na Kenya ambapo takwimu zimeshafanyiwa uchambuzi na ripoti inaendelea kuandaliwa kwa kila nchi husika. Aidha Sensa ya Uvuvi (*Frame Survey*) ilifanyika mwezi Septemba 2016 katika Ziwa Victoria ikihusisha nchi zote tatu (Tanzania, Uganda na Kenya) ambapo ripoti ya awali ilijadiliwa na wadau wa nchi husika. Watafiti wa nchi zote tatu wanatarajia kukutana kabla ya mwezi Juni 2017 ili kutoa ripoti ya pamoja itakayoonyesha matokeo ya sensa hiyo ya uvuvi.

**274.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, TAFIRI ilifanya utafiti wa uhifadhi wa mazingira kwa lengo la kupunguza upotevu wa misitu na kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi katika vijiji vilivyo katika mwambao wa Ziwa Tanganyika. Kazi iliyofanyika ni kusambaza teknolojia ya ubanikaji mzuri wa samaki na kusambaza majiko sanifu ya kubanikia samaki kwa vikundi vya BMU, wachakataji wa samaki na jamii zinazohusika na uvuvi. Majiko hayo yanatumia mjumuiko wa nishati jua na kuni katika kubanika samaki. Jumla ya wadau 36 kutoka Wilaya za pembezoni mwa ziwa wameshapata mafunzo ya juu ya ubanikaji huo wa samaki na jinsi ya kutumia majiko hayo. Hadi sasa, majiko 45 yamesambazwa katika vijiji/mialo ya Kiziba (4), Mwamgongo (5), Kibirizi (2), Katonga (1) katika Wilaya ya Kigoma Vijijini; Muyobozi (4), Karago (3), Sigunga (3) Herembe (3) katika Wilaya ya Uvinza, Kigoma; Ikola (4) katika Wilaya ya Tanganyika, Katavi; na Karungu (3), Namansi (3), Mkiringa-Ninde (3), Msamba (3), Wampembe (2) na Mpasa (2) katika Wilaya ya Nkasi, Katavi. Majiko mengine 55 yanaandaliwa ili kukamilisha usambazaji katika maeneo yaliyosalia. Teknolojia hii itasaidia kupunguza uharibifu wa mazingira utokanao na ukataji wa kuni, ongezeko la hewa ukaa kutoka katika kuni zilizochomwa, na itasaidia kupunguza uharibifu wa samaki baada ya mavuno (post harvest loss) ambalo ni tatizo kubwa linalopunguza mazao ya uvuvi kabla hayajamfikia mlaji ama

kufika sokoni na hivyo kuathiri kipato cha wavuvi na wachuuzi.

**275.** ***Mheshimiwa Spika,*** TAFIRI imeendelea na utafiti kupitia Mradi wa teknolojia ya ukaushaji wa dagaa wa Ziwa Nyasa kwa kutumia chombo kinachotumia mionzi ya jua (*Solar Dryer*). Tafiti ilifanyika ya kupunguza upotevu wa mazao ya uvuvi (*post harvest loss*) katika samaki wa Ziwa Nyasa ambao hupotea kwa kiasi kinachofikia 30% wakati wa jua na kinazidi na kufikia kati ya 40% - 50% wakati wa mvua, ambapo majiko ya Sola (*solar dryier*) yalifanyiwa tathimini na kuonesha yanakausha samaki vizuri wakati wa jua na hata kipindi cha mvua na kupunguza upotevu kuwa asilimia 0% wakati wa jua na chini ya asilimia 5% wakati wa mvua. Majiko nane (8) yamesambazwa kwa vikundi vya wavuvi katika mwalo wa Matema kuendelea kuyatumia wakati utafiti zaidi ukifanyika ili yaweze kusambazwa kwa jamii za wavuvi katika ziwa hilo. Mialo mingine 7 (Mbamba bay, Liuli, Manda, Mkili, Lupingu, Kafyofyo na Njambe) itapatiwa jumla ya majiko 10 kwa kila mwalo kwa ajili ya utafiti huo. Aidha, utafiti katika Ziwa Nyasa kuangalia jinsi minyoo ya dagaa (*Ligula intesinalis*) inavyoathiri uvuvi wa dagaa inaendelea kwa kuangalia fiziolojia (*physiology*) ya dagaa inavyoathiriwa na minyoo hao. Tafiti hii inafuatia ile iliyoonyesha ya kuwa minyoo wana athari kubwa kwa dagaa wa jinsia zote kwa kuathiri viungo vya uzazi.

**276.** ***Mheshimiwa Spika,*** TAFIRI kwa kushirikiana na wadau wengine imeendelea na tafiti katika maziwa madogo na mito katika mabonde ya Tanzania kwa lengo la kutambua samaki waliopo na wanaofaa kufugwa katika Bwawa la Mtera, Mto Ruaha, Bonde la Ziwa Victoria na Bonde la Malagarasi. Matokeo ya tafiti hizi zitasaidia kujua aina ya samaki waliopo na wanaofaa kufugwa katika bonde husika na kuondoa changamoto ya kuingiza samaki kutoka bonde moja kwenda lingine. Tafiti hizi zitakapohitimishwa zitasaidia kuainisha samaki mbalimbali walioko katika mabonde 11 (Pangani, Wami, Ruvu, Rufiji, Ruvuma, Ziwa Nyasa, Ziwa Rukwa, Ziwa Victoria, Ziwa Tanganyika, Malagarasi na Ukanda wa Pwani) ndani ya Tanzania na kutambua wale

ambao wafaao kwa ufugaji. Matokeo ya awali ya tafiti hizo yamewezesha kutambuliwa samaki wapya wapatikanao katika mabonde hayo tu walio katika jamii ya perege (*tilapines*) na furu (*haplochromines*). Vilevile, tafiti zinaendelea katika maziwa tisa (9) ya Volkano yaliyo katika Wilaya ya Rungwe ambayo yana furu wa aina yake ambao hawapatikani popote ulimwenguni na ambapo utaratibu wa kuwapatia majina bado unaendelea. Pia maeneo ya maziwa haya yameainishwa kuwa yanafaa kwa utalii wa mazingira (*eco-tourism*), utunzaji wa mazingira, tafiti na elimu.

**277.** ***Mheshimiwa Spika,*** TAFIRI iliendelea na Utafiti mkoani Tanga kuangalia mabadiliko ya tabianchi baharini yanavyoathiri uzalishaji wa kibaolojia (*biological productivity*) na uvuvi. Takwimu za samaki wadogo elezi (*small pelagic fish*) na mazingira zimeanza kuchukuliwa kutoka mwezi Augosti, 2016 na zitaendelea kuchukuliwa kwa muda wa miaka miwili. Utafiti huu utasaidia kujua madhara yanayojitokeza kutokana na mabadiliko ya tabianchi na hivyo kuwa na mikakati endelevu ya kukabiliana na madhara hayo.

**278.** ***Mheshimiwa Spika,*** TAFIRI imeendelea kufanya tafiti kwa kushirikiana na wafugaji wa samaki wa Mikoa ya Morogoro, Mwanza, Mara, Kagera, Simiyu, Arusha, Iringa, Ruvuma, Mbeya, Pwani na Dar es Salaam ili kuboresha ufugaji wao uwe wa tija. Tafiti hizo zililenga utengenezaji wa vyakula bora vya samaki kwa kutumia malighafi zipatikanazo karibu na wafugaji, uzalishaji mbegu (vifaranga) bora za samaki na ufugaji wa mfumo wa mseto unaojumuisha samaki, kilimo cha mbogamboga na kuku. Vilevile, TAFIRI imeendelea na uzalishaji wa mbegu bora za samaki kwa kushirikiana na wafugaji wa samaki. Wafugaji 15 wa samaki wa kikundi cha Nyasoro, Rorya wamepewa mafunzo ya uzalishaji vifaranga vya Kambale baada ya kujengewa kitotolishi (*hatchery*) cha samaki na TAFIRI chini ya ufadhili wa COSTECH. Aidha, mafunzo haya yamewasaidia wana kikundi kuzalisha mbegu bora za kambale na pia kuzalisha kambale watakaotumika kama chambo kwa wavuvi wa sangara.

**279.** ***Mheshimiwa Spika,*** TAFIRI inaendelea na utafiti wa ufugaji katika vizimba (cage culture) katika Maziwa Makuu ya Nyasa, Tanganyika na katika Bahari ya Hindi. Ufugaji katika vizimba katika Maziwa Makuu ya Nyasa na Tanganyika unahusisha samaki asili wapatikanao katika maziwa hayo, ambao ni *Oreochromis shiranus* (Nyasa) na *Oreochromis tanganicae* (Tanganyika). Utafiti huu utasaidia kuainisha maeneo na aina ya ufugaji stahiki wa vizimba katika Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika. Pia utafiti wa ufugaji mseto wa mwani na samaki kwa kutumia vizimba katika Bahari ya Hindi, eneo la Mbweni JKT, Dar es Salaam unaendelea ambapo utafiti huu utakapokamilika wakulima wa mwani watapatiwa teknolojia ya ukulima na ufugaji wa kisasa kwa kutumia vizimba.

**280.** ***Mheshimiwa Spika,*** TAFIRI imeendelea kutekeleza Mradi wa vivutia samaki (Fish Aggregating Devices – FADs) kwenye maji mafupi (mita 20 - 60) ya Bahari ya Hindi. Aidha, mradi wa kuangalia maeneo yenye samaki wengi (*potential fishing zones*) baharini kwa kutumia picha za kwenye Setilaiti unaendelea, ambapo matokeo ya awali yanaonesha kuwa maeneo yenye viashiria vya samaki yamekubaliana na takwimu za wavuvi waliovua katika maeneo hayo. Mradi huu utakapokamilika utawawezesha wavuvi katika Bahari ya Hindi kupata taarifa ya maeneo wanayoweza kwenda kuvua kutokana na uwepo wa samaki wengi.

**281.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, TAFIRI iliwezesha watumishi 23 kuendelea na mafunzo katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu (17), Uzamili (5) na ya kwanza (1) kwa ufadhili wa COSTECH na wafadhili wa nje. Aidha, watumishi 31 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi katika fani mbalimbali ndani na nje ya nchi.

**282.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, TAFIRI kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea na tafiti za samaki na mazingira katika maziwa makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa), maziwa ya kati (Rukwa, Kitangiri na Eyasi), maziwa madogo, mabwawa, mito na Bahari ya Hindi;

kufanya tathmini ya uwingi wa kamba miti, samaki elezi na jodari na pweza chini ya ufadhili wa Mradi wa SWIOFish. Aidha, itafanya tafiti za ufugaji samaki na upatikanaji wa mbegu na vyakula bora vya samaki na teknolojia bora ya ufugaji katika maeneo tofauti. Pia, itaendelea kufanya tafiti za kupunguza upotevu wa mazao ya samaki baada ya uvunaji; kuimarisha miundombinu ya Taasisi kwa kujenga ofisi na maabara ya kituo cha Dar es Salaam na Sota, kukarabati na kununua vitendea kazi vya kitafiti pamoja na vifaa vya maabara kwa vituo vyake vinne vya Dar es Salaam, Mwanza, Kigoma na Kyela. Vilevile, itaimarisha kituo kidogo cha Sota (Rorya) na Makao Makuu na kueendelea kusambaza taarifa za kitafiti kwa wadau mbalimbali wa uvuvi.

### *Mafunzo ya Uvuvi*

**283.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kuimarisha Wakala wa Elimu na Mafunzo ya Uvuvi (FETA) katika vituo vya Mbegani (Bagamoyo), Nyegezi (Mwanza), Mwanza South (Mwanza), Kibirizi (Kigoma), Mikindani (Mtwara) na Gabimori (Rorya). Wakala umedahili wanachuo 1,196 kwa Kozi za Stashahada na Astashahada. Aidha udahili umepungua ikilinganishwa na mwaka 2015/2016 ambapo jumla ya wanachuo 1,205 walidahiliwa. Upungufu huu umetokana na kuwepo kwa mfumo mmoja wa udahili wa pamoja (*Central Admission System-CAS*) unaoratibiwa na NACTE ambapo wadahiliwa wengi hawajawa na uelewa wa mfumo huo, hivyo baadhi kushindwa kujisajili. Aidha, FETA imetoa mafunzo ya muda mfupi kwa wavuvi na wafugaji samaki 2,286. Vilevile, Wakala imendelea kushirikiana na Taasisi za Kitaifa (SUMATRA na NACTE) na Kimataifa kama vile World Wide Fund (WWF), Food and Agriculture Organization of United Nation (FAO), Belgium Technical Cooperation (BTC) na Japanese International Cooperational Agency (JICA). Katika mwaka 2016/2017, Mashirikiano hayo, yaliwezesha Wakala kutoa mafunzo kwa maafisa uvuvi 55 kutoka Somalia na Angola.

**284.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wakala imefanya kazi ya kuweka vivutio vya samaki (*Fish Aggregating Devices-FADs*)

katika kingo za mwishoni mwa bahari ya ndani (*Teritorial Waters*). Kazi hii inalenga kuwa na sehemu rejea (*reference points*) ambazo zitavutia samaki wanaopita mbali katika ukanda wa bahari kuu, ili waweze kusogea maeneo ya karibu ambayo wavuvi wetu wadogo wanaweza kuyafikia. Vilevile, Wakala imeandaa mafunzo mahsusi ya uvuvi yanayolenga uvunaji wa rasilimali zilizoko katika Bahari Kuu. Aidha, Wakala imeanzisha mafunzo maalumu ya usalama kwa waendesha boti ndogo (chini ya mita 15) zenye ithibati ya SUMATRA ili kupunguza ajali zinazotokea baharini, kwenye maziwa na mito.

**285.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara imepanga kuendelea kuimarisha vituo vya Wakala vilivyoko Mbegani (Bagamoyo), Nyegezi (Mwanza), Mwanza South (Mwanza), Kibirizi (Kigoma), Mikindani (Mtwara), na Gabimori (Rorya) kwa kuviongezea vifaa vya kufundishia na kujifunzia pamoja na kuongeza idadi ya wakufunzi. Aidha, katika kujenga uwezo wake wa kitaasisi na raslimali watu, Wakala itaendelea kushirikiana na Taasisi za Kitaifa (SUMATRA na NACTE) na Kimataifa (WWF, FAO, BTC na JICA). Wakala imepanga kuendeleza mahusiano hayo ya kimkakati ili kujiongezea ujuzi na uwezo wa kutoa elimu na mafunzo ya uvuvi kwa ubora na tija. Aidha Wakala itaendelea kushirikiana na NACTE ili kuwezesha kueleweka kwa mfumo wa usajili wa kimtandao (CAS) kwa wanaoomba kujiunga na vyuo vya FETA.

***Huduma za Ugani wa Uvuvi***

**286.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara imeshiriki katika maonesho ya Nanenane Mkoa wa Dodoma na Lindi ambapo jumla ya wadau 409 wa uvuvi walishiriki na 205 walipatiwa elimu ya uendelezaji wa rasilimali za uvuvi na ufugaji bora wa samaki. Aidha, maonesho ya Siku ya Mvuvi Duniani (Mvuvi Day) yalifanyika Mkoa wa Dar es Salaam katika Soko la Kimataifa la Samaki la Magogoni Feri ambapo jumla ya washiriki 53 wakijumuisha wavuvi, wachakataji samaki, wafugaji samaki, viwanda vya samaki, watengenezaji bidhaa mbalimbali za samaki na Mashirika

yasiyo ya Kiserikali walishiriki. Jumla ya wadau 1,459 walitembelea mabanda na kupewa elimu mbali mbali inayohusiana na Sekta ya Uvuvi.

**287.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, mahitaji ya wagani kwa Sekta ya uvuvi ni wagani 16,000 ikilinganishwa na wagani 750 waliopo ambapo ni pumgufu ya wagani 15,250 kati ya wanaohitajika. Katika kusambaza teknolojia mbalimbali za uvuvi, Wizara iliandaa vipindi kumi na mbili (12), vinane (8) kati ya hivyo vilirushwa na TBC Taifa, na vinne (4) vilirushwa na Wapo Radio. Aidha, vipindi vinne (4) na Makala moja (1) za luninga viliandaliwa na kurushwa na TBC 1. Vipindi vya radio na luninga vilihusu ulinzi wa rasilimali za uvuvi, ufugaji bora wa samaki (upandikizaji na ulishaji wa samaki), kilimo cha mwani na uzalishaji wa Chaza wa lulu.

**288.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, machapisho mbalimbali ya kutoa elimu ya ugani yalichapishwa na kugawanywa kwa wadau wa sekta ya uvuvi yakiwemo nakala 250 za mwongozo wa ugani katika Sekta ya uvuvi, vijitabu 350, vipeperushi 2,650 na mabango 300. Machapisho haya yaligawanywa wakati wa Maonesho ya Nanenane, Maadhimisho ya Siku ya Mvuvi Duniani na wale waliotembelea ofisi za ugani kwa ushauri. Aidha, ushauri ulitolewa kwa wafugaji wa samaki 15,000 wenye mabwawa 7,672 kati ya mabwawa 22,702 yaliyopo walipata elimu juu ya ulishaji samaki, utunzaji bora wa mabwawa na usalama wa mazingira ya ufugaji samaki na udhibiti wa magonjwa.

**289.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itaandaa na kurusha hewani vipindi 30 vya radio na 10 (vya kaiwaida 7 na Makala 3) vya luninga juu ya ufugaji bora wa samaki, matumizi ya teknolojia sahihi za uzalishaji wa samaki, utunzaji wa rasilimali za uvuvi na uendelezaji wa sekta ya uvuvi. Pia, Wizara itahamasisha na kujenga uelewa kwa wadau 100 wa uvuvi kujikita katika uanzishwaji wa shughuli mbadala ili kupunguza nguvu ya uvuvi (fishing pressure) katika maji ya asili. Aidha, Wizara itaendelea kushauriana na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili zitenga nafasi

na kuomba kibali cha kuajiri maafisa ugani ili kupunguza pengo la mahitaji ya wagani katika Sekta ya Uvuvi.

### *3.32 Uwekezaji kwenye Sekta ya Uvuvi*

**290.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara imeendelea kuhamasisha sekta binafsi iwekeze katika viwanda ambapo Cold Storage Facilities 4 katika maeneo ya Kigamboni (2), Kinondoni (1) na Temeke (1) zimejengwa kwa ajili ya kuhifadh samaki na mazao ya uvuvi. Aidha, Mtaalamu Mwelekezi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa Ujenzi wa Bandari ya uvuvi ambapo kampuni ya M/s Royal Haskoning DHV – Netherlands ilishinda zabuni.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kuhamasisha sekta binafsi kuwekeza katika sekta ya uvuvi hususani ujenzi wa viwanda 3 vya kuchakata samaki aina ya jodari kwenye ukanda wa pwani wa Bahari ya Hindi, ununuzi wa meli za kufanya uvuvi katika bahari kuu ya Tanzania na ujenzi wa maeneo ya kuhifadhia samaki na mazao yake. Vilevile, Wizara itaanza utekelezaji wa Pogramu ya Kuendeleleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (Agricultural Sector Development Programme –ASDP 2).

### *3.33* Tozo za leseni katika Sekta Kuu ya Uvuvi

**291.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara imefanya mapitio ya tozo/kodi na ada mbalimbali katika sekta ya uvuvi zinazotozwa na Wizara na Taasisi chini ya Wizara na kubaini baadhi ya kodi, tozo na ada hizo ni kero kwa wavuvi na maendeleo ya sekta ya uvuvi kwa ujumla. Hivyo, katika mwaka 2017/2018, Serikali itafuta kodi, tozo na ada tano (5) ambazo ni kero kwa wavuvi, wafugaji viumbe kwenye maji na wawekezaji; na kubakiza zile tu zenye uhusiano wa moja kwa moja katika uendelezaji wa sekta ya uvuvi. **(Kiambatisho Na.12)**

### *3.34 Masuala ya Mtambuka ya Mifugo na Uvuvi Utawala Bora, Jinsia na UKIMWI*

**292.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017 Wizara iliendelea kuwahamasisha watumishi 557 kupima afya

zao kwa hiari na watumishi wanne (4) wanaoishi na VVU wanaendelea kupatiwa huduma ya chakula na lishe. Aidha, Wizara iliwaelimisha watumishi 583 kuhusu maadili, haki na wajibu katika Utumishi wa Umma na watumishi 51 wamewezeshwa kuhudhuria mafunzo ya kitaaluma ambapo kati ya hao 30 ni mafunzo ya muda mrefu na 21 muda mfupi. Vilevile, katika kutekeleza Agizo la Serikali lililotolewa mwezi Julai, 2016 la kuhamishia Makao Makuu Dodoma, Wizara iliwawezesha watumishi 128 kuhamia Dodoma.

**293.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/2017, Wizara ilifanya uhakiki wa watumishi 1,171 pamoja na taarifa zao za kiutumishi na ajira mpya za watumishi 40 zilishughulikiwa. Vilevile, Wizara ilifanya zoezi la uchambuzi wa kazi ili kubaini mahitaji halisi ya watumishi ambayo ni 1,978 ikilinganishwa na idadi ya watumishi 1,211 waliopo. Kwa hiyo, pungufu ni watumishi 767. Taarifa za vyeti vya elimu ya kidato cha nne na sita za watumishi 830 ziliwasilishwa Baraza la Mitihani la Tanzania kwa ajili ya uhakiki na zoezi hili linaendelea. Aidha, Muundo wa Wizara na taasisi zake ulifanyiwa mapitio na kuwasilishwa kwa Mamlaka husika.

**294.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kutekeleza Mkakati wa Kuzuia na Kuziba Mianya ya Rushwa na kuhimiza watumishi kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya kazi katika Utumishi wa Umma. Aidha, Wizara itasimamia utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja; kuimarisha Dawati la Jinsia; kutoa mafunzo ya Mfumo wa Wazi wa Upimaji wa Utendaji Kazi (OPRAS) pamoja na kusimamia Mfumo Shirikishi wa Taarifa za Utumishi na Mishahara (HCMIS). Pia, Wizara itawahamisha watumishi 70 kwenda Makao Makuu ya Serikali; itaendelea kuhakiki watumishi; kuwezesha kufanyanyika vikao vya Baraza la Wafanyakazi na TUGHE. Vilevile, Wizara kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea kuwaelimisha watumishi wake kuhusu kupima afya zao kwa hiari na kuwapatia huduma ya chakula na lishe watumishi wanne (4) wanaoishi na VVU na kugua UKIMWI.

***Habari na Mawasiliano Serikalini***

**295.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara ilitangaza matukio na taarifa mbalimbali kuhusu sekta za Mifugo na Uvuvi kupitia vyombo vya habari, ambapo jumla ya Vipindi vitano (5) vya redio na kumi (10) vya luninga viliandaliwa na kurushwa. Aidha, mikutano nane (8) na waandishi wa habari, mikutano 12 ya sekta ya uvuvi, mikutano 25 ya Sekta ya Mifugo na mikutano sita (6) ya Wadau mbalimbali ilifanyika na kutangazwa. Mikutano ya kitaaluma ya Siku ya Vetenari, Siku ya Wanyama, Siku ya Kichaa cha Mbwa, Siku ya Chakula Duniani, Siku ya Mvuvi Duniani, wiki ya maziwa na maonesho ya Nane Nane Mkoani Lindi na Dodoma yalitangazwa. Vilevile, ziara 20 za Viongozi wa Wizara kuhusu uendelezaji wa Sekta za Mifugo na Uvuvi katika maeneo mbalimbali na mikutano iliyohusu utatuzi wa migogoro kati ya wakulima na wafugaji na watumiaji wengine wa ardhí ilitangazwa.

**296.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itaendelea kutekeleza mkakati wa mawasiliano kwa kuandaa na kurusha vipindi 15 vya Redio na 15 vya Luninga kuhusu maendeleo ya sekta za mifugo na uvuvi, kuandaa mikutano 12 na Waandishi wa Habari. Aidha, Wizara kupitia kitengo cha Habari itatayarisha na kuzirusha makala sita (6) za luninga kuhusu mafanikio mbalimbali katika sekta za mifugo na uvuvi na kutangaza ziara mbalimbali za viongozi wa kiwizara.

***Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)***

**297.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2016/2017, Wizara imejenga, kuimarisha na kusimamia mifumo ya TEHAMA iliyopo Wizarani ya kukusanya mapato/maduhuli ya serikali katika minada ya mifugo *Livestock Revenue Correction System* (LRCS), na sekta ya uvuvi *Fisheries Revenue Correction System* (FRCS), mfumo wa kufuatilia taarifa za magojwa ya milipuko yanayovuka mipaka *Transiboundary Animal Diseases Information* (TADINfo), mfumo wa utambuzi,

usajili na ufuatiliaji wa mifugo-*Tanzania National Livestock and Identification and Traceability System* (TANLITS), mfumo wa kukusanya na kutunza takwimu za samaki uitwao *Catch Assessment System* (CAS), mfumo wa taarifa za kimaabara SILAB *Labaratory Infomartion Management System* (SILAB- LIMS ) mfumo wa usajili wa wataalam na vituo vya kutoa huduma za mifugo *Livestock Facilities and Proffesional registration System* (LFPRS) chini ya VCT na Mfumo wa kutuza taarifa za mishahara na kumbukumbu za watumishi LAWSON na tovuti. Aidha, Wataalam watatu (3) wa Kitengo wameshiriki katika mikutano sita (6) ya kitaaluma ya TEHAMA. Pia, Wizara imeboresha mawasiliano ya mdahalisi (internet) na kutumia simu za mdahalisi.

**298.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara itajenga kanzidata ya taarifa za Bodi ya Maziwa, mfumo wa kielektroniki wa kukusanya maduhuli ya Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (LITA) na kuboresha mfumo wa kielektroniki wa kukusanya maduhuli ya uvuvi; vilevile wizara itasimika mifumo ya kielektroniki ya kukusanya maduhuli ya mifugo katika minada ya upili ya Kizota, Mhunze, Weruweru na Meserani. Aidha, Wizara itaendelea kujenga mfumo wa mawasiliano katika ofisi mpya za Wizara za Dodoma ili kurahisisha mawasiliano miongoni mwa ofisi za Wizara, taasisi na wadau pamoja na kuboresha tovuti ya Wizara ili kuwawezesha wadau kupata taarifa mbalimbali za sekta ya mifugo na uvuvi.

**FUNGU 24**

### 3.35 Kuimarisha Ushirika na Asasi za Wananchi katika Kilimo na Sekta Nyingine za Kiuchumi

**Kuhimiza misingi ya utawala bora na uwajibikaji katika vyama vya Ushirika**

***299. Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17, Wizara kupitia Tume, imesimamia chaguzi na kutoa mafunzo ya uendeshaji wa vyama kwa viongozi wapya wa bodi za vyama vya ushirika 116 na kutatua migogoro 13. Katika

mwaka 2017/2018, Tume itasimamia chaguzi na kutoa mafunzo ya kuimarisha utendaji na usimamizi kwa wajumbe wa bodi na watendaji kwa Vyama vya ushirika 6,000 nchini.

**300.** ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume imekagua na kuchunguza vyama vya ushirika 75 visivyo vya kifedha na 154 vya Akiba na Mikopo. Pia Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO) lilifanya ukaguzi wa nje kwa vyama vya ushirika 2,103. Kaguzi hizo zilibaini uwepo wa ubadhirifu kwenye baadhi ya vyama uliosababishwa na usimamizi na utendaji mbovu wa viongozi na watendaji. Kufuatia matokeo ya kaguzi hizo jumla ya bodi za vyama vya ushirika 214 ziliondolewa madarakani zikiwemo; AMCOS 197 za mikoa ya Mtwara (135), Lindi (55), Tabora (4), Katavi (2) na Manyara (1); SACCOS 14; Vyama Vikuu vya WETCU, SONAMCU, SIFACU na Shirikisho la Vyama vya Ushirika (TFC). Aidha, taratibu za kisheria dhidi ya watuhumiwa wa ubadhirifu zinaendelea kuchukuliwa ikiwemo kulipa fidia ya hasara waliyoisabisha ambapo tayari waliokuwa viongozi wa vyama vya ushirika vya Mazombe, Mpanda Kati, Ukonongo, Mbinga Kurugenzi na Mbinga Teachers wameandikiwa notisi za madai (*notice of surcharge*). Aidha watuhumiwa 17 kutoka SACCOS za Wazalendo (6), Rorya Teachers (6), JKT (5) wamefikishwa mahakamani baada ya kusajiliwa kwa Hati za Madai (*Certificate of Surcharge*) na kesi zao zinaendelea.

**301.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara kupitia Tume itaandaa na kusambaza miongozo miwili ya Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika nchini. Aidha itakagua na kusimamia utendaji kazi wa Vyama Vikuu vya Ushirika, Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo na Vyama vya ushirika visivyo vya kifedha.

**Kujenga na kuimarisha uwezo wa kiuchumi katika vyama vya ushirika**

**302.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/17, Wizara imeendelea kuhamasisha wananchi kujiunga na kuanzisha vyama vya ushirika katika sekta mbalimbali

ambapo vyama vya ushirika 101 vimeanzishwa vikiwemo ushirika wa akiba na mikopo (SACCOS) 51, Kilimo na Masoko (AMCOS) 21, madini 13, viwanda 1, ushirika wa wastaafu 1, huduma mbalimbali 2, mafundi 2, biashara 1, uvuvi 1 , usindikaji 1, umwagiliaji 1 na ufugaji 6. Hatua za usajili kwa vyama vikuu vya Uvuvi, zao la Alizeti na SACCOS ya kanda ya ziwa zinaendelea. Aidha, mwongozo wa uendeshaji wa majukwaa ya wadau wa ushirika na kamati za elimu ya ushirika za mikoa na wilaya umeandaliwa.

**303.** ***Mheshimiwa Spika,*** Tume kwa kushirikiana na Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) imetekeleza dhana ya kilimo cha mkataba kwa kununua mahindi kupitia vyama vya ushirika kwenye mikoa ya Iringa na Ruvuma kwa bei shindani ya Shilingi 530 kwa kilo. Vilevile, Tume imehakiki mali za Vyama Vikuu vya Ushirika 37, Miradi ya Ushirika ya pamoja 7 na benki 2 za ushirika.

**304.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2016/2017, Wizara kupitia Tume imefanya tathmini ya kubaini mahitaji ya mafunzo kwa vyama vya ushirika katika Mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Tabora, Tanga, Ruvuma na Mbeya. Tathmini hiyo imebaini kuwepo kwa uhitaji wa elimu ya usimamizi wa rasilimali za vyama, mbinu za kujenga mtaji wa ndani, uingiaji mikataba na dhana ya uwekezaji. Matokeo ya tathmini yamewezesha kufanyika kwa mafunzo kwa viongozi na watendaji 650 wa vyama vya ushirika vya msingi 258, miradi ya ushirika ya pamoja 6, benki za ushirika 2 na Shirikisho la vyama vya ushirika nchini. Aidha, mafunzo ya usimamizi na uendeshaji wa SACCOS za vijijini yametolewa kwa wakufunzi wawezeshaji (ToT) na Wakaguzi 95 ambao ni Maafisa Ushirika wa Mikoa na Wilaya.

**305.** ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara kwa kushirikiana na wizara za kisekta, mamlaka za serikali za mitaa na wadau itaendelea kuhamasisha ushirika kwa kuwezesha uundwaji wa majukwaa ya utoaji elimu ya ushirika katika mikoa 26, kufanya mikutano ya uhamasishaji katika vyuo 7 vya elimu ya juu nchini na kushiriki maonesho ya Kilimo (Nane nane), Siku ya Chakula Duniani, Siku ya

Ushirika Duniani na Maadhimisho ya Siku ya Ushirika wa Akiba na Mikopo Duniani. Aidha, Wizara itaendelea kuhamasisha vikundi vya wanawake na vijana kujiunga au kuanzisha ushirika. Vilevile, Wizara itasimamia na kutathmini mfumo wa stakabadhi ghalani na kilimo cha mkataba kwenye Vyama vya Ushirika wa mazao ya korosho, kahawa, pamba, alizeti na ufuta. Aidha itahamasisha uongezaji wa thamani kwa katika Vyama vya Ushirika nchini.

**306.** ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2017/2018, Tume itafanya tafiti 3 za mwenendo wa biashara ya vyama vya ushirika vya mazao ya pamba, kahawa na zabibu pamoja na kuandaa makongamano matatu (3) ya kuwasilisha na kujadiliana na wadau wa ushirika kuhusu matokeo ya tafiti hizo. Aidha, itaanzisha maktaba ndogo ya taarifa za ushirika sambamba na kuratibu na kufuatilia mafunzo yatolewayo na watoa huduma kwenye vyama vya ushirika nchini.

## 4.0 SHUKRANI

**307.** ***Mheshimiwa Spika,*** naomba nitumie nafasi hii kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia sana Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo. Kwanza napenda kuzishukuru nchi za Japan, Marekani, Uingereza, Ireland, Malaysia, China, Indonesia, Korea ya Kusini, India, Misri, Israel, Ubelgiji, Ujerumani, Finland, Norway, Brazil, Uholanzi, Vietnam na Poland. Nayashukuru pia Mashirika na Taasisi za Kimataifa zifuatazo: Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, AU, IFAD, DFID, UNDP, FAO, JICA, EU, UNICEF, WFP, CIMMYT, ICRISAT, ASARECA, USAID, KOICA, ICRAF, IITA, IRRI, ILRI, CABI, CFC, AVRDC, AGRA, CIP, UNEP, WARDA, ReSAKSS, Shirika la Kudhibiti Nzige wa Jangwani (DLCO-EA), Shirika la Kudhibiti Nzige Wekundu (IRLCO-CSA), *Bill and Melinda Gates Foundation, Gatsby Trust*, *Rockfeller Foundation, Aga Khan Foundation* na *Unilever*. Ushirikiano na misaada ya nchi na mashirika hayo bado tunauhitaji ili tuweze kuendeleza kilimo nchini.

**308.** ***Mheshimiwa Spika,*** napenda kutoa shukrani za pekee, kwa wakulima wa nchi hii kwa kazi kubwa wanayofanya katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara. Ninapenda kumshukuru Naibu Waziri wa Kilimo Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Wiliam Tate Ole Nasha, Mbunge wa Ngorongoro kwa ushirikiano alionipa katika utekelezaji wa kazi za ofisi. Aidha, ninapenda kuwashukuru Eng. Mathew John Mtigumwe, Katibu Mkuu - Kilimo, Dkt. Mary S.H. Mashingo, Katibu Mkuu - Mifugo na Dkt. Yohana L. Budeba, Katibu Mkuu - Uvuvi; Wakurugenzi wa Idara; Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara; Watumishi wote wa Wizara; na Wadau mbalimbali wa Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa juhudi, ushirikiano na ushauri wao uliowezesha kutekelezwa kwa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2016/2017 kama nilivyofafanua katika hotuba hii. Ni matarajio yangu kwamba, Wizara itaendelea kupata ushirikiano wao katika mwaka 2017/2018. Mwisho natoa shukrani kwa Mpigachapa Mkuu wa Serikali kwa kuchapisha Kitabu cha Hotuba ya Bajeti ya Mwaka 2017/2018.

## 5.0 MAOMBI YA FEDHA MWAKA 2017/2018

***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2017/2018, Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi kupitia **Fungu 43, Fungu 99, Fungu 64 na Fungu 24** inaomba jumla ya Shilingi **267,865,782,829** kama ifuatavyo:

### FUNGU 43

**309.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi **214,815,759,000** zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **64,562,759,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **150,253,000,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

### FUNGU 99

**310.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi **29,963,524,000** zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **25,963,524,000** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na Shilingi **4,000,000,000** ni fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

**FUNGU 64**

**311.** ***Mheshimiwa Spika,*** jumla ya Shilingi **16,792,645,829** zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **14,792,645,829** ni fedha za Matumizi ya Kawaida na Shilingi **2,000,000,000** ni fedha za kutekeleza Miradi ya Maendeleo.

***FUNGU 24***

**312.** ***Mheshimiwa Spika***, kiasi cha Shilingi **6,293,854,000** kinaombwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**313.** ***Mheshimiwa Spika,* naomba kutoa hoja.**

**NAIBU SPIKA:** Sasa nitamuita Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2016/2017, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka wa fedha 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na majukumu mengine jukumu la kushughulikia bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Vilevile Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 inataka Kamati kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha unaoisha. Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi inajumuisha mafungu manne ambayo ni Fungu 43, Fungu 64, Fungu 99 na Fungu 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa ushauri wa Kamati; kwanza uchambuzi wa masuala mbalimbali ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Sekta ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Ushirika Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo takribani kumi na tisa, kama yanavyoonekana kwenye Taarifa ya Kamati mliyopewa. Na ninaomba taarifa ya kitabu mlichopewa ndio kiingie kwenye *Hansard,* maana hii ni ufupi wa taarifa ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa ushauri uliotolewa na Kamati kwa kiasi kikubwa haujatekelezwa. Kamati haijaridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Wizara katika utekelezaji wa ushauri wa Kamati katika maeneo ya vipaumbele vya Wizara. Kwa mfano baadhi ya shughuli zilizoshindwa kutekelezwa kikamilifu ni pamoja na:-

(i) Kushindwa kupima maeneo ya kilimo na mifugo, hivyo kusababisha kuendelea kuwepo kwa migogoro ya wakulima na wafugaji.

(ii) Usambazaji wa pembejeo za kilimo kwa kuzingatia msimu wa kilimo wa eneo husika na mfumo unaofaa;

(iii) Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji;

(iv) Ujenzi na ukarabati wa maghala;

(v) Ukarabati wa majengo ya vituo vya utafiti na mafunzo, ukaguzi wa mazao, mimea na viuatilifu;

(vi) Ujenzi wa bandari ya uvuvi;

(vii) Kushindwa kulipa madeni ya wazabuni na wakandarasi;

(viii) Uwekezaji mdogo katika sekta za mifugo na uvuvi;

(ix) Udhibiti usiokidhi wa uvuvi haramu; na

(x) Kuendelea kuwepo kwa uhaba wa maafisa ugani wa kilimo, mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ni kuwa kwa uchambuzi uliofanywa na Kamati katika mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ulijikita katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge, kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumiwa hadi mwezi Mei, 2017 na eneo la ukusanywaji maduhuli kwa kulinganisha makadirio yaliyowekwa na kiasi kilichokusanywa hadi Mei , 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kwamba, kwa miaka miwili mfululizo, fedha zinazoidhinishwa na Bunge hazitolewi kama zilivyoidhinishwa na hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo yaliyopangwa, ikiwa ni pamoja na kutofanyiwa kazi ushauri wa Kamati katika maeneo mengi kama ilivyoelezwa hapo juu. Kwa mfano, katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kiasi cha fedha kilichotolewa ni kidogo ikilinganisha na fedha zilizotengwa na kuidhinishwa na Bunge, kama inavyooneshwa katika jedwali kwenye taarifa ya Kamati.

Kwa upande wa fedha za maendeleo, katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kumekuwa na ongezeko la kiasi cha jumla ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge, lakini kiasi cha asilimia kinachotolewa kimeshuka kikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2015/2016, kama inavyoonekana katika jedwali namba moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 43 linaonyesha kushuka kwa asilimia ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo kutoka asilimia 16 kwa mwaka wa fedha 2015/2016 hadi asilimia 3.3 kwa mwaka wa fedha 2016/2017. Na kwamba hakuna bajeti yeyote ya maendeleo iliyotengwa kwa Fungu 24, kwa miaka miwili mfululizo. Mwenendo huu wa kushuka kwa fedha zinazotolewa za Sekta ya Mifugo, Kilimo na Uvuvi, una athari kubwa katika ustawi wa pato la

wakulima na uchumi wa nchi kwa ujumla kwani asilimia 75 ya Watanzania wanajihusisha na shughuli za kilimo. Kamati inataka kufahamu kwa nini bajeti ya sekta hizi inaendelea kushuka wakati kilimo, mifugo na uvuvi ni chachu ya uchumi wa viwanda na hasa ukiangalia hela zinazotolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 98(1) inaitaka Kamati kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha unaoisha 2016/2017. Kamati haikuweza kutekeleza ipasavyo matakwa ya Kanuni hii ya 98(1) ambayo inaitaka kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha mwaka 2016/2017 kutokana na baadhi ya miradi ya sekta ya kilimo kutopelekewa fedha yeyote na kushindwa kutekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini mambo yafuatayo:-

(a) Mtiririko wa fedha usioridhisha umechangia kutofikiwa kwa malengo ya Wizara yaliyopangwa kutekelezwa katika mwaka huu katika programu mbalimbali za kuendeleza sekta ya kilimo, kama yalivyoelezwa katika kipengele 2.22.

(b) Mara nyingi fedha za nje zimekuwa zikitolewa zikiwa pungufu au kwa kuchelewa wakati fedha za ndani zinazotengwa kwa miradi ya maendeleo mara nyingi hazitolewi kabisa. Hali hii inaathiri kwa kiasi kikubwa ufanisi katika utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa. Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga na kutoa kwa wakati fedha za miradi ya maendeleo kutoka mapato ya ndani, kwani kutumia fedha za ndani kunadhihirisha utayari wa Serikali katika kujitegemea na kuwaletea wananchi wake maendeleo ya kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kutotolewa fedha za miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 kwa sekta ya kilimo, ililazimu Kamati ifanye kazi nyingine nje ya ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha 2016/2017. Kufuatia hali hiyo, Kamati

ilikagua miradi na shughuli zinazotekelezwa na Wizara ambazo zilitengewa na kupelekewa fedha katika bajeti za miaka ya nyuma katika sekta ya kilimo, lakini pia Kamati ilikagua shughuli za sekta binafsi katika maeneo ya mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mantiki ya Kamati kukagua nshughuli zinazotekelezwa na sekta binafsi kwenye masuala ya uvuvi na mifugo ilikuwa ni kujifunza namna sekta binafsi inavyoshiriki katika shughuli za kukuza uchumi kupitia kilimo, mifugo na uvuvi na changamoto wanazokutana nazo hatimae Kamati iweze kuishauri Serikali hatua za kuchukua ili kuiwezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika kuongeza pato la Taifa na kukuza ajira katika ziara hiyo, kama ilivyokagua. Nataka niseme kwamba sekta hii inaendeshwa zaidi na sekta binafsi kuliko Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, maeneo ambayo yamekaguliwa ni kama ifuatavyo; Ghala la Hifadhi ya Taifa la Chakula Mkoani Shinyanga, Kiwanda cha Uchakataji Samaki cha *Tanzania Fish Processors Limited,* Mwanza na Kiwanda cha Kusindika Nyama cha Kampuni ya Chobo, Mwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mpango wa bajeti na uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kamati ilipokea na kuchambua Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Taasisi zilizo chini yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Mpango ambao umeandaliwa kwa kuzingatia Sera na Mikakati ya Kitaifa na Kisekta katika kuandaa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018, ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2017/2018 na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Taifa 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, umuhimu wa Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018 unabainisha kuwa Tanzania

imeendelea kutegemea sekta ya kilimo katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi wake kwa kuwa kilimo kinatoa ajira kwa asilimia 75 ya Watanzania, kinachangia asilimia 100 ya chakula kinachopatikana nchini na kinatoa malighafi ya viwanda. Aidha, kutokana na asilimia kubwa ya wananchi kushiriki katika shughuli za kilimo, kilimo kinachangia kwa kiasi kikubwa katika kupunguza umaskini na kuongeza kipato na kinachangia pato la Taifa kwa asilimia 29 na malighafi ya viwanda. Na nikisema kilimo ni pamoja na mifugo na uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018; kabla ya kuanza kuchambua malengo ya bajeti kwa mwaka wa fedha 2017/2018 napenda kuipongeza Serikali kwa uamuzi wa kutenganisha utekelezaji wa shughuli za sekta ya mifugo na uvuvi ambapo kuanzia mwaka huu wa fedha sekta hizi mbili zitatekeleza shughuli zake kupitia mafungu mawili tofauti yaani Fungu 64 kwa ajili ya Uvuvi na Fungu 99 kwa ajili ya Mifugo. Hivyo uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi inajumuisha mafungu manne na mwaka jana ilikuwa mafungu matatu. Kwa ujumla kwa mwaka wa fedha 2017/2018, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Fungu 43, Fungu 64, Fungu 99 na Fungu 24 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 281,745,995,830. Aidha, Wizara kupitia mafungu yake kwa mwaka wa fedha 2017/2018 inatarajia kukusanya jumla ya maduhuli kiasi cha shilingi 40,122,381,551.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 43 - Sekta ya Kilimo; katika mwaka wa fedha ujao wa 2017/2018 Fungu 43 linaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 214,815,759,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 64,562,759,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 150,353,000,000 ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, Wizara kupitia Fungu 43 imepanga kukusanya jumla ya shilingi 4,017,010,000.

mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 64 - Sekta ya Uvuvi; katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara kupitia Fungu 64 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi 23,900,893,059. Kati ya fedha hizo, shilingi 15,900,893,059 ni kwa ajili ya matumizi

ya kawaida na shilingi 8,000,000,000 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, kwa upande wa maduhuli Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi 19,658,632,051.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 99 - Sekta ya Mifugo; katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara kupitia Fungu 99 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi 29,946,424,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 25,946,424,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 4,000,000,000 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, kwa upande wa maduhuli Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi 16,646,700,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika; katika mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara kupitia Fungu 24 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 10,474,758,000. Kati ya fedha hizo, shilingi 6,309,658,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 4,165,000,000 ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ya Tume ya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, malengo ya utekelezaji na vipaumbele. Fedha zinazoombwa kutekeleza malengo mbalimballi ya Wizara, kama yalivyoelezwa na mtoa hoja na kuainishwa kwenye Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya malengo kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018; Kamati imepitia, kuchambua na kutathimini malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti ya mwaka 2017/2018 na kuona bajeti imeongezeka kidogo. Hivyo, Kamati ina wasiwasi kuhusu uwezekano wa utekelezaji wa malengo hayo kutokana na mwenendo unaojidhihirisha kwa kiasi kidogo cha bajeti inayotengwa na kutolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na umuhimu wa sekta za kilimo kama unavyoelezewa kupitia Mipango, Sera na Mikakati mbalimbali ya Serikali, bado sekta hii imekuwa haipewi msukumo wa kutosha kama kipaumbele cha uhai wa Taifa na ustawi wa sekta zingine za uzalishaji na ustawi wa jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati katika uchambuzi wake imebaini na kuona bado bajeti ni ndogo na kuendelea kushuka kwa fedha zinazotolewa kwa ajili ya sekta ya kilimo kila mwaka. Kuendelea kutenga bajeti ndogo kwa ajili ya sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi kumesababisha uwezekezaji mdogo na hivyo kusababisha ukuaji mdogo wa sekta hii ambapo kwa mwaka wa fedha 2016/2017 ukuaji wa sekta ya kilimo ni asilimia 1.7 ikilinganishwa na sekta zingine kama madini ambayo ukuaji wake ni asilimia 16.6, uchukuzi 15, habari na mawasiliano asilimia 13.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba mwenendo huu wa uwekezaji mdogo kwenye sekta ya kilimo, unakinzana na dhana ya uchumi wa viwanda ambao malighafi ya viwanda kwa kiasi kikubwa yatatokana na bidhaa zinazotokana na kilimo, uvuvi na mifugo. Aidha, uwekezaji mdogo kilimo unaathiri pato na ustawi wa wananchi walio wengi ambao wanategemea kilimo kama njia kuu ya uzalishaji mali na kuongeza pato. Kamati inaitaka Serikali ilieleze Bunge kwanini Serikali haioni umuhimu wa kutekeleza kwa vitendo mkataba wa Azimio la Maputo na Malaba ambayo yanazitaka nchi wanachama kutenga asilimia 10 ya bajeti yote ya Serikali kwa ajili ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa makadirio ya mapato yanayotokana na maduhuli kwa mwaka wa fedha 2017/2018. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 Wizara kupitia Fungu 43, ilikadiria kukusanya jumla ya shilling bilioni nne kutoka vyanzo mbalimbali. Aidha, Sekta ya Mifugo na Uvuvi, Fungu 99 na Fungu 64 inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 36 kutoka vyanzo mbalimbali, ikilinganishwa na makadirio ya mwaka wa fedha unaopita ambapo Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya shilingi bilioni 35 na kufanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 26.9 sawa na asilimia 77 ya lengo la makusanyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio ya makusanyo katika mwaka wa fedha 2017/2018 kwa Fungu 43 hayajaongezeka. Aidha, kwa Fungu 64 na Fungu 99 kuna ongezeko la asilimia tatu ya makadirio ya mwaka wa fedha

2016/2017. Ongezeko hili ni kidogo sana ikilinganishwa na fursa zilizopo katika sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa makadirio ya fedha za miradi ya maendeleo; Kamati ilifanya uchambuzi na ulinganisho wa Bajeti ya Maendeleo iliyotengwa kwa miaka miwili (2016/2017 na 2017/2018) katika mafungu ya sekta ya kilimo. Katika uchambuzi wake, Kamati imebaini kuwa jumla ya fedha za maendeleo zilizotengwa kwa mafungu yote kwa mwaka 2017/2018 ni shilingi bilioni 182.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 117.4 zilizotengwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017, ikiwa ni ongezeko la asilimia 36. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani zikiwa ni asilimia 36 tu. Kwa mjumlisho wa mafungu, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya Fungu 64 ambalo ni Uvuvi ni shilingi bilioni nane wakati Fungu 68 ambalo ni Mifugo ni shilingi bilioni nne tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Sekta ya Mifugo na Uvuvi, Kamati imesikitishwa kwa kushuka fedha za miradi ya maendeleo zilizotengwa, ambapo kwa Mwaka wa fedha 2017/2018 fedha za maendeleo zilizotengwa ni pungufu kwa asilimia 24 ya fedha zilizotengwa kwa mwaka unaopita kama inavyoonyesha kwenye jedwali namba tatu. Aidha, kwa miaka miwili mfululizo Tume ya Maendeleo ya Ushirika - Fungu 24 imekuwa haitengewi fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kwa mwaka huu wa fedha 2017/2018 Tume ya Maendeleo ya Ushirika imetengewa kiasi cha shilingi bilioni 4.1 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga fedha za maendeleo kwa Fungu 24 ili kuiwezesha Tume ya Maendeleo ya Ushirika kujiimarisha na kuinua ushirika wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu ya Taarifa inahusu Maoni na Mapendekezo ya Kamati; baada ya Kamati kufanya uchambuzi sasa inataka kupendekeza kwenye maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji mdogo wa sekta ya kilimo. Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba ukuaji mdogo wa sekta ya kilimo unachangiwa kwa kiasi kikubwa

na uwekezaji mdogo katika sekta hii. Kwa mfano, mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali ilitenga asilimia 4.9 tu ya bajeti ya Serikali kwa ajili ya sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Kamati inaishauri Serikali kuongeza uwekezaji katika kilimo angalau kufikia Azimio la Maputo na Malaba, ambalo linazitaka nchi wanachama kutenga asilimia 10 ya bajeti ya Serikali kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo pendekezo hili litatekelezwa itasaidia kuwa na uhakika wa usalama wa chakula, kuongeza ajira, malighafi kwa viwanda, kuongeza pato na ustawi wa wakulima, lakini pia kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, mtiririko wa fedha za miradi ya maendeleo usioridhisha upo udhaifu mkubwa katika kutoa fedha za maendeleo zinazokuwa zimetengwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtiririko wa fedha usioridhisha umekuwa ukiathiri kwa kiasi kikubwa ufanisi katika kutekeleza miradi hiyo na kuifanya Serikali na wananchi kwa ujumla kutokupata matokeo yaliyotarajiwa. Kwa mfano, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Fungu 43 ilipelekewa asilimia 3.3 na Fungu 99 ilipelekewa asilimia nane kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Hii inaonyesha kwamba kilimo si moja ya vipaumbele vya Serikali, pili, Serikali haitambui umuhimu wa Sekta za kilimo katika ustawi wa sekta zingine na kilimo si sekta mama ya ustawi wa wananchi ambao wengi wanajihusisha na shughuli za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuimairisha na kuongeza utoaji wa fedha kwa ajili ya sekta ya kilimo kama zinavyoidhinishwa na Bunge. Tatu, Mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sera ya Kilimo ya Taifa ya mwaka 2013 inaelezea umuhimu wa kuongeza matumizi ya mbembejeo za kisasa kama muhimili imara wa kuongeza

tija na uzalishaji wa mazao, kupunguza umaskini, na kuwa na usalama wa chakula na lishe. Kwa kuzingatia umuhimu huu, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuwezesha upatikanaji wa pembejeo hapa nchini. Hata hivyo, suala la upatikanaji wa pembejeo za kilimo, bei kubwa, usambazaji wa matumizi yasiyo sahihi bado ni tatizo. Upatikanaji wa mbolea, mbegu bora pamoja na madawa ya viatilifu hayakidhi mahitaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi hayo kidogo ya mbolea hapa nchini yanasababishwa na bei kubwa ya mbolea. Ili kuongeza matumizi ya mbolea na kuhamasisha wakulima wengi zaidi kutumia mbolea, Serikali inatarajia kuanzisha mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja *(Fertilizer Bulk Procurement),* mfumo ambao una lengo la kuwawezesha wakulima wadogo kupata mbolea yenye ubora na kwa bei nafuu na uhakika kuipata. Naipongeza Serikali kwa hotuba iliyotoa leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia faida zinazotarajiwa kupatikana na kwa kuwa mfumo huu utaanza kutumika mara ya kwanza hapa nchini, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao kwa Serikali:-

(a) Wizara iendelee na taratibu za kuanzishwa na kutekeleza mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja.

(b) Wizara iongeze timu ya wataalam mbalimbali ili Serikali iweze kuchukua tahadhari na mapungufu yote yanayoweza kutokea na hivyo Taifa kushindwa kunufaika na mfumo huu.

(c) Serikali iwezeshe na kushirikisha sekta binafsi katika mfumo huu na uanzishwaji wa viwanda vya kuzalisha mbolea ili kuwezesha uzalishaji wa mbolea hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kukamilisha miradi inayoendelea kabla ya kuanza kutekelezwa kwa miradi mipya. Kwa ujumla miradi mbalimbali ya maendeleo inayoombewa fedha kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni

muendelezo wa utekelezaji wa miradi ya mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na miradi michache mipya iliyoibuliwa katika mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa ya kuendelea na miradi ya mwaka wa fedha unaomalizika ni kutokamilika utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati uliopangwa. Kutokamilika kwa miradi hii pamoja na athari zingine kunaongeza gharama za utekelezaji miradi kutokana na kupanda kwa bei na gharama zingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia hali hiyo Kamati inaishauri Serikali kukamilisha miradi iliyopo kabla ya kuanzisha miradi mipya, Ushauri huu ukitekelezwa utasaidia kupunguza mzigo kwa Serikali wa kuwa na miradi mingi isiyokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mikopo yenye riba nafuu itakayoongeza tija katika Sekta za Kilimo. Kilimo kinaajiri asilimia 75 ya Watanzania, vilevile kilimo kinaweza kuchangia upatikanaji wa chakula na manufaa mengine. Pamoja na umuhimu huo wa kilimo, wakulima wengi wanakabiliwa na changamoto ya kutomudu gharama za ujenzi wa miundombinu na teknolojia za kisasa katika shughuli za kilimo, ufugaji na uvuvi kwa sababu ya kukosa mikopo yenye riba nafuu. Ninaomba kwamba Benki ya Kilimo ianze na isambae nchi nzima*. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya *Food and Agriculture Organization (FAO)* inaeleza kuwa wakulima wanaopata mikopo nchini ni chini ya asilimia mbili na kwa hivyo hutengemei kilimo kuendela bila kuondokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, kero ya muingiliano wa shughuli zinazofanywa na taasisi za udhibiti. Kuna malalamiko ya wadau wa kilimo, hususan sekta binafsi, kuhusu uwepo wa utiriri wa kodi zinazotozwa na taasisi mbalimbali za udhibiti, nimesikia mheshimiwa Waziri akielezea lakini tunaomba hilo lifanyike kwa vitendo ili kilimo kiwe ni mahali pa furaha na mahali pa kupata maendeleo ya Taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kukabiliana na migogoro ya ardhi. Serikali imekuwa ikichukua hatua kukabiliana na migogoro ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali hasa wakulima na wafugani. Pamoja na hatua hizo bado vipo viashiria vya kuendelea kuwepo migogoro katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa ujumla migogoro ya ardhi imekuwa ikiathiri sana kilimo, mifugo, uvuvi na sekta nyingine za kiuchumi vilevile. Kamati inashauri Serikali iongeze kasi ya kupima na kumilikisha ardhi sanjari na kuharakisha uwepo wa Sheria ya ardhi ya kilimo na ufugaji ili kulinda ardhi ya kilimo na mifugo. Serikali iwe tayari kuwapunguzia Wakulima na wafungaji kero na malalamiko zinazowakabili. Wakulima wanalia, wafugani wanalia, Serikali ifute machozi ya hao watu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umuhimu wa ujenzi wa maghala kwa ajili ya hifadhi ya nafaka na usalama wa chakula. Maghala ya kisasa ni muhimu katika kuhakikisha usalama wa chakula. Hifadhi ya nafaka huongeza bei kwa asilimia 80 ukilinganisha na bei wakati wa mavuno. Aidha, uhifadhi duni huchangia sumu ya *Aflatoxin* na kuhatarisha usalama wa chakula kwa walaji na hasara kwa wakulima. Naomba Serikali ione namna ya kuhamasisha ujenzi na kutekeleza ujenzi wa maghala imara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu udhibiti wa uvuvi haramu; uvuvi haramu ni jambo ambalo linajulikana ndani ya nchi hii, ninaomba Serikali ichukue hatua ili tuwe kama nchi zinazotuzunguka tusiwe na uvuvi haramu...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba umalize una dakika mbili.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisema bajeti ndogo ya kilimo ionekane na bajeti ndogo ya uvuvi ionekane na ya mifugo ionekane.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mengi ambayo

nimeyatayarisha lakini naomba yazingatiwe katika *Hansard* yetu na Wabunge wataisoma kule.

Ninawashukuru wote hasa wewe Naibu Spika, Ninamshukuru Mheshimiwa Waziri na watu wake, ninashukuru Kamati hii ya Kilimo, Mifugo na Maji kwa kazi nzuri ya kutayarisha taarifa hii n mwisho namshukuru Katibu wa Bunge na wote ambao wanaisaidia Kamati hii. *(Makofi)*

Baada ya maelezo hayo naliomba sasa Bunge lako lipokee lijadili na kuithinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na ninaunga kwa nguvu zote hotuba ya Waziri na hoja yake na Waheshimiwa Wabunge wote waiunge mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana.

**MAONI YA KAMATI YA KILIMO, MIFUGO NA MAJI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

---

**1.0 MAJUKUMU YA KAMATI NA MUUNDO WA TAARIFA**

**1.0 Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**1.1 Mheshimiwa Spika**, Kifungu cha 7(1) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji pamoja na majukumu mengine jukumu la kushughulikia bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**1.2 Mheshimiwa Spika,** vile vile Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 inataka Kamati kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha unaoisha.

**1.3 Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi inajumuisha mafungu manne (4) ambayo ni :-

- Fungu 43 – Sekta ya Kilimo,
- Fungu 64-Sekta ya Uvuvi,
- Fungu 99 – Sekta ya Mifugo na
- Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika,

**1.4 Mheshimiwa Spika,** kufuatia maelezo hayo ya utangulizi, Taarifa hii inafafanua mambo matano (5) yafuatayo:-

i) Mapitio ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/ 2017;

ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2016/2017;

iii) Mapitio ya Ukaguzi wa Miradi ya Mandeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017;

iv) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018; na

v) Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018;

**1.6 Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ya Kwanza

imebainisha msingi wa majukumu ya Kamati katika Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na masuala ya msingi yatakayofanyiwa uchambuzi na kutolewa maoni na mapendekezo. Sehemu ya Pili inahusu uchambuzi wa majukumu yaliyotekelezwa na Wizara na Sehemu ya Tatu inahusu maoni na mapendekezo ya Kamati.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MASWALA MBALIMBALI

**2.1 Mheshimiwa Spika,** sehemu hii inabainisha masuala muhimu yaliyojitokeza katika uchambuzi wa Kamati kwa kuzingatia masuala yaliyoorodheshwa katika Kipengele 1.6 cha Sehemu ya Kwanza.

### 2.2 UTEKELEZAJI WA USHAURI WA KAMATI

**2.2.1 Mheshimiwa Spika**, katika sekta ya za Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Ushirika, Kamati ilitoa maoni na ushauri kwenye maeneo takribani kumi na tisa (19). Maeneo hayo yanajumuisha ushauri kuhusu:-

i) Umuhumu wa fedha za miradi ya maendeleo kutolewa kwa wakati;

ii) Umuhimu wa kukamilisha miradi mbalimbali inayoendelea kabla ya kubuni na kutekeleza miradi mipya;

iii) Kuandaa na kutekeleza Mpango maalum wa ugawaji na usambazaji pembejeo za ruzuku kwa kuzingatia mahitaji halisi ya kalenda ya msimu wa kilimo kwa kila eneo, sanjari na udhibiti wa mianya ya wizi, ubadhirifu na rushwa katika utoaji wa pembejeo;

iv) Umuhimu wa kuwa na akiba ya chakula cha kutosha nchini;

v) Umuhimu wa Tafiti katika sekta za kilimo,mifugo, uvuvi na ushirika ili kuongeza tija katika uzalishaji;

vi) Umuhimu wa kuwa na Maafisa Ugani wa kutosha nchi nzima,ili kueneza na kusimamia teknolojia za kisasa katika sekta ya kilimo,mifugo na uvuvi;

vii) Umuhimu wa sekta za kilimo,Mifugo,uvuvi na ushirika katika kukuza na kuendeleza sekta ya viwanda nchini;

viii) Kuongeza kasi ya upimaji na umilikishaji wa maeneo ya kilimo,ufugaji na watumiaji wengine wa ardhi ili kukabiliana na migogoro ya ardhi;

ix) Mikakati ya Serikali kukabiliana na changamoto ya mabadiliko ya tabia nchi ili kuendeleza kilimo;

x) Mipango ya Serikali kuhamasisha na kuwawezesha vijana kushiriki katika shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi;

xi) Kufanya tathmini kwenye mazao ya chakula na biashara ili kubaini tozo zisizo za lazima na kuzifuta ili kumuondolea mkulima makato yasiyostahili ambayo yamekuwa kero za muda mrefu;

xii) Serikali kuwa na mkakati wa makusudi wa kuviwezesha na kuvilinda viwanda vya ndani vya sukari, ili viweze kuzalisha sukari ya kutosha na kuondokana na uagizaji wa sukari kutoka nje ya nchi.

xiii) Udhibiti wa Uvuvi haramu na biashara ya utoroshwaji wa mazao ya uvuvi nje ya nchi;

xiv) Umuhimu wa kuimarisha doria katika Bahari Kuu;

xv) Kuongeza kasi ya ujenzi wa bandari ya uvuvi;

xvi) Tume ya Maendeleo ya Ushirika kupanua wigo wa shughuli zake kwa kuanzisha vyama vya ushirika katika sekta za Mifugo na Uvuvi;

xvii) Serikali kuiongezea mtaji Benki ya Maendeleo ya Kilimo ili kuiwezesha kutoa mikopo nafuu kwa wakulima wengi ikiwa ni pamoja na kufungua matawi nchini kote ili kurahisisha utoaji wa mikopo kwa wananchi kwa ujumla;

xviii) Serikali kupanga na kutekeleza mikakati ya kuongeza mnyororo wa thamani katika mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi sanjari na uhakika wa masoko;na

xix) Maswala yanayohusu Bajeti kwa ujumla wake.

**2.2.2 Mheshimiwa Spika,** napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ushauri uliotolewa na Kamati kwa kiasi kikubwa haujatekelezwa. Kamati haijaridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Wizara katika utekelezaji wa ushauri wa Kamati katika maeneo ya vipaumbele vya Wizara.

Kwa mfano baadhi ya shughuli zilizoshindwa kutekelezwa kikamilifu ni pamoja na:-

i) Kushindwa kupima maeneo ya kilimo na kuyapatia hatimiliki hivyo kusababisha kuendelea kuwepo kwa migogoro ya wakulima na wafugaji;

ii) Usambazaji wa pembejeo za kilimo kwa kuzingatia msimu wa kilimo wa eneo husika;

iii) Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji;

iv) Ujenzi na ukarabati wa maghala;

v) Ukarabati wa majengo ya vituo vya utafiti na mafunzo, ukaguzi wa mazao, mimea na viuatilifu;

vi) Ujenzi wa bandari ya uvuvi;

vii) Kushindwa kulipa madeni ya wazabuni na wakandarasi;

viii) Uwekezaji mdogo katika sekta za mifugo na uvuvi;

ix) Udhibiti usiokidhi wa uvuvi haramu na;

x) Kuendelea kuwepo kwa uhaba wa maafisa ugani wa kilimo, mifugo na uvuvi.

## 3.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2016/2017

**3.1** **Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ulijikita katika kulinganisha kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge, kiasi cha fedha kilichopokelewa na kutumika hadi mwezi Mei, 2017 na eneo la ukusanywaji maduhuli kwa kulinganisha makadirio yaliyowekwa na kiasi kilichokusanywa hadi Mei , 2017.

### 3.2 SEKTA YA KILIMO - FUNGU 43

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa **Fungu 43**, liliidhinishiwa jumla ya shilingi **211,359,133,000** kati ya fedha hizo shilingi **109, 831,636,000** ni fedha za matumizi ya kawaida na shilingi **101,527,497,000** ni fedha za maendeleo. Hadi kufikia Mei, 2017 fedha za matumizi ya kawaida zilizotolewa ni Jumla ya shilingi **61,702,709,784** ambayo ni **asilimilia 54** ya kiasi kilichoidhinishwa. Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo zilizotolewa zilikuwa shilingi **3,369,416,666** sawa na **asilimia 3.31** ya fedha zilizoidhinishwa**.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kupitia Fungu 43 ilikadiria kukusanya mapato ya shilingi **4,017,010,000.** Hadi kufikia Aprili, 2017, Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya shilingi **3,299,773,587.22** ambayo ni sawa na asilimia **82.15** ya malengo ya ukusanyaji.

## 3.3 SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI - FUNGU 99

**Mheshimiwa Spika,** Fungu 99 iliidhinishiwa jumla ya shilingi **60, 013,252,440.56.** Kati ya fedha hizo shilingi **44,140,037,440.56** zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **15,873,215,000** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2017 jumla ya shilingi **29,845,921,489.56** kwa ajili ya matumizi ya kawaida zilikuwa zimetolewa ambayo ni sawa na **asilimia 68**. Kwa upande wa fedha za miradi ya maendeleo, hadi kufikia mwezi Mei 2017, kiasi cha shilingi **1,252,230,662.49** zilitolewa, sawa na **asilimia 8 %** ya bajeti iliyoidhinishwa.

## 3.4 TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA - FUNGU 24

**Mheshimiwa Spika,** fungu 24 liliidhinishwa jumla ya shilingi **4,894,921,000** kwa ajili ya matumizi ya kawaida tu, fungu hili halikutengewa fedha za maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2017 kiasi cha shilingi **3,425,573,146.45** zilitolewa ambayo ni sawa na **asilimia 67.6** ya kiasi kilichoidhinishwa.

Kamati inaipongeza Wizara kwa kuweza kukusanya mapato ya wastani wa **asilimia 80** ya malengo ya makadirio ya makusanyo. Hata hivyo, Kamati inaitaka Wizara kuongeza jitihada kukusanya mapato zaidi kadiri ya makadirio kwani, Sekta za kilimo, mifugo na uvuvi zina fursa nyingi na za uhakika za kuwezesha Serikali kupata mapato.

**3.5 Mheshimiwa Spika,** uchambuzi uliofanywa na Kamati umebaini kwamba kwa miaka miwili mfulilizo, fedha zinazoidhinishwa na Bunge hazitolewi kama zilivyoidhinishwa na hivyo kuchangia kutofikiwa kwa malengo yaliyopangwa, ikiwa ni pamoja na kutofanyiwa kazi ushauri wa Kamati katika maeneo mengi kama ilivyoelezwa hapo juu.

Kwa mfano katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kiasi cha fedha kilichotolewa ni kidogo ikilinganisha na fedha zilizotengwa na kuidhinishwa na Bunge. Jedwali lifuatalo linaloonyesha muhtasari wa jumla ya fedha zilizotengwa katika bajeti za miaka miwili, 2015/2016 na 2016/2017.

**JEDWALI NA.1: LINAONYESHA MLINGANISHO WA FEDHA ZILIZOTENGWA MWAKA WA FEDHA 2015/16 NA 2016/17**

| FUNGU | 2015/2016 | 2016/2017 |
|---|---|---|
| 43 | 206,816,421,000 | 112,148,702,175.92 |
| 24 | 6,263,383,000 | 4,894,921,000 |
| 99 | 60,373,984,500 | 60,013,252,440.56 |

**28** ya pato la Taifa kwa mwaka 2014 na kupanda kufikia **asilimia 29** mwaka 201
na Mikakati ya Kitaifa na Kimataifa vinatambua Kilimo kama sekta muhimu katil
Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande fedha za maendeleo, kwa katika bajeti ya mwaka 2016/2017 kumekuwa na ongezeko la kiasi cha jumla ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge, lakini kiasi cha asilimia kinachotolewa kimeshuka kikilinganishwa na bajeti ya mwaka 2015/2016.

**JEDWALI NA.2: LINAONYESHA MLINGANISHO WA FEDHA ZA MAENDELEO ZILIZOTENGWA NA KUTOLEWAMWAKA WA FEDHA 2015/16 NA 2016/17**

| Bajeti ya mwaka wa fedha | Fungu | Bajeti ya maendeleo iliyotengwa | Bajeti ya maendeleo iliyotolewa | % ya fedha iliyotolewa |
|---|---|---|---|---|
| 2015/2016 | 43 | 32,713,073,000 | 5,192,797,589 | 16 % |
| | 24 | 00 | 00 | 00 % |
| | 99 | 19,398,607,500 | 00 | 00 % |
| 2016/2017 | 43 | 101,527,497,000 | 3,369,416,666 | 3.31% |
| | 24 | 00 | 00 | 00 % |
| | 99 | 15,873,215,000 | 1,252,230,662.49 | 8% |

**Chanzo: Randama ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika**, jedwali na.2 linaonyesha, kuongezeka kwa kiasi cha jumla ya fedha za maendeleo zilizoidhinishwa

na Bunge na kutolewa na Serikali kwa bajeti za mafungu (Fungu 43 na 99), kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2015/2016. Aidha, kwa fungu 43, linaonyesha kushuka kwa asilimia ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo kutoka **asilimia 16%** kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016 hadi **asilimia 3.31%** kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017. Na kwamba hakuna bajeti yeyote ya maendeleo iliyotengwa kwa fungu 24, kwa miaka miwili mfulilizo.

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo huu wa kushuka kwa Bajeti ya sekta za kilimo, mifugo na uvuvi una athari kubwa katika ustawi wa pato la wakulima na uchumi wa nchi kwa ujumla kwani **asilimia 75%** ya Watanzania wanajihusisha na shughuli za kilimo. Kamati inataka kufahamu kwanini bajeti ya sekta hizi inaendelea kushuka wakati kilimo, mifugo na uvuvi ni chachu ya uchumi wa viwanda.

## 4.0 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA 2016/2017

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni ya 98(1) inaitaka Kamati kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha unaoisha 2016/2017. Msingi wa Kamati kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ni kufanya ukaguzi wa tathimini halisi ya fedha iliyotumika (*Value for Money*) Aidha, msingi wa kuchambua utekelezaji wa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 ni kuiwezesha Kamati kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha unaofuata katika sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**4.1 Mheshimwia Spika,** Kamati haikuweza kutekeleza ipasavyo matakwa ya Kanuni ya 98(1) ambayo inaitaka Kamati kukagua miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka unaomalizika ambao ni 2016/2017 kutokana na baadhi ya miradi ya sekta ya kilimo kutopelekewa fedha yeyote na kushindwa kutekelezwa. Aidha, kwa baadhi ya miradi iliyopata kiasi kidogo cha fedha zilitumika katika hatua za awali za uratibu wa kutekeleza miradi iliyopangwa, hivyo

hakukuwa na miradi iliyotekelezwa kwa namna ya kuweza kukaguliwa katika kipindi kilichopangwa Kikanuni kwa ajili ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo.

### 4.1.1 SEKTA YA KILIMO – FUNGU 43

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa Sekta ya Kilimo, Fungu 43, hadi kufikia Mei, 2017 ilikuwa imepokea fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo kiasi cha shilingi **3,369,416,666** sawa na **asilimia 3.31** ya kiasi kilichoidhinishwa, cha shilingi **101,527,497,000**.

**Mheshimiwa Spika,** mtiririko wa fedha usioridhisha umechangia kutofikiwa kwa malengo ya Wizara yaliyopangwa kutekelezwa katika 2016/2017 katika programu mbalimbali za kuendeleza sekta ya kilimo. Maeneo yaliyoathirika ni pamoja na upimaji maeneo ya kilimo na kuyapatia hatimiliki, usambazaji wa pembejeo za kilimo, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, ujenzi na ukarabati wa maghala, ukarabati wa majengo ya vituo vya utafiti na mafunzo, ukaguzi wa mazao, mimea na viuatilifu, kushindwa kulipa madeni ya wazabuni na wakandarasi, uwekezaji mdogo katika sekta kwa ujumla.

### 4.1.2 SEKTA YA MIFUGO NA UVUVI – FUNGU 99

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2016/ 2017 Miradi ya Maendeleo katika sekta ya mifugo na uvuvi, Fungu 99 ilidhinishiwa jumla ya shilingi **15,873,215,000**. Kati ya fedha hizo shilingi **8,000,000,000 (50.4%)** ni fedha za ndani na shilingi **7,873,215,000 (49.60%)** ni fedha za nje. Hadi kufikia Mei, 2017, kiasi cha shilingi **1,252,230,662.49 (8%)** ya fedha zilizoidhinishwa kilitolewa. Kati ya hizo, fedha za ndani ni kiasi cha shilingi **280,000,000 (4%)** na fedha za nje ni shilingi **972,230,662.49 (12.3%).**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba, mara nyingi fedha za nje zimekuwa zikitolewa zikiwa pungufu au kwa kuchelewa wakati fedha za ndani zinazotengwa kwa miradi ya maendeleo mara nyingi hazitolewi kabisa. Hali hii inaathiri

kwa kiasi kikubwa ufanisi katika utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa.

Kamati inashauri Serikali kuona umuhimu wa kutenga na kutoa kwa wakati fedha za miradi ya maendeleo kutoka mapato ya ndani, kwani kutumia fedha za ndani kunadhihirisha utayari wa Serikali katika kujitegemea na kuwaletea wananchi wake maendeleo ya kweli.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilibaini kuwa, Idara kuu za Mifugo na Uvuvi baadhi ya programu hazikupelekewa fedha za miradi ya maendeleo kabisa licha ya Bunge kuidhinisha fedha hizo. Programu ambazo hazikupelekewa fedha yoyote hadi kufikia mwezi Mei, 2017 ni pamoja na:-

(i) Programu za huduma za mifugo;
(ii) Ukuzaji viumbe kwenye maji; na
(iii) Kutumia teknolojia za kuongeza tija na uzalishaji wa samaki.

**Mheshimiwa Spika,** programu zingine zilipelekewa fedha kidogo ambazo zilitumika kutekeleza shughuli za uratibu pekee.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasikitishwa na mwenendo huu wa Sekta za mifugo na uvuvi kutopelekewa fedha kama zinavyoidhinishwa na Bunge**.** Mwenendo huu umechangia kutofikiwa kwa malengo ya Wizara yaliyopangwa kutekelezwa katika mwaka wa fedha 2016/2017 katika programu mbalimbali za kukuza sekta ya mifugo, uvuvi na ufugaji wa samaki na viumbe wengine wa kwenye maji kwa tija.

**4.1.3 Mheshimiwa Spika,** kutokana na kutotolewa fedha za miradi ya maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 kwa sekta ya Kilimo, ililazimu Kamati ifanye kazi zingine nje ya ukaguzi wa miradi iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2016/2017. Kufuatia hali hiyo, Kamati ilikagua miradi na shughuli zinazotekelezwa na Wizara ambazo zilitengewa na kupelekewa fedha katika bajeti za miaka ya nyuma katika

Sekta ya kilimo, lakini pia Kamati ilikagua shughuli za sekta binafsi katika maeneo ya mifugo na uvuvi.

**Mheshimiwa Spika,** mantiki ya Kamati kukagua nshughuli zinazotekelezwa na sekta binafsi kwenye masuala ya uvuvi na mifugo ilikuwa ni kujifunza namna sekta binafsi inavyoshiriki katika shughuli za kukuza uchumi kupitia kilimo, mifugo na uvuvi na changamoto wanazokutana nazo hatimae Kamati iweze kuishauri Serikali hatua za kuchukua ili kuiwezesha setka binafsi kushiriki kikamilifu katika kuongeza pato la taifa na kukuza ajira. Katika ziara hiyo, Kamati ilikagua:-

**a) GHALA LA HIFADHI YA TAIFA YA CHAKULA MKOANI SHINYANGA**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ziara ya ukaguzi wa ghala la hifadhi ya chakula mkoani Shinyanga ili kujiridhisha na akiba ya chakula iliyohifadhiwa katika kukabiliana na kuwepo kwa upungufu wa chakula mahali pengi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** katika ukaguzi huo, Kamati ilibaini kuwa, ghala la hifadhi ya chakula mkoani Shinyang lilikua na mahindi yaliyohifadhiwa kiasi cha tani **8,622.619,** na kwamba kiasi hicho kinatosheleza mahitaji ya mkoa wa Shinyanga na mikoa jirani. Aidha, Kamati ilibaini pia kuwa, mahindi yaliyohifadhiwa ni ya muda mrefu kwani mahindi hayo yalinunuliwa wakati wa msimu wa mwaka 2014/2015 na endapo mavuno ya msimu wa 2016/2017 yatakuwa ya kutosheleza, huenda shehena iliyopo isiweze kutolewa kwa wakati na kusababisha hasara ya mahindi kuharibika na kutupwa.

**Mheshimiwa Spika**, Ili kunusuru mahindi hayo kuharibika, Kamati iliishauri Serikali kutoa mahindi hayo na kuyauza kwa bei nafuu kwenye maeneo yenye uhaba mkubwa wa chakula ili kupunguza uhaba wa mahindi na kudhibiti bei ya mahindi ambayo imekuwa ikiongezeka siku hadi siku.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulialifu Bunge lako tukufu kuwa

Serikali imetekeleza ushauri wa Kamati na kwa kuanzia Serikali imekwishatoa **tani 500** za mahindi yaliyohifadhiwa katika ghala la Hifadhi ya Taifa ya chakula mkoa wa Shinyanga na kuipatia Wilaya ya Serengeti ambayo ilikuwa na uhaba mkubwa wa chakula kutokana na tembo kuvamia mashamba ya wananchi. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hiyo, hata hivyo Kamati inaitaka Serikali kufanya hivyo kwenye maeneo mengine ambayo yana uhaba mkubwa wa chakula.

**b) KIWANDA CHA UCHAKATAJI SAMAKI CHA TANZANIA *FISH PROCESSORS LIMITED* – MWANZA**

**Mheshimiwa Spika**, katika ziara hii, Kamati ilikagua uwekezaji unaofanywa na sekta binafsi kwenye shughuli za uvuvi ambapo Kamati ilikagua Kiwanda cha Ukataji Samaki cha Tanzania *Fish Processors Limited* kilichoko Mwanza.

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara hiyo, Kamati ilibaini kuwa kiwanda cha Tanzania *Fish Processors Limited* kinaajiria zaidi ya Watanzania 400 pamoja na kulipa kodi mbalimbali za Serikali ( *direct and indirect tax*) kiasi cha **shilingi bilioni 3.2** kwa mwaka ambayo ni **asilimia 5%** ya pato lake ambalo ni shilingi **bilioni 64**[1].

**Mheshimiwa Spika,** katika ziara hiyo, Kamati ilibaini pia kuwa tangu mwaka 2006 uzalishaji wa kiwanda hiki umekuwa ukishuka kila mwaka kutokana na kuendelea kupungua kwa samaki katika ziwa Victoria kunakosababishwa na uvuvi haramu pamoja na biashara ya samaki inayofanywa nje ya mipaka ( *cross border fish trading*).

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilipokea maelezo ya muwekezaji wa kiwanda hiki kwamba, kiwanda kimekuwa kikinunua samaki kutoka kwa wavuvi wadogo na kupima samaki za wavuvi hao bila wao kuwepo. Aidha, yamekuwepo malalamiko kutoka kwa wavuvi wadogo kuwa utaratibu huu unawaibia wavuvi mazao yao kwa kuwa

[1]Taarifa ya *Tanzania Fish Processors Limited* iliyowasilisha kwenye Kamati tarehe 24 Machi, 2017

mwenye kiwanda ndio mwenye wajibu wa kumwambia mvuvi kilo ngapi za samaki zimepatikana.

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia ziara ya Kamati kiwandani hapo, Kamati inatoa ushauri ufuatao kwa Serikali:-

i) Wizara iongeze juhudi katika kudhibiti shughuli za uchakataji samaki usio rasmi.

ii) Wizara iongeze juhudi katika kudhibiti na kukomesha vitendo vya uvuvi haramu;

iii) Wizara iongeze juhudi katika kudhibiti biashara ya kuvuka mipaka (*cross border trade*) na

iv) Wizara, kushughulikia malalamiko ya wavuvi kwa kuweka utaratibu wa kuhakikisha wavuvi wadogo wanapouza samaki kwa wenye viwanda, upimaji wa samaki hao ufanyike mbele ya muuzaji ili awe na uhakika na mafao yake.

**c) KIWANDA CHA KUSINDIKA NYAMA CHA KAMPUNI YA CHOBO – MWANZA**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitembelea kiwanda cha kusindika nyama cha kampuni ya Chobo na kuona uwekezaji mkubwa uliofanywa katika mazao yatokanayo na mifugo aina ya ng'ombe, mbuzi na kondoo.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya kiwanda ilieleza kwamba kiwanda kina uwezo wa kuchinja ng'ombe 600, mbuzi na kondoo 920 kwa siku na kuhakikisha upatikanaji wa soko la uhakika katika mkoa wa Mwanza na mikoa ya jirani. Taarifa ya kiwanda ilisisitiza uwepo wa changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na muingiliano na mgongano wa kimamlaka na utendaji kutoka katika Taasisi na wakala wa Serikali. Kwa mfano Mamlaka ya udhibiti ubora wa chakula na dawa (TFDA), Shirika la viwango nchini (TBS) na Idara ya Afya. Taasisi hizi zinahusika na usalama na ubora wa bidhaa nchini, zimekuwa na muingiliano wa majukumu

unaosababisha usumbufu usiokuwa wa lazima kwa kiwanda.[2]

Kufuatia taarifa hiyo, Kamati inaishauri Serikali kutathimini majumuku ya Mamlaka zake ili kubaini muingiliano wa kiutendaji uliopo na kurekebisha maeneo yanayolalamikiwa na sekta binafsi ili kuweka mazingira rafiki kwa wawekezaji.

## 4.4 MPANGO WA BAJETI NA UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokea na kuchambua Mpango wa Bajeti wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 tarehe 29-30 Machi, 2017. Mpango ambao umeandaliwa kwa kuzingatia Sera na Mikakati ya Kitaifa na Kisekta katika kuandaa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Ukomo wa Bajeti ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2017/2018 na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Taifa 2025.

### 4.4.1 UMUHIMU WA SEKTA ZA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, unabainisha kuwa, Tanzania imeendelea kutegemea sekta ya kilimo katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya wananchi wake kwa kuwa kilimo kinatoa ajira kwa **asilimia 75%** ya Watanzania, inachangia **asilimia 100%** ya chakula kinachopatikana nchini na kinatoa malighafi ya viwanda. Aidha, kutokana na asilimia kubwa ya wananchi kushiriki katika shughuli za kilimo, kilimo kinachangia kwa kisi kikubwa katika kupunguza umaskini na kuongeza kipato. Mfano Sekta ya Kilimo imechangia **asilimia**

---

[2]Taarifa ya *Chobo Investment Company Limited*, iliyowasilishwa kwenye Kamati tarehe 24 Machi, 2017

---

[3]Taarifa ya Baraza la Kilimo Tanzania kuhusu mchango wa sekta ya Kilimo katika pato la Taifa

**28** ya pato la Taifa kwa mwaka 2014 na kupanda kufikia **asilimia 29** mwaka 2015[3] Vile vile Sera na Mikakati ya Kitaifa na Kimataifa vinatambua Kilimo kama sekta muhimu katika Uchumi wa Tanzania.

### 4.4.2 MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/2018

**Mheshimiwa Spika,** kabla ya kuanza kuchambua malengo ya bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 napenda kuipongeza Serikali kwa uamuzi wa kutenganisha utekelezaji wa shughuli za sekta ya mifugo na uvuvi ambapo kuanzia mwaka huu wa Fedha sekta hizi mbili zitatekeleza shughuli zake kupitia mafungu mawili tofauti ( *Two Separate Votes*) yaani Fungu 64 (uvuvi) na Fungu 99 ( Mifugo).

**Mheshimiwa Spika,** hivyo uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi inajumuisha mafungu manne ambayo ni:-

(i) Fungu 43 – Sekta ya Kilimo;
(ii) Fungu 64 – Sekta ya Uvuvi;
(iii) Fungu 99- Sekta ya Mifugo na
(iv) Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi Fungu 43 , Fungu 64, Fungu 99 na Fungu 24 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **281,745,995,830.** Aidha, Wizara kupitia mafungu yake kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 inatarajia kukusanya jumla ya maduhuli kiasi cha shilingi **40,122,381,551.**

#### 4.4.2.1 FUNGU 43: SEKTA YA KILIMO

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Fungu 43 linaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **214,815,759,000**. Kati ya fedha hizo, shilingi **64,562,759,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **150,253,000,000** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, Wizara kupitia Fungu 43 imepanga kukusanya jumla ya shilingi **4,017,010,000.**

#### 4.4.2.2 FUNGU 64: SEKTA YA UVUVI

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara kupitia fungu 64 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi **23,900,893,059**. Kati ya fedha hizo, shilingi **15,900,893,059** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **8,000,000,000** ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, kwa upande wa maduhuli Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi **19,658,632,051** zitakazopatikana kutokana na mapato yatokanayo na ushuru wa soko, leseni za kuvua na kusafirisha samaki na mazao yake na ushuru wa mrahaba.

#### 4.4.2.3 FUNGU 99: SEKTA YA MIFUGO

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara kupitia Fungu 99 inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi **29,946,424,452**. Kati ya fedha hizo, shilingi **25,946,424,452** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **4,000,000,000** ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Aidha, kwa upande wa maduhuli Wizara imepanga kukusanya jumla ya shilingi **16,446,739,500** zitakazopatikana kutokana na lesseni za kusafirisha wanyama na mazao yake nje ya nchi, ada mbalimbali, ushuru wa soko,mauzo ya chanjo na kodi za pango la nyumba za Serikali na mauzo ya zabuni.

#### 4.4.2.4 FUNGU 24: TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara kupitia Fungu Fungu 24 linaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **10,474,758,211**. Kati ya fedha hizo, shilingi **6,309,658,211** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi **4,165,000,000** ni kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo ya Tume ya Ushirika.

### 4.5 MALENGO YA UTEKELEZAJI NA VIPAUMBELE

**Mheshimiwa Spika**, fedha zinazoombwa zimepanga kutekeleza malengo mbalimballi ya Wizara, malengo hayo ni pamoja na:-

(i) Kusimamia matumizi endelevu ya ardhi ya kilimo na maji;

(ii) Kuongeza kilimo chenye tija;

(iii) Kuimarisha usimamizi wa mazao kabla na baada ya mavuno na kuongeza thamani ya mazao na upatikanaji wa masoko kwa mazao yote ya wakulima;

(iv) Kuratibu utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya mazao na kuimarisha huduma za udhibiti;

(v) Kuunda na kupitia sera za sekta ndogo za mazao na sheria zake ili kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji katika kilimo;

(vi) Kuimarisha uratibu,ufuatiliaji na tathmini ya sekta za kilimo,mifugo na uvuvi;

(vii) Kuimarisha masuala mtambuka yanayohusu vijana katika kilimo, jinsia, mazingira, lishe na UKIMWI;

(viii) Kuboresha uzalishaji katika Sekta ya Mifugo;

(ix) Kuimarisha miundombinu ya maji na malisho;

(x) Kuimarisha taasisi za utafiti,mafunzo na ugani wa mifugo;

(xi) Kuimarisha usimamizi na uendelezaji wa rasilimali za uvuvi;

(xii) Kuimarisha na kuendeleza ulinzi wa rasilimali za uvuvi;

(xiii) Kuboresha usimamizi na udhibiti wa ubora,usalama na viwango vya samaki na mazao ya uvuvi;

(xiv) Kuimarisha uvuvi wa Bahari Kuu;

(xv) Kuimarisha utafiti,mafunzo na ugani wa uvuvi;

(xvi) Kuimarisha na kuongeza uzalishaji wa samaki na upatikanaji wa masoko;

(xvii) Kuhamasisha, kuwezesha na kusimamia uvuvi endelevu,uzalishaji bora wa samaki na mazao yake,na utoaji wa huduma bora kwa wadau wa Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi ili kuwa na maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii;

(xviii) Kuhuisha Sera ya maendeleo ya ushirika;

(xix) Kujenga uwezo wa Tume ya Ushirika ili iweze kutekeleza majukumu yake;

(xx) Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa Vyama vya Ushirika;

(xxi) Kufanya uhamasishaji kwa kushirikisha Wizara za kisekta; Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wengine; na

(xxii) Kuendelea kutekeleza Mpango wa Serikali wa kuhamia Dodoma.

## 4.6 TATHIMINI YA MALENGO KWA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2017/2018


**Mheshimiwa Spika,** Kamati imepitia, kuchambua na kutathimini malengo yaliyoainishwa katika Mpango wa Bajeti ya Mwaka 2017/2018 na kuridhishwa nayo. Hata hivyo, Kamati ina wasiwasi kuhusu uwezekano wa utekelezaji wa malengo hayo kutokana na mwenendo unaojidhihirisha wa kiasi kidogo cha bajeti inayotengwa na kutolewa.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na umuhimu wa sekta za kilimo kama unavyoelezewa kupitia Mipango, Sera na Mikakati mbalimbali ya Serikali, bado sekta hii imekuwa haipewi msukumo wa kutosha kama kipaumbele cha uhai na ustawi wa sekta zingine za uzalishaji mali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati katika uchambuzi wake, imebaini kuendelea kushuka kwa bajeti inayotengwa na kutolewa kwa ajili ya Sekta ya Kilimo kila mwaka. Kwa mfano: kwa Mwaka wa Fedha 2010/2011 bajeti ya kilimo ilikua ni **asilimia 7.8%,** ya bajeti yote ya Serikali, Mwaka wa Fedha 2011/2012 ilikua ni **asilimoa 6.9%** ya bajeti yote ya Serikali na Mwaka wa Fedha 2016/2017 Serikali ilitenga **asilimia 4.9%** tu ya bajeti yote ya Serikali kwa ajili ya Sekta za kilimo.


**Mheshimiwa Spika,** kuendelea kushuka kwa bateji inayotengwa kwa ajili ya sekta za Kilimo, kumepelekea uwekezaji mdogo na hivyo kusababisha ukuaji mdogo wa sekta hii, ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 ukuaji wa sekta ya kilimo ni **asilimia 1.7%** ikilinganishwa na sekta zingine kama madini ambayo ukuaji wake ni asilimia **16.6 %,** uchukuzi **asilimia 15.6**, habari na mawasiliano **asilimia 13.5%.**[4]

**Grafu kuonyesha uwekezaji mdogo katika sekta za kilimo**




[4] Taarifa ya Baraza la Kilimo Tanzania kuhusu ukuaji mdogo wa sekta ya Kilimo

**Grafu kuonyesha ukuaji mdogo wa sekta ya kilimo**




**Mheshimiwa Spika**, ni dhahiri kwamba mwenendo huu wa uwekezaji mdogo kwenye sekta ya kilimo, unakinzana na dhana ya uchumi wa viwanda ambao malighafi ya viwanda kwa kiasi kukubwa yatatokana na bidhaa zitokanazo na kilimo, uvuvi na mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** uwekezaji mdogo unaofanywa na Serikali kwenye kilimo unaathari pato na ustawi wa wananchi walio wengi ambao wanategemea kilimo kama njia kuu ya uzalishaji mali na kuongeza pato. Kamati inatahadharisha kuwa, endapo hatua madhubiti hazitachukuliwa katika kuinua Sekta za kilimo, ni dhahiri kuwa mdororo wa uchumi na mnyororo ya umaskini utaendelea kuwa wimbo mahala pengi nchini. Hivyo, Kamati inaitaka Serikali ilieleze Bunge kwanini Serikali haioni umuhimu wa kutekeleza kwa vitendo mkataba wa Azimio la Maputo na Malaba ambayo yanazitaka nchi wananchama kutenga **asilimia 10** ya bajeti yote ya Serikali kwa ajili ya kilimo**.**

## 4.7 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO YATOKANAYO NA MADUHULI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/ 2018

**Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 Wizara kupitia Fungu 43, inakadiria kukusanya jumla ya shilling **4,017,010,000** kutoka vyanzo mbalimbali. Makadirio haya ni sawa na makadirio ya Mwaka wa Fedha 2016/2017. Aidha, Sekta ya Mifugo na Uvuvi - Fungu 99 na Fungu 64 inatarajia kukusanya jumla ya shilingi, **36,105,371,551** kutoka vyanzo mbalimbali ikilinganishwa na makadirio ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 ambapo Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya shilingi **35,191,332,382** na kufanikiwa kukusanya jumla ya shilingi **26,972495,687,** sawa na **asilimia 77%** ya lengo la makusanyo.

**Mheshimiwa Spika,** makadirio ya makusanyo katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 kwa fungu 43, hayajaongezeka. Aidha, kwa fungu 64 na fungu 99 kuna ongezeko la **asilimia 3** ya makadirio ya Mwaka wa Fedha 2016/2017. Ongezeko hili ni kidogo sana ikilinganishwa na fursa zilizopo katika sekta za mifugo na uvuvi zilizopo nchini fursa hizo ni pamoja na uvuvi katika bahari kuu na mauzo ya mazao yatokanayo na mifugo mbalimbali. Kamati inaamini kuwa endapo fursa hizi zitatumika vizuri zinaweza kuchangia katika kuongeza makusanyo na hivyo kuinua pato la Taifa.

## 4.8 UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilifanya uchambuzi na ulinganisho wa Bajeti ya Maendeleo iliyotengwa kwa miaka miwili, 2016/ 2017 na 2017/2018 katika mafungu ya sekta za kilimo kama inavyoonyeshwa katika jedwali lifuatalo.

**JEDWALI NA. 3: ULINGANISHO WA BAJETI YA MAENDELEO ILIYOTENGWA KWA MIAKA MIWILI, 2016/2017 NA 2017/2018.**

| Fungu | Bajet ya Mwaka 2016/2017 | Bajeti ya Mwaka 2017/2018 | % ongezeko |
|---|---|---|---|
| 43 | 101,525,497,000 | 150,253,000,000 | 48 % |
| 24 | 00 | 4,165,000,000 | 100 % |
| 99&64 | 15,873,215,000 | 12,000,000,000 | -24 % |
| | | | |

**Chanzo cha Taarifa: Randama ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi, 2016/2017**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya ulinganisho wa bajeti ya maendeleo iliyotengwa kwa miaka miwili mfululizo kwa mafungu yote ya Wizara. Kamati imebaini kuwa, jumla ya fedha za maendeleo zilizotengwa kwa mafungu yote kwa mwaka 2017/2018 ni shilingi, **182,318,893,059** ikilinganishwa na shilingi **117,400,712,000** zilizotengwa kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, ikiwa ni ongezeko la **asilimia 36 %.** Kati ya fedha hizi, fedha za ndani zikiwa ni **asilimia 36%** tu. Kwa mnyumbulisho wa mafungu, kiasi kilichotengwa kwa ajili ya Fungu 64 (Uvuvi) ni shilingi **8,000,000,000**, wakati Fungu64 ni shilling **4,000,000,000**.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Sekta ya Mifugo, Kamati imesikitishwa na kushuka fedha za miradi ya maendeleo zilizotengwa, ambapo kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 fedha za maendeleo zilizotengwa ni pungufu kwa **asilimia 24%** ya fedha zilizotengwa kwa mwaka 2016/2017 kama inavyoonyesha kwenye jedwali namba tatu. Kamati haijaridhishwa na kiasi kidogo cha fedha za ndani zinazotengwa, kwani fedha za nje zimekuwa hazitoki kwa muda na wakati uliokusudiwa. Kamati inaitaka Serikali kutoa fedha hizo kadiri zilivyotengwa ili kuiwezesha Wizara kutekeleza miradi iliyokusuduwa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa miaka miwili mfululizo Tume ya Maendeleo ya Ushirika - Fungu 24 imekuwa haitengewi fedha yoyote kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Kwa mwaka huu wa fedha (2017/2018) Tume ya Maendeleo ya Ushirika imetengewa kiasi cha shilingi **4,165,000,000** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Kamati inaipongeza Serikali kwa kutenga fedha za maendeleo kwa Fungu 24 ili kuiwezeshaa Tume ya maendeleo ya ushirika kujiimarisha na kuinua ushirika nchini.

## SEHEMU YA TATU

## 5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**5.1 Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kufanya uchambuzi katika maeneo mbalimbali ya majukumu ya Wizara ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa bajeti ya Mwaka wa Fedha 2017/2018. Naomba kuwasilisha maoni na mapendekezo kumi na tatu (13) yafuatayo:-

### 1) UWEKEZAJI MDOGO WA SEKTA ZA KILIMO

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba ukuaji mdogo wa sekta za kilimo unachangiwa kwa kiasi kikubwa na uwekezaji mdogo katika sekta hii.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mfano: kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017, Serikali ilitenga **asilimia 4.9** tu ya bajeti ya Serikali kwa ajili ya sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Kamati inaishauri Serikali kuongeza uwekezaji katika kilimo angalau kufikia Azimio la Maputo, ambalo linazitaka nchi wanachama kutenga **asilimia 10%** ya bajeti ya Serikali kwa ajili ya Kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** endapo pendekezo hili litatekelezwa itasaidia kuwa na uhakika wa usalama wa chakula, kuongeza ajira, maligafi kwa ajili ya viwanda, kuongeza pato na ustawi wa wakulima, lakini pia kuongeza pato la Taifa kwa ujumla na hivyo kuchangia ukuaji wa uchumi wa Taifa.

## 2) MTIRIRIKO WA FEDHA ZA MIRADI YA MAENDELEO USIORIDHISHA

**Mheshimiwa Spika,** upo udhaifu mkubwa katika kutoa fedha za maendeleo zinazokuwa zimetengwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**Mheshimiwa Spika**, mtiririko wa fedha usioridhisha umekuwa ukiathiri kwa kiasi kikubwa ufanisi katika utekelezaji wa miradi hiyo na kuifanya Serikali na wananchi kwa ujumla kutokupata matokeo yaliyotarajiwa. Kwa mfano; kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017 Fungu 43 ilipelekewa **asilimia 3.31%** na Fungu 99 ilipelekewa **asilimia 8 %** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Mwenendo huu unaashiria kwamba:-

- Kilimo si moja ya vipaumbele vya Serikali;
- Serikali haitambui umuhimu wa sekta za kilimo katika ustawi wa sekta zingine; na
- Kilimo si sekta mama ya ustawi wa wananchi ambao wengi wanajihusisha na shughuli za kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuimairisha utoaji fedha kwa ajili ya sekta za kilimo kama zinavyoidhinishwa na Bunge.

## 3) MFUMO WA UNUNUZI WA MBOLEA KWA PAMOJA (*FERTILIZER BULK PROCUREMENT*)

**Mheshimiwa Spika,** Sera ya Kilimo ya Taifa ya mwaka 2013 inaelezea umuhimu wa kuongeza matumizi ya mbembejeo za kisasa (mbolea, madawa ya kilimo, mbegu bora na zana za kilimo) kama mhimili imara wa kuongeza tija na uzalishaji wa mazao; kupunguza umaskini; na kuwa na usalama wa chakula na lishe. Kwa kuzingatia umuhimu huu, Serikali imekuwa ikichukua hatua mbalimbali za kuwezesha upatikanaji wa pembejeo hapa nchini. Hata hivyo, suala la upatikanaji wa pembejeo za kilimo, bei kubwa, usambazaji wa matumizi yasiyo sahihi bado ni tatizo. Upatikanaji wa

Mbolea, Mbegu Bora pamoja na Madawa ya Viatilifu hayakidhi mahitaji.

**Mheshimiwa Spika**, maelezo hayo yanajihidhihirisha kwenye taarifa ya Benki ya Dunia inayoeleza kuwa, ili kuwa na kilimo chenya tija, wastani wa matumizi ya mbolea ni kilo **119.9** kwa **hekta**. Hapa nchini matumizi ya mbolea ni wastani wa **kilo 10** za mbolea kwa **hekta moja**, kiwango hiki ni chini sana ya viwango stahiki.

**Mheshimiwa Spika,** matumizi hayo kidogo ya mbolea hapa nchini yanasababishwa na bei kubwa ya mbolea. Ili kuongeza matumizi ya mbolea na kuhamasisha wakulima wengi zaidi kutumia mbolea, Serikali inatarajia kuanzisha mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja (*Fertilizer Bulk Procurement*), mfumo ambao una lengo la kuwawezesha wakulima wadogo kupata mbolea yenye ubora na kwa bei nafuu.

**Mheshimiwa Spika,** mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja haufuati taratibu za Sheria ya Manunuzi ya Umma kwa sababu mbolea itakayoagizwa au kutengenezwa itagharamiwa na kampuni binafsi. Aidha, kwa kuanzia mfumo huu utanza kwa mbolea za aina mbili ambazo ni mbolea ya kupandia (DAP) na mbolea ya kukuzia (UREA) na endapo mfumo huu utaonyesha mafanikiao itaongeza mbolea zingine.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia faida zinazotarajiwa kupatikana na kwa kuwa mfumo huu utaanza kutumika mara ya kwanza hapa nchini, Kamati ina maoni na ushauri ufuatao kwa Serikali:-

(a) Wizara iendelee na taratibu za kuanzishwa na kutekeleza mfumo wa ununuzi wa mbolea kwa pamoja;

(b) Wizara iongeze timu ya wataalamu mbalimbali ili Serikali iweze kuchukua tahadhari na mapungufu yote yanayoweza kutokea na hivyo Taifa kushindwa kunufaika na mfumo huu; na

(c) Serikali iwezeshe na kushirikisha sekta binafsi katika uanzishwaji wa viwanda vya kuzalisha mbolea ili kuwezesha uzalishaji wa mbolea hapa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na ushauri huo Kamati inatoa angalizo kwa Serikali kuwa uagizaji huo ni lazima uzingatie mahitaji halisi ya udongo wa kila eneo na aina ya mazao. Kwa mfano, mbolea ya UREA inaweza ikaongezewa virUtubisho maalum ambavyo vinakosekana katika udongo wa eneo flani ili kuongeza uzalishaji na wakati huo huo udongo wa aina ingine na mahali pengine unaweza ukahitaji aina ile ile ya UREA isiyo na virutubisho.

**Mheshimiwa Spika,** hii inamaanisha kwamba kama Serikali itaagiza mbolea ya UREA ya aina moja pekee ni dhahiri kuwa mkulima ambaye udogo wake utahitaji UREA yenye virutubisho maalum hatakuwa na tija.

**4) KUKAMILISHA MIRADI INAYOENDELEA KABLA YA KUANZA KUTEKELEZWA KWA MIRADI MIPYA**

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla miradi mbalimbali ya maendeleo inayoombewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 ni muendelezo wa utekelezaji wa miradi ya Mwaka wa Fedha 2016/2017 pamoja na miradi michache mipya iliyoibuliwa katika Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika,** sababu kubwa ya kuendelea na miradi ya Mwaka wa Fedha unaomalizika 2016/2017 ni kutokamilika utekelezaji wa miradi hiyo kwa wakati uliopangwa. Kutokamilika kwa miradi hii pamoja na athari zingine kunaongeza gharama za utekelezaji miradi kutokana na kupanda kwa bei ya gharama za manunuzi ya vifaa vya mradi pamoja na uchakavu wa sehemu za miradi iliyokwishatekelezwa.

**Mheshimiwa Spika,** kufuatia hali hiyo Kamati inaishauri Serikali kukamilisha miradi iliyopo kabla ya kuanzisha miradi mipya. Ushauri huu ukitekelezwa utasaidia kupunguza mzigo kwa Serikali wa kuwa na miradi mingi isiyokamilika.

## 5) MIKOPO YENYE RIBA NAFUU ITAKAYOONGEZA TIJA KATIKA SEKTA ZA KILIMO

**Mheshimiwa Spika,** Kilimo kinaajiri **asilimia 75%** ya watanzania, vilevile kilimo kinaweza kuchangia upatikanaji wa chakula kwa zaidi ya asilimia 100 ya chakula nchini

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na umuhimu huo wa kilimo, wakulima wengi wanakabiliwa na changamoto ya kutomudu gharama za ujenzi wa miundombinu na teknolojia za kisasa katika shughuli za kilimo, ufugaji na uvuvi kwa sababu ya kukosa mikopo yenye riba nafuu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mfano taarifa ya *Food and Agriculture Organization* (FAO) inaeleza kuwa wakulima wanaopata mikopo nchini ni chini ya **asilimia 2%.** Hali hii ni kikwazo katika kufikia uzalishaji wa kilimo chenye tija. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kuimarisha Benki ya Kilimo Tanzania kwa kuiongezea mtaji na kurahisisha taratibu na masharti ya ukopaji ili yawe rafiki kwa wakulima walio wengi.

## 6) KERO YA MUINGILIANO WA SHUGHULI ZINAZOFANYWA NA TAASISI ZA UDHIBITI

**Mheshimiwa Spika,** kuna malalmiko ya wadau wa kilimo, hususan sekta binafsi, kuhusu uwepo wa utiriri wa kodi zinazotozwa na taasisi mbalimbali za udhibiti, na hivyo kupelekea urasimu na usumbufu usiokuwa wa lazima. Kamati inaishauri Serikali kufanya tathimini ili kubaini mwiingiliano wa majukumu katika taasisi za udhibiti na kubaini mwiingiliano uliopo ili kuepusha usumbufu uliopo.

## 7) KUKABILIANA NA MIGOGORO YA ARDHI

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imekua ikichukua hatua kukabiliana na migogoro ya ardhi baina ya watumiaji mbalimbali. Pamoja na hatua hizo bado vipo viashiria vya kuendelea kuwepo migogoro katika maeneo mbalimbali nchini. Kwa ujumla, migogoro ya ardhi imekuwa ikiathiri sana uwekezaji katika kilimo na sekta nyingine za kiuchumi. Kamati inashauri Serikali iongeze kasi ya kupima na kumilikisha ardhi

sanjari na kuharakisha uwepo wa Sheria ya ardhi ya Kilimo na ufugaji ili kulinda ardhi ya kilimo na mifugo.

**8) UMUHIMU WA UJENZI WA MAGHALA KWA AJILI YA HIFADHI YA NAFAKA NA USALAMA WA CHAKULA**

**Mheshimiwa Spika,** maghala ya kisasa ni muhimu katika kuhakikisha usalama wa chakula. Hifadhi ya nafaka huongeza bei kwa asilimia **80%** ukilinganisha na bei wakati wa mavuno. Adha, uhifadhi duni huchangia sumu ya *Aflatoxin* na kuhatarisha usalama wa chakula kwa walaji na hasara kwa wakulima. Kamati inaishauri Serikali kupanga na kutekeleza mikakati ya kujenga na kukarabati maghala ili kuwa na uhakika na usalama wa hifadhi ya nafaka kabla ya kuwafikia walaji. Sambamba na hilo, Kamati inaitaka Serikali kutekeleza kwa vitendo mfumo wa stakabadhi ghalani pamoja na kuwaelewesha wakulima umuhimu wa mfumo huu.

**9) UDHIBITI WA UVUVI HARAMU**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na Wizara kupitia Idara ya Maendeleo ya Uvuvi kuendelea kuchukua hatua mbalimbali kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu, bado vitendo hivyo vimeendelea kushamiri mahali pengi nchini na kusababisha athari kubwa katika ekolojia ya maeneo ya uvuvi**.** Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kukabiliana na uvuvi haramu ikiwa ni pamoja na kuwezesha upatikanaji wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya kufanya doria kwenye maeneo ya maziwa ikiwa ni pamoja na kushirikisha Jeshi la Wananchi katika kufanya doria ili kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu hasa katika kudhibiti uvuvi wa kutumia mabomu.

**10) BAJETI NDOGO YA SEKTA YA MIFUGO ISIYOWIANA NA MCHANGO WA SEKTA HII KATIKA PATO LA TAIFA**

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ina rasilimali kubwa ya mifugo inayojumuisha **ng'ombe milioni 25.8**, mbuzi **milioni 17.1,**

**kondoo milioni 9.2, nguruwe milioni 2.67** na **kuku milioni 42**. Pamoja na takwimu za wingi wa mifugo iliyopo, kwa bajeti ndogo ya Serikali ambayo imekuwa ikitengwa ni dhahiri kwamba haiwezi kuleta kuleta tija katika pato la wafugaji na uchumi wa Taifa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mukutadha huo, Kamati inaishauri Serikali kuwekeza katika miundombinu ya mifugo, kutoa elimu ya ufugaji bora na wa kisasa pamoja na kutengeneza mazingira wezeshi ya uwekezaji na kuhamasisha sekta binafsi kujenga viwanda vya usindikaji nyama, maziwa na ngozi. Ujenzi wa viwanda hivi, vitasaidia kuongeza thamani ya rasilimali hizo.

## 11) KUONGEZA WIGO WA TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeanzisha Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa lengo la kusimamia, kudhibiti na kuhamasisha maendeleo ya ushirika nchini. Mpaka sasa utekelezaji wa majukumu hayo umeonyesha kujikita zaidi katika sekta ya kilimo pekee na kuonyesha mafanikio. Kamati inaishauri Tume ya Ushirika ipanue wigo wa shughuli zake kwa kuanzisha vyama vya ushirika katika sekta za Mifugo na Uvuvi.

## 12) UMUHIMU WA KUTENGA KANDA MAALUM KWA AJILI YA KILIMO CHA UMWAGILIAJI

**Mheshimiwa Spika**, kilimo cha kisasa na chenye tija hakina budi kupewa kipaumbele kwa kuainisha na kutenga kanda maalum za kipaumbele zinazofaa kwa kilimo cha umwagiliaji na kuelekeza fedha katika maeneo hayo. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi ya kujenga skimu za mfano za umwagiliaji kwenye maeneo ambayo yanafaa kwa kilimo cha umwagiliaji, badala ya kuwa na miradi mingi isiyoweza kutekelezwa kwa pamoja.

## 13) KATAZO LA KUUZA CHAKULA NJE YA NCHI.

**Mheshimiwa Spika,** yamekuwepo malalamiko mengi ya

namna ambavyo Serikali imekuwa ikiweka na kuondoa makatazo/zuio la kuuza baadhi ya mazao ya chakula nje ya nchi. Makatazo haya yamekuwa yakikatisha tamaa wazalishaji kwani hawana uhakika wa kurudisha gharama za uzalishaji. Kamati inaishauri Serikali kuunda mamlaka ya usimamizi na udhibiti wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuzi. Hatua hii itaiwezesha Serikali kuwa na takwimu sahihi za uzalishaji na hivyo kuwezesah Serikali kufanya maamuzi sahihi kuhusu mwenendo wa uuzaji mazao hayo ndani na nje ya nchi.

## 6.0 HITIMISHO

**6.1 Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**6.2 Mheshimiwa Spika,** napenda pia kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi Mhe. Charles Tizeba, (Mb) na Naibu Waziri Mhe William Ole Nasha (Mb) pamoja na Wataalamu wote wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa ushirikiano walioipa Kamati wakati Kamati ikichambua na kujadili bajeti ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**6.3 Mheshimiwa Spika**, kwa dhati kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wa Kamati kwa ushirikiano na michango yao walioyoitoa wakati wa kupitia na kuchambua bajeti ya Wizara pamoja na kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake. Naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

| | |
|---|---|
| 1.Mhe. Dkt. Mary Michael Nagu, Mb | Mwenyekiti |
| 2.Mhe. Dkt. Christine G.Ishengoma,Mb | M/Mwenyekiti |
| 3.Mhe. Dkt. Immaculate Sware Semesi, Mb | Mjumbe |
| 4.Mhe. Mahmoud H. Mgimwa, Mb | “ |
| 5.Mhe. Salum Mwinyi Rehani, Mb | “ |
| 6.Mhe. Khadija Hassan Abood, Mb | “ |
| 7.Mhe. Marwa Ryoba Chacha, Mb | “ |
| 8.Mhe. Mashimba Mashauri Ndaki, Mb | “ |

9.Mhe. Matter Ali Salum, Mb "
10.Mhe. John John Mnyika, Mb "
11.Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb "
12.Mhe. James Kinyasi Millya, Mb "
13.Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb "
14.Mhe. Pascal Yohana Haonga, Mb "
15.Mhe. Salim Mbaraku Bawazir Mb "
16.Mhe. Deo Kasenyenda Sanga, Mb "
17.Mhe. Abdallah Hamis Ulega, Mb "
18.Mhe. Haji Ameir Haji, Mb "
19.Mhe. Daniel N. Nsanzugwanko, Mb "
20.Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb "
21.Mhe. Upendo Furaha Peneza, Mb "
22.Mhe. Emmanuel Papian John, Mb "
23.Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb "
24.Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb "

**6.4 Mheshimiwa Spika,** mwisho napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Dkt, Thomas Kashililah pamoja na Sekreterieti ya Kamati ambao ni Ndg. Rachel Nyega , Ndg. Martha Chassama , Ndg. Virgil Mtui na Ndg Mwimbe John kwa kuihudumia Kamati pamoja na kukamilisha taarifa hii kwa wakati.

**6.5 Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naliomba sasa Bunge lako lipokee, lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumiziya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

**6.6 Mheshimiwa Spika**, naunga mkono hoja iliyowasilishwa na mtoa hoja muda mfupi uliopita na naomba kuwasilisha.

Dkt. Mary Michael Nagu, (Mb)
**MWENYEKITI,**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA KILIMO,**
**MIFUGO NA MAJI**
**19 MEI, 2017**

**NAIBU SPIKA:** Sasa nitamwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

**MHE. CECILIA D. PARESSO - K.n.y MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA WIZARA YA KILIMO,MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani naomba kuwasilisha hotuba ya Msemaji Mkuu wa Upinzani Bungeni kwa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa heshima kubwa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili na kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2016/2017 pamoja na Makadirio ya Mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo, mifugo na uvuvi ni sekta muhimu sana kwa uchumi na maendeleo ya nchi na Watanzania kwa ujumla. Sekta hizi zimeendelea kutoa mchango mkubwa ikiwemo kuwa chanzo cha kipato kwa zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania, kuhakikisha usalama wa chakula, kuchangia Pato la Taifa kwa zaidi ya asilimia 28 na mauzo ya nje kwa zaidi ya asilimia 24.

Mheshimiwa Naibu Spika, japo sekta hizi ni muhimu ila zinakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinaathiri ukuaji wake. Changamoto hizo zinajumuisha utengaji na utoaji mdogo wa fedha za bajeti ya maendeleo; upungufu mkubwa wa maafisa ugani, watalaam na watafiti, miundombinu duni ikiwemo ya utoaji wa taarifa za tahadhari na upungufu wa viwanda vya kuchakata bidhaa zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, athari za mabadiliko ya tabia nchi zinaongeza changamoto hizo ikiwemo kuongezeka kwa ukame na magonjwa ya mimea na mifugo, mvua zisizotabirika, kuingia kwa maji ya chumvi katika mashamba na vyanzo vya maji baridi, mafuriko na uharibifu

wa mashamba na miundombinu ya kilimo, ufugaji na uvuvi ikiwemo mazalia ya samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonesha kuwa kwa mwaka 2015 ukuaji wa shughuli za kilimo umepungua na kufika asilimia 2.3 kutoka asilimia 3.4 kwa mwaka 2014. Pia kiwango hicho ni kidogo kwa wastani wa ukuaji wa asilimia 3.2 kwa kipindi cha mwaka 2010 - 2013. Mwenendo huu ni mdogo sana ukilinganisha na shabaha ya asilimia sita iliyoweka nchini chini ya MKUKUTA II na kuelekezwa na *CAADP* na *TAFSIP.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imependa tathmini iliyofanywa na taasisi za wadau wa kilimo kwa mwenendo wa bajeti ya Wizara za Kilimo, Mifugo na Uvuvi kwa kipindi cha miaka kumi iliyopita (2007/2008 – 2016/2017) na kuona kuwa siyo wakuridhisha japokuwa Sekta hizi kutoa mchango mkubwa sana kwa Taifa. Takwimu zinaonesha kuwa wastani wa bajeti za Wizara za sekta hizo kwa kipindi hicho ni 2.2 tu ya bajeti ya Taifa. Kiwango hiki ni kidogo sana ukilinganisha na lengo la kufika asilimia 10 kama Serikali ilivyoridhia katika Azimio la Malabo. Kwa kipindi cha miaka mitano ya kwanza (2007/2008 – 2011/2012) wastani ulikuwa ni asilimia 2.7 tu, wakati kwa kipindi cha miaka mitano ya mwisho (2012/2013 – 2016/2017) wastani ulikuwa ni asilimia 1.8 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kilimo na Ushirika - Fungu 43 imepata wastani wa shilingi bilioni 250 ambayo ni sawa na asilimia 1.8 ya bajeti ya taifa kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 hadi 2016/2017. Kati ya wastani huo, bajeti ya maendeleo ilipata wastani wa shilingi bilioni 80.3 ambayo ni sawa na asilimia 32 tu ya bajeti ya kilimo na ushirika na ni sawa na asilimia 1.6 ya bajeti ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mifugo na Uvuvi imepata wastani wa shilingi bilioni 57.1 ambayo ni sawa na asilimia 0.4 tu ya bajeti ya Taifa kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 hadi 2016/2017. Kati ya wastani huo, bajeti ya maendeleo ilipata wastani wa shilingi bilioni 20.7 ambayo ni sawa na

asilimia 36 tu ya bajeti ya Mifugo na Uvuvi sawa na asilimia 0.4 ya bajeti ya maendeleo ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kama kweli kauli mbiu ya Tanzania ya viwanda kuwa na uhalisia inabidi kuongeza bajeti kwa sekta nzima ya kilimo kinyume na hapo kauli mbiu hiyo itaendelea kuwa kwenye vyombo vya habari tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani imeanza kwa utangulizi huo kwa kupitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/2017, sehemu ya kilimo kifungu cha 3.2.3.3 kinaonesha kuwa lengo ni kuhakikisha uwepo wa chakula cha kutosha na upatikanaji wa uhakika wa malighafi za uzalishaji katika viwanda vya mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Lengo hilo ni zuri lakini halina kipimo yaani *indicators* ambacho Waheshimiwa Wabunge wanaweza kukitumia wakati wa kukagua miradi ambayo inakuwa imetengewa fedha kwenye bajeti. Hoja ya msingi ni mpango lazima uoneshe wazi wazi kazi itakayofanyika kulingana na fedha iliyopangwa, kinyume cha hapo ni kutoa mwanya wa matumizi mabaya ya fedha za walipakodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kama inataka matumizi yanayofanyika yaendane na thamani ya fedha ni muda mwafaka sasa mipango iwe wazi ili Waheshimiwa Wabunge watoe ushauri unaoendana na hali halisi ya mipango husika. Mfano mzuri ni hizi skimu za umwagiliaji ambazo miaka yote inawekwa kwenye bajeti lakini ni nani anayefahamu kwa uhakika kuwa ni kiasi kilichotengwa ndicho kilichotengeneza kwa kiwango kinachoonekana kwa skimu husika kwa mwaka huo wa bajeti *(value for money)?*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapungufu hayo pia yanajitokeza kwenye mpango wa miaka mitano, kwani mpango huo hauoneshi kwa kipindi cha kila mwaka Serikali itakuwa imetekeleza nini ili ipimwe kwa mpango wake huo badala yake inataka kupimwa kwa kipindi chote hadi

mwaka 2020, wakati bajeti inapitishwa kila mwaka. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba haya ni mapungufu makubwa ya Serikali na hivyo basi kutoa mwanya wa kupimwa na kukosolewa kwa utendaji kazi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu migogoro ya rasilimali ardhi kati ya wakulima na wafugaji; Tanzania inakabiliwa na migogoro mikubwa kati ya watumiaji wa ardhi, migogoro hii inatokana na ukweli kwamba idadi ya watumiaji inaongezeka kwa kasi kubwa wakati eneo la ardhi ni lile lile. Katika kutambua suala hili, Waheshimiwa Wabunge katika Bunge la Kumi baada ya kutokea migogoro na mauaji baina ya watumiaji wa ardhi, Bunge lililazimia kuunda Kamati Teule ya Bunge. Kwa muktadha huu wa hotuba hii ya Kambi Rasmi tumefanya marejeo baadhi ya mapendekezo yaliyotolewa na kamati teule ya Bunge kama ambavyo inaonekana katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kamati ilibaini kuwa zaidi ya asilimia 25 ya eneo la nchi ni hifadhi, hivyo Bunge liliazimia Serikali kutekeleza mambo yafuatayo:-

(i) Kuyaachia mapori ya Serikali ambayo yamekosa sifa ili yatumike kwa kilimo na ufugaji kwa kuzingatia mpango wa matumizi bora ya ardhi.

(ii) Migogoro wanayokumbana nayo wafugaji kutokana na kuingiza mifugo kwenye maeneo ya hifadhi pamoja na kero nyingine inatokana na kukosekana kwa miundombinu sahihi na endelevu kwa ajili ya ustawi wa mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa mrejesho maazimio tajwa hapo juu yametekelezwa kwa kiwango gani hadi sasa kwani migogoro baina ya wafugaji, wakulima na hifadhi imekuwa ikiendelea na wananchi wamepoteza mali zao na wengine kupoteza uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani

inaitaka Serikali kurejea tena sera na sheria zinazohusu matumizi ya raslimali ardhi, kwani wakati zinatungwa idadi ya watumiaji wa raslimali hiyo hawakuwa kama ilivyo kwa sasa. Tuangalie idadi ya Watanzania kwa sasa na miaka 50 au 100 ijayo watakuwa wangapi, idadi ya mifugo na idadi ya watumiaji wengine wa rasilimali hii ya ardhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya upatikanaji wa chakula; katika kipindi cha mwaka 2015/2016 Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula uliendelea na ununuzi wa nafaka katika kanda ya Songea, Makambako na Sumbawanga ambako kulikua na uzalishaji wa ziada. Wakati wa kuanza mwaka tarehe 1 Julai, 2015 *NFRA* ilikuwa na tani 353,702.25 za nafaka. Hadi kufikia tarehe 14 Aprili, 2016 ilikuwa imenunua tani 22,335 na kufanya akiba katika maghala yake kufikia tani elfu 65, ambapo mahindi ni tani 61, mpunga ni tani 3,939 na mtama ni tani 19,890. Akiba hii imeiwezesha Serikali kukabiliana na uhaba wa chakula na maafa hususan mafuriko yaliyojitokeza nchini katika sehemu mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya utekelezaji ya Wizara inaonesha takwimu za uzalishaji wa mazao ya chakula nchini kwa msimu wa 2015/2016 na upatikanaji wa chakula 2016/2017 kuwa ni tani 16,172,841 zikilinganishwa na tani 15,528,820 za msimu wa 2014/2015, kati ya tani hizo nafaka zilikuwa ni tani 9,457,108 na mazao yasiyokuwa ya nafaka tani 6,715,733.

Aidha, takwimu zinaonesha kuwa mahitaji ya chakula kwa msimu wa mwaka 2016/2017 ni tani 13,159,326, kati ya hizo mahitaji ya nafaka yalikuwa ni tani 8,355,767 na tani 4,803,560 isiyo nafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taarifa hiyo inaonesha kuwepo kwa ziada ya chakula ya tani 3,013,515 na hivyo taifa kuwa na utoshelevu kwa asilimia 123 ikilinganishwa na asilimia 120 kwa mwaka 2015/2016. Palepale tunaambiwa pamoja na uzalishaji wa ziada Halmashauri 55 zilikuwa na ukosefu wa chakula na jumla ya watu 1,186,028 walikuwa na mahitaji ya jumla ya tani 35,491. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa maelezo yanatakiwa kutolewa na Serikali kuhusu takwimu hizo za ziada ya tani 3,013,515, inawezekanaje Halmashauri 55 zikawa na upungufu wa chakula? Na kama kuna ziada ya nafaka tani 1,101,341 inakuwaje bei ya mahindi inazidi kupanda kila siku? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa ripoti ya utafiti iliyotolewa na taasisi ya TWAWEZA ya Machi, 2017 inaonesha kuwa hali ya upungufu wa chakula imeonekana kuwa mbaya zaidi katika miezi ya hivi karibuni. Hii inajidhihirisha pale ambapo kaya zilizoripoti kupata hofu ya kukosa chakula zilipanda kutoka asilimia 45 hadi asilimia 65 kati ya Septemba, 2016 na Februari, 2017. Vivyo hivyo, idadi ya kaya zilizopungukiwa na chakula ziliongezeka kutoka asilimia 43 mwezi Septemba, 2016 hadi asilimia 51 mwezi Februari, 2017. Kaya ambazo zilikuwa na angalau mtu mmoja aliyeshinda siku nzima bila kula nazo ziliongezeka kutoka asilimia 21 hadi asilimia 35 katika kipindi hicho hicho. Upungufu huu wa chakula umesababishwa kwa kiasi fulani na umasikini wa kipato unaofanya kaya maskini ziwe katika hali tete.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zilizotolewa na Benki Kuu ya Tanzania *(Monthly Economic Review)* ya mwezi Januari, 2017 zinaonesha kwamba bei ya mahindi imepanda kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha miaka miwili iliyopita. Habari zilizoelezwa na wananchi ni kwamba upungufu wa chakula ni tatizo kubwa kwa sasa na hii ilijidhihirisha pale ambapo wahojiwa wengi wa Sauti za Wananchi (asilimia 78) waliripoti upungufu wa chakula katika maeneno waliyokuwa wakiishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Wizara ya Kilimo na vitengo vyake kuhakikisha kwamba Watanzania kwa ujumla wao muda wote wanakuwa na uhakika wa kupata chakula, mengine yanafuatia. Hivyo basi kitendo cha Watanzania kukosa chakula ni dalili kwamba kuna mapungufu ya kiutendaji sehemu fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya tabianchi yana madhara ya moja kwa moja kwa kilimo, mifugo na uvuvi na wahusika wakubwa katika sekta hii ni wananchi wa hali ya chini na ya kati.

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya tabianchi yanaonekana dhahiri nchini Tanzania ambapo uzalishaji wa kilimo unatishiwa na hali ya hewa na mabadiliko ya tabianchi kutokana na matukio kama mafuriko na ukame. Mabadiliko ya tabianchi ni tishio kubwa zaidi la kimazingira kwa maisha hapa duniani linaloathiri mazingira yetu si tu kiuchumi, lakini pia kijamii na kitamaduni. Tanzania imekuwa ikikabiliwa na vipindi vya ukame vinavyotokea mara kwa mara ambavyo vimeathiri shughuli za kilimo na kusababisha uhaba wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika jumla ya kazi 142 zinazotarajiwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni kazi 12 tu ndio zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi. Kazi hizi zimechukua jumla ya shilingi bilioni 25.5 ambayo ni sawa na asilimia 17 tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya kazi 12 zilizoainishwa kuwa na uhusiano na mabadiliko ya tabianchi ni kazi moja tu ndiyo ina kiwango cha juu cha uhusiano wakati kazi kumi na moja zina kiwango cha chini na hakuna hata moja yenye kiwango cha kati.

Maudhui yake katika mabadiliko ya tabinchi ni kupunguza, kukabiliana na vyote viwili. Pia uchambuzi unaonesha kuwa kati ya kazi 12 zilizoainishwa kuwa na uhusiano na mabadiliko ya tabianchi kazi tisa zina maudhui ya kukabiliana na kazi tatu zina maudhui ya vyote viwili na hakuna kazi yoyote yenye maudhui ya kupunguza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mifugo jumla ya kazi 27 zinazotegemewa kutekelezwa, ni kazi tisa tu ndio zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi. Kazi hizi zimechukua jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 1.4 ambayo ni sawa na asilimia 36.

Mheshimiwa Naibu Spika, kati ya jumla ya kazi 23 za Wizara kwa Fungu 64 zinazotegemewa kutekelezwa, ni kazi tano tu ndizo zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi. Kazi hizi zimechukua jumla ya kiasi cha shilingi bilioni 1.5 ambayo ni sawa na asilimia 19 tu ya fungu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema hii ni hatari kwa maendeleo ya nchi yetu na sekta nzima ya uzalishaji kwani kila uzalishaji unategemea mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali na vyombo vyake ina wajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo ambao ndio wazalishaji wakuu wanapatiwa taaluma ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi mashambani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tafiti zinaonesha kwamba wakulima wadogo bado wanalima bila ya kufuata sera za sekta mbalimbali kinachozingatia mabadiliko ya tabia nchi. Maana yake ni kwamba dhana nzima ya kilimo na ufugaji unaozingatia mabadiliko ya tabianchi bado ni dhana mpya katika mipango yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kwamba sasa ni muda mwafaka, japokuwa tumechelewa kama nchi kuwahamasisha wakulima wadogo kujihusisha na kilimo kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi na kuwe na programu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika jamii. Ili kufikia lengo hilo ni lazima kuongeza motisha na vichocheo miongoni mwa wadau wa mabadiliko ya tabianchi nchini kushirikishana na kuchangia uzoefu wao katika mchakato wa kutayarisha Programu za Maendeleo ya Kilimo *(DADPs)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa mbegu na mbolea; tangu mwaka 2009 Serikali imekuwa na miradi kadhaa iliyozinduliwa ili kufanya mapinduzi katika kilimo kwa kuhimiza uwekezaji binafsi katika kilimo. Programu kadhaa zilinduliwa ambazo ni; programu ya *SAGCOT* mwaka 2010, Jukwaa la Kilimo Afrika, Mpango wa Uwekezaji wa Kilimo na Usalama wa Chakula Tanzania, Mpango wa Taifa

wa Uwekezaji Tanzania; Matokeo Mkubwa Sasa na kuanza kwa utekelezaji wa Mfuko wa Kuchochea Kilimo wa *SAGCOT* mwaka 2014.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapinduzi hayo yote kiini chake ni kuhakikisha wakulima wanatumia mbegu bora na mbolea sahihi katika uzalishaji. Programu hizo tajwa zimekuja na makampuni ya kimataifa ya mbegu kuingia kwa nguvu kubwa kwenye soko la pembejeo, yakilenga mbegu zenye faida kibiashara ambayo ilitegemea kwa sehemu kubwa mbegu zinazoagizwa kutoka nje ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, makampuni makubwa ya kimataifa huelekeza rasilimali zao na muda wao kwenye mazao machache yanayoweza kuwapatia faida kubwa. Masoko madogo kwa ajili ya mbegu za kienyeji au zile ambazo zimebadilishwa kwa kawaida hayahudumiwi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona ni muhimu sasa kuhakikisha mbegu zetu za asili zinalindwa na ili zisije zikapotea kabisa na hivyo kupoteza urithi wetu wa mbegu za asili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mbegu kwa ajili ya kilimo hupatikana kutokana na mifumo wa ugavi rasmi na isiyo rasmi. Asilimia 90 hutokana na mfumo wa mbegu unaosimamiwa na mkulima wakati asilimia 10 hutokana na sekta rasmi ya mbegu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya mbegu ya mwaka 2003 haitambui kwa uwazi mifumo ya mbegu inayosimamiwa na wakulima na aina za mbegu za kienyeji na haisemi chochote kuhusu haki za wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta rasmi ya mbegu nchini Tanzania husambaza kiasi kidogo sana cha mbegu bora kwa wakulima nchini Tanzania (takribani asilimia 4 hadi 10) lakini bado ndiyo inayopata uungwaji mkono mkubwa wa Serikali, fedha na taratibu za udhibiti huku mifumo ya mbegu inayosimamiwa na wakulima ambayo hutoa asilimia 90, inabaki kutotambuliwa na haipati msaada. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti uliofanywa na *ACB* mwaka 2014 huko Morogoro na Mvomero uligundua kwamba zaidi ya asilimia 80 ya mbegu za asili za mahindi, mazao aina ya kunde na mpunga zinazotumika na wakulima hazijathibitishwa na wakulima wengi huendelea kutumia kwa kurudia mbegu zinazotokana na mavuno ya msimu uliopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya utekelezaji ya Wizara inaonesha kuwa makadirio ya mahitaji ya mbegu kwa mwaka ni tani 60,000 za mbegu bora. Aidha, Randama inaonesha kuwa Wakala wa Mbegu za Kilimo umeongeza uzalishaji wa mbegu bora za nafaka na mikunde toka tani 2,804 msimu wa 2015/2016 hadi tani 2,884 msimu wa 2016/2017. Uzalishaji wa ndani wa mbegu ni sawa na asilimia 4.81 tu ya mahitaji ya mbegu kwa nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, maana yake ni kwamba asilimia 95.19 ya mahitaji ya mbegu kwa mwaka zinaingizwa na makampuni yanayojihusisha na mbegu kutoka nje ya nchi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ijitafakari kuhusiana na hali hii ya mbegu kwa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa usambazaji wa mbegu uzingatie na uende sambamba na aina ya mbegu ambazo zinazingatia aina ya hali ya hewa na hali ya udongo katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa mbolea, takwimu za Serikali zinaonesha kuwa mahitaji ya mbolea kwa mwaka ni tani 485,000. Aidha takwimu zinaonesha kuwa hadi mwezi Machi, 2017 tani 297,000 ziliingizwa nchini na tani 140,000 zilitolewa(ziliuzwa) nje ya nchi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona hapa kuna tatizo kubwa katika utendaji wa Serikali. Kama mahitaji yetu ni makubwa na hayatimizwi lakini bado tunatoa mbolea ndani na kupeleka nje ya nchi, je, tatizo ni aina ya mbolea inayopelekwa nje haina ubora unaotakiwa kwa wakulima wetu? Kama ndivyo ni kwa nini uzalishaji unakuwa upo chini ya viwango kukidhi matakwa ya wakulima kwa kilimo chetu?

Mheshimiwa Naibu Spika, moja ya changamoto kubwa inayoikabili sekta ndogo ya mbolea ni mfumo wa usambazaji ambao hauna uhakika kuendana na mahitaji ya wakulima kulingana na misimu ya kilimo na hivyo mbolea inapofikishwa kwa wakulima muda stahiki wa matumizi unakuwa tayari umeishapita.

Mheshimiwa Naibu Spika, ruzuku ya mbolea imekuwa ni kichaka kikubwa cha wizi wa fedha za Serikali kwa muda mrefu, lakini kilimo hakioneshi kuwa kinakua. Kwa msimu wa kilimo 2015/2016 Serikali ilitoa vocha za ruzuku 2,999,778 kwa wakulima 999,993 zenye thamani ya shilingi bilioni 78.1 au dola za Marekani milioni 36.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa ruzuku kwa njia moja au nyingine unavunja nguvu mfumo wa kibiashara wa mbolea, na kwa kuwa mfumo wa usambazaji wa mbolea ni shida, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuuimarisha mfumo wa kibiashara ili muda wote wa mwaka mbolea iwepo dukani. Ni dhahiri wakulima si kama hawana uwezo wa kununua mbolea, bali wanachohitaji ni upatikanaji wa uhakika wa mbolea katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu tathmini ya utekelezaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Kwanza *(ASDP-I);* hii ni programu ya miaka 15 inayotekelezwa kwa awamu. Awamu ya kwanza ilikuwa ni ya miaka saba ilianza mwaka wa fedha 2006/2007 – 2012/ 2013 na ilimalizika mwezi wa Juni 2013. *ASDP-I* ililenga kukuza kilimo kufikia asilimia 6 kwa mwaka na hivyo kilimo kwa wakulima wadogo kuwa na tija zaidi katika mazingira ya ushindani kibiashara. Programu nzima ilitarajiwa kutumia jumla ya USD milioni 315.6. Hadi programu inamalizika Serikali na wachangiaji wengine walitoa jumla ya USD milioni 146.5 na kubakiza USD milioni 64.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfuko wa hiyo programu unasaidia miradi ya kitaifa kwa matumizi ya programu za sekta ya kilimo zilizo chini ya Wizara ya Kilimo, shughuli zilizo ngazi ya wilaya na vijiji zinazosaidiwa chini ya mfumo wa

*Local Government Deveolopment Grant* uliokuwa unaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa programu hii ya awamu ya kwanza mafanikio yapo, lakini pia mapungufu yapo. Moja wapo ya mapungufu ni kuchelewa kutolewa kwa fedha katika utekelezaji wa miradi na hivyo kusababisha gharama za utekelezaji wa miradi kupanda. Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kwamba dhana nzima ya umiliki katika miradi ya *DADPs* inayotekelezwa katika ngazi za Wilaya kushuka chini. Uelimishaji wananchi unatakiwa kuwa mkubwa sana katika awamu ya pili ya *ASDP* ili kutimiza malengo ya miradi inayoibuliwa na wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta ya mifugo ni muhimu sana kwani ina mchango wa asilimia 4.4 kwa Pato la Taifa. Pia inahudumia takribani asilimia 10 ya Watanzania wanaoishi kwa kutegemea mfumo huu wa ufugaji na kutoa ajira kubwa hasa mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2015/2016 idadi ya mifugo nchini ilifika ng'ombe milioni 25.8, mbuzi milioni 17.1 na kondoo milioni 9.2. Pia wapo kuku wa asili milioni 42, kuku wa kisasa milioni 34.5 na nguruwe milioni 2.6. Kwa kipindi hicho uzalishaji wa maziwa ulikuwa ni lita bilioni 2.1. Aidha, usindikaji wa maziwa ulikuwa ni lita 167,620. Pia uzalishaji wa mitamba katika kipindi hicho ulifikia mitamba 11,449. Kati ya mitamba hiyo 646 ilizalishwa kutoka mashamba ya Serikali na Ranchi za Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, *VAT* kwenye mazao ya mifugo inabidi kuondolewa kwani kodi hii inafanya vyakula vya mifugo kuwa ghali sana na inalipiwa mara mbili. Wafugaji inawabidi wakati wananunua chakula hicho wanalipa *VAT* wakati tayari watengezaji walikwishalipia wakati wananunua vichanganyio.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukame na vifo vya mifugo; ukame uliopitiliza umeacha majanga makubwa kwa wafugaji katika maeneo mengi ya nchi hii, Kambi Rasmi ya

Upinzani imepata baadhi ya taarifa za wafugaji ambao wamepoteza mifugo yao na wengine kufikia hatua ya kujiua kutokana na hasara walizozipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na ukame huo ulioathiri kwa kiasi kikubwa ufugaji wa kuhamahama lakini kuna matatizo ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iyape kipaumbele kama kweli inathamini mchango wa sekta hii, nayo ni;

(i) Kufanya ushawishi kwa jamii kuhusu maeneo yaliyobainishwa ambayo yanaweza kutengwa kwa ajili ya wafugaji ili kuondoa migogoro ya ardhi iliyopo sasa baina ya wakulima na wafugaji;

(ii) Suala la upigaji chapa mifugo; na

(iii) Kamata kamata ya mifugo na unyanyasaji mkubwa wa wafugaji karibu nchi nzima usitishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa sekta ya uvuvi; Sheria ya Uvuvi Namba 22 ya 2003 ina kasoro na inatia mashaka kama wakati wa kutungwa kwake ulifanyika utafiti wa kina na kuhusisha wadau wote. Sheria hiyo inataka nyavu zote za samaki aina ya dagaa ziwe na upana wa matundu wa 10 mm lakini ukweli ni kwamba dagaa wanaopatikana katika ziwa Tanganyika ni tofauti na Ziwa Nyasa na ni tofauti na Ziwa Victoria na hata wale wa bahari kuu.

Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuifanyia rejea Sheria hiyo ili wavuvi wa dagaa katika Ziwa Victoria wasiendelee kuchomewa nyavu zao za kuvulia dagaa kwa kuwa haziko kwenye viwango vya kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria inataka nyavu za Sangara kuwa na *piece* moja badala ya kuunganishwa hadi *piece* tatu. Kwa kutumia *piece* moja kwa wavu kunawa lazimisha wavuvi kuvua kwenye kina kifupi na hivyo kuharibu mazalia ya samaki tofauti na kama nyavu hizi zingeunganishwa ambapo wavuvi wataweza kuvua katika

maji ya kina kirefu na hivyo kutovuruga mazalia ya samaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, badala ya kutumia nguvu kubwa kuchoma nyavu, Serikali itoe fursa za mikopo kwa wavuvi na kutoa elimu ya ufugaji wa samaki, pia kuweka mpango mzuri wa matumizi ya Ziwa na Bahari. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa unapowachomea wavuvi nyavu na zana nyingine za uvuvi bila kuwapa wavuvi hawa njia mbadala wa kufanya shughuli zao ni kutoondoa tatizo na kusababisha shida kubwa ya maisha kwa watu hawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, wavuvi wanakabiliwa na tozo nyingi sana ambazo zinaathiri kipato chao. Hivyo, basi pamoja na hayo hutozwa kwa kiwango sawa bila kuangalia ukubwa wa mtumbwi. Mitumbwi ukishalipiwa tozo ya leseni, basi itambuliwe mahala popote katika ziwa husika badala ya kuwapa tozo mara mbili mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, sekta ya kilimo kwa muktadha mzima wa sekta nzima ya mazao na visaidizi vyake, sekta ya mifugo pamoja na sekta ya uvuvi ni sekta muhimu sana na ndiyo sekta ambayo kwa upana wake inayotoa ajira nyingi kwa Watanzania wa makundi yote, takwimu za mwaka 2014 sekta inatoa ajira kwa asilimia 66.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wake katika suala zima la kiuchumi, ili Tanzania iweze kutekeleza vyema mpango wake wa pili wa miaka mitano wa maendeleo haina budi kujikita katika kuhakikisha inatoa fedha za maendeleo kwa sekta nzima ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

# HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA UVUVI, MHESHIMIWA DR. SWARE I.SEMESI (MB), KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2016/17 NA MPANGO WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2017/18 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

*Yanatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge, Toleo la Januari, 2016*

---

## I. UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu utekelezaji wa bajeti ya wizara kwa mwaka wa fedha 2016/17 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya wizara kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, aidha, nitoe shukrani kwa Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa kuniamini na kunipa madaraka ya kuwa Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani kwa Wizara hii. Sambamba na hilo ni washukuru viongozi wote wa chama kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu ya kibunge na pia majukumu ya kichama.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa ni kwa familia yangu kwa kunitia moyo na ushirikiano mkubwa wanaonipatia katika kupambana na mazingira magumu ya kisiasa katika mkoa ninakotakiwa kufanyia kazi zangu za kisiasa.

**Mheshimiwa Spika**, Kilimo, Mifugo na Uvuvi ni sekta muhimu sana kwa uchumi na maendeleo ya nchi na Watanzania kiujumla. Sekta hizi zimeendelea kutoa mchango mkubwa ikiwemo kuwa **chanzo cha kipato kwa zaidi ya 65% ya Watanzania, kuhakikisha usalama wa chakula,**

**kuchangia pato la taifa kwa zaidi ya 28% na mauzo ya nje kwa zaidi ya 24%**.

**Mheshimiwa Spika,**Japo sekta hizi ni muhimu ila zinakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo zinaathiri ukuaji wake. Changamoto hizo zinajumuisha: *utengaji na utoaji mdogo wa fedha za bajeti ya maendeleo; upungufu mkubwa wa maafisa ugani, watalaam na watafiti; miundombinu duni* (*ikiwemo ya utoaji wa taarifa za tahadhari);* na *upungufu wa viwanda vya kuchakata bidhaa zake.*

**Mheshimiwa Spika**, Athari za mabadiliko ya tabianchi zinaongeza changamoto hizo ikiwemo: *kuongezeka kwa ukame na magonjwa ya mimea na mifugo; mvua zisizotabirika; kuingia kwa maji ya chumvi katika mashamba na vyanzo vya maji baridi*; *mafuriko* na *uharibifu wa mashamba na miundombinu ya kilimo, ufugaji na uvuvi ikiwemo mazalia ya samaki.*

**Mheshimiwa Spika,** Takwimu zinaonesha kuwa kwa **mwaka 2015** ukuaji wa shughuli za kilimo (*mazao, ufugaji, misitu na uwindaji*) umepungua na kufika **2.3% kutoka 3.4% kwa mwaka 2014. Pia kiwango hicho ni kidogo kwa wastani wa ukuaji wa 3.2% kwa kipindi cha mwaka 2010 - 2013**. **Mwenendo huu ni mdogo sana ukilinganisha na shabaha ya 6%** iliyoweka nchini chini ya **MKUKUTA II** na kuelekezwa na **CAADP** na **TAFSIP**.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani imependa tathmini iliyofanywa na taasisi za wadau wa kilimo kwa mwenendo wa bajeti ya wizara ya(za) kilimo, mifugo na uvuvi kwa kipindi cha **miaka kumi (10) iliyopita (2007/2008 – 2016/2017) na kuona kuwa** si wakuridhisha japokuwa sekta hizi kutoa mchango mkubwa sana kwa taifa. Takwimu zinaonesha kuwa **wastani wa bajeti za wizara za sekta hizo kwa kipindi hicho ni 2.2% tu ya bajeti ya taifa**. Kiwango hiki ni kidogo sana ukilinganisha na lengo la kufika 10% kama Serikali ilivyoridhia katika *'Azimio la Malabo'*. Kwa kipindi cha **miaka mitano ya kwanza (2007/2008 – 2011/2012)** wastani

ulikuwa ni **2.7% tu,** wakati kwa kipindi cha **miaka mitano ya mwisho (2012/2013 – 2016/2017)** wastani ulikuwa ni **1.8% tu**.

- **Kilimo na Ushirika (*Fungu 43*)** imepata wastani wa TZS 250bilioni ambayo ni sawa na 1.8% tu ya bajeti ya taifa kwa kipindi cha mwaka **2007/2008 – 2016/2017**. Kati ya wastani huo, bajeti ya maendeleo ilipata wastani wa **TZS 80.3bilioni** ambayo ni **sawa na 32% tu ya bajeti ya kilimo na ushirika** na **1.6% ya bajeti ya maendeleo taifa**.

- **Mifugo na Uvuvi (*Fungu 99 na 64*)** imepata wastani wa **TZS 57.1bilioni ambayo ni sawa na 0.4% tu ya bajeti ya taifa** kwa kipindi cha mwaka **2007/2008 – 2016/2017**. Kati ya wastani huo, bajeti ya maendeleo ilipata wastani wa **TZS 20.7bilioni** ambayo ni sawa na **36% tu ya bajeti ya mifugo na uvuvi** na **0.4% ya bajeti ya maendeleo taifa**[1].

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali, kama kweli kauli mbiu ya Tanzania ya viwanda kuwa na uhalisia inabidi kuongeza bajeti kwa sekta nzima ya kilimo (mazao, mifugo na uvuvi), kinyume na hapo kauli mbiu hiyo itaendelea kuwa kwenye vyombo vya habari tu.

## II. KILIMO: Fungu 43

### a. Hali ya Kilimo Nchini

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba kama nchi bado tuna mapungufu makubwa kwa jinsi tunavyopanga mipango yetu. Sisi kama wabunge ambao kazi yetu ni kuisimamia na kuishauri Serikali tunaweza kushindwa kutekeleza jukumu hilo la msingi kutokana na ukweli kwamba mipango inayoletwa na Serikali haitupi ni namna gani tuipe ushauri,kwani haina kipimo (target) kwa kila mwaka wa bajeti badala yake ina malengo ya miaka mitano.

______________

[1]Policy Forum, Forum CC, Oxfam na TGNP- Taarifa ya uchambuzi kwa sekta ya kilimo kwa miaka 10

**Mheshimiwa Spika,** kama wabunge tunaendaje kukagua utekelezaji wa miradi bila kuelewa kwa kipindi hicho, utekelezaji wake ulitakiwa kuwa umefikia wapi kwa kulinganisha na fedha zilizotolewa na Bunge?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani imeanza kwa utangulizi huo kwa kupitia Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2016/17, sehemu ya Kilimo kifungu cha 3.2.3.3 kinaonesha kuwa; *"Lengo ni kuhakikisha uwepo wa chakula cha kutosha na upatikanaji wa uhakika wa malighafi za uzalishaji katika viwanda vya mazao ya kilimo,mifugo na uvuvi.*

**Mheshimiwa Spika,** Lengo hilo ni zuri lakini halina kipimo yaani "indicators" ambacho waheshimiwa wabunge wanaweza kukitumia wakati wa kukagua miradi ambayo inakuwa imetengewa fedha kwenye bajeti. Hoja ya msingi ni mpango lazima uoneshe wazi kazi itakayofanyika kulingana na fedha iliyopangwa, kinyume cha hapo ni kutoa mwanya wa matumizi mabaya ya fedha za walipakodi.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kama inataka matumizi yanayofanyika yaendane na thamani ya fedha ni muda mwafaka sasa mipango iwe wazi ili waheshimiwa wabunge watoe ushauri unaoendana na hali halisi ya mipango husika. Mfano mzuri ni hizi skimu za umwagiliaji ambazo miaka yote inawekwa kwenye bajeti lakini ni nani anayefahamu kwa uhakika kuwa kiasi kilichotengwa ndicho kilichotengeneza kwa kiwango kinachoonekana kwa skimu husika kwa mwaka huo wa bajeti? Yaani ***"value for money"***

**Mheshimiwa Spika**, Mapungufu hayo pia yanajitokeza kwenye mpango wa miaka mitano, kwani mpango huo hauoneshi kwa kipindi cha kila mwaka Serikali itakuwa imetekeleza nini ili ipimwe kwa mpango wake huo badala yake inataka kupimwa kwa kipindi chote hadi mwaka 2020, wakati bajeti inapitishwa kila mwaka. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba haya ni mapungufu makubwa ya Serikali na hivyo basi kutoa mwanya wa kupimwa na kukosolewa katika utendaji kazi wake.

**Mheshimiwa Spika,** ukuaji wa Sekta ya Kilimo kwa mwaka 2015 umepungua kufikia asilimia 2.3 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 3.4 katika mwaka 2014 kwa shughuli za kiuchumi za kilimo zinazojumuisha mazao, ufugaji, na uvuvi. Shughuli hizo zimekua na kupungua kwa asilimia 2.2, 2.4, 2.5 na 2.6 mwaka 2015 kwa mfuatano wa sekta tajwa ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 4.0, 2.2, 2.0, na 5.1 ya mwaka 2014.

**b. Migogoro ya Rasilimali Ardhi kati ya Wakulima, Wafugaji na Hifadhi**

**Mheshimiwa Spika**, Tanzania inakabiliwa na migogoro mikubwa kati ya watumiaji wa ardhi, migogoro hii inatokana na ukweli kwamba idadi ya watumiaji inaongezeka kwa kasi kubwa wakati eneo la ardhi ni lile lile. Katika kutambua suala hili, waheshimiwa wabunge katika Bunge la kumi (10) baada ya kutokea migogoro na mauaji baina ya watumiaji wa ardhi na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji, Mheshimiwa Profesa Peter Mahamudu Msolla (Mb),mnamo tarehe 01 Novemba, 2013 akatoa Hoja ya kuundwa kwa Kamati Teule ya Bunge. Kwa hoja hiyo na Bunge lililazimika kuunda Kamati Teule iliyoongozwa na Mhe. Christopher Olenyokie Ole-Sendeka, (Mb) kama Mwenyekiti na wajumbe wengine wanne kati ya watatu ni ni wabunge katika Bunge hili la kumi na moja (11), na iliwasilisha taarifa yake Bungeni tarehe 2 Februari,2015.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha wa hotuba hii ya Kambi Rasmi nitayafanyia marejeo baadhi ya mapendekezo ya taarifa hiyo ambayo ilitoa ufafanuzi wa kina lakini utekelezaji wa maazimio yaliyowekwa bado Serikali imekaa kimya.

**Mheshimiwa Spika**, kamati hiyo ilionesha dhahiri migogoro inapoanzia kuwa ni;

a. Vijiji kutokuwa na Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi;

b. Kutokutengwa kwa Maeneo Mahsusi kwa ajili ya Kilimo na Ufugaji;

c. Kutotengwa kwa maeneo mahsusi kwa ajili ya malisho;

d. Kilimo na Ufugaji wa kuhamahama;

e. Kutambua umuhimu na thamani ya ardhi na kuongezeka kwa mahitaji ya Ardhi kunakosababishwa na:

i. Ongezeko kubwa la idadi ya watu na idadi ya mifugo,

ii. Ongezeko la mahitaji ya maeneo ya shughuli za ufugaji,

iii. Ongezeko la mahitaji ya maeneo ya kilimo,

iv. Upanuzi wa maeneo ya hifadhi za Taifa,

v. kupanuka na kuanzishwa kwa miji mipya,

vi. Ongezeko la vitalu vya uchimbaji madini na uwindaji,

vii. Kupungua kwa ardhi inayofaa kwa uzalishaji kutokana na mabadiliko ya tabia nchi na ukataji hovyo wa miti na uharibifu wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika**, haya yote yapo kwenye sera na sheria mbalimbali za Serikali, lakini kila kimoja kinaona kina haki zaidi ya mwenzie na hapo ndipo tatizo linapozidi kuwa kubwa.

**Mheshimiwa Spika**, mfano mdogo ni pale kati ya maeneo tajwa linapogundulika lina madini na mwekezaji akapatikana ni dhahiri wakaazi katika eneo husika haki zao zinaishia hapo na inawalazimu kuhama, na kama eneo hilo lilikuwa ni nyanda za malisho maana yake wafugaji

wanahamia eneo lingine bila kujali matumizi yake ni ya aina gani. Pia tatizo lingine ni pale Watu wachache kumilikishwa maeneo makubwa ya ardhi na pengine kuanza kuyakodisha kwa wakulima wadogo na wafugaji kwa bei kubwa na hivyo kuzusha migogoro baina ya makundi hayo matatu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Kamati ilibaini kuwa zaidi ya asilimia 25 ya eneo la Nchi ni hifadhi, hivyo Bunge liliazimia Serikali kutekeleza mambo yafuatayo, kwa muktadha wa wizara hii;

i. Kuyaachia mapori ya Serikali ambayo yamekosa sifa, ili yatumike kwa kilimo na ufugaji kwa kuzingatia mpango wa matumizi bora ya ardhi.

ii. Migogoro wanayokumbana nayo wafugaji kutokana na kuingiza mifugo kwenye maeneo ya hifadhi pamoja na kero nyingine inatokana na kukosekana kwa miundombinu sahihi na endelevu kwa ajili ya ustawi wa mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa mrejesho maazimio tajwa hapo juu yametekelezwa kwa kiwango gani? kwani hadi sasa migogoro baina ya wafugaji, wakulima na hifadhi imekuwa ikiendelea na wananchi wamepoteza mali zao na wengine kupoteza uhai wao.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kurejea tena Sera na sheria zinazohusu matumizi ya raslimali ardhi, kwani wakati zinatungwa idadi ya watumiaji wa raslimali hiyo haikuwa kama ilivyo kwa sasa. Tuangalie idadi ya watanzania kwa sasa na miaka 50 au 100 ijayo watakuwa wangapi, Idadi ya mifugo na watumiaji wengine wa rasilimali hii ya ardhi.

### c. Hali ya Chakula Nchini

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka 2015/ 2016 Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula uliendelea na ununuzi wa nafaka katika kanda ya Songea, Makambako

na Sumbawanga ambako kulikua na uzalishaji wa ziada. Wakati wa kuanza mwaka tarehe 1 Julai 2015 NFRA ilikuwa na tani 353,702.25 za nafaka. Hadi kufikia tarehe 14 Aprili 2016 NFRA ilikuwa imenunua tani 22,335.157 na kufanya akiba katika maghala yake kufikia tani 65,275.155 ambapo mahindi ni tani 61,315.586, mpunga ni tani 3,939.630 na mtama ni tani 19,890. Akiba hii imeiwezesha Serikali kukabiliana na uhaba wa chakula na maafa hususan mafuriko yaliyojitokeza nchini katika sehemu mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya utekelezaji ya wizara inaonesha takwimu za uzalishaji wa mazao ya chakula nchini kwa msimu wa 2015/2016 na upatikanaji wa chakula 2016/17 kuwa ni tani 16,172,841 zikilinganishwa na tani 15,528,820 za msimu wa 2014/15 kati ya tani hizo nafaka zilikuwa ni tani 9,457,108 na mazao yasiyo ya nafaka tani 6,715,733. Aidha, takwimu zinaonesha kuwa mahitaji ya chakula kwa msimu wa 2016/17 ni tani 13,159,326 kati ya hizo mahitaji ya nafaka yalikuwa ni tani 8,355,767 na tani 4,803,560 isiyo nafaka.

**Mheshimiwa Spika,** kwa taarifa hiyo inaonesha kuwepo kwa ziada ya chakula ya tani 3,013,515 na hivyo taifa kuwa na utoshelevu kwa silimia 123 ikilinganishwa na asilimia 120 kwa mwaka 2015/16. Palepale tunaambiwa pamoja na uzalishaji wa zaida Halmashauri 55 zilikuwa na ukosefu wa chakula, na jumla ya watu 1,186,028 walikuwa na mahitaji ya jumla ya tani 35,491.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kuwa maelezo yanatakiwa kutolewa na Serikali kuhusu takwimu hizo za ziada ya tani 3,013,515 inawezekanaje Halmashauri 55 zikawa na upungufu wa chakula? Na kama kuna ziada ya nafaka tani 1,101,341 inakuwaje bei ya mahindi inazidi kupanda kila siku?

**Mheshimiwa Spika,** tukumbuke kwamba January 2017, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo alitoa kauli iliyoonesha kwamba wilaya 55 kati ya 169 zikiwemo za Zanzibar zilikuwa zinakabiliwa na upungufu wa chakula na hivyo zilikuwa zinahitajika tani 35,491 za chakula kati ya mwezi February

hadi April 2017 na watu wapatao 1,186,028 walikuwa wanakabiliwa na njaa katika wilaya tajwa hapo juu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa toka kipindi tajwa hapo juu hadi sasa ni dhahiri kuwa wakulima bado hawajavuna mazao yao hivyo ni ukweli ulio wazi kuwa watanzania wengi zaidi wanakabiliwa na tatizo la njaa.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Ripoti ya utafiti iliyotolewa na taasisi ya Twaweza ya March, 2017 inaonesha kuwa; "Hali ya upungufu wa chakula imeonekana kuwa mbaya zaidi katika miezi ya hivi karibuni. Hii inajidhihirisha pale ambapo kaya zilizoripoti kupata hofu ya kukosa chakula zilipanda kutoka asilimia 45 hadi asilimia 65 kati ya Septemba 2016 na Februari 2017. Vivyo hivyo, idadi ya kaya zilizopungukiwa na chakula ziliongezeka kutoka asilimia 43 Septemba 2016 hadi asilimia 51 Februari 2017. Kaya ambazo zilikuwa na angalau mtu mmoja aliyeshinda siku nzima bila kula nazo ziliongezeka kutoka asilimia 21 hadi asilimia 35 katika kipindi hicho hicho. Upungufu huu wa chakula umesababishwa kwa kiasi fulani na umasikini wa kipato unaofanya kaya maskini ziwe katika hali tete".

**Mheshimiwa Spika,** takwimu zilizotolewa na Benki Kuu ya Tanzania "monthly economic review" ya mwezi January 2017 zinaonesha kwamba bei ya mahindi imepanda kwa kiasi kikubwa katika kipindi cha miaka miwili iliyopita. Habari zilizoelezwa na wananchi ni kwamba upungufu wa chakula ni tatizo kubwa kwa sasa na hii ilijidhihirisha pale ambapo wahojiwa wengi wa Sauti za Wananchi (asilimia 78) waliripoti upungufu wa chakula katika maeneno waliyokuwa wakiishi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa utafiti wa bei za mazao ya vyakula uliofanywa kwenye maeneo mbalimbali hapa nchini na kuripotiwa na vyombo vya habari unaonesha kuwa;

Wilaya ya Kilombero, "Mfuko wa kilo 25 za sembe ulikuwa unanunuliwa Sh 18,000, sasa umepanda

mpaka Sh 35,000," na bei hiyo ya kilo hizo 25 za sembe uuzwa mjini, lakini kwa wilayani imefika hadi Sh 40,000.

Soko kuu la Arusha; kilo moja ya unga wa sembe na dona inauzwa kati ya Sh 1,600 na 1,800, wakati debe moja la mahindi likiuzwa Sh 15,000 na gunia la kilo 100 Sh 90,000 hadi 110,000. Mchele unauzwa Sh 2,200 hadi 2,400 kwa kilo moja, huku mazao mengine kama ngano, maharagwe, mbaazi na kunde nayo yakipanda bei.

Wilayani Longido, wananchi wanalazimika kubadilishana mbuzi mmoja mkubwa mwenye thamani kati ya sh 40,000 na 50,000 kwa debe moja la mahindi.

Mkoa wa Dodoma, bei ya mchele ilikuwa kati ya Sh 1,200 na 1,400 kwa kilo moja mkoani Shinyanga, ikiwa ni bei ya jumla huku wao wakiuza kwa Sh 1,500 hadi 1,600 bei ya rejareja.

Mkoa wa Mtwara, mfuko wa kilo 25 wa unga wa sembe unauzwa Sh 40,000 badala ya Sh 27, 000 bei ya msimu wa awali.

Mkoa wa Ruvuma, mkoa ambao unazalisha mahindi kwa kiwango kikubwa hapa nchini na ni moja ya "the big four"kwenye uzalishaji wa mahindi. Kilo moja ya mahindi inauzwa wastani wa Sh 730 na 750.

Mkoa wa Njombe, debe moja la mahindi linauzwa kati ya shilingi 18,000/- na 22,000/- na mkoa huo ni wazalishaji wakubwa wa mahindi.

Mkoa wa Tanga, bei ya gunia moja la mahindi Tanga mjini linauzwa kati ya shilingi 95,000/- hadi shilingi 97,000/- badala ya shilingi 67,000/- za awali na Mfuko wa sembe wa kilo 25 ulikuwa ukiuzwa kati ya shilingi 25,000/- na 24,000/- lakini hivi sasa unauzwa shilingi 30,000/- hadi 27,000/- na ile ya kilo 50 iliyokuwa ikiuzwa shilingi 50,000/- na shilingi 55,000/- hivi sasa inauzwa hadi shilingi 60,000/-. Mkoa wa Mwanza,

bei ya gunia la mahindi linauzwa kati ya shilingi 100,000/- na 125,000/-;

Wilaya ya Ukerewe, Gunia la mahindi linauzwa kati ya shilingi 105,000/- na 120,000/- tofauti na mwaka jana ambapo lilikuwa linauzwa kati ya shilingi 70,000 na 80,000.

Wilaya ya Bunda mkoani Mara, imepanda kutoka shilingi 14,500/- kwa debe moja hadi kufikia shilingi 20,000/-, huku unga wa muhogo ukipanda kutoka shilingi 12,500/- hadi 17,500/-. Nafaka nyingine kama mtama zimepanda kutoka shilingi 10,000/- hadi 17,500/- kwa debe, wakati ulezi unauzwa shilingi 30,000/- kwa debe moja.

**Mheshimiwa Spika,** kupanda kwa bei ya chakula, je, jukumu la serikali ni nini? na jukumu ya NFRA ni nini?

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Wizara ya Kilimo na vitengo vyake kuhakikisha kwamba watanzania kwa ujumla wao muda wote wanakuwa na uhakika wa kupata chakula, mengine yanafuatia. Hivyo basi kitendo cha watanzania kukosa chakula ni dalili kwamba kuna mapungufu ya kiutendaji sehemu fulani.

**d. Mabadiliko ya Tabianchi na Sekta ya Kilimo**

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya tabianchi yana madhara ya moja kwa moja kwa kilimo, mifugo na uvuvi na sekta hii wahusika wakubwa ni wananchi wa hali ya chini na ya kati.

**Mheshimiwa Spika,** mabadiliko ya tabia nchi yanaonekana dhahiri nchini Tanzania, uzalishaji wa kilimo unatishiwa na hali ya hewa na mabadiliko ya tabia nchi kutokana na matukio kama mafuriko na ukame. Mabadiliko ya tabia nchi ni tishio kubwa zaidi la kimazingira kwa maisha hapa duniani, linaloathiri mazingira yetu, sio tu kiuchumi, lakini pia kijamii na kitamaduni. Tanzania imekuwa ikikabiliwa na vipindi vya ukame vinavyotokea mara kwa mara ambavyo vimeathiri shughuli za kilimo na kusababisha uhaba wa chakula.

**Mheshimiwa Spika**, Utafiti juu ya athari za mabadiliko ya tabia ya nchi katika maeneo ya wilaya za Iramba mkoani Singida na Meatu mkoani Simiyu na namna ya kukabiliana nao kwa mtazamo wa kijinsia katika kilimo na maliasili yamebaini; mvua zisizotabirika, magonjwa ya wanyama na mazao pamoja na magonjwa ya binadamu. Hii hali imepelekea zaidi ya asilimia 80 ya watu kuwa masikini huku kaya zinazoongozwa na wanawake zikiwa maskini zaidi kuliko zinazoongozwa na wanaume. Utafiti huo uliofanyika kwa kipindi cha miaka mitano tangu mwaka 2011 hadi 2015, ukiongozwa na Dk. Samwel Kabote Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA).

**Mheshimiwa Spika,** Katika jumla ya **kazi 142** zinazotarajiwa kutekelezwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/18, ni kazi **12 tu** ndio zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi. Kazi hizi zimechukua jumla ya kiasi cha **TZS 25.5bilioni ambayo ni sawa na 17% tu**.

**Mheshimiwa Spika, Kati ya kazi 12** zilizoainishwa kuwa na uhusiano na mabadiliko ya tabianchi, ni kazi moja (1) tu ndio ina kiwango cha 'Juu' cha uhusiano wakati kazi kumi na moja (11) zina kiwango cha 'Chini' na hakuna hata moja yenye kiwango cha 'Kati'. *Maudhui yake katika mabadiliko ya tabinchi – Kupunguza (Mitigation), Kukabiliana (Adaptation),na Vyote viwili.* Pia, uchambuzi unaonesha kuwa **kati ya kazi 12** zilizoainishwa kuwa na uhusiano na mabadiliko ya tabianchi, kazi tisa (9) zina maudhui ya 'Kukabiliana (Adaptation)**'** na kazi tatu (3) zina maudhui ya 'Vyote viwili (Both)**'** na hakuna kazi yoyote yenye maudhui ya 'Kupunguza (Mitigation)[2]'

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa mifugo fungu 99 tika jumla ya **kazi 27** zinazotegemewa kutekelezwa, ni **kazi tisa (9) tu ndio zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi**. Kazi hizi zimechukua jumla ya kiasi cha **TZS 1.4bilioni ambayo ni sawa na 36%**.

______________

[2]Forum CC - taarifa ya tathmini ya Bajeti ya Kilimo 2017/18

**Mheshimiwa Spika,** kati ya jumla ya **kazi 23 za Wizara kwa fungu 64** zinazotegemewa kutekelezwa, ni **kazi tano (5) tu ndio zinazohusiana na mabadiliko ya tabianchi**. Kazi hizi zimechukua jumla ya kiasi cha **TZS 1.5bilioni ambayo ni sawa na 19% tu ya fungu hilo**.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema hii ni hatari kwa maendeleo ya nchi yetu na sekta nzima ya uzalishaji, kwani kila uzalishaji unategemea mabadiliko ya tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,** Serikali na vyombo vyake inawajibu mkubwa wa kuhakikisha kwamba, wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo ambao ndio wazalishaji wakuu wanapatiwa taaluma ya kupambana na mabadiliko ya tabianchi mashambani.

**Mheshimiwa Spika**, tafiti zinaonesha kwamba wakulima wadogo bado wanalima bila ya kufuata sera za sekta mbalimbali kinachozingatia mabadiliko ya tabia nchi, maana yake ni kwamba dhana nzima ya kilimo na ufugaji unaozingatia mabadiliko ya tabia nchi bado ni dhana mpya katika mipango yetu. Kambi Rasmi ya Upinzani, inasema kwamba sasa ni muda mwafaka japokuwa tumechelewa kama nchi kuhamasisha wakulima wadogo kujihusisha na Kilimo Kinachozingatia Mabadiliko ya Tabianchi na kuwe na Programu za kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi katika jamii. Ili kufikia lengo hilo ni lazima kuongeza motisha na vichocheo miongoni mwa wadau wa mabadiliko ya tabia nchi kushirikishana na kuchangia uzoefu wao katika mchakato wa kutayarisha programu za maendeleo ya kilimo-***District Agricultural Development Programmes*** (DADPs).

**e. Upatikanaji wa Mbegu na Mbolea**

**Mheshimiwa Spika**,tangu mwaka 2009 Serikali imekuwa na miradi kadhaa iliyozinduliwa ili kufanya Mapinduzi katika kilimo kwa kuhimiza uwekezaji binafsi katika kilimo program kadhaa zilinduliwa ambazo ni; programu ya SAGCOT mwaka 2010; Jukwaa la Kilimo Afrika

(Grow Africa Forum) mwaka 2011; Mpango wa Uwekezaji wa Kilimo na Usalama wa Chakula Tanzania (TAFSIP), Mpango wa Taifa wa Uwekezaji Tanzania chini ya CAADP mwaka 2011; Matokeo Mkubwa Sasa' (BRN) mwaka 2013, kuanza kwa utekelezaji wa Mfuko wa Kuchochea Kilimo wa SAGCOT mwaka 2014.

**Mheshimiwa Spika,** mapinduzi hayo yote kiini chake ni kuhakikisha wakulima wanatumia mbegu bora na mbole sahihi katika uzalishaji. Programu hizo tajwa zimekuja na Makampuni ya Kimataifa ya mbegu kuingia kwa nguvu kubwa kwenye soko la pembejeo, yakilenga mbegu zenye faida (hasa mahindi chotara na baadhi ya aina za mpunga), biashara ambayo ilitegemea kwa sehemu kubwa mbegu zinazoagizwa kutoka nje.

Makampuni ya Pioneer Hi-Bred, Monsanto na Syngenta kwa sasa ndio makampuni makubwa zaidi ya nje. Kampuni nyingine za mbegu za ukanda wa Afrika pia zinafanya biashara nchini Tanzania, ambazo ni pamoja na East Africa Seed Company (Kenya), FICA (Uganda) na MRI (Zambia, ambayo kwa sasa inamilikiwa na Sygenta). Kampuni ya Mbegu ya Kenya (KSC) pia ipo nchini Tanzania kupitia kampuni zake tanzu za Simlaw (mboga) na Kibo Seed[3]. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema hii ni kuweka reahani kilimo chetu.

**Mheshimiwa Spika,** Makampuni Makubwa ya Kimataifa huelekeza rasilimali zao na muda kwenye mazao machache yanayoweza kuwapatia faida kubwa. Masoko madogo kwa ajili ya mbegu za kienyeji au zile ambazo zimebadilishwa kwa kawaida hayahudumiwi[4], Kambi Rasmi ya Upinzani inasema ni muhimu sana kuhakikisha mbegu zetu za asili zinalindwa na ili zisije zikapotea kabisa na hivyo kupoteza urithi wetu wa mbegu za asili.

---

[3]Kubadili Sheria Za Mbegu Na Ulinzi Wa Aina Za Mbegu Na Mimea Nchini Tanzania – The African Centre for Biosafety, April 2016-

[4]The African Centre for Biosafety, March 2015

**f. Upatikanaji wa mbegu**

**Mheshimiwa Spika**, Mbegu kwa ajili ya kilimo hupatikana kutokana na mifumo wa ugavi rasmi na isiyo rasmi (pia hujulikana kama mfumo wa mbegu unaosimamiwa na mkulima); asilimia 90 hutokana na mfumo wa mbegu unaosimamiwa na mkulima wakati asilimia 10 hutokana na sekta rasmi ya mbegu.

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya mbegu ya mwaka 2003 haitambui kwa uwazi *mifumo ya mbegu inayosimamiwa na wakulima(sekta ya mbegu isiyo rasmi)* na aina za mbegu za kienyeji na haisemi chochote kuhusu haki za wakulima.

**Mheshimiwa Spika,** Sekta rasmi ya mbegu nchini Tanzania husambaza kiasi kidogo sana cha mbegu bora kwa wakulima nchini Tanzania (takribani asilimia 4-10) lakini bado ndiyo inayopata uungwaji mkono mkubwa wa serikali, fedha na taratibu za udhibiti huku mifumo ya mbegu inayosimamiwa na wakulima ambao hutoa asilimia 90, inabaki kutotambuliwa na haipati msaada.

**Mheshimiwa Spika,** Utafiti uliofanywa na ACB mwaka 2014 huko Morogoro na Mvomero uligundua kwamba zaidi ya asilimia 80 ya mbegu za asili za mahindi, mazao aina ya kunde na mpunga zinazotumika na wakulima hazijathibitishwa, na wakulima wengi huendelea kutumia kwa kurudia mbegu zinazotokana na mavuno ya msimu uliopita.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Taarifa ya utekelezaji ya Wizara inaonesha kuwa makadirio ya mahitaji ya mbegu kwa mwaka ni tani 60,000 za mbegu bora. Aidha, Randama inaonesha kuwa wakala wa mbegu za kilimo (ASA) umeongeza uzalishaji wa mbegu bora za nafaka na mikunde toka tani 2,804 msimu wa 2015/2016 hadi tani 2,884 msimu wa 2016/17. Uzalishaji wa ndani wa mbegu ni sawa na asilimia 4.81 tu ya nahitaji ya mbegu kwa nchi kwa mwaka.

**Mheshimiwa Spika,** maana yake ni kwamba asilimia 95.19 ya mahitaji ya mbegu kwa mwaka zinaingizwa na makampuni yanayojihusisha na mbegu toka nje ya nchi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali ijitafakari kuhusiana na hali hii ya mbegu kwa nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa; usambazaji wa mbegu uzingatie na uende sambamba na aina ya mbegu (breed) ambazo zinazingatia aina ya hali ya hewa (microclimate) na hali ya udongo katika maeneo husika.

## g. Upatikanaji wa Mbolea

**Mheshimiwa Spika,** takwimu za Serikali zinaonesha kuwa mahitaji ya mbolea kwa mwaka ni tani 485,000,aidha takwimu zinaonesha kuwa hadi mwezi machi,2017 tani 297,000 ziliingizwa nchini na tani 140,000 zilitolewa(ziliuzwa) nje ya nchi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaona hapa kuna tatizo kubwa katika utendaji wetu, kama mahitaji yetu ni makubwa na hayatimizwi lakini bado tunatoa mbolea ndani na kupeleka nje ya nchi. Tatizo ni aina ya mbolea inayopelekwa nje haina ubora unaotakiwa kwa wakulima wetu? Kama ndio ni kwanini uzalishaji unakuwa upo chini ya viwango kukidhi matakwa ya wakulima/ kilimo chetu?

**Mheshimiwa Spika,** moja ya changamoto kubwa linaloikabili sekta ndogo ya mbolea ni mfumo wa usambazaji ambao hauna uhakika kuendana na mahitaji ya wakulima kulingana na misimu ya kilimo na hivyo mbolea inapofikishwa kwa wakulima muda stahiki wa matumizi unakuwa tayari umeishapita.

**Mheshimiwa Spika,** ruzuku ya mbolea imekuwa ni kichaka kikubwa cha wizi wa fedha za Serikali kwa muda mrefu, lakini kilimo hakioneshi kuwa kinakua. Kwa msimu wa kilimo 2015/16 Serikali ilitoa vocha za ruzuku 2,999,778 kwa wakulima 999,993 zenye thamani ya shilingi bilioni 78.1 au dolla za Marekani milioni 36.4[5].

[5]East African Business Week, November 24, 2015

**Mheshimiwa Spika,** mfumo wa ruzuku kwa njia moja au nyingine unavunja nguvu mfumo wa kibiashara wa mbolea, na kwa kuwa mfumo wa usambazaji wa mbolea ni shida, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuuimarisha mfumo wa kibiashara ili muda wote wa mwaka mbolea iwepo madukani. Ni dhahiri wakulima sio kama hawana uwezo wa kununua mbolea, bali wanachohitaji ni upatikanaji wa uhakika wa mbolea katika maeneo yao.

**h. Tathmini ya Utekelezaji wa Programu ya kuendeleza sekta ya Kilimo awamu ya kwanza (ASDP-I)**

**Mheshimiwa Spika,** program ya ASDP ni program ya miaka 15 inayotekelezwa kwa awamu, na awamu ya kwanza ilikuwa ni ya miaka 7 ilianza mwaka wa fedha (2006/07 – 2012/13) na ilimalizika mwezi wa Juni 2013. ASDP1 ili lenga kukuza kilimo kufikia asilimia 6 kwa mwaka na hivyo kilimo cha wakulima wadogo kuwa na tija zaidi katika mazingira ya ushindani kibiashara. Programu nzima ilitarajiwa kutumia jumla ya USD Milioni 315.6 sawa na UA Milioni 210. Kati ya fedha hizo, hadi program inamalizika Serikali na wachangiaji wengine walitoa jumla ya UA Milioni 146.564 na kubakiza UA 64236,000 tu.

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa hiyo program unasaidia miradi ya kitaifa kwa matumizi ya program za sekta ya kilimo zilizo chini ya Wizara ya kilimo, shughuli zilizo ngazi ya wilaya na vijiji zinazosaidiwa chini ya mfumo wa Local Government Deveolopment Grant uliokuwa unaratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu-TAMISEMI.

**Mheshimiwa Spika,** ni dhahiri kuwa Programu hii ya awamu ya kwanza mafanikio yapo, lakini pia mapungufu yapo, moja wapo ya mapungufu ni kuchelewa kutolewa kwa fedha katika utekelezaji wa miradi na hivyo kusababisha gharama za utekelezaji wa miradi kupanda. Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza kwamba dhana nzima ya umiliki katika miradi ya DADPS inayotekelezwa katika ngazi za wilaya kushuka chini, uelimishaji wananchi unatakiwa kuwa mkubwa sana katika awamu ya pili ya ASDP ili kutimiza malengo ya miradi inayoibuliwa na wananchi.

### i. Mpango wa SAGCOT

**Mheshimiwa Spika**,mpango wa SAGCOT unahusisha vijiji 359 vilivyo katika wilaya 30 zilizo katika mikoa 8 vinakadiriwa kuwa na eneo lenye ukubwa wa hekta 6,131,771 sawa na asilimia 60 ya ardhi yote iliyo katika mpango wa SAGCOT ni ardhi ya vijiji, na asilimia 2 ni ardhi ya jumla na asilimia iliyobakia ni maji na eneo la hifadhi.

**Mheshimiwa Spika,** taarifa ya Kamati teule ya Bunge iliyowasilisha taarifa yake humu Bungeni mwezi wa februari, 2015 inaonesha kuwa migogoro mikubwa ya vijiji kuporwa ardhi na taasisi za Serikali, pamoja na wawekezaji ni mingi kwenye vijiji vya wilaya za Kilombero, Bagamoyo, Rufiji, Chunya, mbalali, Sumbawanga.

Wilaya hizo zote ni sehemu ya wilaya 30 za mpango wa SAGCOT, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kama mitafaruku ya ardhi ipo katika vijiji husika kwa mujibu wa taarifa ya kamati teule ya Bunge iliyoongozwa na Mhe Christopher Ole Sendeka, je mpango huo si unatashindwa kuwa na manufaa kwa wananchi katika maeneo yenye migogoro? Na kama maeneo yatatwaliwa bila ridhaa ya vijiji husika, je ule mkakati wa **"nucleus-outgrowers model"** utafanyaje kazi? Kwani wananchi/ wanavijiji wengi si watakuwa ni manamba katika mashamba hayo ya SAGCOT?

**Mheshimiwa Spika,** ni muda mwafaka sasa kwa Bunge kupata mrejesho wa maazimio yake yaliyotokana na ***"Taarifa ya Kamati Teule ya Bunge iliyoundwa kuchunguza sababu za migogoro baina ya wakulima, wafugaji, wawekezaji na watumiaji wengine wa ardhi nchini".***

## III. MAPITIO YA BAJETI YA UTEKELEZAJI WA MIRADI

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo Mifugo na Uvuvi kupitia fungu 43 kwa mwaka wa fedha 2015/16 ilitengewa jumla ya Shilingi **206,816,421,000/-**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **174,103,348,000/-** zilikuwa ni fedha za matumizi ya kawaida na Shilingi **32,713,073,000/-** ni fedha za maendeleo. Hadi

mwaka huo wa fedha unamalizika Wizara ilipokea shilingi **2,663,428,542/-** kwa ajili ya miradi ya maendeleo zikiwa ni fedha za ndani na shilingi **5,035,062,321/-** zikiwa ni fedha za nje, na hivyo kufanya jumla ya fedha za maendeleo kwa fungu 43 zilizopokelewa kwa mwaka 2015/16 kuwa shilingi **7,698,490,863/-** sawa na asilimia 23.53 ya fedha za maendeleo zilizopitishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2016/17 Fungu 43 lilitengewa jumla ya Shilingi **210,359,133,000** zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **109,831,636,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **100,527,497,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Fedha za maendeleo zilizoongezwa ni fedha za madeni ya wakandarasi wa skimu za miradi ya umwagiliaji na hivyo kuifanya jumla ya fedha za maendeleo kuwa shilingi **101,527,497,000/-**. Fedha za ndani zilikuwa shilingi **23,000,000,000/-** na fedha za nje shilingi **78,527,497,000/-** Hadi kufikia mwezi Machi, 2017 fedha zilizokuwa zimetolewa na shilingi **2,251,881,250/**- sawa na **asilimia 2.22** tu na kati ya fedha hizo fedha za ndani zilikuwa shilingi **1,382,191,924/-** na fedha za nje shilingi **349,081,000/-**

**Mheshimiwa Spika,** kama fedha za maendeleo/ miradi hazipo, iwaje kuna fedha za OC? matumizi yake ni nini?

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2017/18 wizara inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **216,019,071,000/-** kati ya fedha hizo shilingi **151,456,312,000/-** ni fedha za maendeleo, ambazo ni ongezeko la shilingi **49,928,815,000/-** Kwa kulinganisha na maombi ya mwaka wa fedha 2016/17. Kambi Rasmi ya Upinzani baada ya kupitia kitabu cha Maendeleo –Juzuu ya IV fedha za maendeleo kwa fungu 43 inaonesha jumla ya shilingi **150,253,000,000/-** na hivyo kufanya tofauti kati ya Taarifa ya Wizara na ile ya Hazina kuwa shilingi **1,203,312,000/-**. Hii ni tofauti kubwa sana na kwa vyovyote vile tunaomba maelezo ya nini kimetokea.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa miaka 5 inaonesha kuwa bajeti kwa ajili ya

maendeleo ya kilimo (fungu 43) zitengwe shilingi bilioni **1,134.07/-** na Mifugo (fungu 99) ilitarajiwa kutengewa jumla ya shilingi bilioni **156.52/-**, na Uvuvi (fungu 64) shilingi bilioni **1,024.78/-,** hivyo kuifanya sekta nzima ya kilimo kama inavyosomeka kwenye Mpango wa Maendeleo wa miaka mitano kuwa shilingi bilioni **2,314.99/-**. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni kwanini mpango wa miaka mitano uliopitishwa na Bunge hili hili haufuatwi katika utekelezaji?

**Mheshimiwa Spika**, Makusanyo kwa mwaka 2016/17, sekta ya Kilimo ilikuwa shilingi **2,903,760,494.43/-**. Makusanyo haya ni ya chini kabisa ukilinganisha na sekta ya Uvuvi (Fungu 64) shilingi **10,321,908,868.10/-**, na sekta ya Mifugo (Fungu 99) ilikusanya shilingi **21,756,818,934.30/-**. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuweka na kusimamia malengo na vipaumbele vyake kiuhalisia kwani Kilimo ndio uti wa mgongo wa nchi yetu.

**IV. SEKTA YA MIFUGO: Fungu 99**

**Mheshimiwa Spika,** sekta ya mifugo ni muhimu sana kwani ina mchango asilimia 4.4 kwa pato la taifa,pia inahudumia takriban 10% ya watanzania wanaoishi kwa kutegemea mfumo huu wa ufugaji na Kutoa ajira kubwa hasa mijini- machinjio mbalimbali, mabucha, vifaa vitokanavyo na ngozi, kutunza maliasili wanyama, utalii na mazingira nk.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2015/2016, idadi ya mifugo nchini ilifika ng'ombe milioni 25.8, mbuzi milioni 17.1 na kondoo Milioni 9.2. Pia, wapo kuku wa asili milioni 42.0, kuku wa kisasa milioni 34.5 na nguruwe milioni 2.67.

**Mheshimiwa Spika**, kwa kipindi hicho uzalishaji wa maziwa ulikuwa ni lita bilioni 2.14. Aidha, usindikaji wa maziwa ulikuwa ni lita 167,620. Pia, uzalishaji wa mitamba katika kipindi hicho ulifikia mitamba 11,449. Kati ya mitamba hiyo, 646 ilizalishwa kutoka mashamba ya Serikali na Kampuni ya Ranchi za Taifa-NARCO na 10,803 kutoka sekta binafsi.

Aidha, dozi 80,000 za mbegu bora za uhimilishaji zilizalishwa na kusambazwa kwa wafugaji ambapo ng'ombe 221,390 walihimilishwa.

**Mheshimiwa Spika**, uzalishaji wa nyama umeongezeka kwa asilimia 8.54 kutoka tani 597,757 (ng'ombe 319,112; mbuzi na kondoo 124,745; nguruwe 54,360; na kuku 99,540) mwaka 2014/2015 hadi tani 648,810 (ng'ombe 323,775; mbuzi na kondoo tani 129,292; nguruwe tani 91,451; na kuku tani 104,292) mwaka wa 2015/2016. Pia, uzalishaji wamayai kwa mwaka 2015/2016 ni mayai bilioni 4.35 ikilinganishwa na mwaka 2014/15. Aidha, mifugo iliyouzwa minadani ni ng'ombe 1,470,805, mbuzi 1,161,840 na kondoo 253,243 wenye thamani ya shilingi bilioni 976.474 kwa mwaka 2015/16 ikilinganishwa na thamani ya shilingi bilioni 1,027.4 ya waliouzwa mnadani mwaka 2014/15, sawa na upungufu wa asilimia 5.22

**Mheshimiwa Spika**, VAT kwenye mazao ya mifugo inabidi kuondolewa kwani kodi hii inafanya vyakula vya mifugo kuwa ghali sana na inalipiwa mara mbili, wafugaji inawabidi wakati wananunua chakula hicho wanalipa VAT wakati tayari watengezaji walikwishalipia wakati wananunua vichanganyio.

**a. Ukame na vifo vya mifugo**

**Mheshimiwa Spika,** ukame uliopitiliza umeacha majanga makubwa kwa wafugaji katika maeneo mengi ya nchi hii, Kambi Rasmi ya Upinzani imepata baadhi ya taarifa za wafugaji ambao wamepoteza mifugo yao na wengine kufikia hatua ya kujiua kutokana na hasara waliyoipata.

**Mheshimiwa Spika,** yafuatayo ni baadhi ya maeneo yaliyoathirika na ukame na kupoteza mifugo;

*Mkoani Morogoro, zaidi ya ng'ombe 15,000 wamekufa katika vijiji vitano wilayani Mvomero kutokana na ukame. Katika vijiji vya Dakawa, Sokoine, Kambala,Mera na Melela, baadhi ya wafugaji wakilalamikia mifugo yao kuanguka na kufa baada ya kukosa chakula na maji.*

*Katibu wa Chama cha Wafugaji Mkoa wa Morogoro, Kochocho Mgema, alivitaja vijiji vilivyoathirika zaidi na ukame na idadi ya ng'ombe waliokufa kwenye mabano ni Dakawa (2,723), Sokoine (4,246), Kambala (1,328), Mera (1,284) na Melela (1,057).*

*Kwa upande wa Wilaya ya Kilosa, zaidi ya ng'ombe 3,328 wamekufa.*

*Mfugaji katika Kitongoji cha Chaua, Mamlaka ya Mji Mdogo wa Chalinze, Hamisi Meya, amepoteza ng'ombe zaidi ya 100, ndugu Karanga kutoka Mdaula, Bagamoyo, akipoteza ng'ombe 220.*

***Mkoa wa Manyara:** Simanjiro kata zilizoathirika na ukame kwa kiasi kikubwa ni Remiti, Losoboit, Kitwai na Leseinyai. Monduli ni Mswakini, Lokisale, makuyuni n.k. Kiteto ni Lengatei, Sunya, Laiseri, Lorela na Kijungu.*

**Mheshimiwa Spika,** kuna wafugaji wengi kutoka mkoa wa manyara, Dodoma na maeneo mengine ya wafugaji ng'ombe wao walikufa kutokana na ukame uliopitiliza. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge lako na wafugaji ni hatua gani za makusudi za kuhakikisha wafugaji waliopoteza mifugo yao wanafidiwa kwa kupatiwa mitamba bora ili waendelee na maisha yao ya kawaida?

**Mheshimiwa Spika,** mbali na ukame huo ulioathiri kwa kiasi kikubwa ufugaji wa kuhamahama, lakini kuna matatizo ambayo Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali iyape kipaumbele kama kweli inathamini mchango wa sekta hii, nayo ni;

1. Kufanya ushawishi kwa jamii kuhusu maeneo yaliyobainishwa ambayo yanaweza kutengwa kwa ajili ya wafugaji ili kuondoa migogoro ya ardhi iliyopo sasa baina ya wakulima na wafugaji.

2. Suala la upigaji chapa mifugo bado elimu haijatolewa kwa wafugaji na kupelekea malalamiko mengi sana toka kwa wafugaji. Wizara ilisitisha kuanza zoezi hilo lakini baadhi ya mikoa kama Morogoro na Singida wilaya ya Manyoni zoezi linaendelea kwa nguvu.

3. Kamata kamata ya mifugo na unyanyasaji mkubwa wa wafugaji karibu nchi nzima usitishwe. Mfano huko Kagera mifugo inapigwa mnada kila siku na kuwaacha wafugaji wakiwa maskini kabisa. Pia kuwaondoa bila kuwaonyesha maeneo mbadala ya kupeleka mifugo yao inaongeza migogoro ya ardhi na baina yao na watu wanaowakuta tayari kwenye maeneo wanapokwenda. Maeneo ya Pwani ambapo wafugaji wameuawa bila kuwa na kosa lolote-Mfano, Waziri wa mambo ya ndani alipowaomba wafugaji wa Kibarbaig wawazike wapendwa wao waliouwawa na Polisi.

### b. Mapitio ya Bajeti ya Utekelezaji wa Miradi

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2015/16 Idara kuu za mifugo na uvuvi haikupokea fedha yoyote toka ndani bali ilipokea fedha za nje jumla ya shilingi **547,375,920/-**. Kwa mwaka wa fedha 2016/17 Fungu 99 ilitengewa na bunge jumla ya shilingi **60,013,252,440.56/-** na kati ya fedha hizo shilingi **15,873,215,000/-** (fedha hizi zimejumuisha Mifugo & Uvuvi) zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Upatikanaji na utekelezaji wa bajeti kwa mwaka 2016/17, sekta hii ya mifugo imetengewa shilingi **4,000,000,000/-** tu (kwa ajili ya huduma ya mifugo, na uzalishaji wa mifugo), kati ya fedha hizi ni shilingi **130,000,000/-** tu ndizo zilizotelewa kwa ajili ya shughuli za uzalishaji wa mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa kuna umuhimu wa sekta ya mifugo kuboreshwa na kupewa kipaumbele katika uzalishaji na soko; aina ya mifugo, aina ya ufugaji na masoko.

## V. SEKTA YA UVUVI: Fungu 64

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya uvuvi namba 22 ya 2003 ina kasoro na inatia mashaka kama wakati wa kutungwa kwake ulifanyika utafiti wa kina na kuhusisha wadau wote (hasa wavuvi).

- Sheria hiyo inataka nyavu zote za samaki aina ya dagaa ziwe na upana wa matundu wa 10 mm lakini ukweli ni kwamba dagaa wanaopatikana katika ziwa Tanganyika ni tofauti na Ziwa Nyasa na ni tofauti na Ziwa Vitoria na hata wale wa bahari ya Hindi. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuifanyia rejea Sheria hiyo ili wavuvi wa Dagaa katika Ziwa Viktoria wasiendelee kuchomewa nyavu zao za kuvulia dagaa kwa kuwa haziko kwenye viwango vya kisheria.

- Sheria inataka nyavu za Sangara kuwa na “piece” moja badala ya kuunganishwa hadi “piece” tatu. Kwa kutumia “piece” moja kwa wavu kunawa lazimisha wavuvi kuvua kwenye kina kifupi na hivyo kuharibu mazalia ya samaki tofauti na kama nyavu hizi zingeunganishwa ambapo wavuvi wataweza kuvua katika maji ya kina kirefu na hivyo kutovuruga mazalia ya samaki.

**Mheshimiwa Spika,** badala ya kutumia nguvu kubwa kuchoma nyavu, Serikali itoe fursa za mikopo kwa wavuvi na kutoa elimu ya ufugaji wa samaki, pia kuweka mpango mzuri wa matumizi ya ziwa na Bahari. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa unapomchomea mvuvi nyavu na zana nyingine za uvuvi bila kuwapa wavuvi hawa njia mbadala wa kufanya shughuli zao ni kutoondoa tatizo na kusababisha shida kubwa ya maisha kwa watu hawa.

**Mheshimiwa Spika,** Wavuvi wanakabiliwa na tozo nyingi sana ambazo zinaathiri kipato chao. Wavuvi wana tozo zaidi ya (tisa) 9 kulingana na maeneo wanayofanyia shughuli zao. Tozo hizi ni kama vile: Ada ya SUMATRA, leseni ya uvuvi, zimamoto, maegesho, leseni ya mtumbwi, kodi chini ya TRA, leseni ya usafirishaji n.k.

Pamoja na hapo, leseni ya mtumbwi;

a. Hutozwa kwa kiwango sawa bila kuangalia ukubwa wa mtumbwi. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, Mitumbwi itozwe kulingana na ukubwa.

b. Mitumbwi ukishalipiwa tozo ya leseni, basi itambuliwe mahala popote katika ziwa husika badala ya kila eneo kutoza tozo yake.

**Mheshimiwa Spika,** kukosekana kwa usalama katika maziwa jambo linalopelekea wavuvi kuvamiwa mara kwa mara na kunyang'anywa zana zao za kazi, na wakati mwingine watu hawa hujeruhiwa na hata kuuwawa. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kufuatilia suala hili na kuweka mikakati mbalimbali ya kuimarisha ulinzi na usalama katika 'madago'

**Mheshimiwa Spika**, elimu ya ufugaji wa samaki (aquaculture) kama ingetolewa vyema lingekuwa ni jambo ambalo lingepunguza uvuvi haramu katika maziwa na bahari, na pia ni fursa nzuri ya kuongeza kipato kwa wafugaji samaki.

**Mheshimiwa Spika,** kuna umuhimu mkubwa sana katika kuboresha na kusimamia shughuli na miuondo mbinu za uvuvi na rasilimali zake. Katika mwaka 2016/17 ni shilingi **544,461,000/- tu** zilitengwa kwa ajili ya shughuli za doria. Lakini hadi mwezi machi, 2017 zilitolewa shilingi **108,792,464.** sawa na shilingi 20.

## a. Mapitio ya Bajeti ya Utekelezaji wa Miradi

**Mheshimiwa Spika,** fedha zilizotolewa wa mwaka 2016/17 kwa matumizi ya maendeleo ya uvuvi ni shilingi **5,369,160,000/-** tu (shilingi 4,369,160,000/- kati ya hizi ni fedha za nje kutoka mradi wa SWIOFish). Kiasi hiki cha fedha ni kidogo sana.

## VI. HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, Sekta ya kilimo, kwa muktadha mzima wa sekta nzima ya mazao na visaidizi vyake, sekta ya mifugo pamoja na sekta ya uvuvi ni sekta muhimu sana na ndiyo sekta ambayo kwa upana wake inayotoa ajira nyingi kwa watanzania wa makundi yote, takwimu za mwaka 2014 sekta inatoa ajira kwa asilimia 66.9[6].

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na umuhimu wake katika suala zima la kiuchumi ili Tanzania iweze kutekeleza vyema mpango wake wa pili wa miaka mitano wa maendeleo, haina budi kujikita katika kuhakikisha inatoa fedha za maendeleo kwa sekta nzima kama ambavyo wataalam walivyopanga na baadae Bunge hili kupitisha. Kwa kuwa tayari Bunge lilikwisha toa Baraka za utekelezaji wa mpango huo na hivyo kuwa ndiyo dira kwa kila mpango wa maendeleo hadi pale miaka mitano itakapo malizika, hivyo basi, kitendo chochote cha Serikali kutoufuata mpango huo; Kambi Rasmi ya Upinzani inaliona jambo kuwa ni Serikali kulidharau Bunge au kulidanganya Bunge kwa kuleta taarifa ambazo hazina uhalisia na hivyo kushindwa/ kukataa kwa makusudi kufuata kile walichokipanga.

**Mheshimiwa Spika,** Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, kwa "trend"ya utoaji wa fedha kwa sekta hii ni dhahiri Tanzania kuwa nchi ya viwanda na hivyo kuwa na uchumi wa kati itakuwa ni njonzi za mchana.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

**.......................................................**
**Dr. Sware I. Semesi (Mb)**
**Waziri Kivuli na Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani-**
**Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi**
**19.05.2015**

[6]National Five year Development plan 2016/17-2020/21, pg.55

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge tumeshamsikia mtoa hoja, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi, Mwenyekiti wa Kamati na Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani. Sasa tutaanza uchangiaji kwa muda wetu uliobaki; tutaanza na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Kepteni Mstaafu George Mkuchika na kama muda wetu utakuwa bado unaruhusu Mheshimiwa Anne Kilango Malecela atamalizia.

**MHE. DKT. CHRISTINA G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuchangia kwenye Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Kwanza kabisa nianze kwa kukushukuru wewe na pia kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais na tatu kwa kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na watendaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuzungumzia kilimo. Kwa kweli asilimia 65 ya wananchi wa Tanzania wanategemea ajira kutokana na kilimo, wananchi wanategemea chakula kutoka kwenye kilimo na malighafi ya viwanda yanategemewa kutoka kwenye kilimo. Nashauri tena kilimo kiweze kupewa kipaumbele kama inavyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye upande wa bajeti; bajeti bado ni ndogo. Kuna makubaliano yaliyofanyika kwa nchi husika, makubaliano ya asilimia kumi ya Malabo pamoja na Maputo, lakini mpaka sasa hivi bado hayajatimilika. Kwa mwaka 2016/2017 ni asilimia 4.9 tu ya bajeti nzima ya Serikali ndio imepelekwa kwenye kilimo. Kwa hiyo, kwa kuwa bado Watanzania wengi wanategemea kilimo, kwa hiyo, naomba kizidi kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha za maendeleo bado zinakwenda kidogo. Tumeona kuwa kwa upande wa kilimo ni asilimia 3.31 tu ndio zimekwenda kwenye fedha za maendeleo na hizo fedha za maendeleo hazitolewi kwa wakati. Kama hatupeleki hizo fedha tunategemea mipango itafanyikaje? Naishauri Serikali iweze kupeleka fedha za maendeleo tuweze kuendelea vizuri na miradi ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili tuweze kuwa na kilimo bora lazima tuweze kufuata kanuni bora za kilimo na baadhi ya kanuni bora za kilimo ni pamoja na kuwa na na maji, mbegu bora, mbolea pamoja na viuatilifu ambavyo vitatuwezesha kupata mazao bora ya kilimo ambayo yatatuwezesha kupunguza utapiamlo ambao umekithiri kwenye nchi yetu; ambao umefikia takribani asilimia 34. Ili kwa pamoja tuweze kuinua kipato cha Mtanzania lazima tuweze kufuata mambo kama haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mbegu ni asilimia 35 tu ambazo zinazalishwa Tanzania na asilimia 65 zinatoka nje na hizo asilimia 35 tukitaka kuzipeleka zina kodi, zina *VAT,* lakini zile za nje hazina. Kwa hiyo naomba sana Wizara, mnajitahidi sana nimewapa pongezi, kuna wanaozalisha mbegu, kuna taasisi mbalimbali kama za Magereza, JKT wanazalisha mbegu, kuna utafiti unafanyika kwenye vyuo vya utafiti na taasisi za utafiti, naomba sana tujitahidi tuweze kuzalisha mbegu zetu hapa nchini ili wananchi waache kutumia mbegu ambazo ni za kiasili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitumia mbegu za kiasili huwezi kupata mazao bora ambayo yanahitajika. Tukitumia mbegu bora pamoja na mbolea ndipo tutaweza kuzalisha mazao ambayo yanastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa mbolea, naongelea manunuzi ya mbolea kwa pamoja. Mfumo huu tuliusubiri kwa muda mrefu, tulikuwa na mfumo ambao ulikuwa unatumia vocha, mfumo wa kutumia vocha uligubikwa na taswira za rushwa. Lakini sasa hivi tumepata mkombozi, naomba Waheshimiwa Wabunge tuweze kuupitisha mfumo huu na ninaipongeza sana Serikali na Wizara kwa kuja na mfumo huu ambao ni mzuri sana ambao utamnufaisha mwananchi na kila mwananchi ataweza kupata mbolea kwa wakati na itakuwepo kwa wakati wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nawapongeza sana Serikali kwa kuja na Mfumo huu wa *Fertilizer Bulk Procurement* ambao mwananchi yeyote anaweza kutumia

mbolea kwa wakati wowote na ninaamini kuwa bei ya mbolea itapungua. Hata ninyi Waheshimiwa Wabunge mtaweza kutumia mbolea hii kwa sababu ule mfumo wa vocha ulikuwa unawanufaisha wakulima wachache. Kwa hiyo ni mfumo mzuri, mimi naupenda, naomba uweze kuendelea. Naipongeza Serikali kwa kuweza kuufikiria mfumo huu ambao utaanza hivi karibuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa tena pongezi sana kwa Serikali kwa kupunguza tozo nyingi sana kwa upande wa kilimo, mifugo na kwa upande wa uvuvi. Hii italeta unafuu sana kwa wakulima, wafugaji na wavuvi ili waweze kuendeleza maisha yao kwa sababu tozo zilizidi na zilizidi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee *NFRA* ambayo inafanya kazi vizuri, naomba sana iendelee kufanya vizuri. Hata hivyo angalizo, naomba sana hayo maghala ambayo mmesema mtayajenga yaweze kujengwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninashauri mnunue chakula kwa wakati, msisubiri walanguzi waanze kuingia ndipo ninyi muanze kununua na bei elekezi iweze kutolewa mapema, pamoja na mambo mengine ya mizani na magunia yasilete matatizo kwa sababu wakati mwingine huwa yanachelewa kuwafikia wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Halmashauri 55 ambazo zilikuwa na uhaba wa chakula, naomba kujua mpaka sasa hivi ni Halmashauri ngapi ambazo zinahitaji chakula? Kwa sababu najua mvua zimenyesha kwa hiyo Halmashauri nyingine ambazo zilikuwa na uhaba wa chakula sasa hivi zinavuna mazao, sasa tujue kama bado zina uhitaji wa chakula ziweze kupelekewa chakula kuliko chakula kukaa kwenye maghala. Kwa sababu chakula si vizuri kukaa kwenye maghala zaidi ya miaka mitatu, la sivyo kitaharibika, kwa hiyo, naomba sana tuangalie hali hiyo ya chakula na Halmashauri ambazo bado zinahitaji chakula ziweze kupelekewa chakula, naamini mmeanza kupeleka lakini ziweze kupelekewa chakula, nashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, migogoro ya wakulima na wafugaji. Ni kweli tulikuwa na migogoro mikubwa sana ya wakulima na wafugaji, Mkoa wangu wa Morogoro ukiwa unaongoza. Hata hivyo nashukuru kwa sababu ya hii Kamati ambayo tumeambiwa imeleta taarifa, tutaiangalia wakati ukifika. Pia ninaishukuru Serikali kwa sababu Mawaziri mbalimbali walifika huko Morogoro na walifanya kazi nzuri sana. Sasa hivi naamini migogoro imepungua. Lakini kwa nini imepungua, kwa sababu mvua inanyesha, malisho yapo, kwa hiyo inaendelea vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naishauri Serikali iweze kuangalia miundombinu ambayo ni pamoja na majosho na malambo; iangaliwe ili tusije tukarudia kwenye mgogoro huu wa wakulima na wafugaji. Pia naishukuru Serikali kwa sababu imeanza kupima ardhi kwa upande wa Ulanga pamoja na Kilombero. Ukipima ardhi na kutoa hati miliki kila mmoja atakuwa na ardhi yake na hivyo tutaendelea kupunguza migogoro ya wakulima pamoja na wafugaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile naomba elimu ya malisho iendelee kutolewa ili wananchi waweze kujua kujitengenezea majani yao ya kulishia mifugo yao. Nashauri tena elimu ya kuvuna mifugo, yaani tuweze kufanya ufugaji wa kisasa na wenye tija, iendelee kutolewa na hapohapo Mheshimiwa Waziri Mwijage akituletea viwanda vya nyama.

Mhehimiwa Naibu Spika, Afisa Ugani; kuna sera inasema kuwe na Afisa Uganikwa kila kijiji, lakini mpaka sasa hivi bado hatujapata Afisa Uganikwa kila kijiji, ukimuuliza hapa Mbunge mmoja mmoja anaweza akasema hajawahi kumuona Afisa Uganikwenye kijiji chake.

Kwa hiyo, naomba mkakati wa kuendeleza na kuongeza Maafisa Ugani kwa kuomba kibali kwa Waziri mhusika aweze kutoa kibali. Maafisa Ugani wapo… *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, narudia kusema Mwenyezi Mungu akubariki, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Kepteni George Mkuchika.

**MHE. KEPT. MST. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nipate kuchangia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Newala Mjini. Mimi nataka kutangulia kusema naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka nichukue nafasi hii kuwapongeza vijana wangu wa *Young Africans Sports Club* kwa kuchukua ubingwa wa nchi hii kwa mara ya tatu, kama nilivyowaagiza vijana, nataka mje Dodoma, mcheze mpira hapa Dodoma lakini mje na kikombe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka pia niwapongeze vijana wetu wa *Serengeti Boys* kwa kazi nzuri waliyoifanya jana kuifunga Angola. Nataka niwashukuru Watanzania wote waliochangia *Serengeti Boys* kufika mpaka pale na mimi nina imani watafika mbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mkulima wa korosho, kwa hiyo nitazungumza masuala ya korosho. Kwanza, nataka nichukue nafasi hii kuwapongeza sana wakulima wote wa korosho katika nchi hii...

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MHE. KEPT. MST. GEORGE H. MKUCHIKA:** ...kwa sababu mwaka huu zao...

**T A A R I F A**

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kepteni Mkuchika unataka kupewa taarifa na Mheshimiwa Dunstan Kitandula.

**MHE. DUNSTAN L. KITANDULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu nimpe taarifa Mheshimiwa Kepteni mstaafu, kwamba pamoja na pongezi hizo kwa Yanga lakini ipo ile timu bado inaota kupata pointi za mezani, sasa sijui yeye anafikiriaje. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kepteni Mkuchika, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. KEPT. MST. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo nimeipokea na ninawaagiza vijana wa Yanga wakashinde mechi iliyobaki ya Mbao ili mjadala wa mezani usituhusu kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nimesema nawapongeza wakulima wa korosho nchi nzima, mwaka huu limekuwa zao la kwanza kwa kuingiza mapato mengi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, leo mimi nina furaha sana, hakuna mjadala wa Wizara ya Kilimo ninaouchangia kwa raha kama leo kuliko mwaka wa jana. Kuna sehemu moja tu sijaridhika na nitawaambia, lakini nataka nianze kuipongeza Serikali kwa kutufanyia yafuatayo wakulima wa korosho. Kwanza Bodi imeundwa upya, juzi tulikuwa na mkutano wa wadau, ulikuwa mzuri, nawapongeza, hatujawahi kuwa na mkutano wa wadau mzuri kama wa mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka nikupongeze ndugu yangu Waziri kwa kuvunja ule uongozi wa Mfuko wa Uendelezaji wa Zao la Korosho, pale palikuwa pananuka rushwa. Watu waling'ang'ania pale, kila mwaka ni hao hao, ukitaka uwabadili haiwezekani, walikuwa wanafanyaje, wanajua wao. Na tumeona matunda sasa kwamba ule

mfuko umekuja kwenye bodi mwaka huu, nitaeleza baadaye matunda yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza tena Serikali, juzi mmetutangazia, na ninataka wakulima wote wa korosho Mtwara, Mkinga, Pwani, Lindi mjue kwamba Serikali yenu juzi imetutangazia mwaka huu tutagaiwa *sulphur* bure, hiyo ndiyo neema ya Serikali ya Awamu ya Tano, tutagawiwa magunia bure, Mungu akupe nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia nataka kuchukua nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuondoa kero, mimi sitaki kurudia, lakini nataka kutaja zinazonihusu mimi mtu wa korosho. Kero ya unyaufu, mtunza ghala, *task force,* usafirishaji, ushuru wa chama kikuu; ninaiomba tu Serikali mkishafuta haya mhakikishe kwamba mikoani kule inatekelezwa kama mlivyoagiza. Kwa sababu msimu wa mwaka jana kuna mikoa ilipindisha baadhi ya maagizo ambayo mliyatoa, watu kule wakatozwa unyaufu, wakatozwa *task force.* Mheshimiwa Waziri, mimi naomba maagizo yatekelezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nichukue nafasi hii kupongeza sana Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani. Sisi kule Mtwara, Lindi, tunasema Mfumo wa Stakabadhi ya Mazao Ghalani ndiyo mkombozi wetu. Tumepata bei nzuri ya korosho mwaka huu, kubwa sana. Na hii imetokana na ushindani, siku zote wananunua India peke yake, mwaka huu wamekuja Vietnam, ushindani ule ndio umetufanya tupate bei nzuri. Wapo watu wanasema wao ndio wameongeza bei ya korosho, kama wewe umeongeza bei ya korosho, je, nani ameongeza Lindi, nani ameongeza Mkinga?

Mheshimiwa Naibu Spika, korosho mwaka huu tumepata bei nzuri kwa sababu ya ushindani katika mtindo wetu wa stakabadhi ya mazao ghalani kwa sababu ya ujio wa watu wa Vietnam.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkitaka kujua Watanzania kwamba kweli mwaka huu tumenufaika na korosho, mwaka jana wakulima wa korosho tuligawana shilingi bilioni 203 tu

basi, lakini msimu huu uliomalizika tumegawana bilioni mia nane na tisa, kutoka shilingi bilioni 203 mpaka shilingi bilioni 809, hii ni hatua kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nihame hapo niende kwenye ushirika; hapa ndipo niliposema, nimesema na kusema. Mheshimiwa Waziri ushirika una misingi yake, *Rochdale Principles* za *Cooperative Unions. Rochdale Principles* za *Cooperative Unions* zimekuwa ndizo zinazofuatwa na *International Cooperative Alliance.* Moja inasema *democracy* ndani ya vyama, Serikali ihakikishe kwenye ushirika kuna *democracy.* Sisi kule Mtwara tuna chama kinaitwa *TANECU,* kina vyama 55 Newala na 124 Tandahimba, jumla vyama 179, hawawezi kusimamia hawa, kama ingekuwa kompyuta unasema *computer overload,* ndivyo ilivyo *TANECU,* Newala, uongozi unashindwa kwenda chama kwa chama.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepeleka miaka mitatu iliyopita, wameomba vyama Newala kwa muhtasari, Tandahimba kwa muhtasari, tunaomba mkutano mkuu *union* tugawe chama hiki, Mrajisi akaandika barua akasema gaweni, Mrajisi aliyekuwepo amehudhuria mikutano yote, agizo lake la kusema gaweni halikujadiliwa hata siku moja. Naomba Serikali kwa madaraka ya Mrajisi gaweni *TANECU* kwa sababu ndiyo matakwa ya watu wa Tandahimba na Newala. Mwaka jana, mwaka huu *Council* ya Newala, *Council* za Tandahimba wameomba kugawa *TANECU* ili pawe na ufanisi. Ndugu yangu Mheshimiwa Waziri, mimi na wewe tunapatana kweli, tunakosana katika hili moja tu basi, hili ukilimaliza basi! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi nilitaka kusema hayo, lakini neema ya hela iliyoingia mwaka huu Mtwara imesababisha watu wengine kujitokeza uhodari wa wizi hasa kule Masasi, wizi mkubwa kwenye vyama vya msingi, mmekagua mmekuta shilingi bilioni tatu zimeliwa mmewabana wamerudisha, sasa bado shilingi bilioni 1.4 hazijarudi. Mimi naiomba Serikali, viongozi na watendaji walioshirikiana na vyama vya ushirika kutuibia hela yetu ya

korosho wote washughulikiwe na vyombo vya dola, wote, msibague, msishughulike na vingozi wa vyama vya msingi peke yake, tazameni nani alishirikiana nao na yeye aende akasimame mahakamani. Hapo ndipo watu wa Mtwara na Lindi tutafurahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nataka niseme ushirika wa *TANECU* umeandikishwa kama ushirika wa mazao, lakini wananunua korosho peke yake. Naomba Waziri, Vyama vya Ushirika vinunue na mazao mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kwa ushirika, nasema moja ya misingi ya ushirika niliyosema *(Rochdale Principles)* inasema *corporate social responsibility,* chama kikitengeneza faida kirudishe kiasi cha hela ile kwenye jamii, watengeneze barabara, wasaidie shule, wasaidie hospitali, vitanda vya wagonjwa; *TANECU* tangu imetengenezwa faida miaka nenda rudi, tumewasema, juzi ndiyo wameanza kutoa mifuko kumi ya saruji kwa ajili ya sekondari. Hivi hela inayotengenezwa *TANECU* unatoa mifuko kumi, si aibu? Mbona mifuko kumi mimi naweza kuitoa hata ukiniamsha usingizini? Kwa hiyo, wasimamieni, waulizeni kuhusu *corporate social responsibility* wanafanya nini.

Sasa mimi nataka kurukia kwenye suala la mihogo. Mimi nimeshukuru Serikali yetu imesaini mkataba na China, sisi Mtwara ndio wakulima wakubwa wa mihogo, mwaka 1974 nchi hii ilipata njaa, wakati *National Milling* inanunua mihogo tumelisha mikao kumi, mihogo iliyokuwa imenunuliwa na *National Milling* Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mtwara tuko tayari kupeleka mihogo China, Mheshimiwa Waziri tuambie lini inahitajika, tumeacha kulima mihogo kibiashara *(commercially)* tunalima tu ya kula sisi wenyewe, tumefurahi kusikia neema hiyo ya China.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho, naona kengele kama inapiga, sisi kule pia tunalima soya, soya ile imesimama kwa sababu haina soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mwisho, naomba ndugu yangu simamia vile viwanda viwili vya korosho Newala vifufuliwe, wale watu walionunua, kimoja kinafanya kazi kwa robo na kingine hakifanyi kazi kabisa. Ahadi ya Rais alipokuja Newala ilikuwa kwamba viwanda hivi tutavifufua ili wananchi wa Newala wapate ajira...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa, muda wako umekwisha.

**MHE. KEPT. MST. GEORGE H. MKUCHIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Nampongeza sana mdogo wangu Waziri, ameanza vizuri aendelee vizuri pamoja na Naibu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa uchangiaji kwa sasa. Nitasoma majina machache ya Waheshimiwa Wabunge ambao watachangia mchana amabo ni Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko, Mheshimiwa Agness Marwa, Mheshimiwa Oran Njeza, Mheshimiwa Daimu Mpakate na Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali.

Wengine ni Mheshimiwa Joseph Haule, Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Mbaraka Dau, wengine tutaendelea kuwasoma kadiri tutakavyokuwa tunaendelea na uchangiaji.

Baada ya kusema hayo, nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Tukae, Katibu!

**NDG. THEONEST RUHILABAKE – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 - Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na majadiliano tuliyoanza nayo asubuhi, tutaanza na Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko atafuatia, Mheshimiwa Agness Marwa ajiandae.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kupata nafasi, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba yangu nilianzia kwnye bajeti ya Waziri Mkuu nikatoa *50 percent,* nikazungumzia suala la tangawizi ka ulimwengu, nikazungumzia suala la tangawizi kwa Afrika na nikasema nusu nitazungumzia suala la tangawizi kwa Tanzania na ninaanza hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utakapozungumzia tangawizi Tanzania moja kwa moja utaigusa Wilaya ya Same, upande wa Mashariki mwa Wilaya ya Same ambao wao wenyewe katika nchi hii wanalima takribani asilimia 60.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna asilimia 40 iliyobaki, asilimia 40 sasa hivi inalimwa na Songea Vijijini ukienda Jimbo la Madaba wanalima tangawizi sana, ukienda Mkoa wa Kigoma wameanza kulima tangawizi sana kwa hiyo, ukiangalia vizuri Tanzania sasa hivi zao la tangawizi linakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuzungumzie safari ya maendeleo. Maendeleo ni safari ambayo ina misuko suko sana, hasa niongelee maendeleo yanayotupeleka kwenye viwanda na uchumi wa kati. Tusitegemee tufike kwenye viwanda, tufike kwenye uchumi wa kati kwa lele mama ni lazima tukutane na misukosuko mingi. Sasa mimi naomba niizungumzie hii hii tangawizi ya Same Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilianza kuwa Mbunge mwaka 2005 Same Mashariki, niliwakuta wananchi wanalima tangawizi. Mwaka 2007 mimi ndiyo nikaasisi wazo la kujenga Kiwanda cha Kusindika Tangawizi pale Same Masharuki. Tulianza kwa misukosuko mingi, lakini nakumbuka mwaka 2008 Mheshimiwa Waziri Mkuu aliyepita Mheshimiwa Mizengo Pinda alikuja akaweka jiwe la msingi, tukajenga, tukahangaika mimi na Halmashauri na wananchi wakati huo tulikuwa na wana ushirika 613, wao walichangia shilingi 6,000, mimi kama Mbunge pamoja na Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne tulifanya *fund raising* tukapata shilingi milioni 301; Halmashauri ikachangia shilingi milioni 45, lakini na Serikali ikatujengea *godown* lenye thamani ya milioni 287 na safari ikafikia hapo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nizungumze kitu ambacho kinanipa nguvu sana leo na ninaomba Waheshimiwa Wabunge mfurahi pamoja na mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Rais amekuja na kauli ya Tanzania ya viwanda, lakini Mheshimiwa Rais kazi anayofanya ni kuchochea na kuwavuta watu, kuivuta mifuko ya jamii iwekeze kwenye viwanda kwa sababu *by principle* Serikali haijengi viwanda, lakini ina-*facilitate.* Sasa nianze kwa kumshukuru Mheshimiwa Rais, lakini nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI na nashukuru kwamba yupo hapa. Leo nazungumza jambo ambalo limenifariji sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani zangu za pili, tena hizi ni shukrani za unyenyekevu na moyo uliopondeka sana

nipeleke kwa Bodi ya Wadhamini wa *LAPF,* nipeleke shukurani zangu za dhati kwa Mkurugenzi Mkuu wa *LAPF* Ndugu Eliud Sanga kwa sababu *LAPF* imekubali kuingia ubia na kile kiwanda nilichokijenga miaka ile. Leo tunazungumza *LAPF* inakwenda Same Mashariki, inakwenda Miamba, inakwenda kuingiza zaidi ya shilingi bilioni moja kwenye kile kiwanda, sasa hapo unazungumzia ile ndoto niliyokuwa naiona kila siku. Nilikuwa natamani tupate kiwanda kama cha Kaduna, Nigeria kwasababu gani sasa mimi nimepata furaha? *LAPF* inadhania imefanya kitu kidogo, hapana, imefanya mambo matatu makubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, *LAPF* kwa kuingia ubia na Kiwanda kile cha Same Mashariki cha Tangawizi cha Miamba inepanua kilimo cha tangawizi Tanzania kwa sababu wakulima wa tangawizi wa nchi nzima watakuwa na uhakika wa kupata soko. Kiwanda kile kinajengwa na watu wenye uwezo wa kifedha, kinapanuliwa lakini walima tangawizi wote wa nchi hii, walima tangawizi wa Madaba, Wilaya ya Same, Kigoma wote watakuwa wana mahali pa kuuza tangawizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, inatuweka kwenye nafasi nzuri ya sisi kuingia kwenye *export.* Nigeria wenyewe kupitia kiwanda chao cha Kaduna kinachoitwa Kachia wana-*export* asilimia tisa yaani katika soko la dunia ile tangawizi iliyoko kwenye soko la dunia kuna asilimia tisa kutoka Kaduna. Hii ni kwa sababu wana Kiwanda kikubwa cha Tangawizi cha Kachia ambacho kiko kwenye *state* ya Kaduna ambapo wananchi wa Nigeria wanaolima tangawizi wote wanauzia pale na kile kiwanda kina-*export 92 percent* ya tangawizi ambayo inasindikwa pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi ninakiona Kiwanda cha Miamba, hiki ambacho *LAPF* sasa inaingia ubia pale kama ni pacha wa hiki Kiwanda cha Kaduna cha Nigeria. Hivyo hapo lazima tukubali kwamba *LAPF* imemuunga mkono Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Rais anazungumzia viwanda kwenye nchi hii, anachochea viwanda kwenye nchi hii, *LAPF* ilipokwenda kuingia ubia na

kile kiwanda cha tangawizi imemuunga mkono Mheshimiwa Rais, ninawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la tatu ambalo si dogo; hakuna kitu kinachomuumiza mkulima kama alime halafu hana soko. Mimi ninalima tangawizi si kwamba ninaihubiri tu, mimi ni muanzilishi wa kile kiwanda, nalima tangawizi. Kule Same nimekosa nafasi kwa sababu ardhi ya Same yote imejaa tangawizi kwa hiyo imebidi nitafute makazi, mimi nina makazi yangu Madaba kwa Mheshimiwa Mhagama, nalima tangawizi, nimeanza na hekari 20, kuanzia Julai navuna. Hata hivyo siri ya tangawizi si lazima nivune Julai, naweza nikaiacha kwa mwaka mzima, itategemea kama nina soko. Tangawizi unaweza ukaiacha chini ya ardhi kwa mwaka mzima na ikakusubiri upate soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo naomba niseme ukweli kuwa wakulima wa tangawizi ambao tuko Madaba na tuko wengi tunalima tangawizi kwa wingi na sisi hiki kiwanda ni faida kwetu kwa sababu kile kiwanda kitachukua tangawizi ya nchi nzima.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine lazima tujifunze, hiki kiwanda kikubwa kilichoko Nigeria ni mali ya Serikali. Ni Serikali ya Kaduna imekijenga sasa lazima sisi tujipe *big up,* tumeanza wananchi, mimi kama Mbunge nimetoa lile wazo, wananchi 613 wakachangia shilingi 6,000, Rais Kikwete akaniunga mkono kwenye *fund raising* tukapata shilingi milioni 301, Halmashauri ikaniunga mkono na sasa *LAPF* inakuja inatuunga mkono hapo ni lazima tuone kwamba Serikali ya Chama cha Mapinduzi inafanya vizuri. *(Makofi*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumalizia, sitaki kuogongewa kengele. Kwa moyo uliopondeka na kwa unyenyekevu mkubwa niishukuru *LAPF,* nawashukuru sana na huko walipo wajue wameitendea nchi, hawakumfanyia mtu, wameifanyia nchi ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu mkubwa nakushukuru kwa dakika ulizonipa, nampongeza

Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI amesaidia hili kuwezekana namshukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, naona Mbunge wa Madaba amepiga kwa bidii sana pale makofi. Mheshimiwa Daniel Nsanzugwanko atafuatiwa na Mheshimiwa Agness Marwa, Mheshimiwa Oran Njeza ajiandae.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii na mimi. Kwa namna ya pekee naomba nianze kwa kuwatia shime na kuwapa hongera kubwa sana wewe Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu wako, Makatibu Wakuu watatu maana ndiyo Wizara yenye Makatibu Wakuu watatu, hongereni sana kwa kazi pamoja na wataalam walio katika Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni Wizara kubwa na ningeshauri, Mheshimiwa Jenista wewe ni *co-ordinator* wa mambo ya Serikali Bungeni. Hii Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi ni Wizara kubwa sana, mshauri Mheshimiwa Rais aangelie upya muundo wa Wizara hii. Ni Wizara yenye mambo makubwa na yanayogusa watu wetu kwa asilima zaidi ya 75. Ni Wizara yenye mifugo, kilimo, uvuvi pamoja na taasisi 130 chini yake, lakini ni Wizara moja na ina Waziri mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nafikiri kwamba wakati umefika kwa Bunge hili kupitia kwenu Baraza la Mawaziri mumshauri Mheshimiwa Rais wakati mnakunywa naye chai aangalie namna bora ya kui-*restructure.* Wizara hii ni kubwa mno na hata kwenye Kamati sisi tunapata shida kweli kwa sababu ina mambo mengi sana na mambo yote yanagusa maslahi ya wananchi wetu ambao ndio wapiga kura wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hilo pia nitoe pongezi nyingi kwa wataalam wetu, Waheshimiwa

Wabunge sijui mmeangalia ukurasa wa 42, wataalam wetu wa Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi wamepata Tuzo ya *African Union* kwa kuandika mradi ambao umewezesha Wizara yetu kupata shilingi bilioni 44. Mheshimiwa Waziri hongera sana na wataalam wako, na mimi ningedhani sasa pengine hii ndiyo iwe *trend.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo mna wataalam wengi sana, mna wasomi wengi sana, kuna Makatibu Wakuu wataalam wazuri kabisa, nilikuwa nafikiri hii ndiyo iwe *trend* sasa kwamba kwenye mashindano kama haya ambayo yanatolewa na *AU,* hizi nazo ni fursa nyingine za kutuongezea fedha kwenye sekta ya kilimo, hongereni sana kwa kupata shilingi bilioni 44 ambazo zimepatikana kwa kushinda *Award* ya *Global Agriculture and Food Security;* watalaam wa Wizara hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa niliseme, jana Mheshimiwa Waziri Mwijage amelisemeaa vizuri, kwamba Serikali hii ni moja maana kuna baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wanafikiri Serikali hii ni Serikali ya vipande vipande, kwamba kuna Serikali Wizara ya Fedha, kuna Serikali Wizara ya Kilimo, kuna Serikali Wizara ya TAMISEMI. Serikali ni moja, na kwa ushahidi aliouonesha jana Waziri Mheshimiwa Mwijage na wewe ulioutoa leo umefanya vizuri sana kuondoa tozo zilizokuwa kero kwa wakulima wetu, hongereni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kahawa, mimi natoka katika zone ambayo pia tunalima kahawa; tumeshukuru sana hizi tozo 17 ambazo zilikuwa ni kero kwa wakulima wetu, na nina hakika zitasaidia sana kuongeza *morally* ya kuendeleza zao letu la kahawa. Sasa nina mambo mawili, matatu ya ushauri kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza ni kuhusu upatikanaji wa mbolea. Mheshimiwa Waziri tumezungumza sana kwenye Kamati, bahati nzuri mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo. Hili tumelizungumza sana, juu ya umuhimu wa upatikanaji wa mbolea na Serikali mmekuja na mkakati wa

ununuzi wa mbolea kwa pamoja, sisi Wabunge wote tunawaunga mkono kwa asilimia 100. Zoezi hili ni zuri, mbolea hii itatusaidia sana. Jambo ambalo ningeomba tu kulisisitiza ni yale mambo ambayo Mheshimiwa Waziri tuliyazungumza kwenye Kamati ambayo ni muhimu kuyazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli, jana nimemsikia Waziri Muhongo anatuhamasisha kuhusu ujenzi wa Kiwanda chetu cha Mbolea kule Lindi na Mtwara, lakini uko ukweli Waheshimiwa Wabunge kwamba kiwanda hiki kimekuwa kinahujumiwa na taarifa hizi ni za uhakika. Sasa nikutie shime Mheshimiwa Waziri wewe na timu yako, wataalam wako wa *Tanzania Fertilizers Regulatory Authority* wana uwezo mkubwa sana, wasimamie zoezi hili la ununuzi wa mbolea kwa pamoja ili hatimaye bei ya mbolea iweze kushuka na iweze kupatikana katika maeneo mengi ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niweke angalizo dogo tu, kwenye ununuzi wa pamoja kuna changamoto zake kama ambavyo zilikuwepo kwenye ununuzi wa pamoja wa mafuta. Ziko changamoto nyingi na moja ya changamoto kubwa ni hujuma, lazima kutakuwa na watu wenye Makampuni yao watakuwa wanataka kuhujumu *effort* hii ya kuanzisha *bulk procurement.* Nikuombe Mheshimiwa Waziri, mambo ya msingi ya kuzingatia iwe ni pamoja na ku-*mitigate* hizo hujuma, hiyo ni muhimu sana ili isitokee hata siku moja katika nchi yetu tukakosa mbolea eti kwa sababu utaratibu huu wa kununua mbolea kwa pamoja umekuwa na matatizo na umeshindwa kusambaza mbolea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yetu kwamba utaratibu huu wa kununua mbolea kwa pamoja utasaidia mbolea ipatikane kwa bei ya chini kama ilivyo ndoto yetu ya awali, kwamba tungependa mbolea hii ipatikane nchi nzima kama ilivyo *Cocacola* au vocha ya simu. Nina hakika, Mheshimiwa Waziri bahati nzuri tumeyazungumza kwa kirefu kwenye Kamati kwamba haya yote mtayazingatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kushauri na nimelisema sana Mheshimiwa Waziri

ni kuangalia uwezekano wa kuwekeza katika Mikoa inayopata mvua ya kutosha na Mikoa hiyo siyo mingine ni Mkoa wa Katavi, Mkoa wa Kigoma na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Kagera. Haya ni maeneo ambayo yana fursa kubwa sana kwa sababu jiografia yake inaruhusu na tumeshazungumza sana, ni matumaini yangu kwamba jambo hili utalizingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri ametufariji sana juu ya migogoro ya ardhi ya wakulima, wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi pamoja na Mamlaka, Hifadhi za Misitu na Hifadhi za Wanyamapori. Mimi niombe jambo moja, Mheshimiwa Waziri wewe katika jambo hili ni mdau mkuwa sana, jambo hili sasa limalizike. Yale maeneo ambayo yamekosa sifa ya uhifadhi yarejeshwe kwa wananchi ili wayatumie, msing'ang'anie maeneo ambayo hayana faida kwa wananchi wetu. Mheshimiwa Waziri wewe unajua pale kwetu Kasulu kuna hifadhi ya msitu wa Kagera Nkanda, msitu ulioko Makere Kusini, watu wanasumbuka, eneo lenyewe limeshakosa hadhi ya uhifadhi kwa kweli. Ni vizuri maeneo kama haya kama ambavyo tumekuwa tukishauri maeneo yarejeshwe kwa wananchi wayatumie kwa shughuli za kilimo ili waweze kujikimu kwa maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu upatakanaji wa mbegu. Mheshimiwa Waziri nikukumbushe kwamba kuna shamba kubwa la Bugaga, nitapata *comfort* sana kama utakapokuja ku-*wind up* utanieleza namna gani mnajipanga kutumia shamba la Bugaga lenye hekta zaidi ya 1,000. Shamba lile ni kubwa sana, limekaa tu, liko *idle.* Sisi Halmashauri tulilitoa kwa ajili ya kuzalisha mbegu, lakini shamba hili limekaa halitumiki na kama Wizara hamuwezi kulitumia basi nimeshakwambia siku zote mturejeshee kwenye Halmashauri sisi tulitumie kadiri tutakavyoona inafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu Mawakala wa Mbolea kwa masimu wa 2016/2017. Mheshimiwa Waziri umeshatueleza na wadau wamekuja wamezungumza na Waziri Mkuu pia, mmeahidi kuwalipa mawakala wale waliohakikiwa katika kipindi cha mwezi

mmoja, fanyeni zoezi limalizike. Wale mawakala wa mbolea ambao makaratasi yao yako vizuri, ambao hawana matatizo basi walipwe fedha zao, na wale wenye matatizo ndio wasubiri; lakini wale ambao mikataba yao iko vizuri, wamesambaza mbolea kwa wakulima wetu walipwe fedha zao ili kuweza kupunguza tatizo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo linguine, nimeshazungumza a wewe ni kuhusu Chuo cha Kilimo cha Mbondo, tafadhali sana angalia namna bora ya kuweza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Kengele ya kwanza? Ya kwanza eeh? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ni ya pili muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. DANIEL N. NSANZUGWANKO:** Basi nakushukuru Mheshimiwa Waziri naomba uzingatie Mbondo, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Agness Marwa atafuatiwa na Mheshimiwa Oran Njeza, Mheshimiwa Daimu Mpakate ajiandae.

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru sana kunipa nafasi hii ya kipekee ili nichangie Wizara hii. Kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Tizeba kwa kazi nzuri anayoifanya pamoja na Wizara yake nzima kwa sababu kwa kuanzia nimeona kwa kweli mnafanya kazi. Kuna mambo ambayo tumewaomba siku si nyingi sana lakini mmeshayarekebisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kama mvuvi; mimi nimetokea kwenye dagaa dagaa kwa hiyo mimi pia ni mvuvi; nimeona hapa kuna baadhi ya tozo tulizokuwa tunazilalamikia. Kwa mfano kuna hii tozo ya *movement*

*permit,* kuna hizi ada za ukaguzi wa kina wa viwanda na maghala zimepunguzwa, vilevile kuna tozo za vyeti vya afya ambayo ilikuwa inawasambua sana wavuvi hawa. Pamoja na hayo vile vile pia kuna ada za usajili wa vyombo vya uvuvi ambayo ni kati ya vitu ambavyo Mheshimiwa Tizeba na Wizara yake wamevishughulikia, kwa kweli pongezi sana nakupa na Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kipekee bado niendelee kuomba baadhi ya vitu ili waviangalie, pia vipate punguzo kwa ajili ya kuwasaidia wavuvi hawa au hawa wafanyabiashara wa samaki. Kwa mfano sasa hivi ushuru umeongezwa ambapo gunia moja kutoka shilingi 1000 kwenda shilingi 2000, kitendo kinachowapelekea wale wafanyabiashara kukosa faida ambayo wangeitegemea na faida yao ni kidogo sana. Kwa hiyo, wanapotozwa tozo kubwa inasababisha faida zao kupungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia kipekee nimuombe sana Mheshimiwa Tizeba, Mkoa wetu wa Mara ni Mkoa uliozungukwa na Ziwa Victoria, lakini ni kati ya mikoa ambayo mara kwa mara huwa tunakuwa na upungufu wa chakula. Nimuombe Mheshimiwa Tizeba ashughulikie suala hili kwa kushughulikia kilimo cha *irrigation,* kwa maana ya kwamba tuwe na kilimo cha kudumu mkoani kwetu ili sasa tuepukane na hili suala la shida ya chakula cha mara kwa mara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee suala ambalo limezungumziwa jana na Mbunge mwenzangu wa Jimbo la Serengeti, Mheshimiwa Ryoba, kwa kweli Mkoa wa Mara kumekuwa na upungufu wa chakula na ni hali ambayo ipo nchi nzima na dunia nzima ya mabadiliko ya hali ya hali ya hewa. Lakini Mbunge mwenzangu aliongela kwamba chakula sasa hivi hakuna kabisa kwa sababu ya tembo. Mimi nimwambie Mheshimiwa Ryoba, Serikali sikivu, Serikali ya Mheshimiwa Magufuli imeshapeleka chakula mpaka sasa tani 500 na mimi nilimuomba Mheshimiwa Tizeba ambaye aliomba chakula Ofisi ya Waziri Mkuu na wamela na wataleta katika Mikoa mingine yote walioomba. Kwa hiyo, nimuombe

Mheshimiwa Ryoba kwa kuwa yeye ni Mbunge wa Serengeti, mimi ni Mbunge wa Mkoa kwa hiyo kuna taarifa nyingine anapaswa kuniambia mimi ili niwe nampa kwa sababu ameshindwa kusimamia wananchi wake na mimi ndiye nasimamia mambo hayo na nimeomba na wameshaleta chakula. *(Makofi)*

Lakini kutokana na hili suala la tembo, ni kweli linasumbua lakini wanakuja kwa msimu, sio wanakuja siku zote, tembo huwa wanakuja wakati mvua hazinyeshi, yaani wakati wa kiangazi.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Taarifa Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agness kuna taarifa. Mheshimiwa Ryoba.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Agness kwamba mimi Mbunge wa Jimbo la Serengeti na nilisimama hapa Bungeni kuomba Mwongozo kwa mujibu wa Kanuni ya 69(1) na ukamuelekeza Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Tizeba na ndiyo amepeleka mahindi. Sasa hiyo anayosema yeye alishughulika, sijui alishughulika wapi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Agness Marwa unaipokea hiyo taarifa?

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei hiyo taarifa kwa sababu Mheshimiwa anaongopa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, chakula kimeletwa tangu juzi na ripoti ipo, lakini yeye ameomba Mwongozo siku ya jana. Kwa hiyo, Mheshimiwa Ryoba nikuombe unishukuru kwa kazi ninayokufanyia jimboni kwako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna hili suala la tembo. Ni kweli suala sumbufu kwa Wilaya ya Serengeti na

Wialaya zingine. Hawa tembo huwa wanakuja wakati wa kiangazi, wakati mvua zikinyesha hakuna tembo anayekuja kutafuta maji kwa sababu huwa wanakuwa wana maji. Hata hivyo Serikali yetu sikivu imelishughulikia pia suala hili na inaendelea kulishughulikia, na mimi niliongozana na Mheshimiwa Ramo Makani, Naibu Waziri kwa ajili ya kufanya mipango jinsi ya kuziba au kuzuia yale maeneo ili hawa tembo wasiwasumbue wananchi. Nafikiri Mheshimiwa siku hiyo sijui alikuwa na mawazo mengi, lakini tulikuwa naye, sijui kama alisahau. *(Makofi)*

Mheshimwia Naibu Spika, kwa hiyo mimi nimuombe tu Mheshimiwa Mbunge mwenzangu kwamba tukae na tuongee na wananchi wetu, tuwaombe lakini pia tuwaeleweshe kwa sababu ukweli ni kwamba sisi tunapokaa yale maeneo ni maeneo ambayo yamepakana na hifadhi, ambako zile ndizo njia za tembo, kwa mfano, kuna Robanda, Manchila, Kisangula, Sedeko, Mbalibai, Mashoswe, Nata, Mosongo, Nyamatale, Uwanja wa Ndege (maeneo ya Ngalawani), haya yote ni maeneo ya ukanda wa hifadhi. Ki ukweli ni kwamba yale maeneo tunayokaa sisi ni kweli tunaathirika lakini ni maeneo ambayo sisi ndo tumewafuata wale tembo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mimi niwaombe ndugu zangu Wana-Serengeti, kwa hali hii tuvumilie katika kipindi hiki ambacho Serikali yetu inalishughulikia suala hili, na nina imani kabisa ni suala ambalo litaisha na haya matatizo yote yataisha. Hata hivyo tusiwape imani wananchi wote kwamba eti njaa inaletwa na tembo, kuna maeneo mengine ambayo tembo hawafiki, je, huyu Mheshimiwa ambako tembo hawafiki anawapeleka yeye?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna mambo ambayo tunapaswa sisi kuyaongelea kama Wabunge, lakini kuna mambo ambayo hatupaswi kuyalalamikia na kulia kwa muda wote. Tukiwa tunalia sisi wananchi wetu watafanya nini? Tunapaswa sisi tuongee na Serikali yetu kwa lugha ya kuwaonesha au kuwaelekeza kwamba kuna matatizo kwa sababu sisi ndio tunaishi kule, isiwe tu tunakuja tunasema

kwamba ooh kuna hiki kuna hiki, kibaya zaidi tunaenda kufanya kule siasa. Wananchi sasa hivi hawataki siasa wanataka vitendo.

Mheshimiwa Mbunge mwenzangu, basi mimi na wewe tujipange, kile chakula kimeshaletwa, twende tukawagawie wananchi wetu kusudi waepukane na hili tatizo lililokuwepo kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapoongea mabaya na mema pia tuongee. Kuhusu hili hili suala la tembo, kuna fidia ambazo zimeshalipwa na Serikali, sijamsikia Mheshimiwa Mbunge mwenzangu hapa anaisifia Serikali, na bado kuna pesa nyingine ambazo Mheshimiwa Rais ameandaa zitakazokuja kwa awamu nyingine ya pili. Kwa hiyo, wanasema mnyonge mnyongeni, haki yake mpeni. Serikali yetu ni sikivu, Serikali yetu ina nia njema...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Agness Marwa, muda wako umekwisha.

**MHE. AGNESS M. MARWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Daimu Mpakate atafuatiwa na Mheshimiwa Bobali ambaye simuoni, Mheshimiwa Joseph Haule na Mheshimiwa Aida Khenani ajiandae.

**MHE. DAIMU I. MPAKATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi siku ya leo kuchangia katika hotuba hii muhimu ya Wizara ya Kilimo, Uvuvi na Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha leo kusimama katika Bunge letu kuchangia hoja hii. Pili, niishukuru Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kile kilichokifanya katika

Wilaya ya Tunduru kwa kukamilisha ujenzi wa barabara kwa kiwango cha lami, ambao umewezesha wananchi wa Tunduru kupata fursa kubwa ya kusafirisha mazao yao kwa wakati na kwa muda mfupi kuelekea kwenye masoko ya Dar es Salaam na maeneo mengine. Ninaishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili nitakuja kwenye hoja ya Hotuba ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. La kwanza nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuunda mbinu nzuri ya usambazaji wa pembejeo, pembejeo ilikuwa ni kero kubwa sana hasa kwa wakulima wa Tunduru na maeneo mengine kwa sababu mfumo wa ruzuku ulikuwa unagombanisha wakulima pamoja na viongozi wao. Hata hivyo naomba sana jambo hili lichukuliwe maanani sana na lifanyike haraka kwa sababu wale wenzetu, wafanyabiashara ambao walikuwa wanafanya biashara hii hawatapenda mfumo huu uweze kufanikiwa. Kufanikiwa kwa mfumo huu inatakiwa mbolea ije mapema na kwa wakati na isambazwe katika maeneo yote ili wakulima waweze kununua mapema ili waweze kufanikisha malengo ya kilimo chao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kilimo huwezi kuliongelea bila kuliongelea suala la ushirika. Mimi ni mwana ushirika, nimekuwa mtumishi wa ushirika miaka minane, kwa hiyo kuna jambo ambalo ni muhimu Serikali ilitilie maanani sana; na a hii mara ya pili naliongelea suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Tume ya Maendeleo ya Ushirika. Tume hii tangu imeundwa mwaka 2013 bado haijawa na uongozi kwa maana ya Mwenyekiti na Makamishna wake, jambo ambalo linafanya utendaji wa kazi kuwa hafifu zaidi kwa sababu wanafanya bila kuwa na uongozi kamili unaosimamia ushirika.

Pamoja na hayo hata watumishi wa Tume ya Ushirika walio wengi wanakaimu. Unajua mtu akikaimu muda mwingi maamuzi yanakuwa ya mashaka mashaka kutokana na kutokuwa na *title* kamili ya nafasi yake anayoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara ifanye juu chini ili wale wanaokaimu wapewe nafasi ya kuweza kuwahudumia Watanzania na kama hawafai basi wateuliwe wengine ili kuhakikisha kwamba Tume hii inaenda vizuri. Pamoja na hilo, watumishi wa Tume wapo katika ngazi mbili tu, ngazi ya Taifa na Mkoa, huko Wilayani hakuna mwakilishi wa Tume. Walio wengi wanategemea Maafisa Ushirika ambao wapo chini ya Mkurugenzi wa Halmashauri. Hawa wote wanafanya kazi ya ushirika, lakini wanakuwa chini ya Mkurugenzi, Mkurugenzi ana Mamlaka ya kumpa kazi nyingine nje ya ushirika ili aweze kutimiza malengo yake kama Mkurugenzi wa Halmashauri. Kwa hiyo naomba suala la watumishi kutoka Makao Makuu Mkoani basi wafike mpaka Wilayani ili kazi ya Tume iende sawa sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukizungumzia suala la Tume huwezi kuacha shirika hili la *COASCO. COASCO* ndio wasimamizi wakubwa, ndio wanaokagua vyama vya ushirika vyote nchini. *COASCO* hawana watumishi wa kutosha, vyama vyetu vinachukua muda mrefu bila kukaguliwa. Na nilizungumza mara ya mwisho, hata kama ni mtoto wangu umempa ndizi auze mwezi mzima hujamkagua, siku ukienda kumkagua mambo hayataenda vizuri. Hilo ndilo linajitokeza kwenye vyama vyetu vya ushirika. Vyama vyetu vya ushirika vinakaa muda mrefu bila kukaguliwa, naomba sana muimarishe kitengo hiki cha *COASCO* kwa maana ya fedha na watumishi ili kuhakikisha kwamba kila mwaka chama cha ushirika kinakaguliwa ili kujua hesabu zake zinaenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni suala la korosho. Mfumo wa Stakabadhi Ghalani Tunduru ulikwama kwa muda mrefu, mwaka 2011/2012 wakulima hawakupata mafao yao kwa kuwa Mfumo wa Stakabadhi ulileta hitilafu na wakulima wa Tunduru walikosa zaidi ya milioni mia sita themani kutokana na bei ya mazao yalivyouzwa kuwa nje na matarajio ambayo yalikuwepo. Kutokana na hili mwaka jana tumejitahidi tukawahamasisha wakulima wakakubali na sasa mfumo umeenda vizuri, bei imekwenda vizuri, nashukuru tena kwa barabara zile, imeleta wanunuzi wengi Tunduru.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo bado kuna wakulima mpaka leo wanadai korosho zao ambazo ziliuzwa chini ya mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Jambo ambalo linarudisha nyuma jitihada tulizozifanya mwaka jana kuwalazimisha wale wakulima waingie kwenye mfumo wa stakabadhi ghalani.

Kwa hiyo, naomba Wizara kupitia Tume ya Ushirika iende ikakague vyama vile, tuone ni wangapi wamekosa na tuone namna gani hatua gani inachukuliwa kwa wale ambao wamehusika katika kutumia pesa zile za wakulima na wao kusababisha kukosa hela halali kwa ajili ya korosho zao ambazo waliziuza.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado ninaenda huko huko kwenye korosho kwenye suala la *export levy. Export levy* tangu imeanzishwa ilikuwa na lengo kubwa la kuzuia usafirishaji wa korosho nje zikiwa ghafi, na ku-*encourage* kubangua korosho tukiwa ndani ya Tanzania. Hata hivyo lengo hili bado halijakamilika mpaka leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *export levy* asilimia 65 inaenda Bodi ya Korosho, katika asilimia 65 kuna kiasi cha fedha kinachotakiwa kitumike katika kuendeleza ubanguaji; lakini tangu imeanzishwa *export levy* hakuna kiwanda chochote kilichojengwa hadi leo. Naomba sana Mheshimiwa Wizara kupitia Bodi ya Korosho wafikirie namna ya kuitumia *export levy* kubangua korosho kwa wananchi wetu na kutumia *export levy* kuwakopesha wale walioonesha nia ya kuweza kubangua korosho ili kuongeza kipato cha mkulima wa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, ningepena sana Serikali iliangalie suala la kuainisha pembejeo kwa wakulima ili uzalishaji uende sambamba na kalenda ya kilimo kama inavyoeleweka kila mara ambapo kilimo kinatumika. Tunduru na Mkoa wa Ruvuma kwa ujumla ni wakulima wazuri, tuna mahindi mengi, Mpunga Tunduru tunalisha takribani asilimia nusu ya Mkoa wa Lindi na Mtwara wanapata mazao ya mpunga kutoka Tunduru. Mkituletea

mbolea mapema naamini wananchi wetu watanunua mbolea hiyo mapema ili waweze kuzalisha zaidi na kuweza kuepukana na njaa kwa maeneo mengine ambayo hayazalishi kwa wingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Haule, atafuatie na Mheshimiwa Aida Khenani, Mheshimiwa Maftaha Nachuma ajiandae.

**MHE. JOSEPH L. HAULE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuanza kuchangia kwanza nitoe pole kwa wananchi wa Mikumi kwa tahayari kubwa na mshtuko mkubwa ambao umetokea jana baada ya vijana saba kupotea kwenye mazingira ya kutatanisha kwenye Hifadhi ya Mikumi. Hatuna uhakika kama hawa wenzetu wako salama huko waliko au itakuwa ule utaratibu wa kuzika nguo ndugu zetu hatuwaoni. Niwaambie tu ndugu zangu wa Mikumi kwamba tupo pamoja, na mimi nitaungana nao kesho kuangalia ndugu zetu wana hali gani. Niwatoe hofu tu kwamba tumeshalifikisha kwenye sehemu zinazohusika, naamini watatumia muda wao na upendo wao kama Watanzania kuweza kujua wenzetu wapo wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kuchangia kwenye Wizara hii nyeti, Wizara ambayo ni uti wa mgongo wa Tanzania, ambayo inatoa zaidi ya asilimia 75 ya ajira, lakini pia kwa mwaka 2016 imeweza kutoa asilimia 29 ya pato la Taifa. Pia katika Wizara hii ambayo tunasema ni nyeti kumekuwa na changamoto nyingi sana, lakini changamoto kubwa ambayo tunaiona ni changamoto ya bajeti yenyewe. Kwa kuwa kwa mwaka 2016/2017 tunaona kwamba fedha za maendeleo zilikuwa zimetengwa shilingi bilioni 100 lakini mpaka Mei 4, 2017 ilikuwa imekwenda asilimia tatu tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza ukaona ni jinsi gani ambavyo bado kama nchi tuna tatizo. Hii ni shida

kubwa sana kama kweli tunasema kilimo ni uti wa mgongo na unatoa ajira kubwa kwa Watanzania kama hivi; nadhani tunapaswa kujiongeza zaidi ili tuweze kuona jinsi gani tunaweza kuwasaidia wakulima wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hizo pesa ambazo ni shilingi bilioni 100 kuwa zimetengwa, lakini fedha za ndani zinaonekana ni shilingi bilioni 23 tu na fedha ambazo tunategemea wafadhili ni shilingi bilioni 78. Kwa hiyo, hapo napo unaweza ukaona kwamba wafadhili wakileta migomo kama ambavyo inaonekana sitofahamu nyingi, hii nchi inaelekea pabaya zaidi na ndiyo maana kila siku na kila kona unasikia watu wanalia njaa, watu wanalia kuna uhaba wa chakula ingawa visingizio ni vingi kwamba tabianchi nayo inachangia. Hata hivyo pia sisi wenyewe kama nchi hatujajipanga ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2017/2018 inaonekana bajeti kwa ujumla imetengwa shilingi bilioni 267 na kati ya hizo shilingi bilioni 156 ni za maendeleo, shilingi bilioni 150 zipo kwenye Kilimo, shilingi bilioni nne kwa ajili ya Mifugo na shilingi bilioni mbili kwa ajili ya Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ninatokea kwenye Mkoa wa Morogoro ambao Serikali ina mpango wa kuufanya Mkoa wa Morogoro kuwa Ghala la Taifa, kwa sababu Morogoro tumebarikiwa ardhi nzuri, lakini pia ina rutuba na pia inalima aina nyingi za mazao na kila mmea unakubali, na ndiyo maana tumeamua kuwa hivyo, na sababu pia Morogoro ni *center* na vitu kama hivyo. Lakini kwa *style* hii ya kutenga bilioni nne kwa ajili ya mifugo si dhani kama tunakwenda kumaliza tatizo la migogoro ya wakulima na wafugaji. Pia kwenye bajeti hiyo kwa miaka mitatu mfululizo pale Wilayani kwangu Kilosa pesa za bajeti hiyo hazijaweza kufika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nikuombe Mheshimiwa Waziri, utakapokuja utuambie ni kwa nini Kilosa inakuwa inasahaulika sana na kuna upendeleo wa maeneo mengine mengine, lakini Wilaya ya Kilosa ambayo ni Wilaya

nyeti yenye ardhi nzuri na yenye rutuba, imekuwa ikiwa nyuma sana ikipelekewa pesa za maendeleo basi ni kwa miaka mitatu mfululizo. Na kwa *style* hii Mheshimiwa Waziri nataka nikuahidi tutakabana sana mashati kwa sababu sasa tumeamua kuwekeza kwenye kilimo na tunajua ndicho kitakachotutoa kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo wananchi wa Tindiga, Mabwerebwere, Kilangali, Masanze, Muhenda, Malolo ambao wanategemea sana kilimo wamekata tamaa kwa sababu wanaona kama Serikali inawaacha peke yao. Hata zile pembejeo pamoja na madawa, mbolea zinaonekana hazifiki kwa wakati, na ndiyo maana wananchi wa kule wamekuwa na tabu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ni kuhusu wakulima wa miwa ambao ni asilimia kubwa sana katika jimbo letu la Mikumi kwenye kata za Ruhembe, Kidodi pamoja na Ruaha, lakini pia hata watu wa Vidunda na Mikumi wameonekana kulima kilimo hiki cha miwa. Kilimo cha miwa kimetoa ajira kubwa sana kwetu na ninashukuru sana kiwanda cha Ilovo juzi wametangaza bei ya muwa kutoka shilingi 79,000 sasa hivi ni shilingi 101,000, hilo Mheshimiwa Waziri nitakupongeza kidogo; hii ni kwa sababu wakulima wamekuwa wakilia kwa muda mrefu. Hata hivyo bado haitoshi, tunataka kusema kwamba wakulima wa miwa bado wamekuwa na shida kubwa na Mheshimiwa wanakusubiri kwa hamu kwa sababu kilio chao kimeonekana bado hakiwezi kupata *solution* ya kudumu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa miwa sasa hivi wameambiwa na wamepata agizo kutoka Serikalini watoke kwenye vyama vyao vya hiyali vyama vyao vya kiraia waweze kujiunga na vyama vya ushirika. Hilo ni wazo zuri ni wazo jema na mimi kama Mbunge nali-*support* lakini naona kama muda ambao tumewapa wale wakulima ku-*shift* kutoka kule kwenda huku bado ni muda mdogo sana wanahitaji kupata elimu kwa sababu tumeona vyama vingi vya ushirika vikiwa na matatizo kadha wa kadha lazima tuwaeleze faida na hasara hiyo iliwakiweza kujitoa wajitoe

kwa umuhimu na wajue jinsi gani ya kushirikiana na sisi, maana naamini tukiwapa elimu ya kutosha wanaweza nao kushirikiana na sisi. Lakini sasa hivi kuna mgomo baridi Mheshimiwa Waziri wakulima wengine wanagoma wengine wanaenda lakini tunasema tukienda kwa pamoja tukawapa elimu tunaweza tukafanikiwa kwenye hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wa miwa wamekuwa na tatizo lingine, wananchi wengine na wakulima wa nchi zingine wanalipwa pia masuala ya *bagasse* lakini na wanalipwa masuala ya *molasses*. *Bagasse* ni tatizo kubwa ambalo pia kiwanda kinawalipa utamu peke yake yaani *sucrose*. Lakini ingeweza kuwalipa *bagasse* ambayo inatengeneza mashudu, mbolea, pia umeme lakini wakulima hawapati faida yoyote kupitia hiyo. Vilevile *molasses* ambayo inatengeneza *spirit* na inatengeneza pombe, pale pale ilovo kwa pembeni kuna kiwanda cha pombe; lakini wakulima wa kule bonde la Ruhembe hawanufaiki kwa njia yoyote na vile vitu, wanalipwa utamu peke yake, yaani *sucrose. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na hata huo utamu wenyewe umekuwa ukionekana kuwa na walakini, inaonekana *gauge* yenyewe inakwenda kwenye saba mpaka nne wakati wataalamu waliokuja kule wanasema hakuna *gauge* ya saba wala ya nne bali utamu unatakiwa kwenye *gauge* 11 na kuendelea Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbuke kwamba wakulima wa bonde la Ruhembe wanalalamikia kuhusu utamu na wanalalamika sana kwa kusema kwamba hakuna *gauge* nne wala *gauge* saba bali wanapunjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia wana tatizo lingine la mzani, wamekuwa wakiomba kila siku kwamba wanataka wakulima wa nje wawe na mzani wao binafsi kabla ya kuingiza kule kiwandani kwa sababu mtu wa kiwanda yeye ndiye anayepima, yeye ndiye anayepanga bei na yeye ndiye anayefanya kila kitu inawaumiza sana wakulima wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kwa sababu nchi hii inajua umuhimu wa sukari na inatoka kwa wingi kule Kilombero basi jaribu kuwashika mkono wakulima wa miwa wa kule Kilombero ili waweze kufanya na kulima kwa bidii, naamini wakilipwa kwa uwiano huo itawasaidia sana. Ndiyo maana juzi Mheshimiwa Waziri mmekamata magari ya kupeleka miwa ya kutoka Kilombero kwenda Kenya, ni kwa sababu watu wanakimbilia bei nzuri, na hawalipwi utamu peke yake wanalipwa *bagasse,* wanalipwa *molasses* na vitu vingine. Kwa hiyo na sisi naamini tukijiongeza tutaweza kuwatengeneza wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia wakulima wamekuwa wakilalamika kuhusu *DRD,* wanasema zile asilimia za kuingiza miwa mule kiwandani zimekuwa ndogo, iko 40 kwa 60 angalau ingekuwa 50 kwa 50 au 55 kwa 45 ingeweza kuwasaidia kidogo ili miwa iweze kuwa inapatikana kwa wingi. Lakini pia kulikuwa na wazo la kutengeneza kiwanda kingine kule Mfilisi, sasa hatujui hicho kiwanda kimefikia wapi sasa nategemea Mheshimiwa Waziri utakuja kunijibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu migogoro ya wakulima na wafugaji. Nashukuru sana wakati ndugu yangu Augustine Mtitu alipopigwa mkuki wa mdomoni ukatokea shingoni, baada ya kilio kidogo Mheshimiwa Waziri ulifika ingawa ulininyatianyatia, hukufika kwa wakati na hukanishtua vizuri nilisikia tu kwamba umetokea na ukaingia mitini. Napenda siku nyingine ukija jimboni unitaarifu nikiwa kama Mbunge na muwakilishi wa wananchi ili tuweze kujadiliana kwa kina na tuweze kujua jinsi gani tunaweza tukawasaidia wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini migogoro ya wakulima na wafugaji halijakwisha, bado kuna migogoro mingi na ninaamini hili suala ni mtambuka linahitaji Waziri wa Ardhi, Waziri wa Maliasili na Utalii lakini pia na Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi na pamoja na Waziri wa Mambo ya Ndani tuweze kukaa na kulijadili kwa sababu inaonekana upimaji wa ardhi imekuwa ni tatizo kubwa kule Kilosa, lakini pia yale maeneo tengefu yamekuwa yanaongezwa kila siku,

vile vile ardhi imekuwa ni tatizo sana kwa wananchi wa Jimbo la Mikumi na Wilaya ya Kilosa kwa ujumla. Kwa hiyo niombe Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, tumekuomba sana, utakapokuja uturudishie yale mashamba makubwa, mashamba kama Sumagro, Kisanga, *Kilosa Estate, Miyombo Estate* ni mashamba ambayo yameachwa mengi nimashmba pori tunaomba uturudishie iliwananchi waweze kufanya kazi yake yao...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa Joseph Haule, ahsante sana. Mheshimiwa Khenani atafuatiwa na Mheshimiwa Maftaha Nachuma Mheshimiwa Doto Biteko ajiandaae

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana, lakini napenda pia kumshukuru Mwenyezi Mungu kuweza kunifikisha siku ya leo salama na kuchangia Wizara muhimu sana kwa wananchi wangu wa Mkoa wa Rukwa. Tunapozungumzia kilimo, tunazungumzia kitu muhimu sana ndani ya Taifa letu, tunazungumzia kitu muhimu sana kwa wananchi wa Mkoa wa Rukwa, lakini pia tunatazama hali ya uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika haya mazingira tunapozungumza kilimo kunajambo la msingi ambalo ni bajeti. Bajeti ni tatizo; na hata tutakapochangia mambo mengi hapa tunarudi pale pale kwenye bajeti, tutatoa maelezo mengi ushari mwingi suala linarudi pale pale kuhusu bajeti.

Naomba utakapokuja Mheshimiwa Waziri wa Kilimo utuambie mikakati uliyonayo tofauti na miaka iliyopita. Hali ya chakula umeiona, hali ilivyo mbaya unajua ingawa imefikia mahali sasa mnatoa kauli za kufurahishana tu unamfurahisha aliyekutua wakati wananchi wanaumia, tukizungumza hapa zinakuwa *story* tu kama *story* zingine za kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumzia kilimo; sasa hivi ukiwatazama watumishi wa Serikali hawategemei tu mshahara, wamejiingiza kwenye kilimo kwa sababu wanajua kilimo kinalipa; kilimo ndiyo kila kitu. Sasa kama tutashindwa kuwekeza kwenye kilimo tutaondokaje kwenye hii hali tuliyonayo? Pembejeo ni shida, kuna suala tunazungumzia kila kipindi cha bajeti; Benki ya kilimo. Kama maeneo ambayo yanazalisha hiyo Benki haipo, hata wakulima hawaijui tunamalizaje tatizo hili? Hawajui waanzie wapi wala waende wapi na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi kila tunapozungumza majibu yanakuwa ni yale yale. Mimi naomba utakapokuja utuambie angalau mikakati mipya ambayo unayo ili kukitoa kilimo hapa kilipo na hatimaye tuinue uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huwezi kuzungumzia kilimo kwamba wananchi wa Rukwa wananufaika wakati hujawaambia kwamba kwa kipindi hiki ambacho wanategemea kuvuna watauza wapi. Suala la masoko ni muhimu kuliko suala lingine. Sasa hivi tunaendeshwa kwa matamko tu, akipita Mheshimiwa Rais anasema hivi, halafu wewe Waziri wa Kilimo unakuja na matamko mengine, sasa hawa wakulima wamebaki *dilemma,* yaani hawajui wamsikilize nani? Wamsikilize Mheshimiwa Rais wakusikilize wewe Mheshimiwa Waziri wa Kilimo?

Mheshimiwa Naibu Spika, na haya mambo lazima yawekewe utaratibu. Tunajua itifaki zilivyo, lakini tunapozungumzia uchumi kuna watu ambao ni wataalamu panapokuwa na siasa pia tuwasikilize wataalamu hawa, wakulima tunawakatisha tamaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pembejeo tumekuwa tunalizungumza kila siku na hakuna majibu ambayo yanaonesha mwelekeo moja kwa moja wa kuondokana na haya matatizo ambayo wanayapata wakulima juu ya pembejeo. Tunaomba Serikali ipeleke pesa kwa wale wanaonunua pembejeo kwa wakati ili muda ukifika yale maduka yauze kwa bei ya ruzuku na wasaidie wale wakulima. Nilizungumza hapa, ukitazama Mkoa wa

Rukwa mkiwapa pesa wale wakulima wanaopata shida, hawana hata pesa za pembejeo, mkiwapa kipindi cha mwenge hamjawatimizia malengo yao; wapeni kipindi cha kilimo ziwasaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, zitawasaidia wanawake zitawasaidia vijana pia. Kuhusiana na suala hilo utakaa tu wewe na Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, mkatoa tu mwongozo ukafika kule. Sijajua Kiswahili ambacho kinaweza kikawasaidia ni kipi kwa sababu kama maneno tunasema mambo mengi tunazungumza lakini bado utekelezaji unakuwa mgumu. Kipindi nasema nakuja kuchangia Mbunge mmoja akaniambia unaenda kuchangia nini? Nikajiuliza maswali kwa nini ananiambia naenda kuchangia nini, nikamwambia naenda kuchangia kilimo; nini kwenye kilimo, bajeti yenyewe ndio hii! Nimetafakari sana, lakini tutasema tu kwa sababu ndiyo kazi yetu kusema, kama mtasikia sawa msipo sikia sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ajira Tanzania ni shida kwa vijana, vijana hawa wanategemea kilimo, kilimo chenyewe kina matatizo, tuambieni hawa vijana mnawapeleka wapi? Yaani kilimo hamjawasaidia, ajira hakuna mnataka waende wapi?

Mheshimiwa Waziri tunaomba mikakati ya kutosha, yaani hali ya kilimo haifurahishi ingawa unakuja hapa unatuambia hali ya chakula iko vizuri, siju iko vizuri wapi? Kwa sababu ukiangalia bei ya mahindi ya mwaka wa jana, bei ya mahindi kwa kipindi hiki sasa msimu huu wa kilimo bei yake unaiona halafu unasema hali ya chakula, Mheshimiwa Waziri unamfurahisha nani yaani?

Mheshimiwa Naibu Spika, yaani haya mambo unakuwa unamfurahisha nani kwa sababu hali halisi inaonekana. Ni bora ukasema ukweli tukusaidie kama suala ni bajeti hupewi pesa sema tukusaidie ndiyo kazi yetu. Lakini ukija hapa ukafanya mambo ya kufurahishana hatimaye tutaanza kuonana wabaya hapa, tunaweza tukakutuhumu kumbe kosa si wewe kosa ni bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la migogoro ya wakulima na wafugaji yaani umekuwa waimbo, hivi mnataka mtuambie kwamba mmeshindwa kabisa kuwa na mikakati ya kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji? Wataalamu wanafanya kazi gani? Yawezekana ninyi ni wanasiasa, wataalam wenu wameshindwa kuwasaidia jinsi ya kumaliza migogoro ya wakulima na wafugaji au mpaka leo hamjajua tatizo lililopo kati ya wakulima na wafugaji ni nini? na kuna migogoro mingine inachangiwa na ninyi wenyewe Serikali kwa kutokufanya maamuzi haraka ya kumaliza midogo kabla haijawa mikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali tena leo yawezekana ikawa mara ya mwisho. Suala la ardhi, ardhi tunajua ni ndogo na watu wanazidi kuongezeka tupeni sasa mikakati...

**MBUNGE FULANI:** Usikate tamaa.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** ...ya kumaliza migogoro hii yawezekana ndugu zenu hawajaumizwa, lakini kuna watu wamekufa...

**MBUNGE FULANI:** Tuendelee hivyo hivyo

**MHE. AIDA J. KHENANI:** ... roho inakuwa inauma tunapokuja kuwaambia nyinyi hamsikii mnataka tuseme nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningefurahi kama Mheshimiwa Waziri wangu vile ambavyo huwa anaonyesha anasikia tukizungumza leo tunapokuja kipindi kingine tunakuja na kauli nyingine lakini kauli ni hizi hizi na mambo haya haya hivi usikivu unafanyika wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi nishauri tu, yale maamuzi ya kwenda kununua ndege yawezekana yalikuwa sahihi, lakini kama kilimo ni kipaumbele maamuzi yale yalikuwa batili. Huwezi kupanda ndege una njaa, huwezi kupanda ndege una utapiamlo, kama kilimo kilikuwa cha kwanza ni bora basi mngechukua nusu kwanza muingize

kwenye kilimo na nyingine iende huko kununua hiyo ndege. Kwa sababu tunasema kilimo ndiyo kipaumbele. Sasa maji ni shida, kilimo cha umwagiliaji kinapatikanaje?

**MBUNGE FULANI:** Ajabu hapo.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Pembejeo ni shida, bajeti yenyewe uliyopewa shida, haya kwenye masoko yenyewe mpaka leo hamjasema lakini toka acha wakulima wauze bei wanayotaka, sawa watauza halafu wakiuza hiyo bei kwa sababu shida sio bei shida ni pesa hakuna hata hiyo bei atakayopanga nani ataenda kununua hela hamna. Kwa hiyo, kunamazingira mengine matamko haya hayasaidii na yenyewe yanatengeneza migogoro tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mabadiliko ya hali ya hewa imekuwa ndiyo kisingizio, hawa watabiri wa hali ya hewa nao wanaweza wakatusaidia au wakatuathiri, kwa sababu wakulima wanapokuwa wanakwenda kulima wanataka kujua mwaka huu mvua ni nyingi au chache, wanatakiwa kuambiwa walime nini kulingana na hiyo hali ya hewa ya kipindi hicho. Sasa hayo mazingira yanapokuwa yanajitokeza na wakulima nao wanaanza kulima kwa mazoea. Ukitazama hii bajeti ina maana kwa kipindi hiki cha mwaka 2016/2017 wakulima walikuwa wanafanya kazi wao binafsi, ni kama Wizara haipo, kwa utekelezaji huu, Wizara haijawasaidia chochote.

Mheshimia Naibu Spika, suala hili sasa hivi mawakala kule Mkoa wa Rukwa hawajalipwa mpaka leo, kuna watu wameuziwa nyumba zao, kuna watu wamefilisiwa. Lakini kosa sio la kwao ni kosa la Serikali kwa nini inashindwa kuwalipa. Mheshimiwa Waziri ni vyema ukawa mkweli na muwazi tukusaidie. Tukiwa tunazungumza hapa masuala ya kilimo uti wa mgongo sijui kilimo kwanza yaani kauli nyingi ambazo haziendani kabisa na mazingira ya kilimo chenyewe kinavyokwenda. Ni vyema mkawa mnatoa matamko yanayoendana na mazingira mliyonayo. Lakini ukisema hamna pesa wala si dhambi kwa sababu utakuwa umesema ukweli... *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani muda wako umekwisha, Mheshimiwa Aida leo isiwe mara ya mwisho kuzungumza kwa sababu kuna bajeti tatu zinakuja, kuna miaka mitatu mingine ya bajeti inakuja halafu pia hata kipindi hiki cha bajeti hakijaisha bado, kwa hiyo uendelee kuwepo tafadhali na uendelee kuchangia. Nilikuwa nimemuita Mheshimiwa Maftaha Nachuma, nikisema atafuatiwa na Mheshimiwa Doto Biteko, lakini Mheshimiwa Almas Maige atawatangulia hao wawili, Mheshimiwa Almas Maige atafuatiwa na Mheshimiwa Maftaha Nachuma atafuatiwa na Doto Biteko.

**MHE. ALMAS A. MAIGE**: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kuniruhusu na mimi nichangie bajeti hii ya Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Msemaji aliyenitangulia mimi amesema sana, lakini mimi naomba niseme ukweli kwamba Wizara hii inafanya kazi sana. Tuseme ukweli Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi inachukua asilimia 75 ya Watanzania wote, lakini bajeti yao si asilimia 75 ya bajeti yote, hili lieleweke hivyo pia. *(Makofi)*

Kwa hiyo kidogo ambacho wanapata kinatufikia vijijini lakini hakitoshi, si mapungufu ya Wizara hii, ni mapungufu ya hali halisi ya uchumi wa nchi. Nina uhakika Mheshimiwa Rais akifanikiwa katika malengo ambayo anataka kutupeleka tukapata hela za kutosha ataangalia kundi kubwa hili la asilimia 75 ya Watanzania wanaoishi vijijini. Kwa sasa twende kama tulivyo. Hata hivyo tusahihishe makosa ambayo tunafikiri tunayoweza tukayasahihisha ili kuweza kuleta ufanisi zaidi kwenye Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze na kero za asilimia 75 ya Watanzania wote wanaoishi vijijini ambayo ni mbolea au pembejeo za wakulima, lakini pia vyama vya ushirika na tozo kwenye mazao ya wakulima. Nimesoma sana hotuba hii na yote nimemaliza. Ingawa tumeipata leo lakini sikupumzika mchana. Yako mambo ambayo tunaweza

tukayasahihisha, yako mambo tunaweza kusema *okay,* twende nayo mpaka hali itapopendeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na suala la mbolea. Mimi nimegombana, nimepigana sana kupata zile vocha za ruzuku lakini hazisaidii, mbolea haifiki kule, vocha zinafika, wazee wale wasiojua kusoma wanasainishwa vocha lakini mbolea hawakupata, wanapewa hela kidogo na wanaosambaza hizi mbolea za ruzuku wanachukua hela. Lakini nimeona leo Serikali inakuja na mfumo mzuri ambao nillikuwa sikuutegemea kabisa. Mfumo huu tuliutumia kwa ubunifu mkubwa kwenye ununuzi wa mafuta kwa pamoja na *EWURA* wakasimamia. Sasa naambiwa tutanunua mbolea kwa pamoja *(bulk procurement)* halafu Shirika la Mamlaka ya Uboreshaji wa Ubora wa Mbolea lisimamie ununuzi huu. Hii pekeyake ndiye mkombozi wa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kila treni bora ina kasoro yake isije ikatokea usimamizi ukalegalega na hili shirika la usimamizi wa ubora wa mbolea sasa lisimamie usimamizi wa ununuzi wa mbolea bora. Neno ununuzi liongezeke pale ili tuweze kupata bei nzuri na wakulima waweze kununua mbolea kwa hela yao. Sasa hivi haiwezekani mbolea mimi nimekwenda Ulaya kufuatilia bei za mbolea mfuko mmoja wa mbolea dola 25 na hapa tunasema imepunguzwa bei dola 42, 43 mara mbili/mara tatu zaidi. Lakini mbaya zaidi kampuni inayoagiza mbolea iko moja tu, kwa mfano *NPK* na sitaki kuitaja kampuni hiyo. Hiyo ndiyo inayogawa mbolea kwa wauzaji wengine halafu nayo ina-*bid* kwenye *tender* hiyo. Cha kushangaza wale walionunua mbolea kutoka kwake wanakwenda kuuza, yeye anauza ghali ana-*bid* bei ya juu, haiwezekani. Mimi nauza vitu nawagawia wenzangu wanakwenda ku-*bid,* mimi na-*bid* bei ya juu kuliko ninaowauzia mimi, haiwezekani lazima kunaujanja fulani sasa hii itakoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahi sana, nakupongeza sana Mheshimiwa Waziri pamoja na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa kubuni mfumo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala la tozo, tozo imekuwa ndiyo sumu kubwa sana ya kuchukua mapato ya wakulima. Niongelee wakulima wa tumbaku, ambako ndiko natoka. Tozo imekuwa kubwa kiasi kwamba wakulima hawaoni faida yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ku- *declare interest,* nimetembea nchi tano za Ulaya kutafuta wanunuzi wa tumbaku kwa gharama yangu. Nimekwenda Uturuki, Greece, nimekutana na Wakorea kutafuta wanunuzi wa tumbaku. Kwa gharama yangu! Nimeshindwa kupata mnunuzi hata mmoja! Sababu ni nini? Bei ya tumbaku ya Tanzania ni ghali sana kuliko bei zote duniani; na matokeo yake mimi nina bei ya wakulima waliouza Uturuki mwaka 2016. Ubelgiji imeuza Uturuki kilo 34,967,318, kilo milioni na kitu, wakati Tanzania imeuza Uturuki kilo 32,000. Mnaweza mkaona tofauti yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimewauliza kwa nini hamnunui kutoka Tanzania? Sababu kubwa wanasema bei iko juu sana. Bei iko juu kwa sababu ya tozo hizi! Tozo ambazo nimeziona katika hiki kitabu cha Mheshimiwa Waziri, itatusaidia kupunguza bei ya tumbaku ya Tanzania nje. Kwa hiyo, wanunuzi hawa watauza tumbaku nyingi na hivyo watanunua tumbaku nyingi kwa wakulima. Naomba, imesahaulika tozo moja muhimu sana; tozo ya unyaufu, ambayo ndiyo peke yake inayowasaidia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, wale ambao hamjui maana ya unyaufu ni kwamba, wakulima wakiuza tumbaku leo, aliyenunua haji kuichukua. Akija kuichukua kutoka kwenye ghala anaipima tena, anakuta imepungua kilo 400, mia ngapi, wanamkata mkulima. Kwa nini wasinunue na kuichukua tumbaku yao ile? Wanasema kama tungeweza kuiuza kwenye *center* moja, basi gharama ya *center* watalipa wao. Gharama ya kuibeba watabeba wao wenyewe lakini suala la unyaufu halitakuwepo tena. Naomba Mheshimiwa Waziri afute tozo ya unyaufu na atusaidie kuanzisha masoko ya pamoja. Hii itasaidia moja kwa moja kupunguza gharama na kuongeza bei ya mkulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, liko suala lingine ambalo linanisumbua sana, nalo ni ushirika. Vyama vya Ushirika Mheshimiwa Waziri anisaidie sana. Nimemwomba mara nyingi sana kwamba Sheria ya Ushirika ina kasoro nyingi sana; ilitungwa ile Sheria na Wanunuzi. Sheria inasema, bei ya tumbaku itapangwa na wanunuzi na wakulima. Wakulima darasa la saba, wanunuzi wana *degree* tatu. Kutakuwa na ukweli hapo? Matokeo yake wamekuwa wakulima wanaitwa kwenye mikutano mikubwa, wanapewa posho, halafu bei wanapanga wanunuzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja kusema hapa, alete sheria hii. Bunge linatengeneza sheria hapa, turekebishe kipengele kinachosema Serikali hairuhusiwi kabisa ku-*discuss* bei, bei itapangwa na wakulima na wanunuzi. Wanunuzi wana *degree* tatu, wakulima darasa la nne. Inawezekana kweli! Nyie Wanasheria humu ndani mnaona *balance* iko kweli pale! Wala haruhusiwi hata mtu mmoja nje ya mkulima na mnunuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Waziri Mkuu. Waziri Mkuu amesikia maneno mabaya na mambo mabaya, madudu ya Tabora kule kuhusu tumbaku. Waziri Mkuu amevunja Bodi ya Tumbaku jambo ambalo nimekuwa nikimwambia kila siku kwenye mikutano ya mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwambia Waziri wa Kilimo vunja Bodi ya Tumbaku, ilikuwa ngumu, lakini pia Mheshimiwa Waziri Mkuu amevunja Bodi ya *WETCU,* Chama Kikuu cha Ushirika, ambacho wamekuwa wanaogelea kwenye mihela kama vile baharini. Zitakuja na mfumo mzuri wa ununuzi wa tumbaku pamoja na *bulk procurement* ya mbolea, kwa sababu hawa ndio wanaotangaza tenda ya kununua mbolea. Nafikiri atawashirikisha kwenye bodi mpya, wapate Bodi nzuri ambayo itawasaidia wakulima wangu kule Uyui. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa, kuna kituo kinaitwa *OXEN Training Center* kituo cha ku-*train* Maksai pale Upuge kilifunguliwa na Mwalimu Nyerere. Mwalimu amefariki amekwenda mara mbili kuangalia kituo kile. Baada ya kufariki Mwalimu, kituo kimekufa. Hamna aibu! *Land Mark* ya Mwalimu mmeiua! *Mile Stone* ya Mwalimu mmeiua! Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja aniambie *future* ya kituo cha kufundishia wanyama kazi pale Upuge.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku zote nawaachia wenzangu waongee. Naunga mkono hoja hii na kabisa kabisa namuunga mkono Mheshimiwa Rais. Ahsanteni sana kwa kunisikiliza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Maftaha Nachuma, atafuatiwa na Mheshimiwa Doto Biteko na Mheshimiwa Mbaraka Dau ajiandae.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia Wizara hii. Kabla ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu, kwa kuendelea kunipa afya njema, lakini kwa namna ya pekee kabisa, nashukuru kiti chako kwa kuendelea kutenda haki hasa katika upande wetu huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtaalam mmoja anaitwa Kunzi mwaka 1988/1989 aliandika kitabu chake cha *Managerial and Planning* ambacho aliweza kueleza kwamba "*failure to plan is planning to fail,"* yaani siku zote wewe ukishindwa kupanga jambo maana yake ni kwamba unapanga kufeli. Alizungumza Kunzi maneno haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma kitabu hiki cha hotuba hapa, kwa kiasi kikubwa naomba niishukuru Wizara hii kwamba imeweza kuondoa tozo nyingi sana katika zao ambalo kwa kiasi kikubwa linalimwa Mikoa ya Mtwara na Lindi; zao la korosho. Tozo nyingi sana zimeondolewa. Tunashukuru sana Wizara hii kwa sababu kupitia kuondoka ama kuondolewa kwa hizo tozo, hivi sasa bei ya korosho iko juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishukuru pia Wizara hii kwa kuhamasisha wanunuzi wengine kwamba mwaka wa 2016/2017 wanunuzi wa korosho waliweza kuongezeka. Miaka yote tulikuwa na Wahindi tu, lakini mwaka 2016 tumeweza kuona Vietnam na watu kutoka Uturuki wamekuja kununua korosho Mikoa hii ya Mtwara na Lindi na Tanzania kiujumla; na bei sasa imekuwa kubwa kwa sababu kuna ushindani huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo yote, naomba nizungumzie changamoto kadhaa ambazo zipo katika zao hili la korosho hasa mwaka 2016 kwa maana kwamba msimu wa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wakulima wameweza kutueleza Wawakilishi wao, sisi Wabunge; kwa mfano, pale kwangu Mtwara Mjini tuna *AMCOS* mbili; kuna *AMCOS* ya Mikindani na kuna *AMCOS* ya Naliendele. Hivi Vyama vya Msingi vimechukua korosho za wakulima lakini kwa bahati mbaya wameweza kuchukua hizo korosho kupitia minada. Imefanyika, minada zaidi ya minne; mnada wa kwanza mpaka wa nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la ajabu sana, la kushangaza ambalo naomba Mheshimiwa Waziri akija atuletee majibu ya kina kwa wananchi hawa, kwamba hizi *AMCOS* zimeweza kulipa minada miwili ya mwisho, yaani mnada wa tatu na mnada wa nne na wakaacha mnada wa kwanza na wa pili, ambao bei zake zilikuwa ni kubwa kuliko hii minada miwili ya mwisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba akija Mheshimiwa Waziri atupe taarifa, kwa nini hawa wanunuzi wa korosho kupitia hivi vyama vya msingi? Wameruka bei zile kubwa ambazo zilikuwa ni Shi.4,000/= na ilitangazwa kupitia vyombo vya habari kwamba korosho sasa mwaka huu zimepanda, zinauzwa Sh.4,000/= kwa kilo, lakini hawakulipa bei hiyo ya Sh.4,000/= wakaja kulipa minada ya mwisho ambayo imekuja kununuliwa na Wahindi kwa bei ya Sh.3,700/= na Sh.3,600/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa anipe maelezo ya kina katika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naishukuru Wizara hii, imeelezwa hapa kwamba mwaka huu 2017/2018 kutatolewa pembejeo za *sulphur* bure kwa wakulima wa Korosho. Nimesoma kitabu chote hiki mpaka kwenye bajeti yenyewe ambayo ni shilingi bilioni 266, sijaona hata eneo moja hilo ambapo wameweza kueleza kwamba pesa hiyo ya kununua *sulphur* ambayo itaenda kugawiwa bure kwa wakulima wa korosho, imekuwa *indicated* kwenye hiki Kitabu cha bajeti. Sasa isije ikawa tunazungumza tu lakini kwenye bajeti humu hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la kugawa pembejeo bure, ni suala kubwa sana kwa sababu wakulima wa korosho ni wengi; na kama likifanikiwa hili kwa kweli Wizara hii itakuwa imefanya jambo kubwa sana. Kwa hiyo, naomba maelezo ya kina, hizi pesa zimewekwa katika fungu gani? Kama hazijawekwa zinapatikana sehemu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala hili la Taasisi ya *TFC,* Taasisi hii ya kushughulikia pembejeo na mbolea Tanzania. Ni Taasisi ambayo wakati tunapitia kwenye Kamati yetu ya *PIC* ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma, tuliweza kupitia *documents* zake. Ni Taasisi mfu, yaani wanapewa ruzuku kila mwaka, wanapewa pesa nyingi na Serikali, lakini wana madeni kweli kweli! Hawana hata kiwanda kimoja cha kuzalisha mbolea Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashangaa sana, kwa nini tunaendelea kuienzi na kuilea *TFC?* Kwa nini isifutwe? Naomba Mheshimiwa Waziri aje atueleze, kwa nini hili Shirika linaendeshwa kihasara? Halileti tija kwa Taifa letu, halisaidii wakulima lakini bado tunaendelea kulilea. Naomba maelezo ya kina kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa Kilimo na Mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze pia suala hili la uvuvi. Tunashukuru hivi sasa pale Mtwara Mjini kuna jengo lile ambalo inasemekana kwamba litakuwa ni Chuo cha

Uvuvi. Ni muda mrefu hivi sasa, lile jengo limejengwa, hakuna vifaa, hatuoni mkakati wowote wa kuhakikisha kwamba kile chuo kweli kinaanza, wanafunzi wanaanza kusoma pale. Mwaka 2016, tuliongea kwenye bajeti hapa, walieleza katika bajeti yao pia kwamba hiki Chuo kitaanza. Sasa naomba kujua hiki Chuo cha Uvuvi Mikindani pale kitaanza lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, maeneo yale ya Kusini mwa Tanzania lakini maeneo yale ya Magharibi kule, tuna bahari hii ambayo ni bahari ya Hindi ambayo ina samaki wengi sana. Nilieleza hapa mwaka 2016 kwamba Waingereza wanasema maeneo yale ya Kusini yanaitwa, tunasema *it is just virgin sea;* yaani ni bahari bikira ambayo ina samaki ambao hawajawahi kuvuliwa tangu tupate uhuru.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujua kwamba Serikali ina mkakati gani wa kuhakikisha kwamba inanunua vifaa vya uvuvi kwa wavuvi wa maeneo haya ya Kusini? Pia hata kule Ziwa Tanganyika kuna samaki wa kila aina; kule Kigoma ukienda kuna samaki wa kila aina, lakini hawana vifaa vya kisasa vya uvuvi. Naomba Wizara itueleze kwamba mkakati wao wa kusaidia wavuvi ukoje katika kuwasaidia kununua zana za kisasa za uvuvi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kwamba wakati tupo katika *RCC* pale Mtwara tuliweza kupewa taarifa na TAKUKURU kwamba mwaka 2015/2016 wakulima wa Kkrosho wa maeneo ya Mtwara wanadai vyama vya msingi shilingi bilioni 30. Yaani vyama vya msingi vimechukua korosho kwa wakulima, wameenda kuuza, lakini hawajawapa pesa wananchi wale. Shilingi bilioni 30 hazijalipwa, kwa taarifa ya TAKUKURU.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Kiti chako kiamrishe hii Wizara ipeleke TAKUKURU waende kukagua kwenye Vyama hivi vya Msingi kwa sababu wanawaibiwa wakulima sana. Tulivyohoji, tulivyowauliza, wakatuambia siyo shilingi bilioni 30 ni shilingi bilioni 11, lakini taarifa zinasema

na chombo cha uhakika kabisa, TAKUKURU kwamba wakulima wameibiwa shilingi bilioni 30. Tunaomba *CAG* aende akakague Vyama hivi vya Msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, kuna taarifa ambazo siyo rasmi sana, lakini zinazungumzwa na wafanyabiashara wa korosho. Naomba Mheshimiwa Waziri hapa akija atupe majibu kwamba mwaka 2016 kulikuwa na *fraudulent* iliyofanyika bandari ya Mtwara ili iweze kuzuiwa kusafirisha Korosho kupitia bandari ya Mtwara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na wajanja inasemekana ndani ya Wizara yake ambao walikuwa wanaweka vingingi; na inasemekana kwamba ilikuwa kusafirisha korosho kutoka Mtwara tani moja kuelekea Soko la Dunia, ilikuwa ni dola karibu 14,000; lakini kutoa mzigo kutoka bandari ya Dar es Salaam ilikuwa ni dola 400.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba tupate ufafanuzi, kama hilo ni kweli kwa nini iwe hivyo? Lengo ni nini? Kuzuia bandari ya Mtwara isiweze kusafirisha korosho au tatizo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri atuletee majibu ya kina atakapokuja kuhitimisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa haya, naomba kushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Doto Biteko, atafuatiwa na Mheshimiwa Mbaraka Dau na Mheshimiwa Bobali ajiandae.

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii na naomba nimshukuru Mungu kwa kunipa kibali cha kusimama tena ili niweze kuchangia bajeti hii ya Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasahau, naomba nitangulie kuunga mkono hoja iliyowasilishwa na mkwe

wangu, Mheshimiwa Dkt. Tizeba, Waziri wa Kilimo, Mifugo na Uvuvi. Kwa kweli nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, kwa hotuba yake nzuri aliyoiwasilisha hapa Bungeni. Kama tutakuwa wakweli, tutaona kwa vitendo kile ambacho Mheshimiwa Rais wakati wa kampeni alikiahidi Tanzania nzima wakati anazunguka; lile jambo la kuondoa tozo za kero na ushuru mbalimbali wa kero kwa wakulima. Jambo hili watu wengine walikuwa wanadhani ni ndoto, sasa limekuwa kweli kwa sababu leo Mheshimiwa Waziri ametuletea orodha ndefu sana ya tozo mbalimbali ambazo zimefutwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Bukombe, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza jambo hili, kama kawaida yake, mambo mengi ambayo ameyaahidi yamekuwa yakitekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Bukombe wanashukuru sana kwamba Wizara hii kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu tumejengewa soko kubwa sana la kisasa kwa ajili ya wakulima wa muhogo ambalo liko Namonge. Soko hili litasaidia sana wananchi wa Wilaya ya Bukombe na Mkoa wa Geita na nchi jirani, kwa sababu ni soko kubwa sana, linawasaidia hawa wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ile mbegu ya mihogo inayoitwa mkombozi, inazalishwa kwenye Wilaya ya Bukombe, *multiplication* yake inafanyika kwenye Wilaya ya Bukombe ambapo Kata nne na vikundi 52 vinafanya kazi hii. Kazi nzuri sana hii imefanywa na Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Bukombe. Tunawashukuru sana, kwa kweli hili jambo litatusaidia kwa sababu mihogo tuliyokuwa nayo mbegu yake ilikuwa imechoka, isingeweza kuwapatia tija wakulima wa Wilaya ya Bukombe na Mkoa wa Geita. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, natamani nizungumze kidogo juu ya zao la pamba. Tanzania tuna *potential* ya kuzalisha pamba takriban tani milioni moja, lakini kwa sasa

kwa taarifa ambayo Mheshimiwa Waziri amewasilisha hapa, tunazalisha pamba kwa mwaka mzima tani 122,000 peke yake. Kwa hiyo, pamba kwa kweli ambalo lilikuwa ndilo zao muhimu sana kwa wananchi walilokuwa wanalitarajia sana kubadilisha maisha yao, limeanguka na kila mwaka ukiangalia *graph* ya *trend* inashuka kila wakati. Kwa mfano, msimu wa mwaka 2012/2013 tulipata pamba tani 350,000; mwaka 2013/2014 tukapata pamba 249,000; mwaka wa 2015/2016 tukapata tani 149,445; na mwaka huu 2017/2018 Mheshimiwa Waziri ametuonesha dhahiri pale tumepata tani 122,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tumefika hapo? Tumefika hapo kwa sababu tunaona kama zao hili limetelekezwa na wananchi wengi wamekata tamaa ya kulima pamba. Ukienda kwenye Mkoa wa Geita, kwa mfano, msimu wa mwaka 2015/2016 jumla ya ekari 119,701 zililimwa, lakini msimu uliopita pamba imeshuka. Wakulima wengi wamehama kulima pamba, wamelima ekari 73,546 peke yake. Wananchi wamekata tamaa kwa sababu yako maudhi madogo madogo ambayo naomba Mheshimiwa Waziri ayaangalie kwa haraka ili tuweze kuyatatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la kwanza, mbegu ya pamba tuliyonayo (UK 91) ni mbegu ya zamani sana, ya miaka 24 iliyopita, bado iko kwenye *circulation,* matokeo yake mbegu hii haiwezi kuhimili magonjwa, haiwezi kuhimili mabadiliko ya tabianchi na mbegu hii haitupi tija. Sasa hivi Tanzania ekari moja tunazalisha pamba kiasi kidogo sana ukilinganisha na wenzetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitatoa mfano; wastani wa kuzalisha pamba duniani kwa heka, ni tani 2.2. *South Africa* wanazalisha tani tisa; Burkina Faso wanazalisha tani 1.2; Syria tani 4.9; Egypt tani 2.9; na Tanzania 0.7 na Mheshimiwa Waziri anafahamu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningekuwa naruhusiwa na Kanuni za Bunge, nikasema Wabunge wote ambao wamesoma kwa pamba wasimame hapa na wapige kelele,

waseme ndiyo! Utapata kazi sana kuwanyamazisha. Kwa sababu wengi waliomo humu wameishi na wamesomeshwa kwa zao la pamba. Hata hivyo kwa sasa zao hili limekuwa yatima! Kuna kiongozi mmoja kule Wilaya ya Bukombe aliwahi kuwaambia wananchi kwenye mkutano wa hadhara, kwamba achaneni na pamba limeni viazi kwa sababu hakuna mtu anayehangaika nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atuhangaikie zao letu la pamba. Mauzo ya nchi kwa mujibu wa taarifa ya *BOT* yameshuka. Hata hayo yenyewe, utaweza kuona kwa taarifa ya mwezi wa Nne iliyopita, mauzo ya pamba tumeuza dola milioni 43 peke yake, wakati mwaka uliopita tu tuliuza 53.1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri aje na mkakati wa kuwasaidia wakulima juu ya upatikanaji wa pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, najaribu kujiuliza, hivi kwa nini mkulima huyu asiingizwe kwenye *value chain* ya pamba? Tujenge *ginnery* hizo, mkulima aende akauze pamba yake pale; akiwa pale auze sufi, mbegu, achukue mashudu yake akafanyie kazi nyingine. Hivi inakuwaje mkulima anabeba pamba, humo ndani ya pamba anauza na *byproduct* nyingine zote zinakwenda nje ya nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaambiwa pamba yote inayozalishwa Tanzania 70% inakwenda nje ya nchi. Maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba tunapeleka ajira nje ya nchi, tunapeleka uchumi kwa watu wengine. Saa imefika Mheshimiwa Waziri tuje na mkakati, hizi *ginnery,* tupeleke pamba yetu kama mkulima anavyopeleka alizeti kule Singida. Mashudu yawe ya mkulima, mafuta yawe ya mkulima na mbegu iwe ya mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri, mbegu hii tunayotumia ya UK 91, hapa leo atuambie tunaachana nayo lini? Tunahitaji mbegu ya UK M08 ambayo

imethibitishwa kitaalam ambayo *GOT* yake ni 44%. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri hili na lenyewe tuliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine limezungumzwa hapa kuhusu habari ya ushirika. Ushirika ndiyo ilikuwa dawa ya kumsaidia mkulima wa Tanzania. Ushirika umekufa kwa sababu ya wajanja wachache. Kipindi kilichopita Serikali ilipeleka fedha kwa ajili ya kufufua ushirika, ikapeleka *management* kwa ajili ya kuinua ushirika. Leo ushirika huu badala ya kuwasaidia wakulima na wao wamebadilika kuwa wanunuzi wa pamba kama *ginneries* wengine. Nyanza ananunua pamba kama ambavyo sijui shirika gani linanunua pamba; haiwezekani kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakulima wana shida ya pembejeo. Ndiyo maana msimu uliopita wakulima walipatiwa mbegu ya pamba ambayo haikuota, wakulima wakapatiwa madawa ambayo hayakuua wadudu, lakini ikashangaza *ginners* bila aibu wakaenda siku ya kununua pamba wanahitaji kukata fedha kutoka kwa wakulima kwamba walichukua madawa na mbegu. Madawa gani ambayo hayakuua?

Mheshimiwa Naibu Spika, nani alikwamisha? Kwenye mlolongo mzima wa kuagiza pembejeo ni mrefu mno! Kuna *producer* huko juu, kuna *agent* hapa katikati, kuna mtu mwingine ni *quality assurance* ambaye ni *TPRI. TPRI* wakati ule tuko kwenye mgogoro wa madawa, tulihangaika naye sana. Bodi ya Pamba wanaonesha kwamba *TPRI* hajawahi kuleta majibu, kwa nini mbegu haioti? Kwa nini madawa hayakuua wadudu?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri awaonee huruma wananchi hawa, wananchi hawa walisomesha watoto wao kwa pamba na benki yao iliyokuwepo pekee kwa wananchi wa Kanda ya Ziwa na hasa Mkoa wa Geita na Wilaya ya Bukombe kila shilingi waliyokuwa wanaipata walikuwa wananunua mifugo. Mifugo kwa sasa

na yenyewe ina changamoto yake. Sasa hivi kila mtu anayezunguamza anaiona kama jambo baya, jambo ambalo ni laana, mharibifu wa mazingira mkubwa. Wafugaji hawajasaidiwa, kwa namna gani waweze kufuga kisasa?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna watu wanazungumza, punguzeni mifugo; hivi wanapunguza vipi mifugo wakati hata viwanda vya kuchakata nyama hatujavijenga? Namwomba sana Naibu Waziri atusaidie.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nataka kuzungumzia ni kuhusu matrekta...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. DOTO M. BITEKO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mbaraka Dau atafuatiwa na Mheshimiwa Bobali na Mheshimiwa Elias Kwandikwa ajiandae.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia fursa hii. Nami nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia uzima. Nielekeze shukrani zangu kwa mtoa hoja Mheshimiwa Waziri Dkt. Charles Tizeba na Msaidizi wake ndugu yangu, Mheshimiwa William Olenasha.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ilibahatika kuwa na wataalam wenye kuijua Sekta yao. Nampongeza sana pia Katibu Mkuu upande wa Uvuvi, ndugu yangu Dkt. Yohana Budeba ambaye kiasili naye ni mvuvi kama mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesimama hapa kwa huzuni kidogo kwa sababu haya nitakayoyazungumza leo,

kwa kiasi kikubwa sana ndiyo kilio cha wananchi wa Mafia. Kuna Taasisi ya Serikali inaitwa Hifadhi ya Bahari na naamini wapo hapa. Taasisi hii imekuwa ni kero kwa wananchi wa Mafia. Lazima nianze kusema mapema kabisa, hakuna mtu wa Mafia yoyote anayepinga uhifadhi, wote tunaunga mkono uhifadhi; lakini aina ya uhifadhi unaoendelea Mafia na hii Taasisi ya Hifadhi ya Bahari, maarufu kama *HIBAMA* siyo uhifadhi bali ni uporaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi kama jina lake lilivyo, wanatakiwa wahifadhi, lakini badala yake hifadhi ya bahari wamekuwa ni waporaji na wauzaji wa ardhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka nimuulize ndugu yangu Mheshimiwa Dkt. Charles Tizeba, hawa amewatuma waje kuuza ardhi au waje kuhifadhi maeneo ya mazalia ya samaki? Tunataka aje na majibu mazuri kabisa, kwa sababu hivi sasa, hivi ninavyozungumza, hifadhi wameshauza visiwa viwili. Kisiwa cha Shungimbili kimeuzwa, sasa hivi wako katika mchakato wa kuuza Kisiwa cha Mbarakumi na baadaye wanakwenda Nyororo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Hifadhi inasema wakati wanawaondoa hawa wavuvi katika hivi visiwa sheria inasema haya ni maeneo tengefu; na maeneo tengefu hayatakiwi kuwa na makaazi ya kudumu. Wanachofanya hifadhi, wanawaondoa wavuvi, vile visiwa wanaviuza kwa wawekezaji. Sasa inapingana na dhana nzima ya maeneo tengefu. Pale Shungimbili wameuza, imejengwa hoteli ya nyota tano; usiku mmoja dola 10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nikuhakikishie, toka imeuzwa kisiwa kile, Halmashauri ya Mafia haijapata hata senti tano, hatuujui mkataba uko wapi? Tuna sababu gani sisi tena ya kuipenda Hifadhi ya Bahari?

Mheshimiwa Naibu Spika, hoteli ile ya nyota tano iliyojengwa pale, wale wanaoitwa wawekezaji wamebadilisha mpaka jina. Mheshimiwa Simbachawene

nimemwona hapa, labda watusaidie wenzetu waliopo Serikalini, mamlaka ya kubadilisha majina ya maeneo, ni mamlaka ya nani?

Mheshimiwa Naibu Spika, inayoitwa Thanda Hoteli, wala si majungu unaweza uka-*google* ukaiona, Thanda –*'T' for tangle, 'h' for hotel, 'a' for alpha, 'n' for November, 'd' for delta and 'a' for alpha*. Thanda hoteli utaiona pale ukiisha-*google* tu, unaona Thanda Hoteli Mafia. Thanda *Ireland* Hoteli Mafia. Hakuna kitu kama hicho Mafia. Mafia kuna Kisiwa kinaitwa Shungimbili, hakuna kisiwa kinaitwa Thanda *Ireland.* Sasa Mheshimiwa Waziri atakapokuja hapa atuambie mamlaka haya ya kubadilisha mpaka jina la kisiwa wameyapata wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, wamejenga pale hawana hata *building permit. Building permit* anatoa Mkurugenzi wangu wa Halmashauri, yeye mwenyewe anashangaa anasema mimi naona majengo yanaota tu pale kama uyoga. Sasa tunataka kujiuliza wakati wanavichukua visiwa hivi kuvifanya maeneo tengefu, hoja ilikuwa kwamba kuna kiumbe kinaitwa kasa. Kasa anakwenda kupanda pale kutaga mayai.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa leo mmeshawauzia hawa wawekezaji, wameweka miamvuli pale Wazungu wanapunga hewa muda wote; huyo kasa atapanda juu kwenda kutaga mayai saa ngapi katika mazingira kama hayo? Kuna mambo ya ajabu sana yanaendelea pale Mafia. Kuna aina ya uporaji unaoendelea pale. Sasa tunawauliza ninyi mmekuja kuhifadhi, mmekuja kuuza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema wala sitatoa shilingi, lakini nitakachofanya, tutamwandikia Mheshimiwa Rais tumwambie kwamba Mafia inauzwa. Visiwa viwili vilishauzwa, watauza cha tatu, watauza na kisiwa kikubwa, mtatuhamishia sehemu nyingine kwa sababu tumewaambia miaka miwili, hamtaki kusikia. Kwa nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha sana. Hata wananchi kuulizwa basi juu ya ule uwekezaji! Sheria zinasema, hawa watu wa hifadhi wamekuwa na kiburi na ni wababe sana. Wao wanaamini hiyo inayoitwa Sheria ya Hifadhi ina *supersede* sheria zote za nchi; *Local Government Act* mpaka Katiba ya nchi haimo. Wanakwambia hii hifadhi imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge, kwa hiyo sheria nyingine zote hazifai, inayofaa ni Sheria ya Hifadhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana yule bwana anakuja pale anajenga hoteli, hahitaji *building permit*, hawataki kuwashirikisha wananchi, wananchi hawakuulizwa na hakuna mihtasari. Leo hapa nina hii *document;* nilipowauliza mbona wananchi hamkuwauliza? Wanasema wananchi tumewauliza, wakaenda kukaa na watu wanane pale Kirongwe baadaye ndiyo wanasema wananchi tumewauliza sisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda sana nimwulize ndugu yangu Mheshimiwa Tizeba, kaka yangu, tena rafiki yangu sana; mambo haya yangefanyika kule Buchosa, yeye angekubali? Yeye ana visiwa kule; vingeuzwa visiwa vya Buchosa angekubali? Kwa sababu kila siku namwambia kitu hiki hiki kimoja hataki kusikia, kwa nini? Tunataka aje na majibu thabiti kabisa, kwa nini hifadhi ya bahari wanaendelea kuuza visiwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huo unaoitwa uhifadhi. Nenda pale Kigamboni Dar es Salaam kule Kijiji *Beach, South Beach* kule maeneo yale kaa kuanzia asubuhi mpaka jioni, yanapigwa mabomu utafikiri nchi iko kwenye vita na Ikulu iko pale pale. Hawa watu wa hifadhi wanaacha kwenda kukamata wapiga mabomu pale, wanakwenda kuuza visiwa kule Mafia, hatutakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi wanahamisha wananchi wa Nyororo, wavuvi wa pale, wamekaa karibuni miaka 15 wanawaondoa wanataka kuweka hoteli nyingine ya Nyota tano. Kisa nini? Wanasema sasa haya ni maeneo ya tengefu. Tunasema maeneo tengefu kusiwe na makazi ya

kudumu. Kwa nini mnawatoa wavuvi halafu mnajenga hoteli? Hatutakubali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Jibondo, kisiwa kingine hiki; ndugu yangu Kwandikwa anafahamu sana haya. Wananchi wa Jibondo hivi sasa wako *siege* hawawezi kwenda kufanya shughuli zozote, wamezuiwa na watu wa hifadhi wasivue. Sasa tunawauliza, mmekuja kuwasaidia wananchi kuwahifadhi au kuwamaliza? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuona kwamba uvuvi umeshindikana, wakaamua kulima kilimo cha mwani baharini. Wakalima wakapata mwani mwingi sana, wakaweka katika ma-*godown* yao. Imekuja meli kupakia ule mwani na kupeleka sokoni. Hifadhi ya bahari wanasema ile meli inavunja matumbawe, inaharibu mazingira. Kwa hiyo, hairuhusiwi kuingia, ule mzigo umeozea ndani. Nataka tuwaulize tu ndugu zangu, hivi ninyi hamna huruma? Hawa watu wa hifadhi hamna huruma? Watu mzigo umejaa ndani, hawaruhusiwi kwenda kuuza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dau, ahsante sana, muda wako umekwisha.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Dau naona Mawaziri wengi wako hapa, nadhani umechangia Wizara nyingi katika huu mchango wako. Nadhani kila Waziri atajichagulia ya kwake yanayomhusu, kwa hiyo, Wizara husika itakapofika pengine watakupa majibu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Hamidu Hassan Bobali, atafuatiwa na Mheshimiwa Elias Kwandikwa na Mheshimiwa Omary Mgumba ajiandae.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza nasikitika kwamba nitachangia huu mchango wakati Waziri wa Fedha hayupo na hata Naibu wake hayupo, kwa hiyo, mambo mengi ambayo nitayasema hapa wao hawatayasikia.

**NAIBU SPIKA:** Nikutoe wasiwasi Mheshimiwa Bobali, Mheshimiwa Jenista, bosi wao yuko pale, kwa hiyo usitie shaka, atawapelekea ujumbe.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante naomba awafikishie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo. Kiukweli kabisa naunga mkono hotuba yetu ya Kamati yetu ya Kilimo. Waheshimiwa Wabunge mtakuwa mashahidi, hii Kamati katika Bunge hili la bajeti tumekuja na hotuba ambazo ni *very constructive.* Tumefanya hivyo kwenye Wizara ya Maji na leo tumerudia tena. Nampongeza zana Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Mary Nagu kwa kazi nzuri aliyoifanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mheshimiwa Waziri, hebu ajaribu kuchukua ile hotuba ile ya Kamati yetu tunafanya kazi pamoja, aiangalie. Tumeshauri vitu vya msingi sana kwa maslahi ya Taifa. Shida ninayoiona ambayo siku zote tunaeleza kwenye Kamati, Mheshimiwa Waziri hauna fedha. Hapewi pesa! Watu wanasema zaidi ya 75% ya Watanzania ni wakulima. Haifanani na fedha ambayo anaipata na ndiyo maana nikasema Waziri wa Fedha labda angekuwepo angetusikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengi wanalalamika humu ndani, kwa nini hii Wizara haipewi fedha inazotengewa? Kwa nini Wizara ya kilimo ambayo ndiyo tunasema uti wa mgongo wa Taifa letu, fedha zinazotengewa tunapata pungufu? Mheshimiwa Waziri, sijui kama kuna Wizara ambayo imepata fedha chache kuliko hii!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunavyochangia hapa tujue kwamba tunachangia kwa hotuba nzuri ya Waziri na kwa maneno mazuri aliyotuambia, lakini *in reality* hii Wizara haijapata fedha. Mwenyekiti wetu amesema hapa, fedha ya *development* ni asilimia 3.8; ni jambo la aibu sana! Sasa kama tunapata fedha ndogo kiasi hicho, tunadhani haya mambo tuliyoyazungumza yatafanikiwaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Jenista amfikishie Mheshimiwa Waziri wa Fedha; tumemkosea nini Watanzania; ambapo 75% ya Watanzania ni wakulima? Kwa nini hapeleki fedha kwenye Wizara ya Kilimo? Hilo ndio jambo langu la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, katika hotuba yetu ya Kamati tumezungumzia suala la *bulk procurement* ya mbolea. Kama kuna mtu yeyote aliyejiandaa kupinga huu mfumo, sisi kama Wajumbe wa Kamati, nami nasema huyo mtu kwa kweli labda ana maslahi yake mengine lakini siyo maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mbolea linajulikana namna lilivyokuwa na utata, lakini jambo hili sisi pale Kilwa kunajengwa Kiwanda cha Mbolea. Kwa hiyo, tunahitaji na hawa ambao leo wanapinga, ndio hao hao wanafanya mipango ya kuhujumu kile Kiwanda cha Mbolea. Kwa hiyo, jambo hili linabeba maslahi ya Taifa, linabea maslahi mapana kabisa ya nchi yetu. Naomba jambo hili lianze haraka, mbolea ianze kuagizwa kwa mfumo huo; litakuja kutusaidia kama Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposimama kwenye maslahi ya Taifa, haya mambo ya itikadi zetu na mambo mengine tunaweka pembeni kwa sababu tunajenga nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nizungumze pale alipoishia jirani yangu ndugu yangu Mheshimiwa Dau; amelalamika sana kuhusu masuala ya uvuvi. Kwenye fikra

yangu nafikiri hii Wizara kubwa kwa sababu hata kwenye matamshi yake inaitwa Wizara ya Kilimo, Mifugo, yaani huo uvuvi wenyewe ndiyo umetamkwa mwishoni kabisa "na Uvuvi;" yaani *as if* ni *supplementary,* yaani uvuvi ni kama *additional. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoamini ni kwamba kuna nchi kadhaa duniani zimepiga hatua kubwa ya maendeleo kwa kutegemea uvuvi na tunayo mifano mingi katika hili. Sasa Mheshimiwa Waziri hebu angalia namna gani unatoa kipaumbele kwenye sekta ya uvuvi, leo tuna uvuvi wa bahari kuu, kuna nchi zinaendesha nchi zao kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu tu. Wapo wazungumzaji wamesema hapa kwamba lipo eneo kama Lindi na Mtwara ni kama ni *virgin sea,* bahari ambayo haijatumika kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna mifano mingine, kulikuwa na samaki walikamatwa hapa, walikuwa wanaitwa samaki wa Magufuli, wakati ule Mheshimiwa Rais alikuwa Waziri wa Uvuvi. Wale samaki walikamatwa walivuliwa siku tatu tu walipokwenda kuuzwa thamani yake ilikuwa zaidi ya bilioni tatu, kwa mtu ambaye tulimpa leseni ya shilingi milioni 800 kwa mwaka kuvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo hili liangaliwe. Tukitegemea kupata mapato ya uvuvi wa bahari kuu kwa kutegemea leseni, *we are very wrong* na hatutaendelea. Tuwekeze sisi wenyewe, tuwawezeshe wavuvi wetu wa ndani waweze kuwa na uwezo wa kuvua bahari kuu. Tuna samaki wengi kule. Vile vile jambo hili liende sambamba na ujenzi wa bandari ya uvuvi, ili hata hawa wavuvi ambao leo tunawapa leseni, wakishavua waweze kushushia mzigo wao hapa Tanzania tuweze kukusanya kodi. Jambo hili kila siku tunalisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bahari kuna lasilimali nyingi. Leo ukitoka Tanga mpaka Mtwara watu walio karibu na bahari kwa bahati mbaya ndio maskini, yaani nchi hii ukikaa karibu na bahari wewe ndio kama umepigwa laana; wewe ndio maskini; wakati bahari ni utajiri. Leo

tunajua kuna mikoa mingi nchi hii wanategemea uvuvi, ukiwemo na Mkoa anaotoka Mheshimiwa Waziri; hawa wavuvi tunawasaidiaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo uvuvi tumeuweka ni kama *additional,* kama *supplementary.* Naomba sana, Katibu Mkuu wa Wizara namfahamu, ni mtu mzuri, ni mchapakazi, wamwezeshe, wampe pesa! Hawezi kufanya kazi! Hili nalalamika tena kwa Waziri wa Fedha, leo Sekta ya Uvuvi imeachwa kabisa. Ukiangalia mafungu, fedha walizozipata ni *as if* sisi nchi hii hatuna wavuvi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri naomba sana suala hili tulizingatie kwa umakini mkubwa sana, litatusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais aliyepita alianzisha harakati za ujenzi wa bandari ya uvuvi, nataka kujua wameishia wapi? Tunataka tupate majibu ya kutosha kwamba ile bandari ya uvuvi iliyokuwa inataka kujengwa, mpaka leo imefikia wapi? Naamini kuna hatua kadhaa zilishachukuliwa, sasa je, wao ndio wameacha kabisa au wanaendelea? Mheshimiwa Waziri, naomba atakapokuja aje kunijibu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la *NFRA.* Suala la chakula ni jambo muhimu sana. Hatuwezi kuwa na nchi ambayo haina chakula na hatuwezi kuwa na watu ambao watakuwa wanafanya kazi vizuri kama chakula hakuna. Mwaka huu tumeingia kwenye matatizo makubwa, wengine wanasema kuna njaa, wengine hakuna njaa, wengine kumekuwa na shida. Pia, hebu tujipime kama nchi; hifadhi yetu ya chakula ina kiasi gani cha chakula cha kuweza kutulisha? Kumekuwa na majanga mengi sasa hivi yanatokea kama ukame. Unaona Mkoa wa Dodoma uko na ukame mwaka huu na mikoa mingine. Uzalishaji wetu wa chakula umekuwa mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NFRA* hawaipi kabisa kipaumbele. Nawaambia, ukitokea mwaka mmoja hapa kama Wabunge wangekuwa wanajua kwamba ingetokea

Mwenyezi Mungu akatupiga gharika hapa miezi mitatu; siyo jambo la kuombea na siombei na leo siku ya Ijumaa, Mwenyezi Mungu hili jambo atuepushie.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikitokea miezi mitatu tu nchi hii ikaingia njaa, nchi hii tunaparaganyika kabisa, kwa sababu hifadhi yetu ya chakula haiwezi kukidhi haja hata ya miezi miwili kulisha nchi hii. Leo mwaka 2017/2018 bajeti iliyopita *NFRA* ilitengewa shilingi bilioni 18 iweze kununua mahindi na nafaka. Mpaka hivi sasa tunapozungumza, mmeipa shilingi bilioni tisa tu. Yaani ni nusu ya fedha ambayo tumeitengea. Hata hii tulilalamikia kwamba ilikuwa ni fedha ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakupa mfano, mwaka 2014/2015, wakati wa Serikali ya Awamu ya Nne, Serikali ilitenga shilingi bilioni 109,656 kwa ajili ya *NFRA,* lakini ilitoa zaidi ya asilimia 110; Serikali ilitoa shilingi bilioni 111. *9.* Leo mwaka 2016/2017 tunatoa bilioni tisa, *are we serious?* Hatuoni kwamba kuna mabadiliko ya tabianchi? Hatuoni kwamba hali ya uzalishaji wa chakula inapungua? Kwamba tumeifanyaje hiyo *NFRA? (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, suala la chakula; chakula ni siasa, *food is politics, food is life;* chakula ni maisha pia. Kwa hiyo, tusicheze na jambo hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie jambo la mwisho, naona muda unakwenda. Mheshimiwa Esther, naomba kidogo Mheshimiwa Waziri wa Maliasili anisikilize na Mheshimiwa Waziri wa Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilisema pale Wizarani kwamba sisi tunafanya kazi kubwa kuwahimiza wakulima waweze kulima ili baadaye wajinasue na matatizo yao ikiwepo kuondoa njaa. Leo ndovu (maana nikisema tembo kuna watu wengine nawakwaza) mpaka hivi sasa ninavyokwambia, tangu juzi nimeomba Mwongozo hapa, mpaka hivi sasa wameshakula zaidi ya ekari 45 za wakulima. Mwaka 2016 zililiwa ekari 183, hakuna hatua iliyochukuliwa.

Hivi sasa ninapowaambia, hao ndovu wako Mchinga wanatembea tu kama mbuzi. Kwa hiyo, nasema na mwaka 2016 nilisema hapa, msituone wapole, nasi tunawaachia kwa sababu sisi tunajua kwamba ndovu ni rasilimali ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkulima ni mtu mnyonge. Ikifika siku akachoka, akaamua kufanya hicho anachokiweza, tusije tukalaumiana. Lazima tuliseme hilo! Haiwezekani mtu ambaye mwaka 2016 ameliwa ekari 183 hakuna hatua iliyochukuliwa. Naibu Waziri wa Maliasili amekwenda anasema kwamba tutawaletea hiyo laki moja kwa kila ekari, tangu mwaka 2016 amekwenda, mpaka leo hakuna hatua iliyochukuliwa. Leo hao hao ndovu wanakula tena!

Mheshimiwa Naibu Spika, ndovu wanatoka mbali sana, sisi hatujapakana na hifadhi, wamekuja kwa sababu ya mazingira mazuri tuliyonayo kwamba tuna misitu ya asili, tuna maeneo yana maji na bahari. Wakifika wanakaa msituni, usiku wanakwenda kula kwenye mashamba ya watu, mchana wanakwenda kupata upepo wa bahari, ndiyo mazingira yaliyowavutia! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema *very serious,* juzi nimeomba Mwongozo hapa lakini mpaka sasa hakuna hatua iliyochukuliwa Mheshimiwa Waziri. Nazungumza kwenye Wizara hii kwa sababu wale watu watakapoishiwa chakula, watapeleka tena. Juzi walipeleka tani 500 kwa sababu chakula kimekwisha. Nikienda tena kuwaomba tani 1,000 wasininyime kwa sababu ndovu ambaye anawatunza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili wanakula vyakula vya wakulima wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Elias Kwandikwa, atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Mgumba na Mheshimiwa Ignas Malocha, ajiandae.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia katika hii hotuba muhimu. Kwa kweli kwanza nianze kwa kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru sana Serikali; naishukuru sana Wizara hii, naungana na wasemaji waliotangulia, ukiangalia hotuba hii kwa kweli imeanza kutupa suluhisho la matatizo katika kilimo. Mambo mengi ambayo yameonekana kwenye hotuba hii nawiwa kutoa shukrani sana kwa Mheshimiwa Waziri Tizeba na timu yake. Naona sasa kwamba iko dhamira ya kusaidia wakulima tuweze kuinua uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru pia wananchi wa Ushetu kwa kutoa mchango mkubwa sana katika kilimo. Kilimo chetu katika eneo letu ndiyo kinatupa pia mapato ya kutosha katika Halmashauri kupitia mazao ya biashara; pamba na tumbaku, tunaweza kuendesha vizuri na kutoa huduma vizuri katika Halmashauri yetu. Kwa hiyo, nawapongeza sana wananchi pia kwa uvumilivu. Tumekuwa na shida kubwa, katika msimu uliopita hatukupata kabisa pembejeo kwa mazao mengine, lakini pamoja na hayo naona tulikuwa tumeweka nguvu kubwa sana kuhakikisha kwamba tunaweza kuzalisha chakula na mazao mengine ya biashara vya kutosha. Kwa hiyo, nawapongeza sana wananchi wa Ushetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ni uti wa mgongo. Utaona katika hotuba hii, Mheshimiwa Waziri amerejea kutukumbusha kwamba kilimo kinachangia sehemu kubwa la pato la Taifa, kinaajiri watu wengi. Sisi tuseme kwa upande wa kwetu Ushetu, kilimo ndiyo hicho ambacho tunakitegemea kiweze kututoa katika huu umaskini. Kwa sababu mimi naweza kusema kwamba asilimia mia moja ya wananchi wa Ushetu tunajihusisha katika kilimo. Iwe ni Mbunge, nalima; Diwani, analima; awe ni mfanyabishara, analima. Kwa hiyo, watu wote wanajishughulisha na shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaona kabisa sisi ni wadau wakubwa na tunahitaji sana hii Serikali itusaidie ili tuweze kusonga mbele zaidi. Kwetu hata wanafunzi pia wana mashamba. Kwa wale wenzangu wanajua jilaba, kwamba tuna mashamba madogo madogo ya wanafunzi. Hata watoto wadogo wa shule wana *part time* ya kulima, wanakuwa na mashamba. Kwa maana hiyo, tunaona uko umuhimu sana kwamba tunawazoesha watoto kwa nia ya kuona kwamba wanathamini hiki kilimo kweli na ni uti wa mgongo wa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo hapa nataka niyaseme tu kwa ufupi sana. Kwanza naiomba sana Serikali kupitia Wizara hii, iweke dhamira ya kweli kuweza kuhakikisha kwamba haya ambayo yapo kwenye hotuba yanatekelezwa ili yaweze kutusaidia. Kwa sababu utaona kabisa kwamba ni muhimu tuzalishe ili tuwe na chakula cha kutosha na kwa kweli tutakuwa tunaweza kuinua uchumi katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri sana Serikali pia iangalie na kuchambua, kuna mambo ambayo tunayaona kwenye ripoti. Kwa sababu nilikuwa nikiangalia taarifa ya *BOT* ya Mwezi Machi, 2017, naona ile *trend* ya uzalishaji mazao, bei na mauzo ya nje imekuwa ikishuka. Sasa naishauri tu Serikali ifanyie kazi, ichambue vya kutosha ili baadaye tuweze kupata suluhisho la kuona kwa nini wakati wote uzalishaji, bei na mauzo yanaendelea kushuka?

Mheshimiwa Naibu Spika, naweza kutolea mfano katika zao la tumbaku ambalo sisi tunalizalisha kwa wingi. Nimeona mauzo ya tumbaku yamekuwa yakishuka sana. Kuanzia mwaka 2013 tuliweza kuwa na mauzo ya dola milioni 7.3 lakini mwaka uliofuatia (2015) tuliweza kufikia dola milioni 41.2; lakini utaona kabisa mwaka 2017 kuna dola 9.4, tulishuka sana. Sasa na mazao mengine ya kahawa, pamba, katani, korosho na karafuu, utaona kuanzia mwaka 2013 mpaka 2017 tumekuwa tukiendelea kushuka, lakini pia ule uzalishaji kwa ujumla utaona nao umeshuka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa nasoma nikaona kwamba mwaka 2013 pia tulikuwa na tani chache ambazo tulikuwa tumezalisha, lakini mwaka 2015 kulikuwa na uzalishaji mkubwa wa zao hili la tumbaku lakini mwaka 2017 pia tumeshuka karibu nusu. Lazima tuseme kwa nini tunashuka hivyo? Kwa hiyo, nafikiri hizi *data* zinazopatikana ni vizuri Serikali ikazifanyia kazi ili tuweze kuinua uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli kilimo ni muhimu kwa sababu nilikuwa naangalia uwiano tu wa mazao ambayo tuliuza nje, ukilinganisha na maeneo mengine ambayo tulikuwa tumejipatia kipato, tumesafirisha madini na bidhaa nyingine za plastiki na kadhalika. Sasa kwenye kilimo, mifugo na uvuvi tulikuwa tumepata kati ya asilimia 59 hadi 64 ndiyo mchango wake. Kwa hiyo, unaona kabisa kwenye eneo hili ni muhimu sana kulitazama ili tuweze kusonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwetu tunapata mvua mapema kuanzia Septemba. Kwa hiyo, niisihi tu Serikali yangu kupitia Wizara hii kwamba suala la pembejeo liwekewe umuhimu wa hali ya juu kwamba ikifika mwezi wa Tisa tuweze kupata hizi pembejeo mapema kama mbolea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeze sana Serikali kwa kuja na utaratibu huu wa kuagiza hii mbolea kwa pamoja kwa sababu ilikuwa ni tatizo kubwa sana. Hili zoezi la mbolea likisimamiwa vizuri kwa kuzingatia kwamba wananchi katika baadhi ya Kata zetu zimekuwa ni *model,* tunazalisha kuanzia gunia 25 hadi 30 kwa ekari endapo tunalima kwa wakati na kutumia pembejeo kwa usahihi. Ziko Kata ambazo zimeonesha mfano, kama Kata ya Kinamapula, Kata ya Ubagwe, Kata ya Ulewe, zimeweza kuzalisha hadi magunia 30 kwa ekari.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa mwaka uliopita 2016 hatukupata pembejeo hizi kabisa kwamba wananchi wamekuwa na manung'uniko kwa kukosa mbolea. Kwa hiyo, naiomba tu Serikali kwa kipindi hiki kinachokuja na kwa vile tumeendelea kuwaahidi wananchi kupitia vikao vyetu

kwamba Serikali inajipanga katika utaratibu mzuri, ambao ndiyo huu sasa Wizara imekuja nao, kuhakikisha wananchi wapate hii mbolea ya kutosha lakini waipate kwa wakati ili sasa twende tukazalishe; na tuweze kuhakikisha kwamba hili suala la njaa linaondoka kabisa na uchumi unakwenda juu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine Mheshimiwa Waziri atusaidie; kwa vile tunazalisha chakula cha kutosha na kumekuwa na shida sana ya soko la mazao ya chakula hapo mwanzoni tunapoanza kuvuna, kama inawezekana kupitia Halmashauri zetu Mheshimwia Waziri asaidie tupate maghala ya Halmashauri ili tuweze kuhifadhi chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati huo huo wananchi wanahitaji tena kupata fedha kwa haraka kwa ajili ya maandilizi ya kilimo, waweze kuuza na kupata fedha. Wakati huo tutakuwa tunahifadhi chakula kwa ajili ya matumizi ya Taifa kwa ujumla na wananchi wanapata fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana tuliangalie hili, kwa sababu kama chakula kinazalishwa kwa wingi na wananchi wanategemea kuweza kupata fedha kutokana na ziada kwa ajili ya kushughulikia mambo yao mbalimbali pamoja na maandalizi ya kilimo kwa msimu unaofuata, tunavyofanya zuio la wananchi kufanya mauzo ya chakula hiki cha ziada, kwa kweli inatuharibia ile *trend* nzuri ya kwenda kuzalisha kwa wingi msimu mpya. Naomba hii tuitazame. Kwani wengine wanaendesha kilimo kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, niongelee na suala la mbegu. Tumeona mkazo mkubwa umekuwa kwenye mbegu chache, zaidi kwa mbegu za mahindi. Kwa mfano, tunaweza kupata mbegu za mahindi kwenye maduka, lakini tumeacha kwenye maeneo mengine kama mbegu za pamba kupata zenye ubora, kupata mbegu za mpunga na zenyewe hatuzipati. Kwa hiyo, nafikiria Serikali iangalie pia zoezi hili la mbegu za kila aina.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia matumizi ya maabara. sisi kwetu Ushetu tumekuwa na maabara ndogo ambazo Serikali imetusaidia, nashukuru sana. Katika Kata ya Mpunze tunacho kituo kwa ajili ya kufanya majaribio ya hizi mbegu, lakini hakijatumika sawasawa. Naomba Serikali iweze kuweka msisitizo ili kama mbegu mara zinapopatikana, basi maabara hizi zianze zenyewe kuotesha ili tuone kama *germination rate* iko nzuri ili wananchi wanavyonunua hizi mbegu tuwe na uhakika kwamba mbegu hizi hazijachezewa, tumepata mbegu zenye ubora na tuweze kusonga mbele bila wasiwasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba sana, kama tumekuwa na maabara hizi zitumike, lakini zitupe majibu; nasi tutadakia kwa ajili ya kuelimisha wananchi wetu umuhimu wa kutumia hizi mbegu ambazo ziko bora inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo napenda nishauri ni kwa kumalizia tu ni kuhusu matumizi ya hizi nyenzo; trekta na *power tiller,* lakini utaona kwamba mashine hizi zinapatikana mjini tu. Wizara ijipange, ione namna ambavyo itatuwekea vituo angalau kidogo tuwe na *sample* ya hizi mashine au vitendea kazi. Wananchi wayaone waweze kuhamasika kuweza kutumia haya matrekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Jimbo langu kwa sehemu kubwa tunalima sana kwa kutumia maksai. Kwa maana hiyo wananchi wako na utayari sasa wa kurahisisha kilimo chao na sisi baada tu ya mvua kunyesha wiki moja ile ya kwanza tunaweza kukamilisha mashamba yetu. Wananchi wana *speed* kubwa, hawataki kupoteza wakati pale mvua za mwanzo zinavyoanza kunyesha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nasi maeneo yetu Mheshimiwa Waziri atazame ili haya matrekta ambayo yako kwenye mpango wa kuzalisha yatakapokuwa tayari, basi yasogee katika maeneo yetu ya uzalishaji ili pia wananchi

waweze kupata hamasa. Tunao uwezo wa kununua matrekta ili tuweze kuzalisha kwa wingi zaidi. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. ELIAS J. KWANDIKWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Naunga mkono hoja. Ahsante sana kwa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Omary Mgumba, atafuatiwa na Mheshimiwa Ignas Malocha na Mheshimiwa Felister Bura, ajiandae.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana nami kwa kunipa nafasi nichangie Wizara hii muhimu ya Kilimo, Wizara ambayo ni uti wa mgongo wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba uniruhusu nitoe pole nyingi sana kwa wananchi wangu wa Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki hususan wananchi wa Kata ya Kinole, Tegetelo na Mkuyuni kwa athari kubwa ya mvua iliyowapata ambayo imesababisha uharibifu mkubwa wa barabara hasa ile ya Madam – Kinole na Bigwa – Kisaki. Niwaambie kwamba suala hili tumeshalifikisha kwa Serikali na naishukuru sana Serikali kwa kuanza kutengeneza, kurudisha miundombinu, ile ya barabara ya Bigwa - Kisaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu kwa Serikali ni kwamba kutokana na hali halisi ya Kinole, leo ni siku ya 15 watu hawana mawasiliano ya barabara. Zaidi ya kilometa 30 watu wanatembea kwa miguu. Naomba na hii barabara itolewe jicho ili iweze kurudisha mawasiliano haraka iwezekanavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, kwanza naishukuru sana Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi

kwa hotuba yao nzuri ingawa tutatoa mchango kwa ajili ya kuboresha tu, lakini kila kitu kimekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, niende moja kwa moja kwenye matatizo. Nianze na Jimbo langu kuhusu matatizo ya migogoro ya wakulima na wafugaji. Naipongeza sana Serikali kwa hatua ambazo imezichukua za kuunda Kamati za Wizara tano ili kutafuta suluhu la tatizo hili. Kama ulivyoshuhudia mwenyewe Mheshimiwa Waziri, kwenye kitabu chako kuhusu migogoro mingi, leo mauaji mengi ya mifugo kwa ajili ya ukame ni Morogoro; mapigano mengi ya wakulima na wafugaji ni Morogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawe unafahamu Morogoro kiasili ulikuwa kwamba siyo Mkoa wa wafugaji, leo neema hii iko Morogoro, maana yake kuna wafugaji ambao wamekuja, hawakuzingatia taratibu na Kanuni za Kisheria kufika pale Morogoro. Ndiyo maana migogoro imekuwa mingi na ndiyo maana mifugo iliyokufa imekuwa mingi kutokana na ukame na uvamizi wa ardhi bila kufuata taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ombi langu kwa Serikali, wakati tunasubiri hii taarifa kufanyiwa kazi, lakini tuliona Serikali hii ya Awamu ya Tano imewatoa kwa nguvu kubwa sana wafugaji waliovamia mbuga za wanyama katika Hifadhi za Serikali. Kwa sababu hizo hizo, basi tunawaomba wawatoe kwa nguvu wale wafugaji wavamizi wasio halali, walioingia katika maeneo ambayo sio yao. Isiwe na kisingizio cha kusema hakuna pa kuwapeleka. Kama wale waliotolewa kwenye misitu walipatikana pa kuwapeleka na hawa wavamizi watafutiwe sehemu ya kwenda ili kumaliza tatizo hili la wakulima na wafugaji katika maeneo yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kuhusu madeni ya Mawakala wa Mbolea, huu ni mwaka zaidi ya wa pili na nusu sasa tunazungumza kwamba Serikali inafanya uhakiki. Nami naiunga mkono sana Serikali yangu kwa sababu sishabikii na siko tayari Serikali iwalipe watu ambao ni

wababaishaji na wadhulumaji ambao hawakutoa huduma Serikalini, walipwe kwa jasho ambalo hawajalitumikia. Niko pamoja na Serikali yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ucheleweshaji huu umeleta athari kubwa sana kwa watoa huduma hizi. Watu wameuziwa nyumba zao, ndoa zao zimesambaratika, yaani maana yake watu wameachana na wake na waume zao kutokana na migogoro kwamba hakuna kipato ndani *ya* nyumba, lakini pia watu wamefilisiwa. Wengine wamejiua na kupoteza maisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ombi langu kwa Serikali leo hii, kwa mfano, mtu aliyekopa shilingi milioni 100 benki, miaka miwili anadaiwa na benki zaidi ya shilingi milioni 40 kama riba aliyochukua asilimia 20. Itakuwa ni kuwaonea. Kwa wale watakaokuja kugundulika ambao ni halali na wametoa huduma kuja kuwalipa kiasi kile kile kama wanachoidai Serikali, kwa sababu siyo kosa lake kwa kuchelewa, ni kosa la mtu mwingine. Ni vizuri mkalichukulia hili kuwalipa pamoja na fidia na gharama za riba walizochukua mikopo kule benki ili kuwarudisha watu hawa katika sehemu tuliyowakuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kufanya hivyo, maana yake tumewapeleka kwenye umaskini mkubwa sana. Leo hii kuna watu wangu kule walikuwa wanatoa ajira ya kujiajiri kwa wenzao, lakini leo wamekuwa ombaomba, wameshafika zaidi ya mara nne hapa kufuatia madai haya Wizara ya Fedha, kwa Waziri Mkuu na Waziri wewe mwenyewe, mpaka leo hawajapata. Wanashindwa kujilipatia mpaka nauli. Leo huyo mtu aliyejiajiri mwenyewe anatakiwa asaidiwe! Jua kwamba tatizo hili ni kubwa na limesababisha ombaomba wengi miongoni mwa watu wengi waliokuwa na uwezo mkubwa wa kujihudumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, la nne, kwenye wabanguaji wa korosho, yaani kama Taifa mpaka sasa hivi

ninachanganyikiwa; tunataka Tanzania ya viwanda au tunataka Taifa la kuzalisha malighafi kwa ajili ya viwanda vya wenzetu? Kwa nini ninasema hivi?

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ni zaidi ya mwaka wa 20 tangu tuanze kuingia kwenye *private sector,* lakini zaidi ya asilimia 90 ya korosho inayozalishwa nchini inapelekwa nje ya nchi huko India au Vietnam kubanguliwa. Wakati mwingine Mheshimiwa Waziri mwenyewe anasifia kabisa, tumeuza korosho tani 4,000 imeenda Vietnam. Tunaona kama sifa! Naona kwamba hatujaelewa mustakabali au nia kubwa ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tano Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Rais alisema anataka viwanda na alisema hakuna mtu yeyote atakayemzuia ndoto zake; yule atakayemzuia atakwama mwenyewe. Nimuulize Mheshimiwa Waziri, nani anayemkwamisha katika uwekezaji wa ndani wa Viwanda vya Korosho kubanguliwa? Maana korosho hizi kwenda katika *raw form* India ama Vietnam maana yake tunahamisha utajiri na ajira kwenda kwenye Mataifa mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii kuwashindanisha wawekezaji wa ndani au wabanguaji wa ndani wadogo na wakubwa kwenye mnada na wanao-*export* kwa *raw form,* hakuna mwekezaji yeyote wa ndani ataweza kushinda mnada wowote ule. Kwa sababu nchi hizo za India na *Vietnam, export levy* yoyote wanayoiweka wenyewe wanaenda kurudishiwa. Nani ambaye atashinda mnada kwa hapa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushahidi upo wazi na ndio maana 90% za kusafirisha *raw form* na viwanda vilivyokuwepo; natolea kwa mfano mdogo, kwamba tulisema Wahindi wanyonyaji; wamekuja Wachina, *Sun Shine Group* kampuni kubwa kuliko zote kule China imewekeza leo Lindi ina uwezo wa *ku-process* zaidi ya tani 5,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye mnada wa mwaka 2016 tumezalisha korosho zaidi ya tani 264,000*MTS*, imenunua

tani 180 tu, tena za mwisho wa mnada baada ya wanunuzi ma-*giant* kuondoka, unategemea huyo ni nani atakuja kuwekeza Tanzania kwenye korosho kwenye *processing?* Mtu wa nje anakuja baada ya kuona mafanikio kwa mtu wa ndani kwamba amefanikiwa vipi au mwenzie aliyetangulia kwenye biashara hiyo amefanikiwa nini; naye ndio atavutika kuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu katika hili kwa Serikali, la kwanza ni vizuri kuendesha minada miwili tofauti, tukaiga *model* kama ya Msumbiji. Korosho ukianza msimu, kipaumbele cha kwanza, mnada wa kwanza, wanaletwa *Local Processors* watupu washindane kwa ajili ya kuhakikisha wanapata *raw materials* kwa ajili ya ku-*process* ndani, kutoa ajira kwa wananchi wetu; lakini pia kuongeza thamani kwenye korosho zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii tunavyo-*export raw,* maana yake Wahindi ndio wanaingiza *foreign currency* nyingi zaidi kuliko Watanzania. Mfano mdogo tu, korosho hapa leo wameuza Sh.4,000/= lakini ikibanguliwa zaidi ya Sh.25,000/= kwa kilo. Sasa nani anapata korosho bei kubwa zaidi? Ninyi au Vietnam? Sisi au Wahindi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri tuhakikishe tunawavutia wawekezaji, tuweke mazingira, wawekezaji wa ndani wapate korosho kwanza kama *raw material* kabla ya mtu mwingine yeyote. Wakishajaza ndiyo turuhusu ku-*export,* watu wa nje waje watoe. Katika kufanya hivyo tusije kumlalia mkulima. Serikali iangalie namna gani kwa zile bei watatoa kwa *Local Processors* ili twende sambamba.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, muda wako umekwisha.

**MHE. OMARY T. MGUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ignas Malocha, atafuatiwa na Mheshimiwa Felister Bura na Mheshimiwa Constantine Kanyasu, ajiandae.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuungana na wachangiaji waliopita katika Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa ahadi zake za kuondoa tozo mbalimbali za mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi, nampongeza sana. Nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Makatibu wao kwa taarifa yao nzuri. Tunajua ameingia hivi karibuni, lakini taarifa hii inaonesha mtu huyu ana uwezo wa kuibeba hii Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Kamati ya Kilimo, imechanganua vizuri sana. Naipongeza kwa kweli Kamati mmefanya kazi yenu vizuri sana, hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo ni uhai, kilimo ni viwanda, kilimo ni uti wa mgongo wa uchumi wa Taifa letu. Nchi ikikosa chakula, haina utengamano wa kisiasa, kiusalama na hakuna atakayekusikiliza kwa jambo lolote lile. Ndiyo maana Waswahili wanasema adui mwombee njaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hali hiyo, bajeti ya kilimo kama wenzangu walivyotangulia kusema, ni ndogo sana. Hata tuseme maneno namna gani, tutamlaumu Mheshimiwa Waziri bure, bajeti ni ndogo. Sisi wote tuungane kusukuma jambo hili kwamba bajeti haitoshi. Kama kweli kilimo ni uti wa mgongo, ni wazi kwamba tukubaliane bajeti hii haitoshi. Tusiposhikamana, basi tusilaumiane, turidhike na kilichopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza wananchi wa Mkoa wa Rukwa kwa jitihada walizonazo za kilimo. Wananchi wa Mkoa wa Rukwa

hawahimizwi kulima, hapana. Wananchi wa Mkoa wa Rukwa wanaweza kudhoofishwa na kilimo kwa kukosa soko, kwa kucheleweshewa pembejeo, mbegu na kupewa madawa feki. Ukiwatimizia mambo hayo wananchi hawa ni hodari kwa kilimo. Hata mwaka huu wamelima vizuri sana, wafanyabiashara njooni mnunue mahindi mkoa wa Rukwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ninalotaka kuzungumzia ni kilimo cha umwagiliaji. Lazima tukubali kwamba ili twende mbele bila mashaka, ni lazima tukubaliane kwenda kwenye kilimo cha umwagiliaji. Nchi yetu ina hekta za kilimo milioni 29.4 ambazo zina sifa ya umwagiliaji, lakini mpaka sasa tunatumia hekta 463,000 tu. Kwa hiyo, hatujafikia hata 2% ya eneo tulilonalo la umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafanya nini ili hizi fursa ambazo tumepewa na Mwenyezi Mungu tuzitumie kikamilifu? Kilimo cha umwagiliaji ndiyo kinaweza kulivusha Taifa hili na kuliweka mahali pazuri. Kwa hiyo, tunaomba Wizara na Serikali itambue jambo hili kwamba ni la muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hifadhi ya chakula ni muhimu sana kwa sababu hatuwezi kumpangia Mwenyezi Mungu kwamba mvua hii itanyesha mwaka huu, mwaka kesho; lazima tuweke chakula cha kutosha hata cha miaka mitano. Unapowapa *NFRA* shilingi bilioni tisa, maana yake unategemea kununua tani karibu 180,000 ambazo ni Mkoa wa Rukwa peke yake unaweza ukatosheleza. Lazima tutenge pesa za kutosha kwa ajili ya kununua chakula cha kuhifadhi kama akiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye ujenzi wa maghala. Wananchi wetu wakati mwingine wanaharibu chakula kwa hofu ya kwamba mazao yao watayaweka wapi? Yanaweza yakanyeshewa na mvua, lakini tungekuwa na maghala ya kutosha, wananchi wangeweza kuhifadhi mazao yao pale anapokuwa na shida ya kuuza anakwenda

anauza. Analazimika kuuza kwa lazima kwa sababu hawana mahali pa kuhifadhi; na uwezo wa kujenga maghala hawana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nizungumzie migogoro ya wakulima na hifadhi za akiba. Jambo hili limezungumzwa mara kadhaa; lipo tatizo kubwa sana la mgogoro wa Hifadhi ya Uwanda *Game Reserve* na wananchi. Hili eneo ni dogo. Bahati nzuri nimemwambia Mheshimiwa Waziri mara kadhaa, rafiki yangu, Mheshimiwa Maghembe, ikiwezekana basi aende akaone suluhisho la kufanya juu ya mgogoro ule. Ataacha watu wauane! Aende ikiwezekana akarekebishe mipaka. Namwomba sana angalau uende, wananchi wakuone inaweza kusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni shamba la Malonje. Shamba hili nimelizungumzia miaka sita. Sijui kuna mwarobaini gani katika jambo hili? Kwa mara ya mwisho amekuja Waziri wa Ardhi, Mheshimiwa Lukuvi akasema mimi ndio nitakuwa wa mwisho kuzungumzia mgogoro wa shamba hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami nasema Mheshimiwa Lukuvi ni hodari, anafanya kazi vizuri sana na Naibu wake. Amefanya kazi katika maeneo mengi, tunamsifu, lakini kuna mfupa gani umemshinda katika shamba hili? Kuna tatizo gani? Shamba tumelizungumzia miaka sita na yeye alisema atakuwa mtu wa mwisho kuzungumzia mgogoro huu, kuna tatizo gani katika jambo hili? Huu mfupa hata fisi anang'ang'ania mpaka anaupasua, hata kama ni mkubwa kiasi gani!

Mheshimiwa Naibu Spika, tunamwomba akamalize mgogoro huu, wananchi wamenipigia simu Jumanne wamechangishana pesa wanakwenda ofisini kwake kupata mwarobaini wa jambo hili. Limechukua muda mrefu mno, wananchi hawana mahali pa kulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, jambo hili walishike vizuri

walimalize kwa usalama. Kwanza wanamtia hofu hata mwekezaji mwenyewe, wanamfanya asifanye kazi kwa uhuru kwa sababu ana mashaka na hata wananchi. Pande zote mbili zinahitaji suluhu ili jambo hili liishe na usalama uweze kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na nasisitiza sana, Mheshimiwa Waziri mgogoro huu waweze kwenda kuumaliza ili wananchi waweze kupata mahali pa kulima. Ila namjulisha kwamba wananchi wamechangishana pesa wanakwenda ofisini kwake, vijiji vyote vinavyozunguka shamba lile, Jumanne wanakwenda. Shamba hili limechukua muda mrefu mno.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani kwa leo naishia hapo. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Felister Bura atafuatiwa na Mheshimiwa Constantine Kanyasu na Mheshimiwa Pascal Haonga ajiandae.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, lakini pia namshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya njema aliyotujalia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijasema jambo, nianze kwa kuipongeza Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, kwa maamuzi mazito na makubwa aliyoyafanya kwa kwa sisi wakazi wa Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeomba ardhi ya Manispaa ya Dodoma iwe mikononi mwa wananchi na tumeomba Wabunge wamepita, Wabunge wamekuja wamepita, lakini mwisho wa siku Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Awamu ya Tano imetupa ardhi yetu ya Manispaa ya Dodoma. Sina lugha ya kusema, sina namna ya kushukuru kwa niaba ya wananchi wa Dodoma hasa Manispaa ya Dodoma. Tunaishukuru sana Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho naiomba Serikali hii, iweke mipango mizuri kuhakikisha kwamba wananchi ambao walishalipia ardhi na hawajaoneshwa viwanja vyao, wakaoneshwe viwanja vyao sasa. Uwekwe utaratibu ambao wale ambao walikuwa wanalipia kidogo kidogo wamalizie kulipia na kupata viwanja vyao. Mpango uwekwe wakati mikakati inaendelea, basi liwepo dirisha kwa ajili ya kuhudumia watu ambao walikuwa wanalipia viwanja, hawajaoneshwa viwanja vyao na wale ambao wanalipia kidogo kidogo huduma ziendelee kama ilivyokuwa *CDA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichangie bajeti hii ya Wizara ya Kilimo sasa, kwamba kilimo ndiyo uti wa mgongo wa Taifa hili, karibu asilimia 75 ya Watanzania wanategemea kilimo; na kilimo wanachotegemea ni kilimo cha kusubiri mvua, bila kujali tabianchi, bila kujali kwamba zipo mvua za kutosha. Asilimia 4.9 tu ya bajeti ya Serikali ndiyo imetengwa kwa ajili ya kilimo. Kwa hiyo, tunaona jinsi ambavyo kilimo hakijapewa msukumo mkubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitegemea kwamba Benki ya Kilimo ingepata fedha za kutosha kwa ajili ya Watanzania ili waweze kukopa; wakulima wa kati, wakulima wadogo na hata wakulima wakubwa. Mabenki ya biashara yanashindwa kuwakopesha wakulima wa kati na wadogo kwa sababu ya riba kubwa na kwa sababu hawana dhamana, wanategemea mvua inayotoka kwa Mungu. Hakuna mabwawa makubwa kwa ajili ya kilimo, hakuna makinga maji kwa ajili ya kilimo. Kwa hiyo, wakulima tulio wengi tunategemea kilimo cha mvua. Kwa hiyo, naomba kwamba Serikali ione namna ya kuchimba mabwawa ya kutosha ili wananchi walime kwa kutegemea kilimo cha umwagiliaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la mbegu. Mbegu asilimia 65 inaagizwa nje ya nchi. Hatuwezi kutegemea mbegu kutoka nje ya nchi kwa asilimia 65, *ASA* wanafanya kazi gani? Kama ni fedha, wapewe wazalishe mbegu. Sasa hivi

wakulima wanategemea mbegu kutoka sokoni. Mbegu ya sokoni iliyozalishwa miaka 20 iliyopita, haiwezi kumsaidia mkulima kujiinua kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna Kambi za JKT, tuna Magereza; tungeweza kutumia Magereza na Kambi za JKT kuzalisha mazao ya kutosha kulisha nchi hii. Wana maeneo makubwa. Kama hawana maeneo makubwa, Serikali iwape maeneo JKT walime. Tunao vijana wengi, tunaweza kuanzisha mashamba darasa kwa ajili ya vijana na vijana wakalima na wakajitegemea na wakazalisha kiasi kikubwa sana kwa ajili ya nchi hii na tukauza na tukapata fedha nyingi sana za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kupanga ni kuchagua. Tunaweza tukapanga kwamba kwa kuwa mikoa ya Kanda ya kati hatuna mvua za kutosha, basi tupate Maafisa Ugani watakaotusaidia kuwashauri wakulima juu ya kilimo cha alizeti, karanga, ufuta, mtama kutokana na hali ya tabianchi. Ukimwacha mkulima alime anavyojua, hawezi kujua mvua itanyesha lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi hapa Dodoma mvua inanyesha mwezi wa 12, mwezi wa Kwanza, wa Pili mvua inakatika. Mwaka huu mvua imenyesha mwezi wa Pili mwishoni na mwezi wa Tatu. Wakulima waliopanda mwezi wa 11 hawakuambulia kitu. Hivyo, kuna haja ya kuwa na Maafisa Ugani wa kutosha ili wawashauri wakulima namna ya kukabiliana na tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala ununuzi wa pamoja. Nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa jambo hili la ununuzi wa pamoja, lakini hapo....

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bura, kengele ya pili imegonga.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Constantine Kanyasu, atafuatiwa na Mheshimiwa Pascal Haonga na Mheshimiwa Gimbi Masaba, ajiandae.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nami namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata nafasi hii kuweza kuchangia na kwa niaba ya wapiga kura wangu wa Geita Mjini, naomba nitumie nafasi hii pia kuwataarifu kwamba lile tatizo lao la watu wa *TFS* kuweka alama kwenye nyumba ambazo zipo katikati ya Mji wa Geita wakidai ni hifadhi, nilishamjulisha Waziri wa Maliasili na kwamba tunachosubiri ni maombi ya *RCC* ili waweze kufikia maamuzi ya kuliachia eneo hilo. Maamuzi hayo yanachelewa sana na wananchi wanaendelea kusumbuliwa. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri wananchi wa Geita wanaomba kuona unachukua hatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mbunge, Mheshimiwa Doto Biteko, nimesomeshwa na pamba, lakini pia nimesomeshwa na uvuvi. Nimesomeshwa na uvuvi, natoka kilometa mbili kutoka Ziwani ndiko nilipozaliwa; na eneo letu tulilokuwa sisi tulikuwa na mashamba makubwa sana ya Nyanza wakati ule.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na pongezi nyingi sana ambazo nampatia Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri na Naibu wake kwenye Wizara hii, hasa kwa kuondoa kero nyingi kwenye zao la pamba. Pia ninaomba kumkumbusha Mheshimiwa Waziri ilikuwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais kuhakikisha kwamba Nyanza *Cooperative Union,* mali zake ambazo zilihujumiwa kinyemela, zinarudi na hatimaye Nyanza iweze kusimama imara. *(Mkofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kilimo cha mkataba inaoneka sasa hivi ni suala geni lakini sisi wakati tunakua wakati ule, pamba ndiyo lilikuwa zao la kujivunia kwenye

Kanda ya Ziwa na umaskini wa wananchi wa Mkoa wa Geita na Mikoa ya Kanda ya Ziwa inaonekana kudorora kwa zao la pamba. Wakati huo mashamba yote ya pamba makubwa na mazuri uliyokuwa unayaona, wananchi walikuwa wanalima yalikuwa aidha ni ya Nyanza au ni ya watu walikuwa wanakopa pembejeo. Mfumo wa kukopa pembejeo ulikuwepo tangu zamani wala siyo mgeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, wananchi walikuwa wanapewa mbegu bora, walikuwa wanapewa madawa na baadaye vyama vya ushirika kwa sababu vilikuwa vina nguvu, vilikuwa vinaweza kununua yale mazao kwa wakati na kuwalipa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri kuona namna ya kuimarisha vyama vya ushirika kwa sababu ndiyo *reliable* vinaweza kuwakopesha wakulima. Kama hilo haliwezekani, ni kuona namna ya kuwafanya hawa *private buyers* ambao mnawapa usajili waweze kuwa *engaged* namna ya kuwasaidia wakulima. Bila kutatua tatizo la kuwapatia pembejeo na mbegu bora wakulima, hatuwezi kulifanya zao la pamba likarudi kwenye nafasi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, namna ambayo naiona hapa, kwanza wakulima sasa hivi wamekata tamaa kwa sababu ukiacha wastani wa heka moja kuzalisha tani mbili na kilo 200 wengi wanazalisha kilo 100 au kilo 200. Sasa kilo 200 hata kama ungempa kilo moja Sh.2,000/= bado hawezi kulipa gharama za kilimo, *productivity* imeshuka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mkulima kama ataweza kuzalisha tani moja kwenye heka, hata ukimpa kilo Sh.1,000/= utakuwa umemsaidia. Tatizo kubwa liko wapi? Tunao Maafisa Ugani wengi sana kwenye Halmashauri za Wilaya, lakini nataka nimwambie Mheshimiwa Waziri hawa watu hawapewi *target.* Ameajiriwa, amepewa ofisi, amepewa Kata, hakuna mtu anayemsimamia. Nataka nimshauri Mheshimiwa Waziri, hebu aweke utaratibu wa

kuhakikisha kwamba hawa watu wanakaguliwa, wanapimwa kwa kitu fulani ambacho wamekifanya kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hawa watu wanaamka asubuhi, anakwenda anasaini, anarudi, analala, hata katika kijiji ambacho anakaa wakulima hawafahamu. Hata katika kijiji ambacho wanakaa hajawahi kutoa utaalam wa aina yoyote. Kwa hiyo, matokeo yake wakulima wameligeuza zao la pamba kuwa zao la pili na wengi wamehama. Wengi wanakwenda kwenye mazao mengine kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Geita watu wengi wanalima mpunga; na mpunga kwa sababu pia hata utaalam wa watu wengi wanalima kutokana na ulimaji wa asili, wamehamia huko kwa sababu ni zao la chakula na zao la biashara. Kwa hiyo, ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri Maafisa Kilimo, hata angeajiri wengi namna gani, kama waliopo hawasimamiwi, bado zao la pamba litaendelea kuwa chini kwa sababu hakuna uzalishaji ambao unaendelea vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema kwamba nilisomeshwa na samaki. Naomba hapa Mheshimiwa Waziri anisikilize vizuri. Ipo sheria ambayo ilitungwa mwaka 2003 na kanuni yake ya mwaka 2009. Sheria ambayo inasema *"it is illegal to manufacture, possess, store, sell and use or cause another person to use for a fishing gear of more than 26 mesh deep in the Lake Victoria.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa lugha ya kawaida wanasema ni makosa kuzalisha au kukutwa una nyavu ambayo ina macho 26. Sasa macho 26 nikifanya mikono yangu miwili hapa, tayari ni macho 26 ya mtego.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri anatoka kisiwani, tumevua wote samaki. Naomba nimkumbushe, ukitoka *Mwanza South* pale ukaenda *Nautical Mile 15*, chini ni mita 70, hebu aende na hiyo nyavu ya macho 26 akavue samaki kama atapata kilo tano. Kinachofanyika sasa,

imetungwa sheria, hiyo sheria imeipitishwa lakini inahamasisha watu waende kuvua samaki kwenye *breeding areas.* Wanakwenda kwenye zile *breeding areas* ambazo tungetarajia ziwe hifadhi, samaki wazaliane kwa sababu nyavu wanayopendekeza ambayo wanaiita *illegal,* ni nyavu fupi. Ni mikono yangu miwili hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda Gozba ni mita 100 chini. Nataka nimpe *challenge* Mheshimiwa Waziri, nimefanya kazi ya samaki miaka 25. Kama ana wataalam wake wa uvuvi awaambie waweke nyavu 100 twende Gozba, wakirudi na kilo kumi naacha Ubunge. Naacha Ubunge kwa sababu wanachokifanya ni kuwaonea kabisa wavuvi. Wanaenda wanachukua zile nyavu, wanaita *illegal* wanazichoma moto.

Mheshimiwa Naibu Spika, mvuvi gani anatengeneza nyavu? Nyavu zimepita bandarini, zimelipiwa ushuru, mvuvi amekopa pesa benki, amekwenda kuweka kwenye mtumbwi, *size* ya nyavu anayotaka ni ile ile nchi tano au sita ambazo wameruhusu; lakini wanasema ikishazidi macho 26 ni *illegal.* Sasa wakati inapita bandarini watu wake walikuwa wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hilo tu. Yeye kama ni mvuvi na anafahamu mambo ya uvuvi twende ziwani. Wavuvi wetu wengi ni *local,* wanafanya *traditional fishing*, hakuna mwenye *fish finder;* hakuna mwenye chochote. Kwa hiyo, hakuna anayeona samaki chini. Tuchukue hizo nyavu tuende *nautical mile* 50 tukatege, halafu turudi kesho tukavue; tukipata samaki kilo 50, mimi naacha Ubunge. Kwa sababu nimefanya kazi hii kwa miaka 20 na nimekimbia huko kwa sababu ya masharti mengi yasiyo na maana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachomaliza samaki Ziwa Victoria ni matumizi ya *monofilament* na matumizi ya makokoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili, Mheshimiwa Waziri…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kanyasu kengele ya pili imegonga.

**MHE. CONSTANTINE J. KANYASU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pascal Haonga.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kabla sijaanza kuchangia Wizara hii, naomba niungane na mchangiaji mmoja aliyetangulia, anaitwa Profesa Jay. Mheshimiwa Waziri naomba nimpe ushauri kidogo, kabla sijaendelea kuchangia, anapokuja kwenye Majimbo yetua jaribu kutushirikisha Wabunge wenye Majimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwambia hili kwa sababu mimi huwa sitaki nikae na kinyongo na huwa sitaki tufanye kazi kwa kinyongo na Waziri wangu. Alikuja Jimboni kwangu, ameenda kufanya mkutano na wananchi, anawaambia wananchi Mbunge wenu yuko wapi? Ameanza kuruka sarakasi kama za Bungeni? Mheshimiwa Waziri hii haifai hata kidogo na kwa wananchi wangu hii siyo haki hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri amefanya hivi pia kule kwa Profesa Jay na Majimbo mengine. Alikuja Mheshimiwa Mwigulu Nchemba Jimboni kwangu, ameniandikia *message*, amenipigia simu nimempa ushirikiano mzuri. Kwa hiyo, naomba wakati mwingine ajaribu kuwa na ushirikiano na mahusiano mazuri na Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme kwamba ukuaji wa Sekta ya Kilimo umeendelea kushuka mwaka hadi mwaka. Ukuaji wa Sekta ya Kilimo, tunaambiwa kwamba ni asilimia 1.7 kwa takwimu za *NBS* na hii unakuja kuona sasa hata bajeti ambayo imetengwa kuanzia mwaka 2010/2011

tuliona asilimia 7.8 ambayo ndiyo ilikuwa bajeti kubwa kwa mara ya mwisho. Tumekuja kuona mwaka 2011/2012, ikawa asilimia 6.9 mwaka jana, 2016/2017 ni asilimia 4.9.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kuwasaidia wakulima wa Tanzania kwa kuendelea kutenga bajeti ya kilimo kidogo kiasi hiki. Naomba niseme tu kwamba *Maputo Declaration* walipendekeza kwamba angalau nchi wanachama wa *AU* wajaribu angalau kutenga asilimia 10 kwenye bajeti za kilimo. Hii *Maputo Declaration* kwa Tanzania tutakuja kuitekeleza lini? Kwa hiyo, naomba niseme kwamba ili kuwasaidia Watanzania hebu tujaribu kutenga bajeti ya kutosha. Kwa mazingira haya, hatuwezi kupata viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nimemwona ndugu yangu hapo Waziri wa Viwanda amebeba makabrasha mengi sana, lakini kwa bajeti hii ya kilimo, kwa kweli naamini kabisa hata Waziri wa Viwanda asitegemee kuwa na viwanda kwa sababu hawezi kuwa na viwanda bila kuboresha kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, historia inatuonesha duniani popote pale, walifanya mapinduzi kwenye kilimo. Tunajua ile *Agrarian Revolution* iliyofanyika kule Britain*, tunajua Agrarian Revolution* iliyofanyika kule Marekani, tunajua *Indian Green Revolution*, tunajua ile *China Green Revolution* ndipo tukaona sasa wenzetu viwanda vinakuja. Viwanda ni matokeo ya kuboresha kilimo na kupeleka fedha nyingi na kuhakikisha kwamba wakulima mambo yao yanakwenda vizuri kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano viwanda vya nguo, wanategemea pamba; bila kuwekeza kwenye pamba hatuwezi kuwa na viwanda. Bila kuwekeza kwenye mbegu kwa mfano kama alizeti na ufuta hatuwezi kuwa na viwanda vya mafuta. Kwa hiyo, niseme tu kwamba Mheshimiwa Waziri naomba tafadhali, ajaribu kushauri. Najua tu tatizo la viongozi wetu walio wengi hasa Mawaziri mnamwogopa Bwana mkubwa. Hii ndiyo shida kubwa! Mwambieni ukweli,

msiogope! Ukweli ndiyo utakaokuweka huru. Kwa bajeti hii, hatuwezi kufika popote na mwakani tutarudi kuja kupiga kelele tena hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo ambalo Mheshimiwa Waziri amezungumza kwenye hotuba yake kuhusu suala la *bulk procurement* ya mbolea. Siyo jambo baya, lakini naomba tungekuwa tuna-*focus* zaidi kwenda kujenga viwanda vya mbolea nchini kote.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukijenga viwanda kwa mfano ukajenga Kiwanda cha Mbolea kanda ya Nyanda za Juu Kusini ambao ni wazalishaji wakubwa sana, ukijenga kiwanda kwa mfano Kanda ya Kaskazini, ukajenga Kiwanda cha Mbolea Kanda ya Magharibi, Kanda ya Kati, Mheshimiwa Waziri mbolea itashuka bei. Kwa sababu tunajua kabisa, kwa mfano, hili suala la saruji, leo kidogo bei ni nafuu kwa sababu viwanda vya saruji viko vingi. Watafanya biashara ya ushindani na mwisho wa siku mbolea itashuka bei. Kwa hiyo *bulk procurement* ni jambo moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, hili la kujenga viwanda. Tungeendelea kabisa kufikiria hili zaidi kuliko tukawa na hizi kuzibaziba tu angalau kwa muda mfupi, haliwezi kutusaidia sana. Kwa hiyo, naomba niseme tu kwamba alikuja hapa Mfalme wa Morocco, Mohamed wa Sita, tukamwomba atujengee uwanja wa mpira Dodoma. Nadhani wanapokuja watu wetu, kama hawa wadau wa maendeleo, tungekuwa tunawaomba wawekeze kwenye viwanda vya mbolea. Wakiwekeza kwenye viwanda vya mbolea, wakulima wetu watanufaika. Mbolea itashuka bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nchi yetu zaidi ya miaka 50 baada ya uhuru tunamwomba mtu uwanja wa mpira badala ya kumwomba viwanda vya mbolea! Mheshimiwa Waziri kwa kweli mimi hili naona siyo sahihi kabisa. Naona leo tumeomba viwanja vya mpira, kesho tutaomba jezi, kesho kutwa tutaomba mipira. Hili jambo halitatufikisha popote pale. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa niweze kuzungumzia jambo lingine kwenye bei ya zao la kahawa. Zao la kahawa limeendelea kushuka bei miaka yote. Wenzetu wa korosho mmerekebisha mambo vizuri kabisa kule, leo korosho wananufaika kweli kule Kusini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kahawa imeendelea kushuka bei mwaka hadi mwaka. Ndugu zetu wa jirani tu hapa wa Kenya wanauza kahawa bei nzuri, Uganda wanauza kwa bei nzuri, Tanzania ni nani aliyeturoga? Tatizo liko wapi, Tanzania kahawa yetu tunauza kwa bei ndogo? Leo wakulima wangu Mbozi kule wameamua kuanza kung'oa miche ya kahawa kwa sababu wameona hailipi. Wanaamua walime mazao mengine kwa sababu ya bei ndogo ya kahawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwasaidie wakulima hawa wa Kahawa, tupandishe bei na ikiwezekana kabisa tuweze kuangalia namna gani ya kuweza kupandisha bei. Kwa nini tusiende kujifunza kwa majirani zetu? Mbona Kenya siyo mbali, hata kwa pikipiki unafika hapa jirani Kenya! Mbona Uganda siyo mbali, kwa nini tusiende kuwauliza ninyi mnauzaje kahawa yenu kwa bei nzuri? Kwa nini Tanzania sisi hatuuzi kahawa yetu kwa bei nzuri?

Mheshimiwa Waziri kwenda kujifunza kwa ndugu yako siyo dhambi hata kidogo! Naomba sasa tukajifunze tuangalie wenzetu, kwa nini wanauza kahawa yao kwa bei nzuri, tuone sisi tuliteleza wapi, tuweze kuwasaidia wakulima wa kahawa, zao ambalo linaelekea kwenda kufa siku za hivi karibuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, naomba nizungumzie suala la kuanzisha Mnada wa Kahawa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini. Leo nchi nzima, Watanzania wanaolima kahawa wanaenda Moshi kwenye Mnada wa Kahawa. Tukianzisha Mnada wa Kahawa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, kwa mfano, tukaweka Kiwanda cha Kahawa

pale Songwe au tukaweka Mbeya, wakulima wetu wataenda kushiriki moja kwa moja kwenye Mnada wa Kahawa pale. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kuisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Haonga, kengele ya pili tayari.

**MHE. PASCAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Naomba niseme tu kwamba jambo la mwisho…

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Gimbi Masaba.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi na leo nisimame mbele ya Bunge lako kuchangia Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kutambua hatua iliyoanza au aliyoifanya Waziri wa Kilimo; kwa sababu nilivyokuwa najaza hii nafasi kwa maana ya kuja kuchangia Wizara ya Kilimo na Mifugo, nilidhamiria kuwa mtu mwenye hasira sana, lakini kuna jambo ambalo nimeliona humu, kitendo cha kujaribu kufuta ushuru mdogo mdogo kwa maana ya ushuru wa mazao pamoja na mifugo, nimetambua hatua hiyo. Naomba niseme kwa nini nilidhamiria kuwa na hasira? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wangu wa Simiyu kulikuwa na changamoto moja kubwa sana ambayo ilikuwa inafanyika kwa wafugaji kila wanapokwenda kuuza ngombe kwenye minada kulikuwa na utaratibu anaingiza ngombe kwenye mnada bure. Wakati wa kutoa ngombe anatozwa ushuru wa Sh.1,000/= kila kichwa cha ngombe, awe ameuza au hajauza ushuru lazima atoe. Jambo hili lilipelekea kuleta matatizo makubwa sana kwa wananchi

wa Mkoa wa Simiyu. Kwa kutambua hili kwamba wamefuta ushuru huu, ndiyo maana nikajikuta hasira yangu kidogo imepungua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe ushauri, pamoja na kutoa kodi hizi, naomba basi Mheshimiwa Waziri apeleke waraka haraka sana kwenye Halmashauri zetu, ili jambo hili lianze kutekelezwa kwa haraka na wananchi waweze kunufaika na mifugo yao ambayo wanaitunza kwa muda mrefu, wanatumia gharama kubwa ili waweze kunufaika nayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, masikitiko yangu yalikuwa kwamba sisi Wasukuma ng'ombe ni *ATM* yetu. Ukipatwa na janga la njaa kwenye familia, unachagua ngombe wawili, watatu unapeleka mnadani, unauza unanunua chakula. Sasa walivyokuwa wanaambiwa wauze, wasiuze, lazima walipe ushuru, nilikuwa napata masikitiko makubwa sana, kwa sababu huyu mtu ana njaa halafu unamwambia atoe ushuru wakati ng'ombe hajauzika, ilikuwa ni jambo la aibu sana katika mkoa wetu. Kwa hiyo nashukuru katika hilo kwamba limeonekana na naomba nisisitize waraka upelekwe haraka sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jana nilisimama hapa nikichangia Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji; nilijaribu kugusia suala la pamba, lakini leo nataka nimtafute mchawi wa pamba. Zao la pamba tunamtafuta ni nani aliyesababisha zao hili lipotee? Kumekuwa na historia ya wakulima wa pamba, zamani tumekuwa tukipewa mbegu ambayo ilikuwa na manyoya kidogo, ile mbegu walikuwa wananunua wazazi wetu, tunalima tunazalisha. Mbegu ile ikibaki, ninachokikumbuka tulikuwa tunakwenda tunatengeneza magodoro, tunaendelea kulalia mbegu ambayo ilikuwa inabaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini cha kushangaza sasa hivi, nataka kujua, ni nani aliyeshauri mbegu hii ya pamba

ipelekwe saluni, halafu iletwe sisi tuanze kupanda? Nataka kujua, maana tumeletewa mbegu ambayo ni ya kisasa na mbegu hii haioti na ikiota inaota mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta mwananchi ametumia gharama kubwa kuandaa shamba la pamba matokeo yake anavuna kidogo. Heka moja inatoa kilo 30, anakwenda kuuza kilo ya pamba Sh.1,000/=, halafu tunasema kwamba leo tunamtafuta mchawi ni nani? Mchawi wa pamba ni Serikali yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukiambiwa pamba ya Tanzania ni chafu... *(Kicheko/Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**MBUNGE FULANI:** Kweli.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Masaba, kuna taarifa.

**TAARIFA**

**NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza nimshukuru mchangiaji anachangia vizuri, lakini naomba nimpe taarifa katika hoja yake aliyosema kwamba mbegu zile zilizokwenda saluni hazioti. Nataka nimwambie kwamba bahati nzuri mimi nilikuwa *DC* Butiama na Mkoa wa Mara ulikuwa ni mmoja wa mikoa ambayo ilikuwa imetengwa kama kanda ya uzalishaji mbegu na ilikuwa inafanya kazi hiyo na ikaweza kutoa mbegu nyingi ambazo zilikuwa zinakwenda kupandwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo lililokuwepo ni baadhi ya wakulima kutojua namna ya kutumia zile mbegu. Ile inatakiwa iwe sentimita 10 tu kwenda chini, wao walikuwa wanakata kwa majembe ya ngombe wanazitupia ndani, matokeo yake hazioti kwa wakati. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gimbi Masaba unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na kumheshimu dada yangu, ingekuwa sheria inaruhusu ningemjibu kwa kinyumbani, lakini taarifa yake siipokei, kwa sababu amekubali kwamba tatizo ni kwamba wananchi hawakuelewa matumizi ya ile pamba. Ilikuwa ni jukumu la nani kuwaelimisha hao wananchi kama siyo Serikali? Kama Serikali haikuwajibika kuwaelimisha namna ya matumizi ya hii mbegu, maana yake bado mchawi ni Serikali yenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitoka kwenye suala la mbegu hii kumekuwa na changamoto ya kuchelewesha mbolea. Tunategemea sana kilimo cha msimu. Mvua zetu ni za msimu; kuna mvua za kulimia, kuna mvua za kuoteshea, kuna mvua za mwisho. Sasa wananchi wamekuwa wakiletewa mbolea kwenye mvua ya kuvunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama tatizo ni kuleta mbolea, naomba Mkoa wa Simiyu, jana nilizungumza kwamba sisi tunazalisha mbolea. Kama tunazalisha mbolea, naomba basi wananchi wapewe elimu waweze kuitumia mbolea ambayo wao wanaizalisha kule, ambayo ni mbolea ya ngombe, kuliko kusubiri mbolea ambayo haijulikani itakuja wakati gani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini kabisa kwamba wananchi wale wakifundishwa matumizi ya mbolea wanayoizalisha, hakuna ngombe atakayedondosha kinyesi chochote, watatamani hata kuwafungia maliboro kwenye nanii ili kuhakikisha ile mbolea haipotei. Ni kwa sababu hawajui matumizi yake, ndiyo maana ile mbolea inapotea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumze kuhusu suala la mifugo. Tumekuwa na changamoto sana kuhusiana na suala la malisho. Mwaka 2016 niliuliza swali hapa, kuhusu kutenga maeneo ya kuchungia. Nikadai eneo la *Maswa*

*Reserve* kwamba limekosa sifa, kwa nini lisirudishwe kwa wananchi ili waweze kuchungia ngombe zao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa na changamoto kwenye maeneo ambayo yako karibu na hifadhi...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gimbi malizia, sentensi.

**MHE. GIMBI D. MASABA:** Mheshimiwa Naibu Spika, basi naomba niunge mkono hoja ya Upinzani. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Gimbi mchangiaji wetu wa mwisho.

Waheshimiwa Wabunge nina tangazo moja hapa linatoka Ofisi ya Bunge. Mnatangaziwa kwamba siku ya Jumapili tarehe 21 Mei, 2017 kutakuwa na Semina kwa Wabunge wote kuhusu faida za utalii na umuhimu wa kuhifadhi mapori. Semina hiyo itaratibiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii na itafanyika katika Ukumbi wa Bunge kuanzia saa 4.30 asubuhi. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, leo asubuhi niliombwa mwongozo na Mheshimiwa Devotha Minja, simwoni hapa, lakini naamini kwamba atapata hizi taarifa. Nilisema ningeutoa huo mwongozo baadaye na nitatoa huo mwongozo sasa.

Waheshimiwa Wabunge, katika Kikao cha 29 cha Mkutano wa Saba wa Bunge kilichofanyika leo tarehe 19 Mei, 2017, Mheshimiwa Devotha Mathew Minja aliuliza swali la msingi namba 242 kwa Wizara ya Habari, Utamaduni Sanaa na Michezo kuhusu lini Serikali itaanzisha mfumo wa kutambua kazi zinazofanywa na Tasnia ya Habari? Baada ya swali hilo la msingi kujibiwa Mheshimiwa Devotha Minja aliuliza maswali ya nyongeza kuhusu vitendo vya kuwazuia Waandishi wa Habari kutekeleza majukumu yao kwa kuwaweka ndani na kuvamiwa kwa Kituo cha Utangazaji cha *Clouds TV.*

Maswali hayo ya nyongeza yalijibiwa na Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Pamoja na mambo mengine, alieleza kuwa suala la kuwazuia Waandishi wa Habari kutekeleza majukumu yao, Wizara haijapata taarifa rasmi zaidi ya kumsikia Mheshimiwa Devotha Minja akisema hivyo.

Mheshimiwa Naibu Waziri alimwomba Mheshimiwa Devotha waonane naye ili ampe taarifa kamili ndipo Wizara iweze kulifanyia kazi jambo hilo. Baadaye Mheshimiwa Devotha Minja aliomba mwongozo wa Spika kwa kutumia kanuni ya 68(7) na kanuni ya 46 ya Kanuni za Kudumu za Bunge kwa kueleza kuwa maswali yake ya nyongeza hayakujibiwa kikamilifu.

Kiti kilielekeza kuwa kitaangalia Kumbukumbu Rasmi za Bunge ili kuona namna swali lilivyoulizwa na majibu yaliyotolewa na Naibu Waziri ili kiweze kutoa mwongozo.

Baada ya kuzipitia Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)* kiti kimeridhika kwamba majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo kuhusu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Devotha Minja, yalikuwa ya kuridhisha na yenye kujitosheleza. Kwa ufafanuzi zaidi maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Devotha Minja yalikuwa kama ifuatavyo:-

*"Swali la kwanza, ni kuwa, Sheria ya Huduma za Habari ya Mwaka 2016 inahitaji kazi ya Uandishi wa Habari kuwa ni jukumu la kisheria, Serikali inawachukulia hatua gani watu wanaowazuia Waandishi wa Habari kutekeleza majukumu yao?*

*Swali la pili; kwa kuwa hivi karibuni kumekuwa matukio kadhaa ya waandishi wa habari kuzuiwa kufanya kazi zao kama vile RC kuvamia Kituo cha Clouds, baadhi ya Waandishi kuvamiwa wakiwa kwenye Mkutano wa CUF baadhi ya Wakuu wa Wilaya kuwakamata Waandishi wa Habari na kuwaweka ndani na hata jana, kule Arusha katika Shule ya Msingi Lucky Vicent Waandishi wa Habari 10 walikamatwa*

*wakiwa wanatimiza majukumu yao, ni lini Serikali itaacha tabia hii mbaya ya kuwakamatakamata Waandishi wa Habari wakiwa kwenye majukumu yao?*

Katika majibu yake Naibu Waziri huyo alieleza kama ifuatavyo:-

*"Kwa kutambua kwamba Sheria ya Vyombo vya Habari ya Mwaka 2016 inahimiza kwamba kazi ya Waandishi wa Habari ni jukumu la kisheria, nadhani sote tunakubaliana na hilo; lakini anaposema kwamba kuna watu wanawazuia kufanya kazi zao, mimi naamini kwamba kama kweli Waandishi wa Habari wanafuata maadili na wanatafuta habari kwa ajili ya kujenga na siyo kuvuruga nchi, siamini kabisa kwamba kuna mtu anaweza kuwazuia.*

*Sera yetu ya habari na utangazaji ya mwaka 2003 inahimiza kwamba taasisi zote za Serikali na wadau wote wa habari wanatakiwa watoe taarifa kwa wanahabari na hasa inahimiza kabisa kwamba wale Maafisa Habari katika Mikoa na Halmashauri wawe tayari kutoa ushirikiano kwa wanahabari ili kusudi wanahabari waweze kutekeleza majukumu yao.*

*Sasa kama kuna hili la watu wanaowazuia, mimi naomba baadaye tuonane na Mheshimiwa Devotha Minja aweze kuniambia ni wapi? Kwa sababu ndiyo kwanza ninasikia hilo. Sera yetu inahimiza kwamba ni wajibu kwa Maafisa wa Habari kuwapa ushirikiano wanahabari kwa sababu jukumu lao linatambulika kisheria."*

*Katika swali la pili Mheshimiwa Waziri alilolitolea ufafanuzi vizuri sana wakati anahitimisha hotuba yake hapa Bungeni, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Naibu Spika nisirudie tena maneno ambayo aliyasema Mheshimiwa Waziri hapa Bungeni."*

Kutokana na maelezo hayo ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ni wazi maswali yote yalijibiwa ipasavyo na kikamilifu. Hata hivyo, Mheshimiwa Devotha Minja anaweza kuitikia wito

wa kuonana na Mheshimiwa Naibu Waziri ili aweze kujadili na kulipatia ufumbuzi jambo linalomtatiza kama lipo.

Zaidi ya hayo, ni vema ifahamike kuwa kutokana na uamuzi wa Mheshimiwa Spika wa tarehe 13 Septemba, 2016 kuhusu Mbunge ambaye hataridhika na majibu ya swali la nyongeza haitaruhusiwa majibu ya swali kurudiwa kwa ajili ya kupata majibu ya ufasaha, isipokuwa swali la msingi tu. Ikiwa Mbunge hakuridhika na majibu ni vema akawasilisha swali hilo kama swali la msingi kwa kufuata utaratibu wa kikanuni uliopo.

Waheshimiwa Wabunge, maneno ya Spika wakati huo yalikuwa kama ifuatavyo: Mheshimiwa Spika, alikuwa ameombwa mwongozo kuhusu majibu ya swali la nyongeza na tarehe hiyo niliyoitaja alisema maneno haya wakati akitoa maamuzi. Alisema:

*"Hatuwezi kujikita kuridhisha maswali ya nyongeza ya papo kwa papo kupata majibu ya ufasaha. Laiti kama ingekuwa ni swali la msingi, tungeelekeza kurudia majibu. Hoja hii imefungwa rasmi."* Hayo ni maneno aliyasema Mheshimiwa Spika.

Kwa maelezo hayo nahitimisha kwa kueleza kuwa majibu yaliyotolewa yanajitoshelaza na hayahitaji kupewa majibu mengine. Huo ndiyo mwongozo wa Spika. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema mwongozo huu, naahirisha Bunge mpaka kesho siku ya Jumamosi, tarehe 20 saa 3.00 asubuhi.

*(Saa 1.51 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumamosi, Tarehe 20 Mei, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*